

**TAASHIRA NA UTENDAJI KATIKA NYIMBO ZA HARUSI ZA  
WASWAHILI, KISIWANI UNGUJA**

**ABDULRAHIM HUSSEIN TAIB ALI**

**Tasnifu hii Imewasilishwa katika Shule ya Walohitimu, Kutimiza baadhi ya Mahitaji ya  
Shahada ya Uzamifu (Ph.D) katika Chuo Kikuu cha Egerton.**

**Chuo Kikuu cha Egerton**

**AGOSTI, 2014.**

## UNGAMO NA IDHINI

### UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

Abdulrahim Hussein Taib Ali

AD12/0201/07

Sahihi.....

Tarehe..... 10/08/2014


### IDHINI

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa katika Shule ya Waliohitimu kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton.

Sahihi.....  
Prof. Fugick Wako

Tarehe..... 22/9/14

Idara ya Fasihi, Lughu na Isimu, Chuo Kikuu cha Egerton.

Sahihi.....  
Dkt. Beja S. Karisa

Tarehe..... 17/9/14

Idara ya Fasihi, Lughu na Isimu, Chuo Kikuu cha Egerton.

## **HATI LINZI**

**© ABDULRAHIM HUSSEIN TAIB ALI**

Haki zote zimehifadhiwa. Huruhiswi kuigwa, kunakili, kutafsiri au kuhifadhi kwa mfumo wowote ule au kutoa hata sehemu kidogo ya tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

## **TABARUKU**

Natabaruku kazi hii kwa walimu, wanafunzi na wapenzi wote wanaopenda kusoma fasihi simulizi ya Waswahili.

## **SHUKRANI**

Kwanza kabisa sina budi kumshukuru Allah (S.W) kwa kuniwezesha kukamilisha kazi hii. Watu wengi wamenisaidia katika kufanikisha utafiti huu na, nawashukuru wote. Hata hivyo napenda kutaja majina ya watu walionisaidia zaidi. Nao ni Wasimamizi wangu Prof. F.Wako na Dkt. K.S.Beja kwa kunikosoa, kunishauri na kuniongoza.

Vile vile napenda kuwashukuru walimu wangu Dkt. Chai, Prof. C. Kitetu, Prof Ilieva, Prof. Onyango, na Prof. M.Mukuthuria kwa nasaha na maelekezo waliyokuwa wakinipatia. Bila kumsahau Bi. Grace aliyekuwa muhazili katika Idara ya Lugh, Fasihi na Isimu, ye ye alikuwa kila mara akinipa taarifa zinazonihusu nilipokuwa mbali na chuo. Wote hawa wanatoka Chuo Kikuu cha Egerton. Shukrani pia zimuendee Dkt. P. Mtesigwa wa Chuo kikuu cha Dar es Salaam kwa kunitia moyo na kuisoma kazi hii bila ya kinyongo nilipokuwa naye Libya. Shukrani zangu za dhati pia ziwafikie Prof.T.S.Y. Sengo (Dar), Maalim Amour, Mw. Omar, Bi. Zulekha, Dkt. Ziddy, Dkt Maulid, Mw. Mmanga, Maalim Hussein na Mw.Omar Zaid wote kutoka (SUZA). Aidha napenda shukrani zangu ziwafikie Dkt. Idriss, Dkt. Othman, Dkt. A. Oheida, Dkt. Khalifa, Dkt. Aujari, Maalam Mansoor, Maalam Nura Baba, Maalam Hafidh (Sarki), Mw. Jabir, Mw. Hussein Hamid, Mw. Salim na Mw. M.Yunnus wote kutoka Chuo Kikuu cha Sebha – Libya kwa kunihimza na kunitia moyo niendele na masomo. Bila kumsahau mwanafunzi mwenzangu wa uzamifu Dkt. B. Matasi (IUIU - Uganda), naye namshukuru kwa ushauri wake wa mara kwa mara.

Nitakuwa ni mtovu wa shukrani iwapo sikuwashukuru kina Bi. Amina, Bi. Salma, Bi. Riziki na Bi. Mwanamtumwa wa Maarifa Group -Zanzibar kwa msaada wao wa hali na kuwa nao muda mwingi wakati wa kukusanya data.

Mafanikio ya utafiti huu pia yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na mashirikiano niliyopata kutoka kwa wahojiwa walioteuliwa. Siwezi kuwataja wote lakini baadhi yao ni pamoja na Mzee Haji Gora, Mzee Alawy, Bi. Kidude, Bi. Mwanamkisi na Bi. Sihaba.

Shukrani maalumu zimuendee mpenzi, mke na mama wa watoto wangu Bi. Maimuna (Ummu Nourah) mtafiti msaidizi wangu wakati wa kufanya utafiti. Hakuacha kunitia moyo na kuniombea dua kila wakati. Aidha, shukrani kama hizi ziwafikie wanangu Nourah, Abdul-Latwif na Azzan kwa kunistahamilia kwa kipindi chote.

Aidha, dua za wazazi wangu Maalim Hussein Taibali (Allah amrehemu) na Mama Nuru (Bi Zarina) ambazo naamini zimenisaidia sana katika kufanikisha kazi hii. Nawashukuru sana kwa hilo Allah awe radhi nao. Aidha nawashukuru kaka zangu Murshid (Allah amrehemu), Mahmoud, Badru, Abdul-Razak, Bablee. Bila kuwasahau dada zangu Riziki, Salame, Zulekha na Momo wote hawa walikuwa wakinipa moyo kila nilipokata tamaa.

Watu wote hawa Allah (S.W) atawalipa.

## **ABSTRACT**

This study set out to analyze the use of symbolism and performance of Swahili songs during wedding in Unguja. The research was carried out, completed and the findings given. Chapter one of this thesis mainly explains the statement of the problem which was a knowledge gap on the use of symbolism and performance of Swahili songs during weddings. There are also research questions that include identification of symbols and ritual performances that are significant for the wedding ceremony and the establishment of the meanings of the symbols used in the songs and ritual performances. Chapter two lays down what other scholars have written on symbolisms, Swahili songs and performances. The chapter also explains Performance and Semiotic theories as guiding theories of the study. Chapter three explains the methodology used in the research, which are mainly interviews and participant observations, though in certain song performance contexts where cultural prohibition does not allow a man, a female research assistant was employed. The chapter also explains that the collected data was descriptively analyzed by coding in order to group the songs with symbolisms and songs with ritual performances that are significant to the wedding ceremony separately. Chapter four presents the findings on the use symbolism, which shows that symbolisms in wedding songs have a cultural significance in underscoring to the bride and the groom, the expected life as a couple. In chapter five, the researcher has given findings on performance which demonstrates the necessity of ritual performance as an accompaniment to the wedding songs that are sung as ritual songs. Chapter six discusses the implications of the use of symbolism in wedding occasions to show that they are semantically significant and performance which are ritually significant during weddings in Unguja Island. These findings therefore confirm both research questions which the research had set out to answer and contribute significantly to the field of oral literature, in particular on the songs of the Coastal people of East Africa.

## **IKISIRI**

Utafiti huu ulishughulikia taashira na utendaji katika nyimbo za harusi za Waswahili wa Unguja. Utafiti ulifanywa, na matokeo ya tasnifu hii yalidhihirishwa. Sura ya kwanza ya tasnifu imeelezea mambo ya msingi hasa tatizo la utafiti ambalo likuwa ni pengo la kitaaluma kuhusu taashira na utendaji katika nyimbo za harusi ambalo limezibwa na tasnifu hii. Pia kulikuwa na maswali ya utafiti yalikuwa ni kuainisha taashira na utendaji wa miviga ambayo ni muhimu katika sherehe za harusi, vile vile kubainisha maana za taashira zilizotumika pamoja na utendaji wa miviga katika nyimbo. Sura ya pili ilimulika kwa undani yaliyoandikwa na wasomi wengine kuhusu taashira, nyimbo na utendaji. Halikadhalika sura hii ilielezea nadharia ya Utendaji na Semiotiki kama mwongozo wa nadharia ya utafiti huu. Katika sura ya tatu mtafiti alielezea mbinu za utafiti hususani mbinu ya uchunguzi shirikishi na mahojiano zilitumika wakati wa utafiti, ijapokuwa katika baadhi ya muktadha wa uwasilishwaji nyimbo, utendaji ambao kwa mujibu wa utamaduni ambao ulikuwa ni miko kwa mwanamue kushiriki, mtafiti msaidizi mwanamke aliajiriwa. Vile vile sura hii ilieleza jinsi data zilivyokusanywa na kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo kwa kuainishwa na kupewa vifupisho vya majina, ambapo ziligawanywa katika makundi ya nyimbo zenye taashira na nyimbo zenye utendaji wa miviga ambazo zina umuhimu katika sherehe za harusi. Sura ya nne inawakilishe matokeo ya matumizi ya taashira, ambayo inaonyesha kuwa taashira katika nyimbo za harusi zina umuhimu wa kitamaduni na manufaa katika kuwaelezea bwana na bibi harusi matarajio ya maisha yao kama wenza. Katika sura ya tano, mtafiti ameelleza utendaji ambayo unasisitiza miviga ya utendaji unaombatana na nyimbo za harusi wakati zinapoimbwa kama nyimbo za miviga. Sura ya sita inaeleza kauli ya jumla kwa kuonyesha kwamba, nyimbo za harusi za Waswahili zinatungwa kisanaa na kutumia taashira zenye maana na umuhimu katika matukio ya harusi, na utendaji katika nyimbo una umuhimu wa kimiviga wakati wa uwasilishaji nyimbo za harusi kisiwani Unguja. Hivyo basi, matokeo haya yanathibitisha maswali ya utafiti ambayo mtafiti alitarijia kuyajibu na kuchangia katika umuhimu wa uwanja wa fasihi simulizi, hususan kwenye nyimbo za Waswahili wa pwani wa Afrika Mashariki.

## YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI .....	Error! Bookmark not defined.
HATI LINZI.....	iii
TABARUKU .....	iv
SHUKRANI.....	v
ABSTRACT.....	vii
IKISIRI .....	viii
YALIYOMO.....	ix
SHERIA ZA UNUKUZI.....	xii
VIFUPISHO.....	xiii
ORODHA YA PICHA.....	xiv
SURA YA KWANZA .....	1
UTANGULIZI.....	1
1.1 Usuli wa Mada .....	1
1.1.1 Mazingira na Utamaduni wa Waunguja .....	2
1.1.2 Nyimbo za Harusi .....	5
1.1.2.1 Nyimbo na Sherehe katika Harusi za Waunguja .....	8
1.1.3.Taashira katika Nyimbo za Harusi.....	24
1.1.4 Utendaji katika Nyimbo za Harusi.....	29
1.2 Mada ya Utafiti .....	31
1.3 Madhumuni ya Utafiti.....	32
1.4 Maswali ya UTafiti .....	32
1.5 Umuhimu wa Utafiti .....	32
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	33
1.7 Matatizo Yaliyojitokeza.....	34
1.8 Maelezo ya Istilahi .....	35
SURA YA PILI.....	39
MAPITIO YA MANDIKO.....	39
2.1 Utangulizi.....	39
2.2 Mapitio ya Maandishi Yanayohusu Nyimbo katika Ushairi Simulizi .....	39
2.3 Misingi ya Nadharia.....	50
2.3.1 Nadharia ya Semiotiki (N.S).....	50
2.3.2 Nadharia ya Utendaji (N.U) .....	54

SURA YA TATU .....	58
MBINU ZA UTAFITI .....	58
3.0 Utangulizi.....	58
3.1 Ukusanyaji wa Data .....	58
3.1.1 Mbinu ya Uchunguzi - shiriki .....	59
3.1.2 Mbinu ya Mahojiano.....	59
3.1.3 Eneo la Utafiti .....	60
3.1.4 Uteuzi wa Sampuli.....	61
3.1.5 Vifaa vya Kukusanya Data .....	63
3.2 Uchanganuzi wa Data .....	64
SURA YA NNE.....	73
UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA TAASHIRA.....	73
4.0 Utangulizi.....	73
4.1 Matumizi na Ufasiri wa Taashira katika Nyimbo.....	73
4.1.1 Ufasiri wa Taashira za Vitu .....	74
4.2.Uchanganuzi na Maana zaTaashira za Tendo katika Nyimbo na Umuhimu wake .....	86
4.3. Matokeo ya Utafiti .....	105
4.3.1 Matokeo ya Maana za Taashira za Vitu Tendo .....	105
4.3.2 Matokeo ya Maana za Taashira za Tendo.....	106
4.4 Hitimisho.....	106
SURA YA TANO .....	108
UCHANGANUZI WA UTENDAJI WAKATI WA UIMBAJI.....	108
5.0 Utangulizi.....	108
5.1 Ufasiri wa Maana ya Utendaji wakati wa Uimbaji Nyimbo Harusini.....	108
5.1.1 Utendaji Ulivoambatana na Taashira wakati wa Kucheza na Kumba .....	109
5.1.2 Utendaji katika Matukio Yanayoashiria Mambo ya Kitaashira wakati wa Uimbaji	123
5.1.3 Utendaji wa Uigizaji wa Vitu vya Bibi Harusi wakati wa Kuimba Nyimbo.....	141
5.2 Matokeo ya Utafiti .....	146
5.2.1.Utendaji wakati wa Uimbaji .....	146
5.3 Hitimisho.....	147
SURA YA SITA .....	148
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....	148
6.0 Utangulizi.....	148
6.1 Muhtasari .....	148

6.2 Hitimisho.....	151
6.3 Mapendekezo .....	156
MAREJELEO .....	158
KIAMBATANISHO CHA I.....	165
KIAMBATANIISHO CHA II .....	167
KIAMBATANISHO CHA III .....	187
KIAMBATANIISHO CHA IV.....	200

## **SHERIA ZA UNUKUZI**

1. Herufi kubwa: Zimetumika katika mada, vichwa vikuu na vifupisho.
2. Wino mzito: Umetumika katika vichwa vikuu na vidogo sawia.
3. Herufi za mlazo: Zimetumika katika tasnifu kutofautisha kati ya matamko ambamo taashira zilizotumika katika nyimbo na maandishi mengine. Vilevile zimetumika kuandika nyimbo zote zilizonukuliwa ili kuweza kutafautisha na maandishi ya nathari katika tasnifu hii.
4. Alama \_\_\_\_\_ : Imetumika kupigia mistari taashira zilizotambuliwa katika nyimbo.
5. Alama ( ): Imetumika kubania miaka ya uandishi, mahali kauli fulani zilipo, na vifupisho kama vile SW na SAW.

## **VIFUPISHO**

Bi.	bibi
Bw.	bwana
h.t	hakuna tarehe
N.U	Nadharia ya Utendaji
N.S	Nadharia ya Simeotiki
P	Picha
(S.A.W)	Swalallah Alyhhi Wasalam
(R.A)	RadhiAllah Anha
Shk	Sheikh

## **ORODHA YA PICHA**

PICHA 1 Sahani ya Somo.....	21
PICHA 2. Bibi harusi Amefinikwa Anamsubiri Bwana Harusi Kuja Kutoa Mkono .....	99
PICHA 3. Maharusi Wakipeana Mikono.....	100
PICHA 4 Kuviringisha Kidole cha Katikati. ....	110
PICHA 5 Ukataji Kiuno Kujifurahisha (Harusi ya Mjini).....	112
PICHA 6 Ukataji Kiiuno Kujifurahisha (Harusi ya Shamba).....	113
PICHA 7 Mizungu ya Ukataji Kiuno.....	114
PICHA 8 Bibi Harusi Anafundishwa Mizungu .....	115
PICHA 9 Upigaji Makofi kwa ajili ya Kuchochea Ari.....	117
PICHA 10 Upigaji wa Miguu Chini na Kutoa Mdundo .....	121
PICHA 11 Uchezaji wa Matao kwa Kufuata Ala za Muziki.....	123
PICHA 12 Mwari Ameelekwa Mgongoni Anapopelekwa Uani Kuogeshwa .....	126
PICHA 13 Mwari Ameelekwa Mgongoni Anapelekwa Chumbani. ....	127
PICHA 14 Bibi Harusi Ameelekwa Akitolewa Nyumbani. ....	129
PICHA 15. Kushikana Mikono Kadhi na Bwana Harusi wakati wa Nikaha.....	134
PICHA 16 Uchoraji hina katika Mikono na Vidole.....	140
PICHA 17 Uchoraji Hina katika Miguu na Mikono.....	141
PICHA 18 Kusasambura Masanduku ya Bibi Harusi.....	142

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

#### **1.1 Usuli wa Mada**

Nyimbo ni utanzu muhimu wa ushairi simulizi. Ni njia mojawapo ya kuwasilisha ushairi similizi. Nyimbo huimbwa kunapokuwa na shughuli mbalimbali za jamii kama vile harusi, matanga na tohara. Kupitia nyimbo jamii inajifunza, inaburudika, inaomboleza, inaonya, inaadibisha, inajipa moyo, inapitisha taarifa za siri na kutunza amali za jamii. Nyimbo zinaelezea pia historia, majukumu, imani na hekima ya jamii.

Wataalamu kadhaa wametoa maana mbalimbali za nyimbo. Matteru katika Msokile (1981:32) anaeleza.

Nyimbo kama aina ya ushairi unaoimbwa peke yake au kwa kuhusishwa na ngoma au pia na kucheza kwa uimbaji wake.

Matteru akifafanua kuhusu mpangilio wa nyimbo hizo anaeleza kuwa "nyimbo zina mfuatano au mpangilio maalumu wa sauti, mwondoko na ishara." Tonya (1978) naye, kwa kiasi fulani anakubaliana na maelezo ya Matteru. Anasema kuwa.

Nyimbo ni aina ya ushairi uliotiwa sauti na uliokusudiwa kuimbwa na kuleta maana au ujumbe kwa jamii.

Kauli hii inasisitiza kwamba wimbo bila ujumbe si wimbo hata kama unaimbwaa. Mawazo hayo yanashadidiwa na Beja (2000) kwa kueleza kuwa,

Wimbo ni utungo wa maneno ya sauti zilizopangwa kwa mahadhi fulani ili kuleta maana iliyokusudiwa.

Kama tulivyoeleza awali kuwa nyimbo ni sehemu ya ushairi. Hivyo basi ni vyema pia tukidokeza maana ya ushairi na uhusiano wake na nyimbo. Imebainika kuwa kuna wataalamu mbalimbali kama vile Abedi (1954); Harris (1962); Abdulaziz (1979); Nabahanny (1985) na Mulokozi na Kahigi (1979) wameeleza maana ya ushairi. Hata hivyo kwa lengo la utafiti huu kuhusiana na maana ya ushairi na uhusiano wake na nyimbo tulizingatia maana iliyotolewa na Mulokozi na Kahigi (1979:21) isemayo.

Ushairi ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalumu wa maneno fasaha na yenye muwala kwa lugha ya mkato, picha, au sitiara au taashira katika semi, maandishi au mahadhi ya wimbo, ili kuelezea wazo au mawzo, kufunza au kueleza tukio au hisi fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo.

Fasili ya maana hii kuitia mawazo yaliyotolewa na Mulokozi na Kahigi imekuwa faafu katika uchunguzi wa utafiti huu. Kwani imebeba dhima mojawapo ya lugha kuwa na vipengele ambavyo hutoa maana na ujumbe kwa jamii. Haya tumeyadhihirisha katika uchanganuzi wa utafiti huu. Tumeonyesha jinsi taashira zilizotumika katika nyimbo kama chombo cha kubeba maana za kitaashira na umuhimu wake kwa hadhira iliyokusudiwa.

Utafiti huu ulijikita katika nyimbo za harusi za Waswahili. Hivyo basi kutokana na fasili zilizotolewa kuhusu maana ya wimbo/nyimbo na kwa azma ya utafiti huu, wimbo/nyimbo za harusi ni maghani yenye mahadhi ya sauti/usemi uliomo katika ubeti moja au zaidi ambao ukamilifu wa maana yake umo katika mutadha wa wimbo unaoimbwa.

### **1.1.1 Mazingira na Utamaduni wa Waunguja**

Waunguja ni mionganini mwa Waswahili waishio mwambao wa Afrika ya Mashariki. Watu hawa wanaishi katika kisiwa cha Unguja. Jirani ya Kisiwa cha Unguja ni Kisiwa cha Pemba. Unguja na Pemba kwa pamoja inajulikana kama Visiwa vya Zanzibar. Visiwa hivi vimeunda jamii moja ambayo inajulikana kwa jina la jamii ya Wazanzibari. Mlacha (1995:43) anayathibitisha haya anapowajumuisha na Wapwani wengine. Kwa upande wa lugha, Wazanzibari wamejigawa katika lahaja zao zinazojitofautisha kieneo hadi eneo. Lahaja hizo ni Kipemba, Kitumbatu, Kimakunduchi na Kiunguja. Hata hivyo, viro visiwa vyengine vidogo vidogo kama vile Kojani, Kisiwa Panza, Makoongwe, Fundo, Njau na Misali viro upande wa Pemba. Kwa upande wa Unguja viro visiwa kama vile Tumbatu, Bawe, Mnembe, Mtogo, Nyange, Pungume, Uzi, na Chumbe.

Kama ilivyo kila jamii inakuwa na mambo yake yaani mila, desturi, maadili, imani na itikadi. Hivyo jamii ya Waunguja wanatambulikana kwa mila, desturi na tamaduni zao zinazorithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Asilimia 99% ya watu wa jamii hii ni Waisilamu ambao utaweza kuwajua kwa kuwaona tu kutokana na mavazi yao, majina, ibada zao na mambo mbalimbali wanayoyafanya katika shughuli zao za kila siku.

Hata hivyo jamii ya Waunguja imetokea kuwa na mchanganyiko wa utamaduni. Mchanganyiko umetokana na kuathiriwa kwake na tamaduni za wageni na jamii nyingine zilizokuwa zinaishi karibu nazo. Haya yanathibitishwa na Farsi (1956:1) alipokuwa akikisifia kisiwa cha Unguja. Farsi anaeleza kuwa, "Unguja ni kisiwa kilichokuwa kikubwa na chenye rutuba na hali ya hewa yenye kupendeza. Tangu zama na zama mpaka hii leo, watu wengi walifanya na wanaendelea kufanya makaazi yao hapa". Uzuri huu ulifanya waliokuwimba kusema kuwa "*Unguja ni njema atakaye aje*".

Kwa ajili Unguja ipo karibu sana na pwani ya Afrika na ipo karibu na Bahari ya Hindi wageni wengi wameizuri, itawala na wametamakani (kuishi) Unguja. Wageni hawa walitokea upande za Misri, Somali, Arabuni, Palestina, Iraq, Ajemu, Bara Hindi, Malay visiwa vya Jawa - Indonesia, China, Japan na Mascut. Wengi katika wageni hawa walikuja kufanya bishara. Biashara zao zikisha na pepo zikibadilika hurejea makwao. Wengine katika hao hutamakani na kuoleana na wenyeji ambaao ni Wa-Bantu. Hawa hufanya maskani yao huku ugenini na vizazi vyao hukufanya ndio kwao. Watu hawa baada ya kutamakani huleta ustaarabu, mila, sheria, dini na maneno ya kwao. Haya huchanganyika na ustaarabu, sheria na dini ya kienyeji.

Farsi (1967: 45-49) anafafanua zaidi kwa kuonyesha baadhi ya asili ya mila na ada za harusi zilizochanganyika katika utamaduni wa Waunguja. Kwa mfano, ada zitokanazo na Waarabu wa Hadhramout ni: kumkosha nywele bibi harusi kwa damu ya mbuzi, kumtia hina bwana harusi kwa sherehe, kutwanga buni, bibi harusi kucaa kanzu ya kijani siku ya kuingia nyumbani, bwana harusi kutompa mgongo mkewe baada ya kumpa mkono bibi siku ya kuingia nyumbani na ada ya kutoa mkono. Ama ada ya bwana harusi kufunga kifungo cha juu cha kanzu akiwa amemkuta bibi harusi ni bikira inatokana na Waarabu wa Oman. Ada za Kingazija zilizoingia katika harusi za Kiunguja ni: kutia pamba, kutona kipaji na kuzungusha sinia ya somo. Waunguja vilevile waliathiriwa na wageni kutoka nchi za Magharibi (nchi za Kizungu) katika harusi zao. Ada za nchi za Magharibi utakazozikuta katika harusi za Waunguja ni kama vile: bwana harusi kumpelekeea bibi harusi pete ya uchumba, kumvalisha veli bibi harusi na kumweka pamoja na watoto "*bridesmaids*", bwana harusi kucaa suti, kupiga picha, bwana na bibi harusi kukaa pamoja mbele za watu na kwenda fungate ("*honey-moon*"). Hata hivyo ada kama za kukosha maji ya ndoa, kuwasinga maharusi, kucaa visuti, kupeleka begi au sanduku kutoka kwa mume na kuwangoja maharusi (yaani kuangalia kama maharusi wamehongera). Hizi ni ada za kiasili za

Kiunguja ambazo zilikuwepo kabla wageni kufanya makaazi yao huko visiwani. Ada nyengine kama kusoma "*nikaha*", walima ya harusi, bwana harusi kumwekea mkono juu ya kichwa cha bib harusi na kumsomea dua, kusali raka mbili kabla ya kukutana kimwili bwana na bibi harusi katika siku ya kwanza zote hizi ni ada zinazotokana na mafundisho ya dini ya Kiislamu. Hata hivyo, mchanganyiko wa ada, desturi, mila na mambo ya wakaazi mbalimbali waliotamakani katika nchi moja, ustaarabu au utamaduni wa nchi hiyo unafanyika. Kwa mujibu huu inaonekana ya kuwa utamaduni wa Kiunguja umefanyika kwa utamaduni wa Kiislamu ulichanganyika na utamadunu wa Kibantu, wa Kiarabu, Kiajemi na Kizungu umejenga ustaarabu wa Kiunguja.

Kulingana na maelezo yaliyoelezwa hapa juu yanadhihirisha kwamba, kipengele cha harusi kimekuwa muhimu kumulikia utamaduni wa jamii ya Waunguja. Kwa kuthibitisha hoja hii, Sengo (1992:53) ana utambulisha utamaduni wao. Sengo anaeleza kuwa, Uswahlini ndoa na harusi ni taasisi ya kwanza kwa uzito wa maisha ya kila siku ya mtu. Kwa mfano suala la ubikira katika jamii hii, ni ada kubwa sana kwa wasichana wa Kiswahili kabla ya kuolewa. Msichana akikutwa ni bikira jamii humpongeza kwa maneno, hupewa zawadi ndogo na hata kuimbiwa nyimbo za hongera. Bibi harusi akikutwa ni bikira siku ya harusi ni jambo ambalo lenye kuleta heshima kwa jamaa zake. Isitoshe, jambo hili linaonyesha kuwa ndoa yao itakuwa ya uaminifu. Kwani ndoa ndicho kitovu cha maisha ya Waswahili. Mfano wa wimbo maarufu utumikao kutoka jadi had sasa anapokutwa bibi harusi ni bikira ni huu ufuatao.

### MHK.3 MAME MWARI

*Hongera mwanangu hongera,  
Nami nihongere wee hongera  
Mama uchungu mama uchungu  
Nyamara mwanangu ooee*

Utamaduni mwengine unaoendelezwa ambayo ni desturi iliyoenea mwote Uswahlini, ni wazazi kuwa washauri wakuu wa ndoa za watoto wao. Kuna hatua kadha wa kadha tangu mtu aposapo hadi kutoa mahari na kufunga harusi. Hatua zote hizi huambatana na tumbuizo za nyimbo na ngoma katika kushereheke harusi zao. Kwa mfano, singo ni chuo ambacho huwashirikisha makungwi na masomo katika kuwaelekeza na kuwafundisha wari kunga za maisha. Hata hivyo kwa waumini wa kweli wa Uislamu, sharia za Kiislamu huwa ndicho kigezo pekee cha kuendeshea maisha ya ndoa. Suala la nyimbo katika harusi limekuwa tete. Wako wambao

wanaliona ni kinyume na mafundiso ya dini yao. Halikadhalika wako wambao wanalionna ni mojawapo ya sherehe katika harusi na lilikuwepo toka jadi.

Hivyo utafiti huu uliazimia kushughulikia kipengele cha taashira na utendaji katika harusi. Kipengele ambacho kukamilika kwake ni lazima kuwepo na nyimbo. Nyimbo hizi huimbwa katika miktadha tofauti katika sherehe ya ndoa na harusi za Waunguja.

### **1.1.2 Nyimbo za Harusi**

Nyimbo za harusi zimechukuliwa na wasomi wengi kuwa kama muingiliano wa masimulizi ya jadi na ukweli wa maisha ya hivi sasa. Nyimbo hizi hushughulikia mambo kama vile nafasi ya mwanamke katika maisha ya ndoa, majukumu ya mume na mke, taasubi za kiume, mwanamke kama pambo la mume, usafi wa nyumba na mwili, uadilifu, uaminifu, usharati, unafiki, malezi, mapenzi na utamaduni wa watu. Kadhalika kupitia nyimbo za harusi utafiti huu ulijaribu kuweka peupe sifa hizi za kumbeza, kumtukuza na kukejeli mwanamke kama kwamba yeze ni chombo tu cha kumliwaza na kumtumikia mwanamume. Kama asemavyo Said Ahmed Mohamed (1984:19) "*Mwanamke ali pambo la macho kutia nuru, nyumbani aimbe nyimbo hana hata maamuri*".

Utafiti ulithibitisha kwamba mambo haya tuliyoyataja hapa yanayopatikana katika nyimbo ni mambo yalikuwepo toka jadi na hadi sasa na huathiri wanajamii kwa njia mbalimbali. Ukweli huu unathibithishwa na kina Ngugi (2000) na Indege (2011) wanaeleza kuwa, nyimbo na ushairi zimekuwa mbinu muhimu ambazo muimbaji au mshairi hutumia katika kuelezea hisia zake. Indege (2011:64) akimnukuu Walibora, anaeleza kwamba" ushairi na nyimbo umekuwa ukidhihirika tangu azali kwa malumbano za ngoma kwenye sherehe za ndoa, matambiko na jandoni".

Uswahilini ilichupukia ushairi na nyimbo kuuona kama kioo mufti cha utamaduni. Kadhalika nyimbo ziimbwazo harusini katika jamii ya Waunguja nazozimekuwa ni kioo cha utamaduni wao. Vile vile nyimbo hizi hutumika kama moja ya utambulisho wa Muungu. Nyimbo zimekuwa zikisawiri nafasi ya mwanamke kulingana na mfumo wa utamaduni unaoishi na aliokulia nao kutoka utotoni hadi utuuzimani. Kadhalika inaaminika kwamba kutokana na dini, itikadi na utamaduni uliojengeka, imetokea kuiathiri nafasi ya mwanamke katika jamii hii.

Kwa mfano kuhusiana na nafasi ya mwanamke katika muktadha wa fasihi ya Kiswahili, nyimbo zimetumiwa na kuendelea kutumiwa na wahakiki wa fasihi kusawiri swala hili. Momanyi (2001) anasisitiza kwamba, wimbo au ushairi umechipuka ndani ya mfumo wa kuumeni. Taasubi za kiumenti zilizoko katika utaratibu za kiishara ndani ya mfumo huu huzingatia kwamba wanawake hawana nafasi ya kudhirisha ile jinsi ya kike halisi. Hivyo mwanamke huishi kulingana na jinsi mwanamume anavyotaka. Wazo la Mamonyi (ameshatajwa) halipingani na wahakiki wengine kama vile: Khamis (2004 na 2005), El-Maawy (2011) na Mulokozi (1999). Misingi ya mawzo haya yamejengwa baada ya kusawiri *Utendi wa Mwanakupona* kutungwa. Huu ni utenzi ambao yakisiwa ilitungwa mwaka wa 1860 (El- Maawy 2011). Huu ni utenzi maarufu ilitumiwa na bado wengine wanautumia kwa ajili ya kuwapa nasaha wari wanaokaribiwa kuolewa. Ni utenzi ambao uliibua hisia mbalimbali kuhusiana na nafasi ya mwanamke hasa mwanamke wa Kiisilamu. Wengi waliurejelea utenzi huu kama sumu kali ambayo inamdhilisha mwanamke na kutompa hali hadhi anayaostahili katika jamii.

Wahakiki wengine wamejaribu kuonyesha nafasi ya mwanamke kupitia *utendi wa Mwanakupona* kama kiumbe dhalili au dhaifu, mtiifu aliyetawaliwa na taasubi za kiume. Kama asemvayo Khatib (1985) anasisitiza kuwa "tungo hii ya Mwanakupona ni zao la fasihi ya kimwambao ilioathiriwa na kupata utomvu wa uhai wake kutokana na utamaduni ulioghoshiwa na maadili ya Kiisilamu katika karne ya kumi na tisa." (uk 46). Hoja za kina Khatib (ameshatajwa) na wenzake zimetolewa kutokana na hali iliyokuwepo ya wanajamii za maeneo ya pwani. Hii ni kutokana na sababu za kihistoria na kukomaa kwa mfumo wa kimwinyi, ambao mwanamke hupaswa kumnyenyeka mwanamume. Sambamba na mwanamke kufanywa kama chombo ambacho mamwinyi hukitumia kwa kujiliwaza. Nafasi ya mwanamke imekuwa ni kuiweka chini ya mwanamume kwa kujitahidi kumfurahisha na kumliwaza.

Mnenuka (2012) ametumia beti za 31 na 32 ziliopo katika *Utendi wa Mwanakupona* kwa kuchangia wazo hili la mwanamke kufananishwa kama chombo. Mnenuka anaona beti hizi zinasitiza utii wa mwanamke kwa mwanamume. Tazama mifano ya beti hizo hapa chini.

- |  |   |
|--|---|
| 31. <i>kilala siikukuse<br/>mwegeme umpapase<br/>na upepo asikose<br/>mtu wa kumpepea.</i> | 32. <i>kivika simwondoe<br/>wala sinene kwa yowe<br/>keti papo siinue<br/>chamaka kakuzengea.</i> |
|--|---|

Kwa mujibu wa beti hizo juu, Mnenuka (ameshatajwa) anaona kuwa hizi ni kati ya mbinu anazopaswa mwanamke kuzitumia anapoishi na mwanamume ni kumkweza mwanamume. Mnenuku anafafanua kuwa, hizi ni beti (31 na 32) zinaonyesha utamaduni na nafasi ya mwanamke katika jamii za kimwinyi. Jambo ambalo wahakiki wengine akiwemo Njozi (1990) analipinga. Njozi alitetea vikali msimamo wa Mwanakupona kwa kuelezea kuwa, "utenzi huu umefasirika vibaya mionganini mwa wanachuo". Njozi (ameshatajwa) anaunga mkono ushauri wa Mwanakupona kwa bintiye. Ushauri huu unatokana na misingi ya *Qur'an* na *Hadithi* (kumbukumbu zihusuzo matendo na matamshi ya Mtume Mohammad *salallah alayhi wasalaam*) ambapo unamwezesha mke na mume kuishi vema katika ndoa. Njozi anaona kuwa wahakiki wanapaswa wasipuuzie kuzingatia matakwa na mfumo wa utamaduni wa jamii husika ulivyokubaliana kabla ya kutoa maoni yao.

Kadhalika nyimbo za harusi za Waswahili ni sanaa isiyo kuwa na mipaka ya makabila yaliyopo pwani ya Afrika Mashariki. Ni sanaa ambayo huwaunganisha watu wa makabila au lahaja mbalimbali zinazotumika pwani ya Afrika Mashariki kwa kutumia lugha inayoeleweka na kuzungumzia tajriba sawa wanazozifahamu. Kama wasemavyo (Othman na Yahya, 2004) kwamba,

"...mila za Unguja ni nyingi na zote zina msingi tangu kale  
hadi sasa kuanzia Kaskazini (Tumbatu) hadi Kusini (Makunduchi).  
Siku za harusi zao hufanya sherehe zao na zote zinafanana  
na za watu wa mjini".

Utanzu wa nyimbo umeimarika zaidi katika jamii za Kiafrika ikiwemo jamii ya Waswahili. Kuimarika kwake kunadhihirika katika umuhimu wake katika maisha ya wanajami. Kwa mujibu Ntarangwi (2001:8) "... kwa muda mrefu sasa, nyimbo za Waswahili zimebakia kuwa fahari ya muziki unaohusishwa na Waswahili wenyewe katika maisha yao". Hoja ya Ntarangwi ina sadifu na ukweli kwamba, nyimbo katika jamii ya Waswahili huimbwa wakati kumkuza na kumkomaza mtoto katika jando/unyago, wakati wa kumsinga mwari wa kike kabla ya ndoa, wakati wa kuwaoza bibi na bwana na jamaa zao kuwaaga maharusi wanapokwenda kuanza maisha yao ya unyumba. Kwa ujumla tunasema wimbo humlea, humkuza na kumkomaza mtoto, humuoza na kumuaga kwenda kuanza maisha mapya ya utu uzima. Mawazo haya yanadhihirika katika nyimbo ziimbwazo wakati wa harusi kama ilivyoonyeshwa katika kazi hii.

Utafiti umebaini kuwa ndoa na harusi ni tukio muhimu katika jamii ya Waunguja. Hushangiliwa kwa vigelegele, nyimbo na tafrija. Ndoa katika jamii ya Waunguja ni jambo linalohimizwa sana kama linavyohimizwa katika dini ya Kiisilamu. Waunguja huwaozesha watoto wao kwa kufuata mafundisho ya dini hii. Ijapokuwa ndoa na harusi zao hufuata sharia ya dini ya Kiisilamu lakini husherehekewa kwa nyimbo zenyе utendaji mbalimbali. Nyimbo na utendaji huu hufanyika katika matukio tofauti ambayo mengine japo yamepingwa au kukemewa na mafundisho ya dini yao. Hata hivyo, sherehe za harusi ndio upeo wa ndoa. Sherehe ya harusi bila ya nyimbo au ngoma bado haijaitwa harusi. Ni kwa mantiki hiyo, jamii ya Waunguja huishangilia harusi zao kwa ngoma, nyimbo na vigelegele.

#### **1.1.2.1 Nyimbo na Sherehe katika Harusi za Waunguja**

Kwa mujibu wa Farsy (1956) kila sherehe inayofanyika katika harusi za Waswahili wa kisiwani Unguja huwa zimesheheni ngoma, miviga na tumbuizo za nyimbo mbalimbali. Nyimbo nyingi za harusi za Waunguja zimefungamana na muktadha wa tukio katika sherehe husika. Sherehe hizi ni kana kwamba zimegawanywa katika awamu mbili. Sherehe kabla ya nikaha na sherehe baada ya nikaha. Nyimbo ziimbwazo katika sherhe hizi, hubeba aina mbalimbali za taashira. Kila taashira inabeba maana za kitaashira kulingana na muktadha wa tukio mahasusi harusini. Zifuatazo ni baadhi ya nyimbo ambazo huwasilishwa kulingana na muktadha tofauti wa tukio katika sherehe harusini:-

#### **Nyimbo Zinazoimbwa wakati wa Kupeleka na Kupokea Mahari.**

Sherehe za Waswahili kisiwani Unguja huanza kutayarishwa baada ya uchumba na posa kukubaliwa. Wazee wanaume wa mchumba huenda kwa wazee wanaume wa mwari na kupatana juu ya mahari na masharti mengine. Wakiafikiana hutafuta siku ya kupeleka mahari. Mahari katika jamii ya Wazanzibari haitolewi kwa siri, aghlabu hupeleka kwa sherehe na nderemo. Ni watu wachache hupeleka mahari kimya kimya. Wimbo unaoimbwa wakati wa kupeleka mahari ni huo hapa chini:

#### **MMH.2. JAHAZI**

*Jahazi yetu twaipeleka kwa pepo njema.*

*Nenda mwanangu amana Llahu Aman Rasuli.*

*Huyo ajaye mwana wa siwa na matuwazi*

Wimbo huu huimbwa na wanawake wa upande wa mume wanapokuwa njiani kupeleka mahari kwa watu wa upande wa mke.

Siku ya mahari inapowadia, wanawake wa upande wa mchumba (mvulana) na wa upande wa mwari (msichana) huwa na sherehe za ngoma, kucheza na kupiga vigelegele. Kabla ya kutoa na kupokea mahari, wanawake wa kwa mwari huimba kumsifia binti wao mbele ya wageni. Nyimbo ziimbwazo katika tukio kama hili huwa zimebeba maana za kitaashira kutokana na taashira zilizotumika nyimboni. Tazama wimbo uliobeba taashira unaoimbwa wakati wa tukio la mahari hapa chini.

#### MMH.1. MNGANAMBA

*Mnganambwa katumba kadogo,  
Mwana huyu kamzaa nani? eeee!  
Mwana huyu kamzaa nani?  
Kidomo katiti kama kasiba  
Chenye mwanya kati mbwake haiba  
Ndiye mke siti mwenye mahaba  
Atwazaye watu mahadharani.*

*Nakwenda alika kwa guu langu  
Tangu majirani hata ndu zangu  
Asiyenijia kwa hili langu  
Akiwa na lake asitumai.*

Wimbo MMH.1 hapa juu umetumia taashira iliyopigwa msitari kumsifu mwari.

Kadhalika watu wa upande wa kwa mke wanapowaona watu wa upande wa kwa mume wamefika, huwakaribsha. Makaribisho haya yanaandamana na nyimbo tofauti. Baadhi ya nyimbo hizo ni:

#### MMH.3. NATAKA TAMBUU

*Nataka tambuu na popoo,  
Na tumbako njema yenye kileo,  
Ladha ya mume kula na nguo,  
Na maneno mema yenye kituo.*

...

#### **MMH.4. TULIVINILE JANGA**

*Mama tulivinile janga eee,!*

*Eeee! Jangaa! Seuze langu mwenyewe*

*Nyumba ya mwari aingia koko: paramia.*

*Utango nautambae: uwe mwana wa Baraka*

...

Wimbo MMH.3 kwenye mshororo wa 3 na 4. unawahabarisha wageni waliokuja kutoa mahari. Unawataka watambue wajibu wa mume ni kumlisha, kumvisha na kuwa na maneno mazuri kwa mkewe (binti yao). Ama wimbo MMH.4 mshororo wa 3 uliopigwa msitari, unadhihirisha jinsi wimbo huu ulivyofungamana na muktadha wa tukio. Yaani nyumbani kwa kina mwari kumekuja mume anayemtaka mwari kumuoa.

Baada ya tukio la mahari, hufuatilia ualikaji wa harusi. Ingawa siku hizi imepungua lakini hapo zamani ualikaji ulifanywa na kundi la wanawake (majaliko). Majaliko wanapokwenda kualika, hutoka na vigelegele na hoe hoe. Miongoni mwa wimbo unaimbwba na majaliko wanapokwenda kualika ni kama huu:

#### **MKH.1. NITUMWA NA MAMA**

*Nitumwa na mama kwenda alike,*

*Tangu Mugudisho hata Marika,*

*Ndiyo mbegu njema isiyo shaka,*

*Na mwenye kupanda hutumaini.*

...

#### **Nyimbo wakati wa Singo**

Singo ni ada muhimu katika jamii ya Waunguja. Siku tano au tatu kabla ya sherehe ya harusi kuanza mwari hufanyiwa singo. Mwari anaposingwa huimbiwa nyimbo zenyenye mafunzo yanayahuusu maisha katika ndoa. Wimbo maarufu unaoimbwa wakati wa kuanza singo ni MSG.1.BISUMILLAH. Wimbo huu huanza kwa kutanguliza jina la Allah (S.W) kama inavyoeleza hapa chini.

#### **MSG.1 BISUMILAH**

*Kungwi: ee oo yaa ee bisumilahi ndio ya kwanza ya kuondokeaa, bisumillahi ndio ya kwanza.*

*Watani: ee oo yaa ee bisumilahi ndio ya kwanza ya kuondokeaa, bisumillahi ndio ya kwanza.*

...

Athari ya Uisilamu imedhihirika hata katika nyimbo za singo. MSG.1. *BISUMILAH* ni wimbo maarufu wa kuanzia singo. Wimbo huu unaimbwaa na kungwi huku watani wakirudia ubeti ulioimbwa na kungwi. Nia hasa ya kutanguliza *Bisumillahi* ni kutaka shughuli hii ipate baraka za Allah (S.W). Kama ilivyo ni desturi ya Waisilamu kutanguliza tamko la *Bisumiilahi* kila wanapotaka kufanya jambo lao. Waisilamu wanaimani kuwa, jambo linalofanywa bila ya kutanguliza *Bisumillahi* linakosa baraka ya Allah (S.W) na kinyume chake linapata ushirika wa shetani. Maelezo haya yamefanuliwa na Shk Khamis Suleiman aliyehojo wa tarehe 18/1/2010. Uwasilishwaji wa nyimbo na matendo anayofanyiwa mwari wakati wa singo, yana dhima zaidi mbali na kuburudisha. Hoja hii inafanuliwa na wasailiwa tofauti. Bi. Salma aliyehojo wa tarehe, 8/12/2009 anaeleza, singo ina lengo la kumtoa bibi harusi katika hatua ya utoto na kumuingiza katika hatua ya utu uzima. Maoni yake yamejikita zaidi anaporejelea ujumbe uliomo kwenye nyimbo za singo na matendo anayofanyiwa mwari katika shughuli nzima ya singo. Kwa mfano wimbo MSG.14.CHAMBA.

*MSG.14. CHAMBA*

*Chamba ukipata maji chamba*  
*Eee chamba ukipata maji chamba*  
*Mbogo ya mgeni hailali*  
*Wee ukipata maji chamba*

Tamko *chamba ukipata maji* lililoko kwenye mshororo wa kwanza (1) katika wimbo MSG.14 linarejelea kuoga janaba. Wimbo huu unaimbwaa wakati mwari yuko chooni (kwenye uzio) akifundishwa na kungwi jinsi ya kuoga (yaani kujitoharisha na janaba). *Janaba* ni kuwa katika hali ya uchafu kwa ajili ya kuingiliana kati ya mume na mke. Kwa mujibu wa mafundisho ya Kiisilamu, mtu akiwa na janaba hutakiwa kuoga ili kujitoharisha. Hivyo, kuoga janaba ni wajibu kwa mke na mume baada ya tendo la ndoa. Ujumbe unaotolewa katika kifungu cha ubeti hapa juu ni kuwa, mwari anaelezewa mambo ya unyumba, ya kiutu uzima na usafi. Kama vile kumstarehesha mume katika tendo la ndoa na kujitoharisha baada ya tendo hilo.

Mwari huanza kusingwa kwa vifaa ambavyo tayari vimekwisha tayarishwa. Kusinga huko huanzia usoni. Uso husingwa kwa rojo la liwa lililochanganywa na maua yenye kutoa harufu nzuri yaliyokaushwa na kusagwa. Mfano wa maua hayo ni asumini, vilua, liwa na mawardi. Pia,

mchanganyiko huo hunyunyiziwa mafuta mazuri kama ya *al uu*. Wimbo unaoimbwa na ambao umefungamana na vitu vilivytajwa wakati wa usingaji ni huu hapa chini:

*MSG.13 MWARI AINGILE CHOONI*

*Bibi aingile chooni kwa maulidi*  
*Angile koga marashi uvumba na udi*

Utafiti umeshuhudia kabla ya singo, kungwi mkuu humuusia mwari. Huu ni wasia wa siri, mwari hatakiwi auelezee nje kwa mashoga zake. Anatakiwa auzingatie ni muhimu katika maisha yake ya ndoa. Utafiti umebaini nyimbo ziimbwazo wakati wa singo huwa na mafundisho kwa wari. Mafundisho hayo hutolewa kwa kutumia lugha ya kitaashira (fiche) au utendaji. Ifuatayo ni mifano ya nyimbo nyengine:-

*MSG.1 BISIMULLAHI*

*Kungwi:*      *ee oo yaa eee muenge enge kama kioo mume nduguyoo,*  
*munge enge kama kioo mume nduguyoo oo.*

*Watani:*      *ee oo yaa eee mume muenge enge kama kioo mume nduguyoo,*  
*munge enge kama kioo nduguyoo oo.*

...

Taashira iliyobuliwa katika wimbo *MSG.1. BISIMULLAHI* ni ya *kioo*. Wimbo umetumia lugha ya kisanaa kwa kutoa ujumbe kwa bibi harusi Wimbo mwengine unaoimbwa wakati wa singo na wenye taashira ni kama huu hapa chini:-

*MSG.5 KUNAILA MOJA*

*Kungwi:*      *Kuna ila moja ila ila baba ila,*  
*Kigongo mkononi ila.*  
*Watani:*      *Kuna ila moja ila ila baba ila,*  
*Kigongo mkononi ila.*

Mafundisho yatolewayo katika singo huambatana na nyimbo na utendaji. Utafiti umeshuhudia kuwa, baada ya mwari kusingwa hupelekwa chooni/uani kuogeshwa. Wakati wa kupelekwa huwa kuna nyimbo zinazoimbwa huku zikiambatana na matendo. Mfano wa nyimbo zinazoimbwa wakati wa kumpeleka mwari chooni/uani ni hizi zifuatazo:

*MSG.12. NENDA NAYE*

*Nenda naye mwanao*  
*Nenda naye nenda naye*  
*Nenda naye mwanao .*

*MSG.13 MWARI AINGILE CHOONI*

*Bibi aingile chooni kwa maulidi*

*Angile koga marashi uvumba na udi.*

Nyimbo hizi, huimbwa wakati mwari anapolekwa mgongoni na kungwi wake na kumpeleka uani (si chooni/bafuni) kwa ajili ya kukogeshwa. Iwapo mwari ni mzito, atasimama nyuma ya kungwi wake na kumshika mabegani. Kungwi atatembea taratibu huku kashika viganja vya mwari wake vilivyoegeshwa juu ya mabega yake mpaka uani kulikowekwa uzio. (Ua ni aina ya boma la miti au mabati lilitengenezwa kuzunguka nyuma ya nyumba). Anapopelekwa uani, huwa amefunika kitambi bila ya kuonekana mwili. Mwari hukogeshwa ndani ya ua uliotengezwa kwa utango. Lengo la kufungwa ua ni kuwa, hatakiwi kuonekana na watu. Wanapofika uani, mwari hufunzwa mambo kadhaa na mwisho anamwagiwa maji (kukogeshwa). Matukio yote haya huandamana na uimbaji wa nyimbo, upigaji makofi na vigelegele. Nyimbo kama hizi huimbwa pia wakati bibi harusi anapopelekwa kutiwa maji ya khutba (maji ya ndoa). Tendo la kumwagiwa maji au kuogeshwa mwari ni tambiko linamaanisha kuwa, sasa mwari ametoka hatua ya utoto na kuingia daraja la utu uzima (kukua upya). Matendo mengine kama kuimba, kukata viuno na kupiga vigelegele yalifanywa na washiriki na watani wa mwari wakiwa nje ya uani. Kulingana na mila na desturi za Waswahili wakati wa shughuli hii, mwari huvalishwa kisutu. Kisutu ni khanga zenyenakshi nyingi na zisizokuwa na mji. Aghalabu kisutu kutoka hapa zamani huvaliwa siku ya furaha na msiba (Farsi, 1967:17).

Nyimbo nyingine zinazoimbwa wakati mwari na kungwi wakiwa uani ni kama huu hapa chini:

*MSG.14. CHAMBA*

*Chamba ukipata maji chamba*

*Eee chamba ukipata maji chamba*

*Mbogo ya mgeni hailali*

*Wee ukipata maji chamba*

Mwari akishamalizwa kumwagiwa maji na kuchezeshwa huko uani hutolewa. Mwari hutolewa kwa wimbo, shangwe, nderembo na vigelegele huku akiwa ameekolewa mgongoni. Kungwi humueleka mwari na kumpeleka chumbani kwa ajili ya kufundishwa kunga za maisha. Tendo hili huambatana na wimbo ufuatao:

<i>MSG.15 TOKANAE</i>	<u>Kiswahili Sanifu</u>
<i>Tokanae mnyakanga,</i>	Tokanae kungwi
<i>Tokanae mnyakanga.</i>	Tokanae kungwi
<i>Ende nae akarore,</i>	Ende nae akajfunze
<i>Ende nae akarore</i>	Ende nae akajfunze

Katika wimbo MSG.15 mnyakanga (kungwi) anaambiwa atoke naye mwari na kumpeleka chumbani *akarore* yaani akajifunze mambo ya kunga katika maisha. Utafiti umeshuhudia kuwa, mwari anapofikishwa chumbani anamofunzwa hufukizwa kwa udi mwilini kabla ya kukaushwa maji baadaye hufukizwa nguoni. Kisha hukalishwa kwenye mkeka kwa ajili ya kupewa mafunzo ya ndoa. Kungwi na msaidizi wake walieleza kuwa, "... mwari atakapokuwa kwake au kukutana na mumewe hutakiwa anukie vizuri mwili na nguo. Harufu nzuri humvutia mume na huongeza mapenzi baina yao ". Utendaji wa kufukizwa hufanywa baada ya wimbo MSG.13. MWARI AINGILE CHOONI na MSG.15. TOKANAE.

Singo ikikamilika kungwi hupiga *cheba*. Hii ni ishara ya kuwajulisha waliohuduria kwamba shughuli ya singo imekamilika. *Cheba* husemwa maneno kwa kupochezana baina ya kungwi na waalikwa. *Cheba* pia, hupigwa punde tu baada ya kufunga nikaha kwa upande wa wanawake. Mapokezano ya *Cheba* ni kama yafuatayo:

<b>MSG.11 KAWAIDA YA SINGO</b>
<i>Kungwi: iyo kawaida ya singo yoyo!</i>
<i>Waalikwa: iyooo!</i>
<i>Kungwi: salama inshaallah salama!</i>
<i>Waalikwa: inshaallah salmin!</i>
<i>Kungwi: salmina akbar shoo!</i>
<i>Waalikwa: shoo!</i>

Baada ya hapa mwari hupewa chai. Mwari anapokunywa chai huimbiwa wimbo huu hapa chini.

#### *MSG.21. CHAI SHARUBATI LOZI*

*Bibi anakunwa chai*

*Chai sharbati lozi*

*Mkate wake laini*

*Chai sharabati lozi*

...

Taashira zilizoibuliwa katika nyimbo tofauti zilizoimbwa katika harusi zimetolewa maana ya kitaashira katika sura ya uchanganuzi.

### **Nyimbo Ziimbwazo kabla ya Kufunga Nikaha**

Kabla ya kuwadia wakati wa kufunga nikaha kawaida huwa kuna sherehe na tumbuizo mbalimbali nyumbani kwa kina bibi harusi. Utafiti ulishuhudia sherehe za harusi za mjini zilitafautiana na zile za harusi za shamba/kijijini. Kwa upande wa harusi za mjini, nyimbo walizokuwa wakiimba kabla nikaha kufungwa ni kama hizi zifuatazo:

#### *MKN.7 MAMA NJOO*

*Mama njoo unifiche dudu laja hilo ooo, x2  
Mwanangu usilie ukaniliza na miye,  
Ndiko kuolewa huko oo.*

Wimbo huu huimbiwa bibi harusi akiwa nyumbani kwao kabla bwana harusi kuja kutoa mkono baada ya kufunga nikaha. Katika wimbo MKN.7.MAMA NJOO unawakilisha hisia, uoga na kilio cha bibi harusi kwa mama yake.

Wimbo mwengine, ambao hupendwa kuimbwa kabla ya kufunga nikaha katika harusi za Unguja Mjini ni huu ufuatao.

#### *MKN.9. KULA MUHOGO*

*Kula muhogo,  
Kula muhogo,  
Utauona utamu wake kula muhogo ,  
Utauona utamu wake kula muhogo .*

Utafiti umebaini kwamba harusi ya shamba (kijijini) mfano Tumbatu kabla nikaha kufungwa huwa kuna nyimba huimbwa. Nyimbo za harusi za shamba huimbwa nje ya nyumba na kikundi cha kina mama. Katika harusi za shamba bibi harusi haonekaniwi na hadhira huwa amewekwa chumbani akiwa na kungwi wake tu. Kungwi huwa anamuusia na kumfunza mambo ya kufanya atakapokuwa na mumewe usiku wa kwanza.

### **Nyimbo ziimbwazo Baada ya Kufunga Nikaha**

Timamy (2002:55) anaeleza kuwa katika sherehe ya harusi za Waswahili nikaha hualikiwa kwa majina matatu. Majina haya yanategemea nani anayealika na anayealikwa. Wanaalume wanaalikwa "Ikdi" msikitini. Mamake bwana harusi, hualika wanawake "***kupiga kilemba***" Mamake bibi harusi hualika wageni wake "***kupokea bwana harusi***". Majina yote haya matatu "Ikdi", "kupiga kilemba" na "kupokea bwana harusi" yana maana sawa na kufunga nikaha au kufunga ndoa.

Nikaha hufungwa msikitini au nyumbani kwa wazazi wa bibi harusi. Iwapo nikaha itafungwa msikitini, huwa hakuna ngoma wala nyimbo za kuimbwa msikitini. Baada ya nikaha kufungwa msikitini bwana harusi ni lazima aende nyumbani kwa kina bibi harusi na kutoa mkono. Utafiti ulishuhudia moja ya harusi iliyofanyika Unguja Mjini kuwa bwana harusi alipotoka msikitini alishindikizwa kwa matwari na qasida zilizoimbwa na watoto wa madrasa. Hali hii inafanana na ushindikizaji wa "*twari la ndia*" au "*diriji*" (Ngoma ya watu wa pwani Afrika Mashariki inayochezwa na wanaume kwa bakora au panga). Timamy (2002:56) anaeleza kuwa "... katika harusi za Waswahili hapo zamani baada ya bwana harusi kufunga nikaha msikitini alishindikizwa kwa *twari la ndia* au *diriji* hadi nyumbani kwa kina bibi harusi na kutoa mkono". Katika harusi uliyoshuhudia utafiti, bwana harusi na watu wazima walikuwa nyuma ya watoto wa madrasa. Walitembea mwendo wa pole pole hadi nyumbani kwa kina bibi harusi. Watoto wa madrasa waliokuwa mbele yao waliimba qasida na kupiga matwari. Qasida walizoimba ni kama hii hapa chini:

#### *MKU.8 OWA*

<i>Owa ndugu yetu owa,</i>	<i>kama ilivyo sheria</i>	<i>X 2</i>
<i>Mtume kafunga ndoa,</i>	<i>na mahari akatowa</i>	<i>X 2</i>
<i>Tuna muomba Karima,</i>	<i>kwa ndoa hii adhima.</i>	
<i>Aijalie Rahimu,</i>	<i>kuijaza nyangi nuru,</i>	
<i>Rabi utukubalie,</i>	<i>dua zetu waumini,</i>	
<i>Baraka umjazie,</i>	<i>za nje na za ndani.</i>	

Qasida mbalimbali wanazoimba wanafunzi huwa zimebeba ujumbe kuhusu harusi na zaidi kuiombea dua ndoa ya maharusi.

Strobel (1974) anaeleza kuwa, sherehe ya twari la ndia haifanywi au kupotea kabisa hasa katika harusi za Waswahili wa Mombasa na Lamu. Kinyume na maeleo ya Strobel, utafiti ulishuhudia kwa upande wa Unguja bado kuna baadhi ya harusi ambazo bwana harusi hushindikizwa kwa matwari.

Baada ya bwana harusi kutoa mkono huimbwa nyimbo. Miongoni mwa nyimbo zinazoimbwa ni hizi zifuatazo:-

#### *MBN.5 CHEZA CHEZA LEO*

*Harusi yooo,*  
*Harusi yooo,*

*Harusi imeshatimia.*

...

Katika wimbo huu, wanaocheza na kuimba ni ndugu wa bibi harusi na si bibi harusi mwenyewe ingawa wimbo unamuelekea yeye. Wimbo ufuatao pia huimbwa sana baada ya nikaha kufungwa:

#### MBN.6. FURAHA

*Na iwe leo ee na iwe leo furaha  
Baba amepata mama,  
Na iwe leo furaha.  
Mama amepata baba,  
Na iwe leo furaha.  
Mtango na utambae,  
Na iwe leo furaha.  
Wende ndani ukazae,*

...

Wimbo MBN.6 japo unaashiria furaha lakini pia umebeba ujumbe maalumu kuitia taashira iliyotumika ya *mtango*. Kadhalika siku ambayo bwana harusi alipokwenda kumchukua mke wake huimbwa wimbo huu hapa chini. Siku hii bwana harusi huwa amefuatana na jamaa zake.

#### MBN.9. TUNAO MTI

*Tunao mti tunao, twende nao pole pole  
Tukaupasue mbao mashina hata vilele  
Mbao ee mbao mashina hata vilele  
Msonobari kwa mbao  
Mashina hata vilele*

Wimbo huu huimbwa na wanawake wa upande wa bwana harusi na huwa umebeba sifa ya majigambo. Majigambo yanaelezwa katika mshororo wa kwanza (1) usemao " *Tunao mti tunao twenda nao pole pole , tukaupasuwe mbao mashina hata vilele*" .Vile vile wimbo MBN.9 unapoimbwa jamaa zake bibi harusi hupata ujumbe kuwa ndugu wa bwana harusi wamefika kwa hiyo wanataka kukaribishwa. Hivyo basi, ndugu wa bibi harusi huwapokea na kuwatandikia mahali pa kukaa. Wanapowatandikia huimba wimbo ufuatao:

#### MBN.10 TANDIKA MGENI AKAE

*Mama harusi tandika,  
Tandika mgeni akae,  
Mgeni shoga,*

Utendaji wa kutandika mikeka hufanyika sambamba wakati wanapoimba wimbo MBN.10.  
TANDIKA MGENI AKAE.

Wakati mwengine jamaa zake bwana harusi hasa wanawake huja na vurumai wanapompeleka  
bwana harusi kutoa mkono. Wakifika nyumbani kwa kina bibi harusi huimba nyimbo zifuatazo:

MKND.1. DAKTARI YUWAJA

*Vumilia huyooo eee kiumble  
Chamtonesha kidonda*

*Dakitari huyoo yuwaja*

*Dikitari huyoo yuwaja  
Ajakitia dawa kidonda*

MKND.2. WEMBE

*Waja huo wembe waja huo wembe  
Mamaee mwari naajitenge  
Waja huo wembe waja huo wembe  
Mwambiee mwana naajitenge*

MKND.4. USICHE BWANA

*Usiche Bwana harusi usiche  
Usiche Bwana harusi usiche  
Usiche Bwana harusi usiche  
Ukiona bahari utaogelea  
Usiche Bwana harusi usiche  
Ukiona bahari utaogelea uvuke  
Usiche Bwana harusi usiche  
Usiche Bwana harusi usiche*

Baada ya kutoa mkono, kula na mambo mengine kama kupiga picha, ndugu zake bwana harusi humchukua mke wao. Bibi harusi huchukuliwa akiwa ameelekwa/amebebwa mgongoni huku wakiimbia wimbo huu ufuatao:

*MBN.18. TWATAKA MKE WETU*

*Twataka mke wetu  
Twende zetu kwetu*

Kwa ufupi ni kwamba, harusi za kisasa, siku ya ndoa kabla nikaha na mume kutoa mkono, bibi harusi huwa nyumbani kwao tayari ameshapambwe. Masomo/makungwi, mashoga zake bibi

harusi na warombo hukusanyika na kumuimbia bibi harusi. Baadhi ya nyimbo zinazoimbwa ni hizi zifuatazo:-

#### MBN.14. KUTANDIKA

Naupiga papapa,  
Naupiga lolo.

Naupiga papapa,  
Naupiga lololo.

*Usione watu kutandika,  
Kutandika kuna maana yake.  
Usione kutandika kitanda,  
Kutandika kuna maana yake.*

*Ukitaka mume asitoke,  
Akilala mguu mpachike.  
Kumea mvi si utu uzima,  
Bora mashini kuwa nzima.*

*Kwenda na gongo si utu uzima,  
Bora kijiti kizima.*

*Ukitaka mume aishi,  
Kutandika ni kukaa uchi.  
Naupiga papapa,  
Naupiga lololo.*

#### MBN.15. SHINDWE.

*Mwanangu cheka eee,  
Taimbo wa kizungu haulali eee kacheka wee,  
Taimbo wa kizungu haulali eee kacheka wee.*

*Ee mwanangu udumbe eee,  
Taimbo wa kizungu kazi yake punde wee,*

#### Kiswahili Sanifu

*Mwanangu cheka,  
Mtaimbo wa kizungu haulali  
mwanangu cheka,  
Mtaimbo wa kizungu haulali  
mwanangu cheka.  
Mwanangu usiliee,  
Mtaimbo wa kizungu kazi yake ni  
kuvunja,*

#### MBN.20. UTAMPARA SAMAKI

*Umetaka mwenyewe kuolewa  
Utampara samaki*

*Samaki anamagamba eee  
Utampara samaki*

*Samaki anajicho moja eee  
Utampara samaki*

#### MKN.9. KULA MUHOGO

*Kula muhogo,*

*Kula muhogo,*

*Utauona utamu wake kula muhogo*

*Utauona utamu wake kula muhogo*

Wanawake hawa huimba huku wakikata viuno katika mitindo tofauti tofauti mbele ya bibi harusi. Mitindo ya ukataji ni kwa ajili ya kumfunza bibi harusi namna atakavyofanya atakapokuwa na mumewe.

Kwa upande wa harusi za Tumbatu siku ya pili ya ndoa, kunakuwa na utendaji wa kutandika mikeka kwa ajili ya bwana na bibi harusi kufunzwa. Katika siku hii manyakanga/mafundi huenda kwa maharusi na kuwafundisha jinsi ya kuishi katika maisha ya ndoa. Manyakanga wakifika karibu na eneo linalofanyiwa shughuli ile huingia kwa wimbo wa kubisha hodi ambao ni MBN 23.HODI. Hapa tena hukaribishwa na kuanza shughuli iliyowaleta ya kuwafunza maharusi.Tazama wimbo walioingia nao manyakanga hapa chini.

#### MBN.23. HODI

*Hodi wee hodi hodi*

*Mama shikamoo marahaba saidi*

Katika harusi za Unguja mjini siku ambayo mume anakwenda kuingia nyumbani huimba nyimbo zinazoambatana na muktadha wa tukio husika. Mfano wa wimbo unaoimbwa wakati mume anakwenda kuingia ndani ni huu ufuatao.

#### MKND.1 DAKITARI YUWAJA

*Vumilia huyooo eee kiumbe*

*Chamtonesha kidonda*

*Dakitari huyoo yuwaja*

*Dikitari huyoo yuwaja*

*Ajakitia dawa kidonda*

...

Taashira zilizotumika katika wimbo MKND.1 ni *dikitari, kidonda, na dawa*. Taashira hizi zilisimamia maana ya kitaashira. Maana hizi zimeelezwa katika sura ya nne.

Kwa upande wa harusi za Unguja Mjini na Makunduchi siku ya pili baada ya mume kuingia ndani aghalabu kungwi huenda kua ngalia kama ndoa imejibu. Huu ni mtindo wa kisasa. Hapo zamani kungwi alilala nyumba moja na maharusi. Asubuhi akaangalia kama kuna majibu au la.

Harusi ikijibu mashangazi na jamaa wa bibi harusi huanza kuimba wimbo wa hongera huu hapa chini.

#### MHK.3 MAME MWARI

*Hongera mwanangu hongera,  
Nami nihongere wee hongera  
Mama uchungu mama uchungu  
Nyamara mwanangu ooee*

Wimbo MHK.3 huimbwa huku sahani ya somo ikiwa imebebwa kichwani ikizungushwa. Lengo la kubeba na kuzungushwa sahani ya somo ni kuwataka hadhira iliyopo watuze. Kutuza huku ni shukrani ambayo watu hutoa kumpa somo au kungwi kwa kazi nzuri ya kumfunza mwari hadi akapatikaniwa kuwa ni bikira. Tazama katika PICHA 12 inayoonyesha jinsi sahani ya somo invyozungushwa.



**PICHA 1 Sahani ya Somo**

*Aliyebeba "sahani ya somo" ni shangazi wa bibi harusi . Anaipitisha mbele ya hadhira ili watuze. Tendo hili linaashiria kuwa harusi imejibu salama. Yaani mwari amehongera. Utendaji huu unaambatana na uimbaji wa nyimbo MHK.2 na MHK.3. Mji Mkongwe - Unguja, 12/12/2009.*  
Nyimbo nyengine zinazoimbwa baada ya harusi kujibu ni

## MHK.2. KOKO

*Koko wee koko*

*Nyumba ya mwari aingia koko*

*Paramira.*

## MHK.4. HONGERA MWANANGU

Hongera mwanangu wee hongera

*Nami ni hongere wee hongera*

*Mwana jaha na jamali, kajamili uso wake*

*Mwarichamba hayawi, mbona yaliwele*

*Wake wacheni kunamba, mnong'ono na ukome*

*Papa kwa papa walana, papa mkubwa kamla mwenzewe*

*Mtama wangu mteto, rijali kaulimbuwa*

*Mwanangu mkembe, hajajua jambo.*

Baada ya harusi kujibu kuna kukabidhiwa sanduku/masanduku kwa bibi harusi.

Kwa kawaida wanapomkabidhi bibi harusi sanduku/masanduku huwa wanaimba wimbo wa MKS.1. Wimbo huu huimbwa huku kila kitu kikisasambuliwa na kuonyeshwa kazi yake. Wimbo wenyewe ni huu ufuatao.

## MKS.1 SASAMBU

*Sasambu sasambu aeee*

*Sasambu sasambu sasambu*

*Sasambure turore sasambure turore*

*Sasambure turore!*

Sherehe nyengine inayofanywa ni kuwatoa maharusi. Siku hii, maharusi hupambwa na kutolewa kweye ukumbi (konyeshwa). Nyimbo na sherehe nyingine hunawirisha shughuli hiyo. Wale ambaa hawataki ghasia za taarabu, huwaita wanafunzi wa madrasa pamoja na mwalimu wao kusoma *Maulidi* ya Mtume Mohammad (S.A.W). Wakati wa kusoma *Maulidi* huimba kasida za kumsifu mtume Mohammad (S.A.W) na kasida zinazohusiana na mnasaba wa sherehe ya harusi. Kasida hizi hubeba maudhui ya kuiombea harusi baraka, kuwasifu na kuwaombea dua maharusi. Aidha, kasida hizi, huimbwa pamoja na kupiga madufu. Baadhi ya kasida na nyimbo maarufu zitumikazo katika kupamba ni:

## MKU.4 SUNA YA MTUME

*Mabibi mabwana na watoto pia*

*Mlokuja hapa kushereheka*

*Harusi ya bwana na bibie pia*

### *Weshatekeleza suna ya Mtume*

Kasida nyingine inayoimbwa ni hii ifuatayo:

#### *MKU.9 UTUPE KILA LA KHERI*

*Leo ni siku tukufu, waumini shangiria,  
Hii ni siku adhima, Yarabbi katuletea,  
Na sote waisilamu, hima hima shangiria,  
Twakuomba ya Karima, utupe kila la kheri.  
Harusi yetu adhima, leo imetufikia,  
Ni harusi ya (wanataja jina la Bw na Bi. Harusi) Yarabbi katuletea,  
Awe mtu mzuri, Yarabbi kamuongoa,  
Twakuomba ya Karima, utupe kila la kheri.*

Bibi harusi anapoingia ukumbini siku ya kupamba huwa kuna vurumai, shangirio zilizoambatana na nderemo na vigelegele. Kila mtu anataka kumuona bibi harusi kama amependeza au la ili apate la kuhadithia. Wimbo maarufu unaoimbwa katika muktadha huu ni huu ufuatao:

#### *MKU.1 MASOMASO*

*Masomaso mwanangu yasimuone  
Masomaso mwanangu yasimuone*

*Jicho la hasidi mwanangu lisimuone  
Jicho la hasidi mwanangu lisimuone.*

Wimbo huo hapa juu umebeba ujumbe wa dua inayoimbwa kwa niaba ya mamake harusi. Mamake harusi anaiomba dua ili mwanawe ahifadhike na jicho/macho ya hasidi yatakapohusudu. Yaani mwanawe asije akadhiruka kwa macho ya watu wabaya.

Bibi harusi akishafika kwenye jukwaa, hukalishwa kwenye kochi zuri akipigwa picha huku tumbuizo nyingine zikiendelea. Waalikwa waliofika hupewa vitafunio na vinywaji. Baadaye, mtu mmoja kwa niaba ya familia ya bibi harusi husimama na kutoa shukrani na kuwatachia kheri wageni wote waliohudhuria. Baada ya hapa, kila mtu anafumkana na kuelekea kwake. Nyimbo zilizoeleza hapa juu, ni mifano michache ya nyimbo zenye taashira na utendaji. Taashira zilizobuliwa na utendaji uliodhihirika katika uwasilishwaji wa nyimbo hizi umetolewa maana zake za kitaashira katika sura ya nne na tano za uchanganuzi.

### **1.1.3.Taashira katika Nyimbo za Harusi.**

Nyimbo kama utanzu wa ushairi hutafautiana na tanzu nyinginezo mathalan riwaya au tamthilia kwa namna ambapo ujumbe na dhamira huwasilishwa kwa matumizi ya lugha. Indede (2011) akimnukuu Powel anasema kwamba "tamathali za semi ndizo hutupitisha kwenye giza tototo". Bila ya tamathali basi nyimbo huwa tu mkusanyiko wa maneno, na hivyo huifanya haina mvuto wowote haijalishi ni wimbo wa kale wa kisasa. Wakati tunapokumbuka nyimbo za harusi mwimbaji (masanii) hutumia maneno anayoyafahamu, kuyasanifu na kutuumbia taswira mpya ya kuutazamia ulimwengu na malimwengu yake. Hivyo hali hii hufanya mhakiki wa wimbo mara nydingi hunaswa na namna ambavyo muimbaji anaelezea na kuwasilisha hisia. Ndiposa hapo awali wahakiki kwa kufuata falsafa ya Aristotile walipuuza kile kinachowasilishwa na wimbo na kuegemea zaidi katika nyezo za uwasilishaji.

Kwenye utangulizi wa *Sikate Tamaa* (1980:vii), Abdilatif Abdalla aeleza kwamba "ala ya kwanza iliyo muhimu katika sanaa itumiliwayo maneno ni umbuji wa lugha. Ili msanii aweze kummakinisha msomaji kwa muda mrefu, anahitaji kuwa na ukwasi wa lugha teule pamoja na kujua mbinu za kutumia ukwasi huo kwa namna itakayoathiri vivilvyo". Vile vile hali ndivyo ilivyo katika utanzu wa nyimbo. Mwimbaji (msanii) ili naye aweze kumridhisha msikilizaji wake kwa muda mrefu kadhalika anahitaji awe na ukwasi wa lugha teule ambao utaathiri hadhira yake.

Ukwasi wa lugha teule katika nyimbo huwa ni chombo mwafaka kinachomwezesha msanii kuufumbata upana na urefu wa maisha katika maneno machache mateule yaliyofinyangwa kisanaa. Uteule huu wa maneno katika nyimbo hujenga picha na tashbiha inayojenga maana na mantiki inayochorwa na mwimbaji, lakini heba yake imo katika kukamilisha hisi kwa msikilizaji: kama hisi za mapenzi au chuki, dhiki au faraja, ari au mapuuzo, uoga au ujasiri, sifa au kero.

Sifa moja ambayo hubainisha nyimbo ni matumizi yake ya lugha hasa zile tamathali za usemi kama vile tashbihi, methali, jazanda, majina ya majazi na taashira. Tamathali hizi zinazotumiwa na nyimbo huwa ama zimebuniwa katika jamii ya mwimbaji au zimebuniwa na mwimbaji mwenyewe lakini akizingatia kanuni za uundaji wake.

Tamathali za semi ni vifananisho au viwakilisho nya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti au zinazofanana. Kwa mujibu wa Mulokozi na Kahigi (1979) wanaeleza kuwa tamathali ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana za dhahiri ama za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu ya kishairi iliyokusudiwa na mtunzi. Kahigi (1995) akifafanua zaidi anasema kuwa msingi wa tamathali za semi nyingi ni uhamishaji wa maana. Uhamishaji wa maana ni mbinu ya kuibua maana ya kiashiria (neno, fungu n.k) kutokana na maana ya kiashiria kingine. Kanuni ya jumla ya uhamishaji wa maana ni maana ya kimethali X inachukua nafasi ya maana ya kawaida Y iwapo X inahusiana na Y kwa njia fulani. Hata hivyo, tamathali za semi ambazo zinahusika na uhamishaji wa maana ni sitiara, tashibiha, tashisi, taswira, methali na taashira. Kwa mujibu wa tasnifu hii imejikita zaidi kuchunguza taashira zinazoibuliwa katika nyimbo za harusi kama aina ya tamathali za semi.

Kwa kutumia taashira mwimbaji ana uwezo wa kuficha au kusitiri ujumbe fulani au maalumu utakaumsababisha msikilizaji ashangazwe au ajiulize nini hasa mwimbaji anachokusudia kuwasilisha. Hata hivyo katika tasnifu hii tumeitafisiri taashira kama ishara ya kitu au tendo, ambayo husimamia kitu chengine. Yaani **taashira** imetumika kusimamia tendo ama kitu fiche ambacho kimetajwa katika nyimbo. Usemi huu huwa na viwango viwili nya maana. Maana ya kawaida na maana ya kitaashira. Ufafanuzi wa maana hizi tumezieleza katika uchanganuzi. Kadhalika, taashira inaweza kuwa na msingi wa kiistiara, kwa mfano maneno kama vile: taa, mwenge ambayo humulika kuwasilisha utambuzi, ujuzi n.k. Vilevile inaweza kuwa na msingi wa kiishara kama: mkono wa mwanamume hutumika kuwasilisha nguvu, ujasiri n.k. (Kahigi 1995). Kwa ufupi tunasema kwamba, taashira inaweza kuwa istiara ama hata ishara yenyе maana fiche iliyokusudiwa ya kitaashira.

Katika tasnifu hii taashira zote zilizoibuliwa zilibainika kuwa na maana ya kitaashira. **Maana ya kitaashira** ni dhana imetumika kumaanisha maana ya ndani ya hali, tendo ama kitu kulingana na jinsi kilivyotumika nyimboni. Maana hii, huwa ni tofauti na ile maana ya kawaida. Katika tasnifu hii tumeweza kuibua aina mbili za taashira nazo ni *taashira ya kitu* na *taashira ya tendo*. **Taashira ya kitu** ni kitu kilichotajwa katika wimbo ambacho husimamia kitu kingine na huwa na maana ya kitaashira. **Taashira ya tendo** ni tendo ambalo lililotajwa katika wimbo na kubeba maana ya kitaashira.

Nyimbo ni chombo cha kubeba taashira mbalimbali. Taashira zilizomo katika nyimbo ziliwa na umuhimu mkubwa katika kuwasilisha maana na ujumbe. Utambuzi wa taashira ulifanywa kwa kupiga misitari maneno ya **vitu** na **matendo** yaliyotajwa nyimboni yaliyoaminika kuwa yanasmamia maana nyingine katika nyimbo. Kwa mfano baadhi ya nyimbo zimetumia maneno *mtaimbo, kisiki, kalamu* na *mshuma* kama taashira yenyenye kumaanisha uume uliosimika. Kadhalika katika nyimbo nyingine, *kitabu au bahari* ilitumika kama taashira na kusimamia uke.

Uhamishaji wa maana kutokana na kiashiria kingine pia umefafanulia na Wafula na Njogo (2007:80) wakimrejelea Freud katika kazi yao. Wanaeleza kwamba, Freud aliibuka na aina mbili za tamathali. Kuna tamathali zinazowakilisha jinsia ya kike, na zile zinawazowakilisha jinsia ya kiume. Tamathali zinazowasilisha jinsia ya kike zina sura ya mpanuko au 'mfunuko' kama ua, na tamathali zinazoashiria jinsia ya kiume kama penseli au mkuki. Tamathali zote zinazosimama wima zinaashiria uume nazo zilizolala au za mviringo zinawakilisha uke.

Kama tulivyoeleza katika kifungu kilichotangulia (1.1.2.1) kuhusu nyimbo za harusi za Waunguja, imedhihirika kwamba nyimbo nyingi ziliwa zimebeba taashira. Kama tulivyoeleza awali kuwa, nyimbo ni chombo cha kubeba taashira. Taashira zilizoibuliwa zilihuushwa na mazingira yaliyowazunguka pamoja na vitu vinavyopatikana katika maisha ya jamii ya Waunguja. Vitu hivyo ni kama vile: vitu vya baharini, vitu vya nyumbani, mimea na sehemu za mwili. Hata hivyo, maneno yenyenye kupigwa msitari chini katika nyimbo zifuatazo ni taashira zilizoibuliwa kulingana na miktadha wa tukio harusini. Kwa mfano: *Jahazi* ni moja ya taashira ya vitu vya baharini, ilibiliwa katika wimbo *JAHAZI*. Taashira hii tunaiona katika ubeti wa kwanza wa wimbo hapa chini.

## MMH2. JAHAZI

*Jahazi yetu twaipeleka kwa pepo njema.*

*Nenda mwanangu amana Llahu Aman Rasuli.*

*Huyo ajaye mwana wa siwa na matuwazi.*

Taashira zilizobainika kama vitu vya nyumbani ziliibuliwa katika nyimbo tofauti ziimbwazo kwenye miktadha tofauti harusini. Taashira hizi tunakutana nazo katika nyimbo zifuatazo.

**MMH.3. NATAKA TAMBUU**

*Kijakazi change si cha kutuma,  
Sikumpa jembe kwenda kulima,  
Nilimpa chuo kwenda kusoma,  
Asome ilimu na Kuruani*

Wimbo mwengine uliobainika kuwa na taashira ni huu hapa chini.

**MKN.9. KUNAILA MOJA**

- Kungwi: *Kuna ila moja ila ila baba ila,  
Kigongo mkononi ila.*
- Watani: *Kuna ila moja ila ila baba ila,  
Kigongo mkononi ila.*
- Kungwi: *Kuna ila moja ila ila baba ila,  
Kusimbulia mke ila.*
- Watani: *Kuna ila moja ila ila baba ila,  
Kusimbulia mke ila.*

'*BISIMULLAH*' ni wimbo pia ulibeba taashira. *Kioo* ni taashira iliyoibuliwa katika ubeti ufuatao hapa chini.

"*muenge enge kama kioo mume nduguyoo,  
muenge enge kama kioo mume nduguyoo"*

*Kasiba* ni taashira nyingine imetumiwa katika wimbo huo hapa chini.

**MMH.1.MNGANAMBWA**

*Kidomo katiti kama kasiba  
Chenye mwanya kati mbwake haiba  
Ndiye mke siti mwenye mahaba  
Atwazaye watu mahadharani*

Baadhi ya nyimbo za harusi zilibeba taashira zinazotaja sehemu za mwili wa binadamu na wanyama. Sehemu za mwili zilizoibuliwa kama taashira ni *ini* na *pembe* Sehemu hizi zilibeba maana ya kitaashira kulingana kwa jinsi zilivyotumika nyimboni na kutoa ujumbe muhimu katika jamii ya Waunguja. *Ini* ni taashira inayoibuliwa katika wimbo MSG.1.BISIMULLAHI kama unavyooneka hapa chini.

*ee oo yaa eee enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini,  
enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini ee.*

*ee oo yaa eee akikuaga mpe ruhusa mwana anakwao ee,  
akikuaga mpe ruhusa mwana anakwao ee.*

Umuhimu wa taashira ya ini iliyotumika katika wimbo MSG.1. *BISIMULLAHI* hutoa fundisho la upendo katika jamii. Ama pembe imeibuliwa kutoka nyimbo mbili MSG.17. HUYO YUWAJA na MKN.1 KINYEMI CHA MWANA kama zinavyoonekana hapa chini:

#### MSG.17. HUYO YUWAJA

*Huyo yuwaja yuwaja mpeni ndia,  
Huyo yutukuzie pembe na pembe mwana mema,  
Huyo yutukuze pembe na pembe mwana mema,  
Atukuze akatuwe mzigo kitwani.*

#### MKN.1 KINYEMI CHA MWANA

*Nimepewa pembe  
Nalilia pembe ee x2  
Nalilia pembe langu x2  
Napewa ni mama  
Nalilia pembe langu x2  
Sikupewa ni baba*

Utafiti umegundua kuwa, maana ya taashira za tendo zilizopatikana zimetokea kujikita zaidi kwa kuhusishwa na matendo yaliyomuhusu mwari/bibi harusi, bwana harusi na machache yalimuhusu mamie mwari/bibi harusi. Taashira zote hizi tulizibainisha kwa kuzipigia misitari. Kwa mfano katika wimbo MSG 13 hapo chini unaonyesha taashira za tendo zilizopigwa msitari zilivyotumika kumuhusu mwari.

#### MSG 13 KISIKI

Kungwi:      *Ukafiche kuche ee, ukafiche kuche ee, ukafiche kuche ee,  
Unakwenda mijini mwa watu, ukafiche kuche.*  
Watani:      *Ukafiche kuche ee, ukafiche kuche ee, ukafiche kuche ee,  
Unakwenda mijini mwa watu, ukafiche kuche.*

Kungwi:      *Unamie chini ee unamie chini, unamie chini ee unamie chini  
Unakwenda mijini mwa watu, unamie chini.*  
Watani:      *Unamie chini ee unamie chini, unamie chini ee unamie chini.  
Unakwenda mijini mwa watu, unamie chini.*

Ama taashira ya tendo iliyomuhusu bwana harusi imetumika katika wimbo ufuatao hapa chini.

#### MBN.16. KITABU

Eeee leo achore  
*Eeee leo achore*  
Bwana harusi asema  
Ataka kitabu achore  
Na kalamu ashachonga  
*Ataka kitabu achore*

Katika wimbo MBN.16 *ataka kitabu achore na kalamu ashachonga* ndiyo maneno ya kitaashira ya tendo. Mifano zaidi ya nyimbo zenyenye kubeba taashira za tendo imetelezewa katika sura ya uchanganuzi.

#### **1.1.4 Utendaji katika Nyimbo za Harusi**

Wakati wa uimbaji wa nyimbo za harusi, hadhira na waimbaji wenyewe hawazingatii tu matini na ujumbe utolewao katika wimbo lakini huzingatia pia muktadha na utendaji. Hata hivyo, jinsi nyimbo zinavyoimbwa (iwe ni kwa mwendo wa polepole au harakaharaka) athari inayotokea kati ya mwimbaji na matini, athari kati ya waimbaji na hadhira inatoa maana muhimu na fasiri tofauti ya nyimbo hizo. Kwa mujibu wa Askew (1997) maana katika uwasiliswaji wa nyimbo hutambuliwa kwa kukutanisha matini na utendaji uliyojumuisha matendo yajulikanayo kwa undani na wenyeji.

Wazo la umuhimu la kuzingatia utendaji kwa ajili ya kupata maana ya nyimbo pia linatiliwa mkazo na Ntarangwi (2001: 24). Ntarangwi katika kazi yake akiwanuku (Earlmann 1996; Sugarman 1997; Turino 1995; Watermann 1990) anaeleza kuwa utendaji kama vile: ukataji kiuno, matendo ya wachezaji kama vile - miondoko na matumizi ya viungo wakati wa uimbaji yote haya huchangia kupata maana ya nyimbo. Utendaji au matendo haya yanatoa ujumbe ambao hauwezi kupatikana na kuchanganuliwa katika matini za nyimbo. Mfano:-vigelegele, kupiga makofi, kukata kiuno, wanawake kunyosha mikono juu kuvingirisha vidole, kupara samaki, kuigiza kuchora na kuchonga kalamu, uvaaji shanga, ufungaji khanga kichwani, kuitupia khanga juu ya mabega na kuteremka chini, kufunga khanga kiunoni.

Katika tasnifu hii utendaji ni istilahi imetumika kurejelea matendo yaliyofungamana na uimbaji wa nyimbo za harusi. Sherehe katika harusi za Waunguja zilifungamana na uimbaji na utendaji. Hata hivyo utafiti ulibaini kulikuwa na utendaji wa aina tatu wakati wa uimbaji nyimbo za harusi. Kwanza utendaji ulioambatana na taashira wakati wa kucheza na kuimba. Pili utendaji katika matukio yanayoashiria mambo ya kitaashira wakati wa uimbaji. Tatu utendaji wa uigizaji wa vitu vya bibi harusi wakati wa kuimba nyimbo.

Kwa mfano utendaji ulioambatana na taashira wakati wa kucheza na kuimba ulidhirikia katika nyimbo mbalimbali. Utendaji huu ulikuwa kama vile Wanawake kuviringisha vidole vya katikakati, kukata/kuvitingisha viuno, kupiga makofi., Kupiga vigelegele na kuigiza kupara samaki yote yalidhihirika katika nyimbo tofauti. Aidha, maana za utendaji huu ulikuwa tofauti kulinga na muktadha wa tukio.

Mathalani kupiga vigelegele, utafiti ulibaini kwamba nyimbo nyingi zilizokuwa zikiimbwa katika harusi za Waswahili Waunguja zilishindikizwa kwa vigelegele. Vigelegele vivilvyopigwa wakati wa uimbaji wa nyimbo harusini vilaminika kuwa na maana tofauti kulingana na tukio mahasusi. Mfano, kigelegele kilichopigwa na kungwi kabla ya kuimba wimbo MSG.11 KAWAIDA YA SINGO katika tukio la singo kilitofautiana na kigelegele kilichopigwa baadya ya nikaha kufungwa walipokuwa wakiimba wa MBN.1.CHEBA. tofauti ya maana ya vigelegele hivi yameelezwa kwa kina katika sura ya tano.

Kadhalika utafiti ulibaini utendaji wa kuigiza kuchora na kuchonga kalamu katika wimbo MBN.16. KITABU uliokuwa ukiimbwa kwenye tukio la bwana harusi kwenda kutoa mkono nyumbani kwa wazazi wa bibi harusi. Wimbo MBN.16. KITABU ulikuwa ni mmoja wa wimbo ambao utendaji wake uliambatana na taashira zilizotajwa wakati wa uimbaji. Tazama taashira zilizoambatana na utendaji katika wimbo ufuatao hapa chini.

#### MBN.16. KITABU

*Eeee leo achore  
Eeee leo achore  
Bwana harusi asema  
Ataka kitabu achore  
Na kalamu ashachonga  
Ataka kitabu achore*

Taashira ya *bwana harusi asema, ataka kitabu achore, na kalamu ashachonga* katika wimbo MBN.16 iliamabatana na uigizaji wa tendo la kuchora katika kitabu na kuchonga kalamu. Utendaji ulifanywa na wanawake wa upande wa bwana harusi. Wanawake hawa walikuwa wakiimba kwa vishindo, huku baadhi yao wakiigizia kuchora kwa kutumia kidole cha kati cha mkono wa kulia juu ya kiganja cha mkono wa kushoto. Aidha, wanawake wengine waliigizia kama mtu anayechonga kalamu ya penseli. Walikuwa wakipenyeza kidole cha kati kwenye kiganja cha mkono wa kushoto kilichofumbwa.

Utendaji mwengine ulifanyika ni katika tukio la singo. Uimbaji wa nyimbo za singo mara nyingi huambatana na upigaji makofi. Makofi zinatumwiwa kama vichapuzi au ala ya muziki kwa ajili ya kuweka mezani ya wimbo. Kadhalika katika tukio hili mbali na kupiga makofi huwa kuna utendaji wa kuimba na kucheza. Waimbaji huimba huku wakimzunguka bibi harusi na kukata viuno. Wachezaji huwa wamejifunga khanga kiunoni au chini ya kiuno katikaati ya makalio. Ufungaji huu humuwezesha mchezaji kuzungusha kiuno chake na makalio yake kwa mitindo mbalimbali. Kila mchezaji anayekuja mbele ya bibi harusi kucheza anaonyesha umahiri wake wa kukiviringisha kiuno kama wanavyofanya katika tendo la ndoa. Mchezaji anapokata kiuno mikono huwa juu hewani kama ndege anayetaka kupaa, shingo huipundua na kuizungusha pia, huku macho kayalimbua na kuyalegeza hamuangalii mtu. Uchezaji unakuwa ni wa kupanda juu na chini mwili mzima.

Hata hivyo, utendaji mbalimbali ulidhirika katika matukio tofauti wakati wa uimbaji wa nyimbo harusini. Mtafiti alichunguza utendaji ili umuwezesha kupata maana na ufaafu wa nyimbo hizo kulingana na muktadha wa ndoa ya jamii ya Waunguja. Kadhalika uchunguzi wa utendaji ulisaidia kuelewa kwa undani jinsi nyimbo hizi zinavyotekelawa jukumu lake katika sherehe za harusi.

Hivyo basi maelezo haya yaliyotolewa katika usuli wa mada yanaoonyesha kuwa utafiti huu ni muhimu kueleza utamaduni na matumizi ya nyimbo katika harusi za Waunguja . Lengo hasa ni kwa ajili ya kupata msingi wa kuelewa yaliyomo katika tasnifu hii.

## **1.2 Mada ya Utafiti**

Baada ya kuititia kazi mbalimbali zilizofanywa kuhusiana na nyimbo za harusi za Waswahili, imenidhirikia kwamba nyingi zilichunguza matumizi ya lugha zikiwemo tamathali za sami mbalimbali. Hata hivyo tamathali ya semi ambayo haikushughulikiwa sana ni taashira pamoja na utendaji wake katika nyimbo za harusi. Mtafiti alibaini kwamba nyimbo nyingi za Waswahili wa Unguja zinazoimbwa katika harusi zilisheheni taashira na utendaji ambao kufikia sasa haukuwa umewekwa bayana kitaaluma hivyo, ilikuwa haujulikani. Kwa hiyo, utafiti huu ukafanywa kwa lengo la kubainisha na kufanua taashira zilizomo katika nyimbo za Waswahili

wa Unguja pamoja na kuangalia mchango wa utendaji katika kupatia kila taashira maana iliyokusudiwa kwa maharusi na hadhira.

### **1.3 Madhumuni ya Utafiti**

Madhumuni ya utafiti huu ni:-

- (i) Kubainisha na kuainisha matumizi ya taashira katika nyimbo za harusi za Waswahili wa kisiwani Unguja.
- (ii) Kufafanua maana za taashira mbalimbali katika nyimbo na umuhimu wake kulingana utamaduni wa jamii ya Waunguja.
- (iii) Kupambanua maana ya utendaji unaofanywa wakati wa uimbaji nyimbo za harusi.

### **1.4 Maswali ya UTafiti**

Utafiti huu uliongozwa na maswali ya fuatayo -.

- (i) Je, Nyimbo za harusi za Waswahili wa kisiwani Unguja zina matumizi ya taashira?
- (ii) Je, taashira zilizotumika katika nyimbo za harusi zinabeba maana gani za kitaashira na huwa na umuhimu kwa jamii?
- (iii) Je, utendaji unaofanywa wakati wa uimbaji nyimbo za harusi una maana wowote?

### **1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu unatoa mchango kwa watafiti, walimu na wanafunzi wa somo la fasihi simulizi kuelewa vyema nafasi ya nyimbo katika harusi za Waswahili waliopo kisiwani Unguja. Utafiti huu pia unachangia utajiri katika fasihi simulizi hasa kuhusu utanzu wa nyimbo.

Utafiti huu utakuwa nyongeza kwa tafiti za hapo awali zilizofanywa juu ya taashira katika nyimbo za harusi pamoja na utendaji wake endapo taashira na utendaji utabainishwa na kutolewa maana zake za ndani. Utawafaidi wachanganuzi wa semi kwa vile unatarajiwu kuweka msingi thabiti ambao wanaweza kuutumia kuchanganua tamathali za semi zozote zile na kudhihirisha maana na umuhimu wake kwa jamii. Aidha, utawafaa wanajamii wakiwemo maharusi endapo tatizo la utafit huu litatatuliwa na kufahamika maana za ndani za taashira na utendaji wake katika nyimbo za harusi. Vivyo hivyo, Wasanii yaani waimbaji wa nyimbo watanufaika, kwa vile utafiti huu utaonyesha umuhimu wa maana hizo za kitaashira kwa jamii.

Kwa kutumia umuhumi huo wanaweza kutahmini uwasilishaji wao wa nyimbo za harusi na kuziboresha ili kufanikisha shuguli nzima ya kuwasilisha nyimbo kwa jamii ipasavyo.

Nyimbo za harusi za Waswahili hutungwa na kuimbwa kwa lugha ya Kiswahili. Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Tanzania, Kenya na Uganda. Pia ni lugha sambazi Afrika Mashariki na Kati. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yanakuwa na umuhimu vile vile kwa watu wa kawaida au wapenzi wa Kiswahili wanaotumia lugha ya Kiswahili. Matokeo yatawafanya kuelewa kwa undani zaidi maana za taashira zilizomo katika nyimbo kulingana na muktadha wa utendaji katika harusi za Waswahili wa Unguja.

Utafiti huu utawachochaea watafiti wengine kushughulikia fasihi simulizi. Utanzu huu haujashughulikiwa ipasavyo ukilinganishwa na fasihi andishi hasa utanzu wa mashairi. Kama alivyosema Whiteley (1966), bado kuna nyimbo nyingi ambazo zimekusanywa tu lakini hazijachanganuliwa kitaalamu ili kuwanufaisha watu wengi - Waswahili na wasio Waswahili.

Kwa kuzingatia kwamba nyimbo za harusi zina dhima mbali ya kuburudisha zinaelimisha maadili yenye umuhimu kwa jamii, utafiti kama huu unaoshughulikia matumizi ya lugha ni muhimu. Hii ni kwa sababu lugha, kama chombo cha kuwasilishia maadili, inatakikana itumike kuwavutia wanajamii ili waendelee kupata mafunzo yatakayowafaa katika maisha yao ya kila siku.

## **1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulishughulikia nyimbo za harusi kisiwani Unguja. Nyimbo hizi ni zile zinazoimbwa katika miktadha mbalimbali yanayofungamana na harusi. Miktadha ni kama vile wakati wa kupelekeka na kupokea mahari, kutoka kualika harusi, singo, kutoa mkono, walima, kumchukuwa bibi harusi, kupokea masanduku ya bibi harusi, bibi harusi akihongera na siku ya kupamba. Nyimbo za taarabu zinazoimbwa katika miktadha hii pia zilihusishwasi. Nyimbo za taarabu zenye kubeba maudhui ya kisiasa pamoja na taarabu za mipasho hazikushughulikiwa. Ijapokuwa taarabu za mipasho zina utendaji lakini utendaji huo una umuhimu mdogo kwa bwana na bibi harusi. Kama dhima mojawapo ya nyimbo za harusi ni kuwafunza maharusi kunga za maisha, uwasilishwaji wa nyimbo nyingi za taarabu za mipasho hugusia mambo mbalimbali

ambayo yako nje ya muktadha wa harusi au kuwahusu maharusi. Taarabu za mipasho hutaja mambo kama vile malumbano na kupigana vijembe kinyume na nyimbo za harusi ambazo zinatoa maana mbalimbali kupitia taashira zilizomo ndani yake.

Maeneo mahususi ambayo mtafiti alishiriki kukusanya nyimbo hizo ni Tumbatu, Unguja Mjini, na Makunduchi. Maeneo haya yameonyeshwa katika kiambatisho cha ramani.

Masuala ya mtindo na ujumi kama vile toni, hisia na maghani japo nayo ni muhimu katika uchanganuzi wa nyimbo, utafiti haukuyachanganua. Vilevile, utafiti haukuchunguza taaluma ya utungaji muziki wa nyimbo hizi.

### **1.7 Matatizo Yaliyojitokeza**

Mtafiti alikumbana na matatizo kadhaa kuanzia kukusanya data hadi uchanganuzi. Baadhi ya matatizo hayo ni yafuatayo:-

Kulikua na nyimbo nyimbo ambazo hazikurekodika vizuri kwa sababu ya ghasia na fujo wakati wa sherehe harusini. Hivyo basi, mtafiti alilazimika baada ya harusi kuwatafuta watu wanaozifahamu nyimbo hizo wamuimbie tena. Mtafiti aliwapata watu hao na alizirekodi tena nyimbo alizoimbiwa kwa uzuri.

Mtafiti na watafiti wasaidizi walipata matatizo wakati wa kurekodi data kwa kutumia kamera ya video. Katika sherehe ambamo mkiimbwa nyimbo na kuchewza na wanawake, baadhi ya wanawake walikuwa wakikataa na hata kujificha au kuacha kucheba ili wasirekodiwe. Kisingizio walichokitoa ni kuwa, kanda za video hutazamwa na watu wengi na wao ni wake za watu, hivyo wasingependa waonekane na watu wengine hasa wanaume.

Mtafiti wakati mwengine alishindwa kupata uhalisia wa utendaji. Hali hii ilisababishwa na baadhi ya wachezaji ambao walikuwa wakitia chuku katika uchezaji wao. Kwani kila wakati walikuwa wakijitokeza mbele ili warekodiwe wao zaidi.

Baadhi ya wasailiwa walikuwa wazito kutoa tafsiri kuhusiana na baadhi ya maana za taashira au utendaji ulivyojitokeza katika nyimbo. Sababu waliyoitoa ni kuwa, kulingana na maadili ya utamaduni wao, mambo haya hayazungumzwi waziwazi.

Mtafiti alielezwa na wasailiwa kuwa, zipo ngoma na nyimbo za kiasili zilizokuwa zikipendwa na kuimbwa sana wakati wa zamani kama *lelemama, bomu, msondo, kidumbak, msewe na beni*. Nyimbo hizi ziliwuwa zikiimbwa katika harusi, lakini ilikuwa vigumu kuzipata. Walipouliza ni kwa nini haziimbwi tena katika harusi, walisema kuwa waimbaji wake wengi wamefariki. Isitoshe gharama za kukodisha ngoma kama hizi ni kubwa. Sababu nyingine waliyotowa ni kuwa, watu wengi siku hizi wameathiriwa na dini ya Kiisilamu, hivyo hawapendelei kuweka ngoma hizo katika sherehe za harusi. halikadhalika ilikuwa vigumu kwa mtafiti kutofautisha nyimbo zinazoimbwa katika sehemu moja na nyingine. Hii imetokana na sababu kwamba, kumekuwa na muingiliano mkubwa wa makabila ya Waunguja na hivyo kusababisha muingiliano wa tamaduni zao na hata utendaji wa sherehe za harusi.

Kwa sababu ya hoihoi na vifijo katika harusi, kazi ya kurikodi ilikuwa ngumu. Mtafiti alilazimika kurekodi nyimbo katika hali hiyo hiyo. Baada ya kuzirekodi nyimbo hizi alikwenda nyumbani ili kuzinakili. Alipokuwa akizisikiliza na kuzinakili nyimbo alipata tabu. Kwani, baadhi ya nyimbo ziliwuwa na sauti kubwa.

## 1.8 Maelezo ya Istilahi

**Kupelekwa chooni:** Mwari au bibi harusi kwenda kuogeshwa kwenye uzio maalum.

**Harusi kujibu:** Kudhihirika ubikira wa bibi harusi.

**Kasida:** Tungo maalumu za kumsifu Mtume Muhammad (s.a.w) au za kumsifu mtu au jambo. Kasida huimbwa wakati wa sherehe mahususi kama kusherehekeza kuzaliwa Mtume au harusi.

**Kitambi:** Hiki ni kitambara laini mfano wa hariri anachofunika bibi harusi usoni wakati akimsubiri bwana harusi.

**Kufunga nikaha:** Kufunga ndoa.

**Kuingia ndani:** Hii ni siku ya kwanza kwa bwana harusi anayokwenda kukutana kimwili na bibi harusi. Ni ada ya muhimu kwa Waswahili. Ni siku inayosubiriwa kwa hamu na jamaa wa maharusi kutaka kujuia iwapo harusi itajibu salama. Yaani kama mwari atakutwa ni bikira Aidha, ndio kilele cha ndoa.

**Kungwi/Somo/Fundi:** Mwanamke anayemfundisha mwari kunga za nyumbani.

**Kutiwa Maji ya Khutba:** Kuogeshwa bibi harusi punde tu baada ya nikaha kusomwa

(kufungwa). Bibi harusi huelekwa mgongoni na kungwi wake kumpeleka chooni *kutiwa maji ya khutba*. Kitendo cha *kutiwa maji* kinaashiria kuwa sasa huyu ni mke wa mtu.

**Kutoa mkono:** Ni kitendo cha bwana harusi kwenda kumsalimu bibi harusi. Kawaida baada ya kutoa mkono, mume anaweza kumchukua mkewe na kwenda naye au akaamua kurudi baadaye kumchukua. Wakati mwengine mume huondoka na akapelekewa mkewe usiku kwake.

**Kupamba/Kuonyeshwa:** Ni siku ambayo bwana na bibi harusi au bibi harusi pekee anapelekwa ukumbini kuonyeshwa mbele ya hadhira.

**Maana ya kitaashira:** Ni maana ya ndani ya hali, tendo ama kitu kulingana na jinsi kilivytumika nyimboni. Maana hii, huwa ni tofauti na ile maana ya kawaida. Yaani taashira fulani husimamia maana fiche.

**Matendo:** Ni matendo yanayotendwa kulingana na tukio la kitamaduni katika harusi. Wakati mwengine matendo haya huambatana na nyimbo. Mfano, kusingwa, kufukizwa bi harusi, bi harusi kuelekwa mgongoni, mwari kutengenezewa njia, mwari kupakatwa, kumwagiwa maji, kunywa chai, kuinamisha kichwa chini na ufungaji khanga kichwani.

**Maulidi:** Sherehe ya kuadhimisha kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (s.a.w).

**Mrombo:** Mtu aliyejata mafunzo unyagoni au jandoni.

**Mshenga:** Mwanamume anayetumwa na upande wa mchumba wa kiume kupeleka posa kwa upande wa mwanamke.

**Msungo:** Mtu ambaye hakupata mafunzo ya unyago au jando.

- Mwari:** Mwanamke aliyekwisha vunja ungo na ambaye tayari ameshapaswa anasubiri siku ya kufunga ndoa kufika.
- Sahani ya Somo:** Hii ni sahani au sinia ambayo huaminika kuwa ni ya somo/ kungwi wa bibi harusi. Hupitishwa mbele ya hadhira baada ya bibi harusi kuhongera ili watu watie pesa/hidaya. Pesa hizi hupewa somo kama shukrani ya kumfunza mwari.
- Singo:** Shughuli wanayoifanya makungwi kuwasugua miili bibi harusi au bwana harusi kwa karafuu, dalia na liwa ili miili yao iwe laini na safi. Shughuli hii hufanywa faraghani huku maharusi hao wakiimbiwa nyimbo za kufundwa.
- Sunnah** Ni matendo au kauli alizosema Mtume Mohamad (S.A.W)wakati wa uhai wake. Mtu anapotekeleza sunnah hupata thawabu anapoiacha hapati dhambi.
- Taashira:** Imetumika katika kazi hii, kusimamia tendo ama kitu fiche ambacho kimetajwa katika nyimbo. Taashira inaweza kuwa jazanda/istiari ama hatataszira yenye maana fiche iliyokusudiwa ya kitaashira.
- Taashira za kitu:** Ni kitu kilichotajwa katika wimbo ambacho husimamia kitu kingine na huwa na maana ya kitaashira.
- Taashira za tendo:** Matendo ambayo hutajwa katika wimbo na kuwa na maana ya kitaashira.
- Utaji (ushungi):** Kitambaa Aghalabu cha rangi kinachovaliwa kichwani na wanawake.
- Utanga:** Utanga ni aina ya mkeka unaotandikiwa mwari wakati wa kuanza kufunzwa mambo ya siri na kungwi.
- Utendaji:** Istilahi hii imetumika kurejelea matendo yaliyofungamana na uimbaji wa nyimbo za harusi. Mfano:-vigelegele, kupiga makofi, kukata kiuno, wanawake kunyosha mikono juu kuvingirisha vidole,kupara samaki, kuigiza kuchora na kuchonga kalamu,uvaaji shanga, ufungaji khanga

kichwani, kuitupia khanga juu ya mabega na kuteremka chini, kufunga khanga kiunoni.

**Watani:** Ni watu wa karibu wa mwari au kijana ambao ndio wanaomsinga mwari wakati wa singo. Wanaweza kuwa mabibi, binamu, wifi, au hata marafiki zake mwari.

## **SURA YA PILI**

### **MAPITIO YA MANDIKO**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii ilimulika tafiti zilizo na uhusiano wa namna moja au nyingine na utafiti huu. Ilionyesha kufanana au kutofautiana kuliopo kati ya kazi hii na zile za wataalamu wengine na pengo la kielimu lililotakikana kujazwa. Mambo yaliyoangaziwa ni pamoja na nyimbo za harusi za Waswahili ziimbwazo harusini zikiwepo zile za taarabu kama ushairi simulizi, matumizi ya lugha hususan taashira zilizotumika kwenye nyimbio za harusi, ujumbe utolewao na taashira zilizotumika nyimboni, utendaji unaofanyika wakati wa uimbaji na ada za harusi za Waswahili. Fauka ya hayo, imeangazia Nadharia ya Semiotiki na (N.S) na Nadharia ya Utendaji (N.U) kwa kuelezea waasisi wa nadharia hizo, mihimili yake na jinsi zilivyotumika kuongoza utafiti huu.

#### **2.2 Mapitio ya Maandishi Yanayohusu Nyimbo katika Ushairi Simulizi**

Farsy (1956) alielezea ada za harusi na jinsi zinavyotekelawa kufuatana na matukio ya harusi katika jamii ya Waswahili wa kisiwani Unguja. Mambo aliyoylezea katika kazi hiyo ni pamoja na posa, mahari, singo, kupamba na nyimbo za harusi. Kazi ya Farsy kwa kiwango fulani inahusiana na utafiti huu kwa sababu ilielezea jinsi Waswahili wa Unguja hufanya harusi zao na kutoa mifano ya nyimbo ziimbwazo katika matukio ya harusi.

Tofauti iliyopo ni kuwa, kazi ya Farsy imejikita zaidi kueleza ada za harusi za Waswahili wa kisiwani Unguja bila kuchunguza matumizi ya lugha pamoja na utendaji wake wakati wa uimbaji kama utafiti huu ulivyofanya. Ingawa kazi yake haikujishughulisha na uchanganuzi wa taashira kulingana na muktadha wa nyimbo za harusi kama utafiti huu ulivyofanya, ilitufa sana kufahamu nyimbo hasa za zamani ziimbwazo pamoja hatua za sherehe katika harusi zifanywazo. Kadhalika kazi ya Farsy ilidhihirisha maelezo ya waziwazi na jinsi nyimbo zilivyo na umuhimu wake katika sherehe ya harusi ya Waswahili, kisiwani Unguja.

Kazi ya Whiteley (1966) pia ni mionganoni mwa kazi za awali kuhusu nyimbo za Waswahili. Whiteley alikusanya nyimbo zikiwemo nyimbo za harusi zilizoimbwa Zanzibar kati ya miaka

1920 hadi 1950. Kazi yake ilikuwa utangulizi ambao unaeleza taarifa nyingi zinazosisitiza umuhimu wa nyimbo kama chanzo cha asili ya msamiati katika lugha ya Kiswahili. Mbali na kukusanya nyimbo hizo ambazo baadhi yake hazijachanganuliwa, Whiteley alitoa taarifa fupi za wasanii na michango yao katika kuelezea muktadha wa matumizi ya baadhi ya nyimbo. Hata hivyo kazi yake haikuchanganua taashira katika nyimbo alizozikusanya kama utafiti huu ulivyofanya. Hata hivyo kazi yake ilitusaidia na kutupatia miongozo katika utafiti huu jinsi ya kuelezea miktadha ya matumizi ya nyimbo za harusini.

Topan (1971) katika kazi yake alichanganua dhima na maana za nyimbo kutokana na muktadha wa miviga ya nyimbo za kupunga pepo, kulingana na jamii ya Waswahili wa Mombasa. Alieleza kwa undani muktadha wa miviga, imani na matendo kwa kurejelea historia na utamaduni wa jamii hii zinavyojitokeza wakati wa kupunga pepo. Kazi ya Topan ni tofauti na utafiti huu. Utafiti huu ulichunguza matumizi ya taashira na maana zake pamoja na utendaji unaowasilishwa wakati wa uimbaji nyimbo za harusi za Waswahili wa kisiwani Unguja. Hata hivyo kazi ya Topan imesaidia kuelewa zaidi uhusiano wa nyimbo na utamaduni wa Waswahili kwa ujumla.

Utafiti mwingine uliofanywa unaohusu nyimbo na ngoma za harusi za Waswahili ni wa Campbell (1976). Utafiti wake ulifanyika pwani ya Kenya sehemu za Mombasa na Tchundwa. Campbell alitoa maelezo ya kimuhtasari ya aina za ngoma za harusi kama vile *chakacha*, *vugo*, na *lelemama*. Mbali na maelezo kuhusu ngoma pia alielezea aina nyingine za nyimbo zilizoko katika jamii ya Waswahili. Kwa mfano, nyimbo ziimbwazo wakati mtoto anapozaliwa, nyimbo za kazi na ya nyimbo za harusi. Hata hivyo mbali na kutoa maelezo yote hayo, kazi yake haikujishughulisha kuchunguza taashira katika muktadha wa utendaj wa nyimbo za harusi. Jambo ambalo utafiti utafiti huu ulilifanya. Hata hivyo kazi ya Campbell ilitusaidia kutuongoza kufahamu aina mbali mbali za nyimbo ziimbwazo katika jamii ya Waswahili mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki.

Kazi za kihakiki za fasihi simulizi ni hazina kubwa za utafiti wa ushairi simulizi. Baadhi ya kazi za kihakiki zilizoshughulikia ushairi wa Waswahili hazikushughulikia kueleza maana za taashira katika nyimbo. Kwa mfano, Allen (1976a na 1976b); Mulokozi (1975); Kezilahabi (1978); Abdulaziz (1979); Topan (1984) na Shariff (1988). Nyingi za kazi hizi, isipokuwa kazi za Allen,

ni kazi za kiutafiti zilizofuata utaratibu wa kitaaluma. Kazi zote hizi zinaunga mkono hoja kuwa, ushairi simulizi wa Waswahili ni kipengele kinachotekeleza dhima ya kijamii. Dhima ambayo, inayoshughulikia matokeo ya kila siku au masuala makuu katika jamii pana ya Waswahili. Ingawaje wataalamu hawa walitambua dhima ya kijamii katika ushairi simulizi lakini hakuna hata mmoja aliyeshughulika kuangalia maana za kitaashira katika nyimbo.

Coppens (1980) katika utafiti wake alieleza ada za harusi za kisiwa cha Lamu, Kenya. Katika kazi hii, alikusanya baadhi ya nyimbo ziimbwazo katika harusi za Waswahili wa Lamu. Pia alitoa maelezo ya baadhi ya nyimbo za harusi na jinsi zinavyowasilishwa katika harusi. Utafiti huu unahusiana na kazi ya Coppens ijapokuwa yeze alizingatia zaidi ada na nyimbo chache za harusi za Waswahili wa kisiwani Lamu. Tofauti uliojitekeza kati ya kazi ya Coppens na utafiti huu ni kuwa,, utafiti huu ulijikita zaidi kuchunguza matumizi ya taashira kulingana na miktadha ya utendaji wa nyimbo za harusi kisiwani Unguja. Coppens alielezea zaidi jinsi nyimbo zinavyowasilishwa harusini. Yeye hakutilia maanani nafasi ya taashira zilizomo nyimboni zinavyosaidia kufahamu maana na ujumbe utolewao katika nyimbo za harusi. Hata hivyo kazi yake ilitusaidia kufahamu utajiri wa nyimbo za harusi zilizoko katika jamii ya Waswahili na vitongoje vyake.

Khatib (1981) katika kazi yake alichunguza ni kwa kiasi gani "Taarabu" muziki wenyewe kupigwa na kuchanganywa na nyimbo, unaweza ukakidhi vitabia vya fasihi simulizi. Mwandishi alivionyesha vitabia hivyo vya taarabu na vile vya kazi nyingine za fasihi simulizi kadiri vinavyoachana na kukaribiana. Vitabia hivyo ni: utendaji, hadhira, mazingira, utambaji, umbuji wa uwasilishaji, tukio, umma, ushuhuda wa muziki, madaha, waitikiaji na lugha. Vitabia hivi vilikuwa na umuhimu wake katika kutafuta jawabu iwapo taarabu imesadifu au kutosadifu kuwa na vitabia vya fasihi simulizi. Khatib aliachia hadhira yake itoe uamuzi juu ya jambo hilo. Mbali na kuiachia hadhira kutoa hukumu ya swali hilo, nadharia tete zifuatazo zilijitokeza katika kazi yake:

Mashairi ya nyimbo za taarabu hutungwa na mtu kwa kukaa na kubuni na kuandika.

Nyimbo hukolezwa na kurithishwa vizazi kwa mdomo tu zinapoimbwa leo, kesho na kesho kutwa.

Taarabu ina utendaji wenye mipaka na ufinyu ukilinganishwa na utendaji wa tanzu zingine za fasihi simulizi.

Kazi hiyo ya Khatib ilitoa dira kwa utafiti huu, kuzingatia vipengele hivyo alivyovitaja mwandishi katika utendaji wa kazi za fasihi. Vitabia kama hivyo vilizingatiwa wakati wa uwasilishwaji wa nyimbo za harusi. Lengo la kuchunguza vitabia hivyo ni kuona jinsi gani vinasaidia kupambanua taashira katika nyimbo hizo.

Campbell (1983) alishughulikia kuchunguza ngoma za Waswahili. Utafiti wake ulifanywa Kenya katika wilaya ya Mombasa, Lamu na Tchundwa. Hata hivyo, jambo muhimu kuliko yote wa kazi hii, ni kule kufafanua maana ya wimbo katika jamii ya Waswahili kwa mtazamo wa kitamaduni na kijamii. Kazi yake inatofautiana na kazi za awali zilizoandikwa kuhusu ushairi wa Waswahili kama vile kazi za Hichens (1962), Harries (1962), na Knappert (1977) ambazo zilifafanua ushairi wa Waswahili kwa umbo linalozingatia kanuni za ushairi wa kimapokeo kuliko maudhui ya kitamaduni na kijamii. Kazi ya Campbell (1983) ijapokuwa haikujishugulisha kuchunguza taashira na utendaji katika nyimbo, hata hivyo kazi yake, ilisaidia utafiti huu kuona jinsi gani utanu wa nyimbo ulivyo na nafasi ya katika harusi za Waswahili wakazi wa kisiwani Unguja.

Kazi ya Nandwa na Bukenya (1983) ni kazi inayozungumzia fasihi simulizi kwa ujumla. Mionganoni mwa mada walizozishughulikia katika kazi hii ni suala la utendaji. Walitoa ufanuzi kuhusu dhana ya utendaji na umuhimu wake katika fasihi simulizi kwa kurejelea utanu wa drama. Kwa mujibu wa maelezo yao utendaji ni dhana ambayo inahusisha maingiliano baina ya mtendaji na hadhira. Mtendaji hapa ni fanani au msimuliaji. Fanani katika masimulizi yake hulusisha matumizi ya lugha, matumizi ya viungo vya mwili kama vile kurusha mikono, miguu, miondoko, kupandisha na kushusha sauti, kuonyesha hisia kwa kuititia viungo vya mwili, kuimba na hata kucheza. Nandwa na Bukenya wanaeleza kuwa, matumizi ya vitendo hivi vyote hutoa picha na maana kamili ya kile kinachosimuliwa kwa hadhira. Matumizi ya ishara hizi za mwili na hisia zinazofanywa, hubainisha pia mawasiliano baina ya fanani na hadhira iliyopo. Maelezo ya wasomi hawa yalikuwa na umuhimu katika utafiti huu kwa kuchunguza uwasilishwaji wa nyimbo za harusi na jinsi unavyosaidia kupambanua maana za taashira katika nyimbo hizo.

Nandwa na Bukenya (1983) walizungumzia kuhusu nyimbo, ngoma na maghani ya mashairi. Walieleza kuwa, nyimbo na ngoma ni maarufu sana katika jamii za Kiafrika na huwa zinatenekeleza dhima mbalimbali za maisha ya watu wake. Isitoshe nyimbo na ngoma hizo pia, huakisi utamaduni wa jamii husika. Katika kazi yao, walitoa mifano ya nyimbo mbalimbali kama vile- nyimbo za kubembeleza watoto, maghani ya kuwasifu mashujaa, majigambo, nyimbo za tambiko na nyimbo za harusi. Ingawa kazi yao ilikuwa pana, utafiti huu ulijikita katika kubainisha maana ya taashira katika nyimbo za harusi kutokana na uwasilishwaji wake.

King'ei (1992) amechambua nyimbo za taarabu. Katika kazi yake ameonyesha jinsi nyimbo za taarabu zinavyoweza kuwa njia ya mawasiliano ili kuonyesha dhima madhubuti za kijamii, za kiutamaduni na za kisiasa katika jamii ya Kenya ya miaka 1992. Uchunguzi wa King'ei uliongozwa na mtazamo wa kisiasa na kijamii na nadharia ya mitindo iliyotumiwa na wahakiki kama vile Eagleton (1976), Ngara (1985) pamoja na utambuzi wa nadharia ya Kitendo neni. Ingawa kazi ya King'ei imeeleza dhima ya kijamii na kiutamaduni katika nyimbo za taarabu nchini Kenya kazi yake haikushughulikia nyimbo za harusi kama utafiti huu ulivyokusudia kufanya. Utafiti huu ulilenga kuchunguza taashira za nyimbo za harusi, kisiwani Unguja. Kazi yake itasaidia kuchunguza uhalisia wa utendaji wa nyimbo za harusi unavyosaidia kupata maana kamili katika maisha kwa Waswahili, hasa wale waishio Unguja.

Topan (1995) alichanganua nyimbo za vugo ziimbwazo katika harusi za Waswahili wa Mombasa. Katika kazi hii alieleza kwa kina, jinsi sherehe ya vugo inavyotekelawa kulingana na muktadha wa tukio lenyewe. Pia alibainisha dhima ya nyimbo za vugo katika harusi yenewe. Tofauti katika kazi ya Topan na utafiti huu ni kuwa, kwanza kazi yake imejikita zaidi katika jamii ya Waswahili wa Mombasa tu. Pili Topan alichanganua nyimbo za vugo peke yake. Nyimbo ziimbwazo katika sherehe nyingine za harusi hakuzishughulikia kama utafiti huu ulivyofanya. Hata hivyo kazi yake ilituongoza kuona jinsi alivyochanganua nyimbo za vugo na kupata maana za maneno kutokana na matumizi ya lugha iliyotumika katika nyimbo hizo.

Mwamzandi (2000) katika makala yake alizungumzia utendaji, kanivali na uundaji wa maana za kijamii. Uchunguzi wake ulijikita zaidi kwa kutumia mifano kutoka taarabu za Waswahili. Ndani ya makala hii alijadili masuala mbalimbali ya kijamii yanayoibuka katika nyimbo za taarabu. Kazi ya Mwamzandi iliuhusiana na utafiti huu kwa sababu kazi zote zilitumia nyimbo

za taarabu. Ijapokuwa utafiti huu hulijikita zaidi na nyimbo za taarabu zilizoimbwa harusini tu pamoja na nyimbo za harusi. Hata hivyo tafiti mbili hizi zilitofautina vile vile. Utafiti wa Mwamzandi haukushughulikia matumizi ya taashira na upatikanaji wa maana za kitaashira zilizomo katika nyimbo za taarabu kama utafiti huu ulivyoazimia kufanya katika nyimbo. Ingawa haikujihusisha na nyimbo za harusi ilitufaa sana kwa upande wa utendaji na uundaji wa maana za kijamii kwa kutumia mifano kutoka nyimbo za harusi za Waunguja.

Ntarangwi (2001) katika kazi yake alijadili kwa undami taarabu kama utanzu wa muziki pendwa. Alijikita katika kuonyesha historia na maendeleo, miktadha ya utendaji, masuala ya kijinsia na nafasi ya dini katika nyimbo za taarabu za Waswahili. Katika uchanganuzi wake, alibainisha jinsi muziki wa taarabu unavyoweza kusaidia kueleza vitendo vyta utamaduni wa kijamii, jinsi marudio na mabadiliko ya desturi za jamii yanavyotokea, na jinsi tathmini binafsi za Waswahili wenyewe na jamii kwa ujumla zilivyo. Ingawa kazi ya Ntarangwi ilijihusisha na nyimbo za taarabu, baadhi yake zilikuwa nyimbo za harusi. Hata hivyo, bado kazi yake ilitofautiana na utafiti huu kwani suala la uchanganuzi wa taashira na utendaji katika nyimbo za harusi hakulitilia maanani. Isitoshe utafiti wake haukuonyesha ni vigezo gani vyta nadharia vilivyotumika katika uchanganuzi kupata maana za nyimbo.

Moshi (2002) alifanya uchambuzi linganishi wa kiisimu katika matumizi ya sitiari katika ngano na mashairi ya Kichaga. Katika utafti wake alichunguza mdafao wa utumizi wa sitiari na kuhitimisha kuwa sitiari sahir ndiyo yenyenye mdafao mkubwa kuliko sitiari nyingine katika ngano na ushairi wa Kichaga. Vile vile, anadai kuwa matumizi ya istiari yanategemea muktadha. Kadhalika amesisitiza kuwa tafsiri ifanyike ndani ya mazingira ya kitamaduni yanayounda mashairi na ngano za jamii husika.

Kazi ya Moshi ina husiana na kazi hii kwa sababu tafiti zote mbili zilichunguza tamathali za semi. Moshi alichunguza sitiri na utafiti huu ulichunguza taashira. Hata hivyo bado kuna tofauti na utafiti huu. Moshi aliangalia kipengele kimoja tu lakini utafiti huu ulichunguza taashira na utendaji katika nyimbo za harusi. Kadhalika tofauti nyengine ni kuwa utafiti wake ulijikita kuonyesha zaidi matumizi ya istiari bila kutilia maanani maana zinazoibuliwa kwazo kama utafiti huu ulivyoofanywa. Utafiti huu ulizingatia matumizi ya taashira, aina za taashira na maana

zilizoibuliwa wakati wa uwasilishwaji wa nyimbo. Hivyo katika kazi ya Moshi hakuonyesha ni jinsi gani lugha ilitumika katika ujenzi wa maana na ujumbe uliokusudiwa. Hata hivyo kazi yake ilikuwa na faida kubwa katika utafiti huu kwa sababu ilimsaidia mtafiti katika kuainisha na kubainisha semi hizo yaani taashira zilizojiteza katika nyimba za harusi.

Timamy (2002) alichanganua matumizi ya lugha ya nyimbo za harusi za wanawake Waswahili wa Mombasa. Timamy alijikita zaidi katika mitindo kwa vigezo vya fonolojia, msamiati, sintaksia, semantiki na utendaji (*paralinguistics*) katika nyimbo hizo. Uchanganuzi wa kazi yake umejikita kwenye Nadharia ya Uhakiki Miundo iliyotumiwa na Ngara (1985), mkabala wa Leech (1969) wa uchanganuzi wa lugha kifasihi na kiisimu, na mkabala wa Okpewho (1992) unaochunguza utendaji. Kwa kuzingatia nadharia na mikabala iliyotajwa, Timamy alifaalu kuonyesha matumizi ya maneno katika nyimbo za harusi. Ingawa kazi ya Timamy ilikuwa mwega kwa utafiti huu vipengele kadhaa havikushughulikiwa. Kwanza, kazi yake haikujishughulisha kuelezea maana za taashira ya (vitu na tendo) na umuhimu wake katika jamii aliyoishughulikia katika uchanganuzi wa nyimbo alizokusanya. Pili, haikujishughulisha kuchunguza utendaji wa nyimbo jinsi unavyoweza kusaidia kupata maana za taashira zilizomo katika nyimbo. Tatu, Timamy alichanganua nyimbo kwa jumla bila kuzingatia muktadha wa utendaji wa nyimbo hizo na matukio yanayoongoza kuimbwa kwake kwenye harusi. Isitoshe, kazi yake ilijengwa katika nyimbo za harusi za wanawake tu. Utafiti huu ulizingatia nyimbo za harusi zilizoimbwa na jinsia zote mbili, ili kuwakilisha jamii pana zaidi. Hata hivyo kazi yake ilitumika kama mwongozo katika kukusanya nyimbo za utafiti huu.

Mwamzandi (2002) alifanya uchunguzi kutafuta sababu za kupungua kwa michezo ya Kiswahili katika sherehe za drama za kitaifa za Kenya. Kulingana na uchunguzi wake alibaini kuwa mionganoni mwa sababu zinazopelekea kupungua kwa michezo hiyo ni uandishi na uwasilishaji. Nadharia iliyomwongoza kufikia malengo haya ni N.U.

Mwamzandi alitumia mitazamo yote miwili ya N.U. Mtazamo wa kwanza ni ule unaoangalia utendaji kama njia ya mawasiliano. Katika mtazamo huu, utendaji huonekana kama uwasilishaji wa dhana dhahania zinazoweza kutendwa mbele ya hadhira. Kwa mujibu wa utafiti wake, dhana hizo huwa katika maandishi na kisha zikawasilishwa jukwaani. Kama asemavyo Reid (1965),

mchezo wa kuigiza juu ya jukwaa ni zao la matini iliyomo katika maandishi. Kulingana na hoja hii, Mwamzandi alichanganua mbinu za uandishi zinazotumiwa na waandishi wa michezo ya kuigiza ya Kiswahili inayowasilishwa katika sherehe za drama za kitaifa za Kenya. Maandishi ya michezo ya kuigiza ndio huamua kwa kiasi kikubwa muundo wa utendaji na mbinu zitakazotumika kupitisha ujumbe jukwaani.

Mtazamo wa pili alioutumia ni ule unaoangalia utendaji kama jamii drama. Katika mtazamo huu utendaji unachukulia kama sehemu ya maisha na unahuishwa na hatua nne, ambazo ni: (i) Kuvunjwa kwa mahusiano ya kijamii (ii) Mgogoro (iii) Juhudi za kupata suluhisho na (iv) Kupatikana ama kukosekana kwa suluhisho. Utendaji ni zao la hatua ya tatu ya mfumo wa maisha ya kijamii ambapo uigizaji hunuiwa kutafuta suluhisho kwa uozo ulioko katika jamii. Aidha hatua hizi nne zilitumiwa na Mwammzandi (2002) kama kigezo cha uchanganuzi kwa ajili ya kutathmini miundo ya michezo ya kuigiza. Uchunguzi huo wa Mwamzandi ulikuwa na umuhimu katika utafiti huu. Kwani kazi yake ilitoa mwangaza wa jinsi ya kutumia N.U. Hata hivyo, utafiti huu ulizingatia tu mtazamo wa kwanza wa utendaji unaoangalia utendaji kama njia ya mawasiliano.

Umuhimu wa utendaji umeelezwa pia kwa muhtasari, katika kazi ya Khamis (1981). Khamis alihuisha umuhimu wa utendaji kwa kurejelea utanzu wa sanaa za maonyesho. Maoni yake kuhusu utanzu huu ni kwamba "... matendo hupewa umuhimu zaidi" Akiendeleza hoja yake hii, anasisitiza kwamba, vitendo katika utanzu huu husaidia kujenga ujumbe utolewao. Aidha alielezea umuhimu wa utendaji uliopo katika ngoma, majigambo na shughuli za ibada. Hoja yake ni kwamba, mambo yote haya hufanyika vizuri panapokuwa na vitendo. Ijapokuwa kazi yake haikujishughulisha na utendaji au uwasilishwaji wa nyimbo za harusi kama utafiti huu ulivyokusudia. Kazi yake inatoa mwangaza wa jinsi utendaji ulivyo na umuhimu na unaweza kuzingatiwa katika utanzu wa nyimbo. Uzingativu huo uliweza kusaidia utafiti huu kuchunguza uwasilishaji wa nyimbo ili kupata maana za taashira.

Khamis (2004) naye alijadili juu ya namna washairi wa taarabu za Kiswahili wanafikisha vitu, dhana, tamathali za semi, ishara na nahau ili kujenga taswira halisi ya sura mbalimbali za mapenzi, mchakato wa mapenzi na hali ya mapenzi. Kazi ya Khamis inahusiana na utafiti huu kwa kiwango fulani kwa sababu ilichunguza mambo kadhaa ikiwemo tamathali za semi ziimbwazo katika taarabu kama vile taashira. Aidha, tafiti zote mbili zinaonyesha jinsi taashira

kama kipengele cha lugha kilivyotumika kusawiri hali ya mapenzi katika nyimbo za harusi na zile za taarabu ziimbwazo harusini.

Tofauti iliopo kati ya kazi hizi mbili ni kwamba utafiti wa Khamis haukujadili suala la matumizi ya lugha katika nyimbo za taarabu ziimbwazo harusini, pengo ambalo utafiti huu umejaribu kuliziba kwa kuchunguza matumizi ya lugha katika nyimbo za harusi na za taarabu. Hata hivyo utafiti wa Khamis ulifaa sana kazi hii kwa sababu ultupatia njia ya kuonyesha jinsi taashira zilivyochanganuliwa kwa lengo la kujenga taswira ya hali ya mapenzi ijapokuwa katika muktadha tofauti. Mtafiti alifaidika nayo katika kudhihirisha hali ya mapenzi katika taarabu na nyimbo za harusi. Aidha aliweza kupendekeza matumizi ya taashira nyengine zilizoibuliwa katika nyimbo ziimbwazo harusini zikiwemo za taarabu kuelezea mambo mengine zaidi ya mapenzi.

Omari (2006) katika makala yake juu ya mitindo na matumizi ya lugha katika muziki wa kizazi kipyta Tanzania, alibainisha jinsi wasanii wa muziki wa kizazi kipyta wanavyotumia lugha katika kazi zao. Amebainisha matumizi ya lugha ya majigambo, nyimbo za watoto, kuchanganya lugha, lafudhi mbalimbali, taswira, misemo, tashtiti, lugha isio tafsida, tanakali sauti, methali, takriri, sitiari, tashbiha, na utohoaji wa maneno. Kazi ya Omari inahusina na utafiti huu kwa kiwango fulani kwa sababu ilichunguza semi zilizotumika katika muziki kama utafiti huu ulivyochunguza matumizi ya taashira. Tofauti iliopo kati ya kazi hizo mbili ni kwamba utafiti wa Omari hakuonyesha ni jinsi gani lugha inatumika katika ujenzi wa maana na umuhimu wake katika jamii. Aidha ye ye alidhihirisha tamathali za semi katika muziki wa kizazi kipyta lakini utafiti huu ulijishughulisha na semi zilizoko katika nyimbo za harusi.

Utafiti wa Omari uliifaa sana kazi hii kwa sababu ultumia semi mbalimbali ijapokuwa katika muktadha tofauti. lakini ilimsaidia mtafiti kutmia njia aliyyotumia katika kudhihirisha jinsi semi zilivyobainishwa na kutumika katika nyimbo za harusi.

Jilala (2008) alishghulikia nyimbo za muziki wa kizazi kipyta huku akichunguza jinsi wasanii wanavyotumia sitiari kisanii katika ujenzi wa maana na ujumbe. Katika utafit wake, alihitimisha kuwa sitiari pana ndiyo yenye mdafao mkubwa zaidi ya sitiari sahir na changamano. Hii ni kwa

sababu nyimbo za kazazi kipyä hutumia vipengele tamathali za semi kisanii katika kujenga maana na ujumbe. Vili vile anaongezea kwa kusema kuwa sitiari hutumika katika kujenga dhamira mbalimbali zitokanazo na maana na ujumbe zilizoibuliwa kutokana na kazi ya fasihi. Jilala anamalizia kwa kusema kuwa muktadha wa utumizi, uzoefu, maarifa, ujuzi na utamaduni wa jamii iliyomlea msanii na hadhira yeke ndiyo huiongoza katika tafsiri ya maana ya tamathali za semi zilizotumika na ubunaji wa kazi ya fasihi.

Pamoja na hayo, kazi ya Jilala ilihusiana na utafiti huu kwa vile ilidhihirisha maana na ujumbe unaopatikana katika tamathali za semi zilizobainishwa katika muziki wa kizazi kipyä kama ulivyobinsha utafiti kuhusiana na nyimbo za harusi. Kwa upande mwingine kazi hiyo inatofautiana na utafiti huu kwa sababu ilishughulikia istiari kama matumizi ya lugha katika nyimbo za kizazi kipyä ilhali mtafiti huyu aliazimia kuchunguza taashira pamoja na utendaji wake unaofanyika wakati wa uwasilishwaji wa nyimbo za harusi hususani kisiwani Unguja.. Hata hivyo, kazi hiyo ilisaidia utafiti huu katika kutoa mwongozo wa jinsi uchanganuzi wa kupata maana na ujumbe ulivyofanyika kutokana na vipengele vya lugha vilivyobainishwa.

Alhabib (2012) katika kazi yake alichunguza matumizi ya lugha katika taarabu. Sababu ya kukuchunguza matumizi ya lugha imejengwa kotokana na ile hoja kuwa, lugha ina vipengele mbalimbali ambavyo wasanii huvitumia ili kuwasilisha ujumbe katika jamii. Alhabib alichunguza baadhi ya vipengele vilivyotumika katika taarabu kama vile sitiari, tashbiha, ishara, twaswira, misemo na methali kwa lengo la kuona ni jinsi gani vipengele hivi vinatumwa na wasanii wa taarabu katika kujenga maana na kuwasilisha ujumbe wa kazi za fasihi. Kadhalika utafiti wake umebaini kuwa dhamira mbalimbali huibuliwa na vipengele vya lugha vinavyotumika. Matokea ya utafiti wake yamebainisha kuwa mashairi ya taarabu hutumia vipengele vya lugha kwa dhima maalumu, hivyo uteuzi wa vipengele fulani vya lugha hufanyika kwa lengo maalumu. Uchanganuzi huu umempelekea kujenga hoja kuwa, katika taarabu, maana na ujumbe hujikita katika lugha.

Kazi ya Alhabib inahusiana na utafiti huu kwa kiwango fulani kwa sababu ilichunguza semi zilizotumika katika taarabu kama utafiti huu ulivyochunguza matumizi ya taashira. Aidha, kazi zote mbili hizi zilijadili kuwa maneno yanayotumika katika taarabu na nyimbo za harusi hubeba maan nasibishi. Tofauti iliopo kati ya kazi yake na utafiti huu ni kwamba, utafiti wa Alhabib

haukujikita kuonyesha aina za vipengele vya lugha alivyovishughulikia na kutumika kwake katika kutoa maana na umuhimu wake katika jamii kwa sababu vilikuwa vingi. Haya ameyakiri mwenyewe katika uk vii wa kazi yake. Aidha yeze alidhihirisha tamathali za semi katika taarabu ziimbwazo katika kumbi za starehe zaidi lakini utafiti huu ulijikita zaidi kuchunguza aina za taashira na utendaji wake katika nyimbo za harusi tu.

Utafiti wa Alhabib ulifaa sana kazi hii kwa sababu ultoa mwongozo katika kutoa maana na ujumbe wakati wa uchanganuzi wa utafiti huu. Kwani kazi zote mbili zilibaini kuwa maana na ujumbe wa kazi ya fasihi haina hurejelezi wa nje na haijengwi na mfumo bali maana hutokana na lugha iliyotumika na mwandishi wala mazingira ya nje haya nafasi katika kujenga maana ya kazi za nyimbo za harusi wala taarabu.

Lugwiri (2011) katika kazi yake alichunguza masuala ya isitiari, taashira na tashibiha katika uwasilishaji wa dhamira katika utenzi wa Tambuka. uhakiki wa kimitindo. Utensi wa Tambuka ni mionganoni mwa tenzi ndefu na za jadi za Kiswahili. Utensi huu wenye beti 1150 unahu su tukio la vita baina ya Waislamu na Wakristo katika mji wa Tambuka vikiongozwa na Mtume Muhammadi(S.A.W) na mfalme Herekali mtawalia. Utensi huu ultungwa na Bwana Athumani bin Mwengo katika mwaka wa 1728. Utafiti huu ulihusu uhakiki wa kimtindo wa Utensi wa Tambuka. Kipengele cha kimtindo kilichoshughulikiwa ni tamathali za usemi hususan sitiari, taashira na tashibiha. Utafiti ulichunguza mchango wa tamathali hizi katika uwasilishaji wa dhamira ya Utensi wa Tambuka. Utafiti ulilenga kudhihirisha kuwa Utensi wa Tambuka una ukwasi wa sitiari, taashira na tashibiha na kwamba tamathali hizi ndizo mihimili ya dhamira ya utenzi huu.

Kazi ya Lugwiri inahusiana na utafiti huu kwa kiwango fulani kwa sababu ilichunguza semi ikiwemo taashira kama utafiti huu ulivyo chunguza matumizi ya taashira. Aidha, kazi zote mbili hizi zilijadili kuwa taashira hutumiwa na wasanii katika kutoa ujumbe na dhamira zilizokusudiwa kwa wanajamii. Tofauti iliopo kati ya kazi yake na utafiti huu ni kwamba, utafiti wa Lugwiri ulishugulikia utenzi wa tambuka tu ilihali utafiti huu ulijikita katika nyimbo za harusi

ziimbwazo katika matukio tofauti harusini. Aidha, utafiti huu ulishughulikia maana ya utendaji uliodhihirika wakati wa uwasilishwaji wa nyimbo jambo ambalo Lugwiri hakulizingatia.

Hata hivyo, utafiti wa Lugwiri ulifaa sana kazi hii kwa sababu ulitoa mwongozo katika uchanganuzi na kuonyesha kuwa taashira ni tamathali ya usemi wenyewe mlinganisho wa hulka. Hali kadhalika tumeweza kutambua kuwa taashira zinazotumiwa hasa zile zinahusu matumizi ya sehemu fulani za mwili wa binadamu kusimamia aidha mwili mzima au jambo fulani kuhusu maisha ya mtu.

## **2.3 Misingi ya Nadharia**

Nadharia ni mawazo , maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani (TUKI,2004). Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Semiotiki (N.S) pamoja na Nadharia ya Utendaji (N.U).

### **2.3.1 Nadharia ya Semiotiki (N.S)**

Semiotiki ni neno lililotoholewa kutoka neno lenye asili ya Kiyunani (semeon), lenye maana ya "sayansi ya ishara". N.S ni kielelezo cha mawazo ya Mwanaisimu wa Kiswizi, Ferdinand de Saussure (1857-1913), pamoja na Mwanafalsafa wa Kimarekani Charles S. Peirce (1839-1914). Mawazo makuu ya de Saussure kuhusu mtazamo wa kisemiotiki yalizingatia zaidi ishara za kiisimu katika kuangalia maana ya msingi au maana halisi bila kuangalia maana batini ya ishara husika.

Pierce (1977), anahuisha ishara na maana msingi na pia maana batini kwa kuegemea mantiki. Kwa mujibu wa Pierce, maana ya msingi ni kile kilichomo katika matini. Maana batini husimbuliwa na mpokezi kwa kufasili namna matini husika ilivyosawiriwa. Anaendelea kusema kuwa, maana hizi huingiliana kiasi kwamba hakuna mipaka mwafaka inayoweza kuwekwa waziwazi kuzipambanua. Hoja hii inaungwa mkono na Voloshinov (1973) ya kuwa, maana ya msingi ni gari la kusafirisha fasili za maana batini na nasibishi, hivi kwamba ung'amuzi na ufasili wa maana hizi hauwezi kutenganishwa.

Chandler (1994) akimnukuu Bathes (1973) na Eco (1976) alieleza kwamba:

Semiotiki hudhamiria kuchukua mfumo wowote wa viashiria, picha, ishara za viungo vya mwili, sauti za kimuziki, vitu na mahusiano tata ya hivyo vyote, ambayo huunda miviga ... utumbuizaji ambavyo kwa kiasi fulani huunda mfumo wa kutoa maana.

Wananadharia hawa walibaini kuwa, semiotiki huchunguza kila kitu kinachoweza kuchukuliwa kama viashiria. Wanasemiotiki mamboleo huchunguza viashiria na maana zake kwa njia ya kuhifadhi uhalisia.

Chandler (1994) anaeleza kuwa, semiotiki mara nyingi hutumika katika uchanganuzi wa matini na kwamba, matini inaweza kuwa njia yoyote ya kuwasiliana, iwe ya usemi au isiyo ya usemi au zote mbili. Matini mara nyingi hurejelea ujumbe ambao umerekodiwa kwa njia yoyote ile, kama vile, kimaandishi, sauti, au picha zilizonaswa. Matini ni mkusanyiko wa viashiria kama vile maneno, picha, au taashira za viungo vya mwili vilivyoundwa na kufasiriwa kwa mujibu wa sheria zinazohusiana na utanzu na hususani njia ya mawasiliano.

Chandler anasisitiza kwamba, semiotiki ni muhimu kwa sababu husaidia kufikia uhalisia. Hufunza kuwa, uhalisia ni mfumo wa viashiria. Kujifunza semiotiki husaidia kupata ufahamu juu ya uhalisia na kutambua kuwa, taarifa au maana haipatikani vitabuni, katika kompyuta au mitambo ya kuona na kusikiliza. Maana haziwasilishwi kwetu bali tunazibuni kulingana na maingiliano tata ya misimbo ambayo kwa kawaida huwa hatuna habari nayo.

Moriaarty's (ht) anaeleza jinsi Nadharia ya Semiotiki (N.S) inavyoweza kutumika katika kazi zisizokuwa za kifasihi. Moriaarty's, anatoa taarifa kuwa semiotiki imewahi kutumika katika nyanja mbalimbali kama vile: filamu, elimu vuimbe, matibabu, sosholojia, vyombo vya habari, biashara utamaduni, biolojia na isimu. Katika kazi yake alifafanua zaidi jinsi gani semiotiki huchunguza mawasiliano ya kuona (visual communication). Ingawaje kazi ya Moriaarty's ilitoa maelezo juu ya ufaafu wa kutumia N.S lakini hakubainisha ni misingi ipi ya nadharia hii itakayomwongoza mtafiti katika uchanganuzi.

Lawes (ht), katika kazi yake alipendekeza miongozo ya kuzingatiwa kwa mhakiki yejote anayetaka kutumia N.S. Kwa mujibu wa maelezo yake alipendekeza kwamba, ni vyema mhakiki

ajiulize maswali kadhaa kama vile:- (a) Semiotiki ni nini na itamsaidia vipi? (b) Semiotiki inafanya kazi namna gani? (c) Ni namna gani unaweza kuhakikisha kwamba matokeo ya semiotiki yatakayopatikana baada ya utafiti ni ya kweli na hayatokani na hisia za mtu binafsi? Lawes anayachukulia kuwa ni maswali haya dira kwa mhakiki katika kumwongoza na kufahamu jinsi N.S. inavyofanya kazi.

Kazi nyingine inayoeleza Semiotiki ni ile ya Wamitila (2002). Katika kazi hii, mwandishi anaeleza masuala mbalimbali ya kinadharia ya uhakiki na waasisi wa nadharia hizo. Miongoni mwa matapo ya kifasihi na nadharia za kihakiki alizozishughulikia ni pamoja na usasa na usasakale, uhalisia, umuundo na umuundo leo, udenguzi, narojzia, umarx, uhakiki wa mtazamo wa-Bakhtin, uhakiki wa mtazamo Foucault na semiotiki. Kuhusu semiotiki Wamitila amejaribu kufafanua kwa kina vipengele muhimu vya kinadharia ambavyo msomaji na mhakiki wa fasihi anapaswa kuvifahamu. Vipengele hivi vimeelezwa kwa njia rahisi. Baadhi ya vipengele vya kisemiotiki vilivyofafanuliwa ni kama vile ishara, yambwa, kifasiri, ishara kielekezi, ishara-tanakali, taashira na misimbo. Wamitila amejaribu kuonyesha nafasi ya vipengele hivi katika uwanja huu wa N.S. Utafiti huu kwa kiasi kikubwa umefaidika kuelewa jinsi gani vipengele hivi hufanya kazi vinapotumiwa na N.S.

Wamitila (ameshatajwa) anabainisha kwamba, mbali ya kuwa N.S ni nadharia yenyе historia ndefu, nadharia hii imetumika kuelezea mielekeo na mitindo wa kazi za kifasihi ambao unachunguza taashira katika kazi hizo. Kimsingi, hii ni nadharia inayoshughulika ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Suala la ishara na uashiriaji limeanza kuwa muhimu katika uhakiki wa kifasihi katika miaka ya karibuni (Culler, 1981). Nadharia ya Semiotiki katika kufafanua suala la uashiriaji, hudhihirisha jinsi kazi hizo zinavyowasiliana na wasomaji.

Nadharia ya Semiotiki haisisitizi masuala ya kufasili au jinsi tunavyofasili kazi fulani tu, bali pia inahusu usomaji wetu wa kazi na kuiuliza kwa nini kazi hizo huwa na maana zilizonazo kwa wasomaji tofauti. Jamii moja huweza kutumia taashira za aina sawa na kuelewana katika ufasili wa maana na ujumbe. Hata hivyo, katika jamii hiyo hiyo ufasili hutofautiana kwa watu binafsi. Kwa mfano neno "mvinyo" huweza likatoa wazo au taashira tofauti miongoni mwa watu wenye tajriba tofauti ndani ya jamii ileile. Wahakiki wa Chuo Kikuu cha Yale – Geoffrey, Hill, Paul na

Horold wakinukuliwa na Blamires (1991), wanaeleza kuwa, kuna uwezekano wa matini kuwa na fasili nyingi zinazolingana au kukinzana na zote zikakubalika. Mhakiki ana wajibu wa kufasili ishara au taashira za kisanaa na kiisimu ili kuweka wazi kilichofichika.

Wahakiki wengine wanaoendeleza hoja hii ya Semiotiki katika uhakiki ni Tordova (1983), Barthes (1973, na 1984), Eco (1977) na Chandler (1994). Barthes ameweka misingi mikuu ya N.S kwa njia ya kutumia msimbo (mhimili). Kwa mujibu wa Barthes, msimbo ndio nguzo au kanuni ambayo huwa muhimu katika kufasili kazi fulani. Hivyo mhimili iliyotumika katika utafiti huu ni **Msimbo wa Matukio (Proairetic Code) na Msimbo wa Kihementiki (Hermeneutic Code)**.

**(A) Msimbo wa Matukio (Proairetic Code):**

Huu ni mhimili unaohusu jinsi matukio yanavyopatikana katika kazi ya kifasihi. Kazi ya mhimili huu, ni kutoa maelezo ya msingi ya kazi ya kifasihi ambayo hufanya usuli wa kazi na mazingira yake kufahamika. Ili kufahamu vyema mambo muhimu yanayofanya usuli wa kazi na mazingira kufahamika, utafiti ulihitaji kufanya mambo yafuatayo:

- (i) Kuandika maelezo yaliyotolewa na wahojiwa yanayohusu taratibu za ndoa na sherehe katika harusi za

Waswahili. Maelezo hayo ni kama vile: sherehe ya harusi hupitia hatua zipyi, ni jambo gani linalotendeka katika kila hatua, ni hatua zipyi zinazopewa umuhimu na wenyeji.

- (ii) Kuchuja maelezo ya wahojiwa hayo na kutenganisha yale ambayo yalihitajika na yasiyohitajika.

- (iii) Kuandika maelezo yaliyohitajika pekee kuhusu ndoa na sherehe katika harusi. Maelezo haya yalitumika

kama msingi wa kuelewa uchanganuzi na jinsi nyimbo zilivyopatikana harusini.

**(B) Msimbo wa Kihementiki (Hermeneutic Code):**

Msingi wa mhimili huu unasisitiza kwamba, neno au maneno katika mfumo wa lugha hutoa fununu ya maana ya neno au maneno. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), majina ya kazi za kifasihi hutoa fununu za maana au dhamira za kazi hizo. Mhimili huu uliongoza utafiti kutambua taashira zilizomo katika nyimbo zilizokusanywa. Taashira hizo zilitambuliwa kwa kufuata mfumo wa uchanganuzi ufuatao:

- (i) Kuandika kwenye daftari nyimbo zote zilizokuwa zimerekodiwa.
- (ii) Kuchunguza na kuchuja nyimbo zote zilizonukuliwa kwenye daftari iwapo zimebeba taashira.
- (iii) Kutambua, kudondoa na kubainisha taashira katika nyimbo hizo. Utambuzi, udondozi na ubainishaji ulifanywa kwa kuangalia na kupiga mstari neno au maneno yanayokisiwa kuwa ni taashira katika nyimbo. Neno au maneno ambayo husimamia tendo au kitu kingine ambacho kimetajwa katika nyimbo. Neno (taashira) hili hubeba maana ya kitaashira.
- (iv) Kuziorodhesha taashira zilizodondolewa.
- (v) Kuziainisha na kuziweka taashira zilizoorodheshwa kulingana na aina zake kama vile: taashira za vitu na taashira tendo.

Hivyo basi, kulingana na mwongozo wa N.S kupitia - mhimili/msimbo wa matukio na kihementiki kama hatua ya kwanza, ulisaidia utafiti kupata mambo mawili. Kwanza, mhimili/msimbo wa matukio uliwezesha kupata maelezo ya msingi kuhusu ndoa na harusi. Pili, mhimili/msimbo wa kimehentiki ulisaidia kubainisha taashira zilizomo katika nyimbo. Baada ya kupata maelezo ya msingi kuhusu utaratibu wa ndoa na harusi na kubainisha taashira, ilifuata hatua ya kupata maana ya taashira kulingana na utendaji wa wimbo husika. Taashira zilizobainishwa zilitolewa maana ya kawaida na maana ya kitaashira. Maana hizo zilitolewa kulingana na aina ya taashira zenyewe kama zilivyojitokeza katika wimbo husika. Kwa hiyo, utafiti ulilazimika kutumia Nadharia ya Utendaji, ili kuweza kupambanua maana za taashira katika nyimbo hizo.

### **2.3.2 Nadharia ya Utendaji (N.U)**

Mtafiti alitumia Nadharia ya Utendaji (NU) ili kutosheleza mahitaji ya madhumuni ya tatu, kubainisha utendaji wakati wa uimbaji nyimbo harusini. Hivyo ni kwa sababu ili kupata utendaji lazima maana itambulikane na NU na kanuni zake ndizo zinazoweza kumwonyesha mchanganuzi matendo yanavyofanyika wakati wa uwasilishwaji nyimbo katika miktadha maalumu. Utendaji ulioambatana na taashira wakati wa kucheza na kuimba. Utendaji katika matukio yanayoashiria mambo ya kitaashira wakati wa uimbaji pamoja na utendaji wa uigizaji wa vitu vya bibi harusi wakati wa kuimba nyimbo unafasiriwa kutokana na jinsi vipengele

maalumu vyatutendaji vinavyotumika katika muktadha maalumu na kupewa maana maalumu. Kwa mfano utendaji wa "kupiga makofi" au "kupara samaki" katika wimbo tutajuaje utendaji huu una maana gani?

Nadharia ya Semiotiki kwa hiyo, ilijalizwa na Nadharia ya Utendaji. N.U ndio inayounganisha aina zote za utendaji katika taaluma moja pana ya utendaji (Schechner na Appel, 1995). Nadharia hii inahusiana na sanaa za utendaji kama vile ngoma, nyimbo, maonyesho, muziki, michezo ya kuigiza na matambiko.

Wananadharia wanaoshughulikia utendaji wameshikilia mitazamo miwili. Mtazamo wa kwanza ni ule unaoangalia utendaji kama njia ya mawasiliano (Bauman, 1977 na Fine, 1984). Mtazamo wa pili unaangalia utendaji kama jamii drama. Katika mtazamo huu wa pili, utendaji unachukuliwa kama sehemu ya maisha. Kwa mujibu wa Turner (1990), utendaji kama jamii drama huwa na hatua au sehemu nne:-

- (i) Kuvunjwa kwa mahusiano ya kijamii. Kwa mfano kuwe na tatizo linalotatiza.
- (ii) Mgogoro – tatizo hilo liletumushkeli na msukumo wa kutaka kuondoa tatizo hilo.
- (iii) Juhudi za kupata suluhisho – namna ya kusuluhisha tatizo. Kwa mfano utekelezaji wa mambo yanayotarajiwaa yataleta suluhisho.
- (iv) Kupatikana ama kukosekana kwa suluhisho.

Mtazamo unaoangalia utendaji kama jamii drama hutumika sana na watunzi wa tamthilia na riwaya. Pia hutumika katika sanaa za maonyesho. Hata hivyo, utafti huu ulijikita zaidi kutumia mtazamo wa kwanza unaoangalia utendaji kama njia ya mawasiliano.

Katika mtazamo wa utendaji kama njia ya mawasiliano, utendaji huonekana kama uwasilishwaji wa ujumbe kwa njia ya kutenda mbele ya hadhira ukitumia ishara zinazokubalika (Bauman, 1977). Kwa mujibu wa utafiti huu, ujumbe huo huwa katika ubongo wa mtunzi. Kulingana na maoni haya, mtafiti alijihuisha na uchanganuzi wa taashira na utendaji katika nyimbo za harus. Utendaji wakati wa uimbaji, ulisaidia kupambanua maana za taashira katika nyimbo.

Kwa mujibu wa Finnegan (1992) mkabala wa utendaji humulika maingiliano kati ya usanii wa mtu binafsi na matarajio ya kitamaduni. Hutoa changamoto kwa watafiti kuchunguza michakato ya utendaji katika hali mbalimbali, fikra na matendo yenye kuhusiana nayo.

Utendaji pia hurejelea hasa tukio litokealo katika kipindi maalum. Pamoja na mambo mengine, utendaji huangazia zaidi matukio yenyewe yanavyowasilishwa. Maswala ya kuchunguza kwa mujibu wa mkabala huo ni - jinsi na wapi matendo kama matukio halisi yanavyopangiliwa na kuandaliwa; ni akina nani waliopo; silka zao na matarajio yao yakoje; jinsi utendaji unavyowasilisha tanzu mahususi na namna hadhira inavyochukulia uwasilishaji huo; namna unavyorandana au kujitenga na maisha ya kila siku.

Maoni ya Finnegan (1992) kuhusu mtazamo wa utendaji kama njia ya mawasiliano pia yalisaidia kupata maana ya taashira kutokana na uwasilishwaji/utendaji wake. Kwa kuzingitia maoni ya Finnegan, utafiti ulichunguza baadhi ya vipengele ambavyo vinahusiana na uwasilishwaji wa nyimbo katika sherehe za harusi za Waswahili. Vipengele vilivyocheinuza ni pamoja na uhalisia wa utendaji, maleba, mazingira na mandhari na mwisho muktadha wa kijamii. Kutokana na uchunguzi wa vipengele hivyo juu, mtafiti aliweza kuelewa kwa undani jinsi nyimbo hizi zinavyotekeliza jukumu lake katika sherehe za harusi.

Finnegan akifafanua zaidi umuhimu wa nadharia hii anaeleza kuwa, N.U imewavutia sana wananthropolojia na wanasanaa jadiya wa Kimarekani na humulika hasa mambo yafuatayo:-

- (i) Umuhimu wa utendaji wa matini yoyote au sanaa ya usemi ambayo sanaa zinazowasilishwa na ushiriki  
wa hadhira ni kiambajengo muhimu.
- (ii) Kusisitiza matukio ya kimawasiliano.
- (iii) Maadili ya kitamaduni yanayojitekeza na pia tanzu mbalimbali katika utendaji.

Utendaji unaweza kuchukuliwa kama muundo wa ndani wa tamko. Hivyo N.U humuwezesha mtafiti ye yote yule kuzingatia mambo yafuatayo:-

- Maana na usanii ujitekezao katika utendaji ambapo mtafiti anapaswa kuzingatia sio tu maneno pia jinsi yanavyowasilishwa. Vipashio kama vile: toni, kiimbo, kasi, uigizaji, mbinu za kibalagha/jazanda na mbinu za utendaji kwa jumla zinapaswa kuzingatiwa.
- Sehemu ya ukweli ambayo hupatikana kutokana na kuingiliana na, au tabia ya washiriki wote wakiwemo hadhira na matarajio yake na pengine mtafiti pia.
- Ufanuzi na maana maalumu za tanzu mbalimbali za fasihi simulizi huweza kutegemea sio tu mitindo ya kisemi bali pia vipengele visivyo na sifa za kisemi kwa mfano: - muziki,

utumiaji wa ishara, kucheza na maleba. Sifa au vipengele hivyo ni muhimu kuchunguzwa.

- Fani za kimasimulizi hupatikana kupitia utendaji unaojengwa na watu. Kwa hivyo maingiliano ya sanaa na sheria za kitamaduni ni mionganini mwa mambo mengine muhimu ya kuchunguzwa.
- Muktadha wa kiutendaji unaweza kuwa muhimu kwa kuelezea maana.

Vipengele hivi vilitoa mwangaza zaidi wa jinsi utafiti ulivyoweza kutumia N.U. Hivyo basi, kulingana mihimili ya N.U kama njia ya mawasiliano uliongoza utafiti huu kuchunguza baadhi ya vipengele vinahusiana na uwasilishwaji wa nyimbo harusini kama vile:

- Uhaliasia wa utendaji
- Maleba,
- Mazingira
- Muktadha wa kijamii.

Vipengele hivyo hapa juu vilisaidia kuelewa kwa undani jinsi nyimbo hizi zinavyotekeleza jukumu lake katika sherehe za harusi. Vilevile vilisaidia kupambanua maana za taashira zilizomo katika nyimbo pamoja na maana za kitaashira zilizofungamana na utendaji wakati wa uimbaji.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.0 Utangulizi**

Sura hii imegawanywa katika sehemu mbili kuu. Sehemu ya kwanza imejadili juu ya ukusanyaji wa data na kuelezea mbinu zilizotumika, eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli na vifaa vya kukusanya data. Sehemu ya pili imejadili juu ya mfumo maalumu wa uchanganuzi wa data ambao ulikuwa kama mwongozo na kueleza jinsi data hizo zilivyochanganiwa katika sura ya nne na ya tano. Utafiti ulifanywa katika awamu tatu. Awamu ya kwanza ulijishughulisha na utafiti wa maktabani kwa kudurusu, na kupitia majorida, vitabu, na tafiti zenyekuhusiana na utafiti huu. Awamu ya pili utafiti, aliingia nyanjani kwa lengo la kukusanya data za msingi. Awamu ya tatu ilikuwa ni uchanganuzi wa data na kuandika taasnifu kamili.

#### **3.1 Ukusanyaji wa Data**

Utafiti ulitumia utaratibu wa nyanjani kwa lengo la kukusanya data za msingi. Mtafiti aliingia maeneo ya utafiti Unguja Mjini, Makunduchi na Tumbatu na kukaa na wenyiji kwa muda wa miezi sita (6) akifanya utafiti. Data zilizokusanya zilikuwa ni nyimbo na uwasilishwaji wake katika harusi. Lengo la kukusanya data hizi ni kwa ajili ya kupata taashira zilizomo katika nyimbo na utendaji. Maelezo ya kimsingi kuhusu taratibu za ndoa na sherehe za harusi za Waswahili Waunguja yalikusanya pia. Ufafanuzi wa maelezo kutoka kwa wasailiwa kuhusu maana za taashira katika nyimbo pia yalizingatiwa. Mtafiti alittuma maaelezo haya katika uchanganuzi wa data. Ukusanyaji wa nyimbo ulifanyika katika sherehe za harusi na nje ya sherehe za harusi. Pia kulikuwa na nyimbo ambazo, mtafiti alizirekodi kutoka kwa waimbaji na makungwi.

Data nyengine zilikusanya na watafiti wasaidizi wanawake wawili. Watafiti hawa waliweza kukusanya data alizozihitaji mtafiti katika sherehe ambayo ni mwiko kwa wanamume kushiriki. Kwa sababu watafiti wasaidizi ni wanawake, waliruhusiwa kuingia kwenye singo ya wanawake ambapo mtafiti asingeruhusiwa kuingia. Watafiti wasaidizi hawa waliteuliwa kwa kuzingatia sifa zifuatazo: Kwanza, walikuwa wamemaliza kidato cha nne katika mfumo wa elimu wa Zanzibar. Kiwango hiki kilizingatiwa kwa sababu, ilikuwa rahisi kwao kufahamu maelekezo waliyopewa na mtafiti, jinsi ya kutumia vifaa vya kukusanya data kisayansi. Pili, wasaidizi hawa walikuwa

wanafahamu vyema mila na desturi za sehemu inayofanyiwa utafiti. Kama anavyoeleza Chai (2003:23) mtafiti msaidizi bora ni yule anayetoka katika sehemu inayofanyiwa utafiti. Isitoshe awe ni mwenye kufahamu mila na desturi za watu wa eneo lile. Kwa msaada kutoka kwa watafiti wasaidizi, niliweza kukusanya nyimbo tisini (90). Mtafiti alichanganua nyimbo sitini (60) kati ya hizi. Hata hivyo, mbinu, uteuzi wa sampuli, eneo la utafiti na vifaa vilivyotumika wakati wa ukusanyaji imeelezwa hapa chini kama ifuatavyo:-.

### **3.1.1 Mbinu ya Uchunguzi - shiriki**

Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kushiriki katika uwasilishwaji kama mmoja wa hadhira na kurekodi nyimbo za harusi. Pia aliweza kushuhudia matendo kadhaa yaliyokuwa yakifanyika wakati nyimbo zilipokuwa zikiimbwa. Ingawa mtafiti alikuwa si Mzanzibari, alikubalika katika jamii hii, kwani panapokuwa na sherehe ya harusi au msiba huwa anashirikishwa kama mwenyeji.

Kwa msaada wa watafiti wasaidizi wanawake kushiriki na kuingia chumbani anamosingwa mwari, waliweza kushuhudia mambo yote anayofanyiwa mwari. Mambo hayo wangeweza kurekodi kwa kamera ya video ili baadaye wamletee mtafiti, lakini walikatazwa na wenye shughuli kupiga picha wala kurekodi kwa kamera ya video. Kwa mwongozo na maelekezo ya mtafiti, watafiti wasaidizi ilibidi watazame, kudasisi na pia kuhifadhi mambo yote waliyoshuhudia ya kitendeka wakati wa singo. Baada ya shughuli walimuelezea mtafiti mambo yaliyotokea katika sherehe hii. Mambo hayo, yaliandikwa kwenye daftari la mtafiti.

Mbali na sherehe ya singo, mbinu hii pia ilimwezesha mtafiti na wasaidizi wake kuandika mambo waliyoyaona na kuyasikia wakati wa harusi. Pia kuandika mambo ambayo yalikuwa na utendaji unaoashiria tendo la ndoa. Vile vile kwa msaada wa mbinu hii mtafiti alishuhudia kwamba, nyimbo nyingi za harusini huimbwa na wanawake. Lakini zipo nyimbo chache alizoshuhudia katika harusi huimbwa na wanaume pekee.

### **3.1.2 Mbinu ya Mahojiano**

Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano ambapo aliwasaili wahojiwa kuhusu taashira za nyimbo zilizoimbwa harusini. Alifanya hivyo ili aechezwe maana zaidi za taashira hizo. Mahojiano yalitumika pia kupata maoni na maelezo juu ya ndoa na sherehe katika harusi za Unguja

kulingana na utamaduni wao. Wahojiwa walisailiwa mmojammoja, ili kila mmoja aweze kupata muda au fursa kueleza analolifahamu.

### **3.1.3 Eneo la Utafiti**

Eneo la kijigrafia lililofanyiwa utafiti huu ni Kisiwa cha Unguja. Maeneo mahususi ya utafiti huu yalikuwa:-

- (i) Tumbatu                   (ii) Unguja Mjini                   (iii) Makunduchi.

Maeneo haya yamechaguliwa kwa sababu zifuatizo:-

Kwanza, wakaaji wa maeneo haya ni kiwakilishi cha jamii pana ya Waswahili waishio kisiwani Unguja. Haya ni maeneo yanayokaliwa na watu wengi ukilinganisha na wilaya kisiwani Unguja. Hivyo upatikanaji wa nyimbo za harusi ulikuwa rahisi kwa sababu harusi huanyika mara kwa mara katika maeneo haya.

Pili, Tumbatu ni makao makuu ya Wilaya ya Kaskazini B; Unguja Mjini ni makao makuu ya Wilaya ya Mjini na Makunduchi ni makao makuu ya Wilaya ya Kusini yaliyoko kisiwani Unguja. Haya ni maeneo yanayofikika kiurahisi kwa usafiri wa gari. Aidha kwa kuzingatia kigezo cha wakati na ubora wa kazi ya utafiti, maeneo yaliyochaguliwa yaliwakilisha maeneo mengine ya wakazi wa kisiwani Unguja.

## RAMANI YA KISIWA CHA UNGUJA



### Kifafanuzi

Maeneo ya fanyiwa tafiti kisiwani unguja .

Asili:<http://www.shoorttravel.com/zanzibarmap.html>

### **3.1.4 Uteuzi wa Sampuli**

Utafiti huu ulihitaji sampuli za aina mbili. Sampuli ya kwanza ni ya wahojiwa na sampuli ya pili ni nyimbo. Chai (2003) akimnuku Milroy na Milroy (1980, 1987) anaeleza kuwa, njia nzuri ya kuteuwa wahojiwa wanaofahamu vyema jamii yao ni ile ya mamlaka. Mtafiti alitumia njia ya mamlaka kuteuwa wahojiwa. Jumla ya idadi ya wahojiwa walioteuliwa ni ishirini na moja (21). Mtafiti aliwatembelea wahojiwa kama mgeni wa kawaida. Alifanya hivyo baada ya kuelekezwa kupitia kwa wenyeji wake katika kila eneo la utafiti. Kwa msaada wa wenyeji wake mtafiti alijitambulisha na kisha alieleza madhumuni ya matembezi yake kwa wahojiwa. Wengi wa wahojiwa hawakuwa na pingamizi walikubali kusailiwa. Ingawa wengine walikuwa wazito kutoa taarifa kwa ukamilifu, kwani mambo mengi ya harusi yalikuwa ni ya siri. Hata hivyo, taarifa alizozipata zilitosheleza kukidhi haja ya kile mtafiti alichokuwa akihitaji kuhusu utafiti huu.

Kipengele cha jinsia ilikuwa ni sifa mojawapo iliyozingatiwa na mtafiti kuteuwa wahojiwa. Wahojiwa hawa pia, waliteuliwa kwa kuzingatia uzoefu, uweledi na ufahamu wao wa kujua taratibu zinazoendeshwa katika harusi. Pia walikuwa wanaelewa maana za taashira zilizotumika pamoja na miktadha ya utendaji wa nyimbo ziimbwazo katika sherehe za harusi. Hata hivyo, mtafiti hakujishughulisha na kipengele cha umri wal kiwango cha elimu. Kwa sababu, kufahamu taratibu za harusi na kujua maana za taashira hakutegemei wahojiwa kuwa na kiwango fulani cha elimu.

Hata hivyo, maelezo yaliyotolewa na wahojiwa yalitoshelza na kumfanya mtafiti apate kila alichokihitaji. Ingawa utafiti ulifanyika katika maeneo tofauti ya kisiwani Unguja maelezo mengi yalionekana kufanana na ya mahali kwingine. Nyimbo zilizokuwa zikiimbwa katika tukio la singo zilikuwa ni zilezile zilizoimbwa Unguja Mjini, Tambatu na Makunduchi. Kama asemavyo Milroy "kundi la watu wachache walioteuliwa kama sampuli humwezesha mtafiti kupata habari za kina katika jamii pana kwa kile anachokitafiti kuhusiana na mada yake".(1987:84).

Sampuli ya pili ilikuwa ni nyimbo. Jumla ya nyimbo zilizokusanywa zilikuwa tisini (90). Kati ya hizi, ni nyimbo sitini (60) ndizo zilizochanganuliwa. Hizi ni nyimbo ambazo zilikuwa na matumizi ya taashira. Ingawa idadi ya nyimbo hizi inaonekana kuwa kubwa, haikuwa tatizo kwa mtafiti kuzikusanya. Hii imetokana na sababu kwamba, nyimbo nyingi zilizokusanywa zilikuwa

ni fupi zenyе mishororo michache. Utafiti huu haukujikita kuchunguza ukubwa au udogo wa nyimbo. Hivyo, mtafiti alikuwa na uhuru wa kukusanya nyimbo kadiri alivyoweza.

### **3.1.5 Vifaa vya Kukusanya Data**

Vifaa kadha vilitumika wakati wa ukusanyaji wa data. Vifaa hivyo ni pamoja na:-

#### **Kinasa-Sauti**

Mtafiti alitumia kinasa-sauti kurekodi mahojiano na nyimbo harusini. Wahojiwa walirekodiwa mmoja mmoja ili kila mmoja aeleze anayoyafahanu kwa uhuru. Mtafiti alikiweka kinasa-sauti karibu na wahojiwa na waimbaji ili aweze kunasa sauti kwa uhakika na vizuri. Maelezo ya wahojiwa yaliyorekodiwa yalisikilizwa. Mtafit aliyachuja na kuandika maelezo ya msingi katika daftari. Vilevile nyimbo zilizorekodiwa zilisikilizwa na baadaye kuandikwa katika daftari.

#### **Kamera ya Video**

Mtafiti alitumia kamera ya video si kurekodi nyimbo tu, bali hata jinsi nyimbo hizo zilivyowasilishwa harusini na utendaji wake. Mambo yaliyorekodiwa kwa kifa hiki yalichunguzwa baadaye. Mambo hayo ni kama vile: uimbaji wa nyimbo ulivyokuwa, waimbaji, matendo ya wachezaji, miondoko, matumizi ya viungo, mavazi waliyovaa na kadhalka. Mambo yote haya yalikuwa na umuhimu wakati wa uchanganuzi wa data ili kuweza kusaidia kupata maana za taashira.

#### **Daftari la Kuhifadhia Maelezo**

Daftari lilitumika kuandikia maelezo muhimu ya wahojiwa wakati wa mahojiano. Aidha, aliandika matendo aliyoshuhudia yakifanyika katika sherehe harusini. Kumbukumbu hizi ni muhimu kwa sababu zilimsaidia mtafiti kupata maswali ya kuwaliza wahojiwa kuhusu baadaye maana ya vitendo hivyo.

Mtafiti alikuwa na daftari lengine, ambalo ndilo lilitumika kunakili nyimbo zote zilizorekodiwa. Kwa kutumia daftari hili, mtafiti aliweza kudondo nyimbo zote ambazo zilikuwa na taashira na kisha kuzianisha kulingana na aina zake. Baada ya kupata data alizozihitaji alizitia katika kompyuta kwa ajili ya uchanganuzi.

Data za msingi zilizokusanywa nyanjani na baadaye kuchanganuliwa ni hizi zifuatazo:-

- (i) Nyimbo katika harusi za Waswahili Waunguja
- (ii) Maelezo ya kimsingi kuhusu ndoa na sherehe katika harusi.
- (iii) Taashira zilizomo katika nyimbo za harusi kulingana na utendaji na uwasilishwaji.
- (iv) Maelezo yaliyotolewa na wasailiya kuhusu maana za taashira na matendo yaliyofanyika wakati wa uimbaji.

Data zilizokusanywa zilichanganuliwa kimaelezo kwa kutumia mfumo maalumu wa uchanganuzi kama inavyoelezwa katika sehemu ya uchanganuzi wa data.

### **3.2 Uchanganuzi wa Data**

Data zilichanganuliwa kwa kufuata mfumo maalumu wa uchanganuzi ulioundwa. Mfumo huu ulikuwa na utaratibu na hatua za uchanganuzi zifuatazo:-

#### **Mfumo Maalumu wa Uchanganuzi wa Data**

Kwa kuzingatia baadhi ya mihimili ya Nadharia ya Simiotiki na Nadharia ya Utendaji yaliyobainshwa, utafiti umependekeza muundo maalumu wa uchanganuzi. Muundo ambao ultumiwa katika uchanganuzi wa data ulikuwa na taratibu wa hatua zifuatazo:-

#### **Hatua ya kwanza: Unukuzi**

Baada ya kukusanya data, mtafiti alifanya unukuzi kulingana na mambo yafuatayo:

Mtafiti aliandika maelezo aliyoypata kutoka kwa wahojiwa na vitabuni yanayohusu ndoa, sherehe, utamaduni na matumizi ya nyimbo za harusi za Unguja. Maelezo hayo yalihu hatua ambazo sherehe ya harusi hupitia. Pia yalihu mambo yanayotendeka katika kila hatua kulingana na harusi za Waswahili wa kisiwani Unguja. Mtafiti alichuwa maelezo ya wahojiwa. Aliyatenganisha maelezo aliyoahitaji na yale asiyoyahitaji. Maelezo ya kimsingi yaliyohitajika ndio yaliyoandikwa katika tasnifu hii.

Mtafiti aliziandika kwenye daftari nyimbo zote zilizorekodiwa harusini kwa kinasa-sauti na kamera ya video. Baada ya kufanya hivyo, alizichuja na kuzitenganisha nyimbo zenye taashira na zisizo na taashira. Wimbo uliokuwa na taashira ulipewa nambari na jina la ufupisho kulingana na muktadha wa tukio harusini.

Tazama mifano ya nyimbo zenyе majina na vifupisho vyake zilizoimbwa katika miktadha mbalimbali harusini.

**(MMH) MUKTADHA WA KUPELEKA MAHARI**

MMH.1. Mnganamba

MMH.2. Jahazi

MMH.3 Nataka Tambuu

**(MKH) MUKTADHA WA KUALIKA HARUSI**

MKH.1. Nitumwa na Mama

**(MSG) MUKTADHA WA SINGO**

MSG.1. Bisumillahi

MSG.2. Usilie

MSG.3. Kisiki

**(MKN) MUKTADHA KABLA YA NIKAHA**

MKI.1. Kinyemi cha Mwana

MKN.7. Mama Njoo

MKN.9.Kula Muhugo

**(MBN) MUKTADHA BAADA YA NIKAHA**

MBN.2. Bibi Aingile Chooni

MBN.6. Furaha

**(MKND) MUKTADHA WA KUINGIA NDANI**

MKND.1. Daktari Yuwaja

MKND.2. Wembe

MKND.4.Usiche Bwana Harusi

**(MHK) MUKTADHA HARUSI KUJIBU**

MHK.1. Koko

MHK.4. Hongera Mwanangu

MHK.7. Kimenichoma

(MKU) MUKTADHA KUINGIA UKUMBINI

MKU.1. Masomaso

MKU.3. Tumejizungua

(MKS) MUKTADHA WA KUKABIDHI SANDUKU

MKS.1 Sasambu

Vifupisho na majina ya nyimbo nyengine zilizokusanywa zimeorodheshwa katika kiambatisho cha II.

### **Hatua ya Pili: Kutambua na Kubainisha Taashira katika Nyimbo**

Katika hatua hii, mtafiti alizipitia nyimbo zote. Alifanya hivi ili aweze kuzitambua na kuziainisha taashira zilizojitokeza katika kila wimbo. Utambuzi huu ulifanyika kwa kupigia mstari maneno kwenye nyimbo ambayo yaliaminika yanasmamia taashira za tendo au kitu kingine. Nyimbo tatu hizi MMH.1, MKN 8 na MKN 9 zimetumiwa kuonyesha jinsi taashira zilivytambuliwa katika nyimbo hizo.

*MMH.1 MNGANAMBA*

*Mnganamba katumba kadogo,*

*Mwana huyu kamzaa nani? eeee!*

*Mwana huyu kamzaa nani?*

*Kidomo katiti kama kasiba*

*Chenye mwanya kati mbwake haiba*

*Ndiye mke siti mwenye mahaba*

*Atwazaye watu mahadharani.*

....

*MMH.2 JAHAZI*

*Jahazi yetu twaipeleka kwa pepo njema.*

*Nenda mwanangu amana Llahu Aman Rasuli.*

*MKN.8 KITAMCHOMA*

*Kitamchoma eee kitamchoma*

*Kisiki cha mpera*

*Wapi?*

*Hapa*

*Patie dawa sana pasije pakabana  
Pakamkera bwana  
Usiku na mchana*

*MKN.9 KULA MUHOGO  
Kula muhogo,  
Kula muhogo,  
Utauona utamu wake kula muhogo,  
Utauona utamu wake kula muhogo*

....

Maneno yaliyopigiwa mstari katika nyimbo hizi hapa juu ndio yaliyotambuliwa kama taashira.

### **Kuzainisha Taashira Zilizotambuliwa Kulingana na Aina zake**

Utambulisho wa taashira katika nyimbo, ulimrahisishia mtafiti kuzidondoa na kuziweka taashira kulingana na aina zake. Kwa mfano, taashira zilizoibuliwa katika nyimbo MMH.1. Mnganamba, MMH.2. Jahazi, MKN.8. Kitamchoma na MKN.9. Kula Muhogo ziliainishwa na kuwekwa katika taashira za vitu na taashira za tendo. Hata hivyo, nyimbo nyengine ziliozokusanywa zilibainika kubeba taashira za vitu na tendo katika wimbo mmoja. Ifuatayo ni mifano ya nyimbo iliyotumiwa kuonyesha taashira za vitu na tendo.

#### **Mifano: Taashira za vitu**

*kasiba* ni taashira iliibuliwa kutoka wimbo MMH.2. Jahazi.

*kisiki, mpera* na *dawa* taashira zilizoibuliwa katika wimbo MKN.8. Kitamchoma.

*muhogo* ni taashira iliibuliwa kutoka wimbo MKN.9. Kula Muhogo.

#### **Mifano: Taashira za tendo**

*kitamchoma, patie dawa sana, pasije pakabana* bwana ni taashira zilizoibuliwa katika wimbo MKN.8. Kitamchoma.

*Kula muhogo* ni taashira iliibuliwa kutoka wimbo MKN 9.

Wimbo MKN.9. Kula Muhogo umebeba aina mbili (2) za taashira nazo ni: Taashira za vitu: *muhogo* na Taashira za tendo: *kula muhogo* na *utauona utamu* wake. Maneno yaliyopigiwa mstari chini yanaonyesha aina za taashira zilizotajwa katika nyimbo hizo. Taashira hizi

ziliaminika kusimamia maana nyingine. Baaada ya uainishaji wa taashira za vitu na tendo, hatua ya tatu ilikuwa ni ufasiri wa taashira zilizoibuliwa katika nyimbo za harusi.

### **Hatua ya Tatu: Ufasiri wa Maana za Taashira**

Hizi ni taashira zilizoibuliwa katika nyimbo za harusi. Uchanganuzi wa kupata maana ya taashira katika nyimbo za harusi ulifanywa kwa kuzingatia utaratibu ufuatao hapa chini:-

- i) Kueleza muktadha wa tukio wakati wa uwasilishwaji wa nyimbo.
- ii) Kutoa maana ya kawaida ya taashira zilizobainishwa
- iii) Kutoa maana ya kitaashira
- iv) Kueleza umuhimu wa wimbo wenye taashira hiyo katika jamii.

Ufuatao ni mfano wa uchanganuzi wa kupata maana ya **taashira ya vitu**. Ufasiri ulifanywa kwa kuzingatia mfumo wa uchanganuzi huo hapa juu.

Mfano: *kasiba* ni taashira hii ilidondolewa katika wimbo huo hapa chini.

MMH.1.MNGANAMBA

*Kidomo katiti kama kasiba*

*Chenye mwanya kati mbwake haiba*

*Ndiye mke siti mwenye mahaba  
mapenzi*

*Atwazaye watu mahadharani*

**Kiswahili Sanifu**

kidomo kidogo kama firimbi

chenye mwanya katikati mwenye uvuto wa hashima

mke mwenye jina la heshima na ajuae  
anayeringa mbele za watu.

Wimbo huu, huimbwa katika muktadha ambao majaliko wanapokuwa njiani kwenda kualika harusi. ( Majaliko ni kundi la wanawake wanaofanya kazi ya ualikaji harusi kwa hapo zamani). Majaliko hualika wanawake pekee. Wanapotoka kwenda kualika huwa wamevalia mabuibui na wengine wamejitanda kwa mitandio huku huimba nyimbo mbalimbali. Miongoni mwa nyimbo wanazoimba ni wimbo wa MMH.1. Mnganamba. Kwenye kifungu cha maneno katika ubeti wa wimbo huu, majaliko wanamsifu bibi harusi kuwa ana mdomo mdogo wenye mwanya kati, hali ambayo imekamilisha uzuri, urembo na haiba ya bibi harusi. Uzuri huu hufanya watu wavutiwe naye. Siku hizi ualikaji wa aina hii umepungua sana kwa sababu ya maendeleo ya sayansi na technolojia kuingia katika jamii nyingi za Kiafrika. Harusi za siku hizi kiswani Unguja hualikwa kwa kutumia kadi.

Taashira iliyoibuliwa katika wimbo MMH.1. ni *kasiba*. Maana ya kawaida ya *kasiba* ni aina ya firimbi au zumari yenyе kutoa sauti ya kuvutia inapopulizwa. Kulingana na muktadha wa matumizi ya taashira katika wimbo MMH.1 maana ya kitaashira *kasiba* husimamia mdomo mzuri unaotoa sauti ya kuvutia.. Sauti nyororo inajumuisha maneno mazuri kama ile methali isemaya "maneno mazuri humtoa nyoka pangani". Maana hii inathibitishwa kwenye mshororo wa 3 na 4 kama inavyoilezwa katika ubeti wa kwanza katika wimbo MMH.1. Majaliko katika mishororo hii 3 na 4 wanaendelea kumsifu bibi harusi kuwa ni *mke siti* yaani mwanamke mwenye heshima na *mwenye mahaba* anayejuwa mapenzi na mwenye maringo mbele za watu. Sikwamba anaringa kwa kiburi bali anaringa kwa haiba yake. Wimbo huu una umuhimu katika jamii ya wa Unguja. Unaonyesha miongoni mwa sifa za mke bora. Mke mwenye sifa bora ni yule mwenye maneno mazuri kwa watu.

Huu ulikuwa ni mfano wakuonyesha jinsi uchanganuzi wa taashira ulivyofanyika katika sura ya nne. Njia hii ya kufuata mwongozo wa mfumo wa uchanganuzi, ndio uliyotumiwa kufasiri taashira za vitu na matendo yaliyosalia. Mbali na ufasiri huu wa kupata maana ya taashira ya vitu na matendo yaliyotajwa katika nyimbo pia kulikuwa na ufasiri wa maana matendo yaliyoambatana na taashira wakati wa uimbaji. Ufasiri wa maana ya utendaji wakati wa uimbaji nyimbo harusini umeelezwa na kutolewa mfano kama hatua ya nne hapa chini.

#### **Hatua ya Nne: Ufasiri wa Maana ya Utendaji wakati wa Uimbaji Nyimbo Harusini.**

Katika hatua hii, uchanganuzi ulizingatia utendaji yaliyofanywa wakati wa uimbaji. Utafiti ulibaini kulikuwa na utendaji wa aina tatu. Kwanza utendaji ulioambatana na taashira wakati wa kucheza na kuimba. Pili utendaji katika matukio yanayoashiria mambo ya kitaashira wakati wa uimbaji. Tatu utendaji wa uigizaji wa vitu vya bibi harusi wakati wa kuimba nyimbo.

Uchanganuzi wa kupata maana wa utendaji ulifanywa kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo hapa chini:

- (i) Kudadisi utendaji unaofanywa na anayefanya wakati wa uimbaji.
- (ii) Ni nani anayefanyiwa?
- (iii) Matendo hufanyika wapi?
- (iv) Matendo hufanyika vipi? (Yaani kuchunguza ishara za lugha na

uambatano wa matendo ya wachezaji kama vile: miondoko na matumizi ya viungo).

- (v) Kuzingatia fasiri za wasailiya kuhusu maana ya matendo yaliyoambatana na taashira.

Kila kipengele hapa juu kilikuwa na umuhimu wake. Vipengele hivi vilitumiwa na mtafiti kuchunguza kwa undani uwasilishwaji wa kila wimbo. Lengo ni kuangazia zaidi matukio na matendo yenye yanavyodhiihirika. Uchanganuzi huu pia, ulimwezesha mtafiti kupata ufaafu wa nyimbo hizo kulingana na muktadha wa ndoa ya jamii ya Waunguja. Mtafiti alitumia mbinu ya kimaeleo kufasiri matendo ya washiriki kwa vile matendo husaidia pakubwa kupambanua maana za taashira katika nyimbo. Uchanganuzi wa utendaji ulitegemea zaidi data zilizorekodiwa kwa kamera ya video pamoja na kumbukumbu zilizoandikwa wakati wa ushiriki na uchunguzi nyanjani.

Mtafiti aliandika maeleo ya utendaji yaliyoambatana na taashira wakati wa uimbaji. Utendaji uliotambuliwa na kuaminika kuwa na maana uliooredheshwa na kufasiriwa. Utendaji huo ulifasiriwa na kutolewa maana kulingana na muktadha wa kila wimbo. Mtafiti aliwaauliza wasailiya kuhusu matendo ya kitaashira yalikuwa na maana gani wakati wa uwasilishwaji wa wimbo. Yafuatayo ni baadhi ya orodha ya utendaji na matukio yenyewe maana ya ndani yaliyodhiihirika wakati wa uimbaji:-

**Mifano ya Utendaji Ulitoambatana na Taashira wakati wa kucheza na Kumba:**

- (i) Wanawake kuviringisha vidole vya katikati.
- (ii) Kukata/kuvitingisha viuno
- (iii) Kupiga mamakofi.
- (iv) Kupiga vigelege.
- (v) Kuigiza Kupara samaki.
- (vi) Kuigiza kuchora na kuchongo kalamu kwa kiganja na kidole.
- (vii) Kupiga miguu chini.

**Mifano ya Utendaji katika Matukio Yanayoashiria Mambo ya Kitaashira wakati wa Uimbaji.**

- (i) Kuelekwa Mgongoni.
- (ii) Kufukizwa.
- (iii) Singo.
- (iv) Kupukuswa mchele kichwani bwana harusi.
- (v) Kukamatana mikono baina ya babake bibi harusi na bwana harusi
- (vi) Bwana harusi kumsomea kichwani bibi harusi.

Kwa kuzingatia vipengele vya uchanganuzi wa utendaji tulivyovitaja hapa juu tumevitumia kuonyesha **mfano** wa ufasiri wa matendo yenye maana yaliyofanywa wakati wa uimbaji.

**Mfano: 1: Wanawake Wakiviringisha Vidole vya katikati**

Taashira ya (kitendo) *huyo ajaye mwana wa siwa* ni taashira katika wimbo wa kupeleka mahari MMH.2. Jahazi, iliambatana na utendaji wa wanawake kunyosha mikono na kuviringisha vidole vya katikati. *Siwa* ni baragumu kubwa Aghalabu la pembe ya ndovu au lilichongwa kutokana na mti maalumu (TUKI: 2006:379). Topan anaelezea kuwa, "*siwa* ni baragumu linalopulizwawakati wa harusi kwa baadhi ya familia wenye uwezo hapa zamani. Kwa kawaida *siwa* humiliwi na watu wanaotoka tabaka la juu, (1993:96)". Wanawake hawa wanapoimba *huyo yuwaja mwana wa siwa* walikuwa wakijigamba kuwa kijana wao (bwana harusi) anatoka katika familia teule. Kwa sababu hii wanawake wa upande wa mume walikuwa wakiimba kwa sauti, huku mikono yao ikiwa juu, wakiviringisha vidole vya katikati na wakijitingisha miili yao. Utendaji huu wa kuviringisha vidole vya katikati wa wanawake wa upande wa mume waliwafanya wanawake wa upande wa mke. Utendaji huu ulisaidia kupambanua maana ya taashira ya *huyo yuwaja mwana wa siwa* katika wimbo MMH.2. Maana iliyoibuliwa ni kuwa, utendaji wa kuviringisha vidole vya katikati husimamia kujigamba.

## **Mfano:2: Kuigiza Kupara Samaki**

### **MBN.20. UTAMPARA SAMAKI**

*Umetaka mwenyewe kuolewa*

*Utampara samaki*

*Samaki anamagamba eee*

*Utampara samaki*

*Samaki anajicho moja eee*

*Utampara samaki*

Wimbo huu MBN.20. uliimbwa wakati bibi harusi anamsubiri bwana harusi kuja kutoa mkono na baadya kumchukuwa mkewe. Wimbo huu uliambatana na uigizaji. Uigizaji ulifanywa na wanawake, wanaimba wakiigiza kwa mikono yao iliyokuwa mbele ya sehemu zao za siri jinsi samaki anavyoparwa. Walikuwa wakiviringisha viuno. Uigizaji wa kupara samaki na kuviringisha viuno ulisimamia kufanya tendo la ndoa.

Haya yalikuwa ni mifano ya kuonyesha jinsi uchaganuzi wa utendaji wakati wa nyimbo ulivyofanywa katika sura ya tano. Uchanganuzi zaidi wa kupata maana za taashira za vitu, tendo pamoja na maaana za utendaji yameelezwa katika sura zifuatazo.

**SURA YA NNE**  
**UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA**  
**TAASHIRA**

#### **4.0 Utangulizi**

Sura hii imejihuisha na uwasilishaji pamoja na uchanganuzi wa data ya utafiti huu ambayo ni nyimbo, taashira na maana za kitaashira zilizolezwa na wasailiwa kuhusu taashira zilizoibuliwa katika nyimbo za harusi. Data hiyo imenorodheshwa na kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo ili kukidhi matlaba ya sehemu ya mada ya utafiti ambayo ilikuwa kubainisha taashira na maana zake zilizotumika kwenye nyimbo za harusi.

Vivyo hivyo, madhumuni ya utafiti yalikuwa kubainisha na kuanisha matumizi ya taashira na kuchunguza maana mbalimbali na umuhimu wake kwa jamii ya wa Unguja. Kwa hiyo, data iliyokusanywa imewasilishwa ili kujibu maswali ya utafiti huu, ikachanganuliwa kimaaelezo kutokana na mwongozo wa Nadharia ya Semiotiki. Hivyo basi sura hii imegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ilijihuisha na uchanganuzi na ufasiri wa taashira za vitu zilizoibuliwa katika nyimbo. Imedhihirika kuwa nyimbo ni chombo cha kubeba taashira mbalimbali. Aidha, iliaminika kuwa taashira zilizomo katika nyimbo zilikuwa na umuhimu mkubwa katika kuwasilisha maana na ujumbe. Sehemu ya pili ilijikita kuchunguza maana za taashira za tendo katika nyinbo na umuhimu wake kwa jamii. Kadhalika taashira za tendo zilizomo katika nyimbo zilikuwa na umuhimu mkubwa katika kuwasilisha maana na ujumbe

#### **4.1 Matumizi na Ufasiri wa Taashira katika Nyimbo**

Utambuzi na ubainishaji wa taashira ulifanywa kwa kupigia misitari maneno ambayo ni taashira katika nyimbo. Taashira zilizotumika katika nyimbo za harusi zinatumiwa kama kipengele cha lugha. Mutembei (2001) anaeleza kuwa, waimbaji hutumia lugha kisanii ili kuunganisha maarifa, uzoefu wao, utamaduni, mila, desturi na hisia za mahali wanapozalishia kazi za sanaa. Kwa mnasaba wa kauli hii, nyimbo za harusi za Waunguja nazo zilitumia lugha ya kawaida na lugha ya kitaashira kuwasilisha ujumbe waliokusudia kutegemea na maudhui, muktadha na wakati maalumu.

Taashira zote zilizotambuliwa zilichanganuliwa na zilifasiriwa na kudhihirika kuwa ziliwuwa zinasimamia maana nyingine. Wakati wa ufasiri, utafiti ulizingatia maelezo ya wasailiwa pamoja na mhimiili wa msimbo wa Kihementiki. Mhimili huu unasisitiza kwamba, neno au maneno katika mfumo wa lugha hutoa fununu ya maana ya neno au maneno hayo. Vilevile ufasiri umezingatia muelekeo wa Culler (1981) unaodai kwamba, jamii moja huweza kutumia taashira za aina sawa na kuelewana katika ufasili wa maana na ujumbe. Hata hivyo, katika jamii hiyo, ufasili hutofautiana kwa watu binafsi na hata mionganoni mwa watu wenye tajriba tofauti.

Hivyo basi, kwa kuzingatia maelezo hayo hapa juu, nyimbo sitini (60) zilichanganuliwa. Uchanganuzi na ufasiri huu ulifanywa kwa mbinu ya kimaelezo. Ulifuata mfumo (muundo) maalum wa uchanganuzi uliououndwa wenye utaratibu ufuatao.

- (i) Kueleza muktadha wa tukio wakati wa uwasilishwaji wa nyimbo.
- (ii) Kueleza maana ya kawaida ya taashira iliyoibuliwa.
- (iii) Kufasiri maana ya ndani (fiche) ya taashira katika wimbo kulingana na muktadha wa utendaji. (Mtafiti alieleza fasiri hizi kwa kuzingatia maelezo ya wasailiwa, umbo na utendaji kazi wa taashira iliyoibuliwa).
- (iv) Kuelezea umuhimu wa wimbo wenye taashira kulingana na shughuli ya ndoa ya Waunguja.

Mwongozo wa mfumo huu hapa juu, ulimsaida mtafiti kuchanganua na kupata maana za kitaashira za vitu na tendo katika nyimbo za harusi.

#### **4.1.1 Ufasiri wa Taashira za Vitu**

Kama tulivyoeleza awali kuwa, nyimbo ni chombo cha kubeba taashira. Taashira za vitu arobaini na tatu (43) ziliibuliwa katika nyimbo thelethini (30). Taashira hizi zilihusishwa na vitu vinavyopatikana katika mazingira ya jamii ya Waunguja. Vitu hivyo ni kama vile: vitu vya baharini, vitu vya nyumbani, viumbe, mimea na sehemu za mwili. Maneno yaliyopigiwa misitari chini katika uchanganuzi wa nyimbo ndio yaliyotambuliwa kama taashira. Zifuatazo ni taashira za vitu zilizoibuliwa katika nyimbo zilizoimbwa kwenye miktadha tofauti.

## **1.Vitu vya Baharini:**

*Jahazi* ni moja ya taashira ya vitu vya baharini, iliibuliwa katika wimbo MMH.2. Ufuatao ni ubeti wa kwanza wa wimbo huo.

### *MMH.2. JAHAZI*

*Jahazi yetu twaipeleka kwa pepo njema.*

*Nenda mwanangu amana Llahu Aman Rasuli.*

*Huyo ajaye mwana wa siwa na matuwazi.*

Maana ya kawaida ya taashira hii *jahazi* ni chombo cha usafiri wa baharini kilichoundwa kwa mbaao. Aghalabu jahazi husafiri kwa mwendo wa polepole au wa kasi kwa kutegemea upopo uvumao baharini. Wimbo huu huimbwa na wanawake wa upande wa mume katika muktadha wa kumpeleka bwana harusi kwenda kuoa au kupeleka mahari. Wakati wa msafara, wanawake huimba, *jahazi yetu twaipeleka kwa pepo njema*. huku wakiviringisha vidole vyao vya katikati, wakijitingisha miili na kupaza sauti juu. Huwa wamevalia mabuibui na kujitanda kwa mitandio. Pia huwepo na wanaume kutoka upande wa mume ambao huwa nyuma ya kundi la wanawake. Wanaume huwa wamevalia kanzu na makofia. Baadhi ya wanaume watu wazima huvaa makoti meusi. (Koti, kanzu na makofia ni vazi la heshima kwa jamii ya Waswahili). Hivyo msafara unaonekana wa heshima na kutoa taswira ya umuhimu wa shughuli hii.

Kulingana na muktadha na taashira iliyotumika katika wimbo huu, Mzee Gora aliyehojo wa tarehe (2/1/2010) anafasiri kuwa maana ya kitaashira ya *jahazi* inasimamimia *safari*. Gora anaendelea kufafanua kuwa ufasiri wa taashira hii ilitumika kumaanisha safari ya amani ya kumpeleka mume kwenda kuoa kama inavyooelezwa katika mshororo huo hapa juu. Wimbo huu unaonyesha umuhimu wa ndoa na umoja katika jamii. Wanajamii wameshirikiana kwa hali na mali katika mambo ya kijamii. Kama inavyooelezwa katika wimbo jamaa wameacha shughuli zao na kuja kujumuika na kumshindikiza kijana wao kwenda kuoa. Lau lingekuwa ni jambo lisilo na umuhimu katika jamii, basi pasingelikuwa na haja ya safari hii.

## **2.Vitu vya Nyumbani**

Vitu vya nyumbani vilivyoibuliwa kama taashira ni pamoja na: *jembe, kioo, kigongo, marashi, ufunguo, wembe*, na *mtaimbo*. Taashira zote hizi zilibeba maana ya kitaashira na umuhimu katika

jamii ya Waunguja. Taashiri hizi zimebainishwa kwa kupigiwa mistari chini katika nyimbo zifuatazo.

*Jembe* kama taashira ya vitu vya nyumbani ilitumika wakati wa kuimba wimbo ufuatao hapa chini.

*MMH.3. NATAKA TAMBUU*

*Kijakazi changu si cha kutuma,  
Sikumpa jembe kwenda kulima,  
Nilimpa chuo kwenda kusoma,  
Asome ilimu na Kuruani*

Wimbo huu huimbwa na wanawake wa upande wa mke. Huwaimbia jamaa wa upande wa mume wakati wa kuja kuleta mahari au kuo. Tonya (1978) anaeleza kazi moja ya wimbo ni kutumia lugha kisanii ili kuitisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii. Katika wimbo MMH.3 umetumia taashira ya *jembe* kutoa ujumbe unaomlenga bwana harusi, kama unavyoelezwa katika mshororo wa kwanza na wa pili usemao: *kijakazi changu si cha kutuma,sikumpa jembe kwenda kulima*. Maana ya kawaida ya *Jembe* ni chombo cha kulimia au kuchimbia ardhi ambacho hushikwa mkononi au kukokotwa na trekta au mnyama. Kawaida jembe hufanya kazi za sulubu.

Taashira ya *jembe* iliyotumika katika wimbo huu inasimamia kazi ngumu. Ufasiri huu, umetokana na utendaji kazi wa taashira (*jembe*) iliyotumiwa nyimboni. Taashira hii inanasibishwa na jinsi kifaa hiki kinavyofanya kazi ya sulubu. *Kijakazi* imetumika katika wambo, kumaanisha mwari au bibi harusi sio mtumishi kama ilivyozoleka. Kama unavyoeleza wimbo "*Kijakazi changu si cha kutuma, Sikumpa jembe kwenda kulima*". Yaani mwanangu (ambaye ni bibi harusi) si mtumishi wa kufanyishwa kazi ngumu. Umuhimu na ujumbe unaotolewa kulingana na taashira iliyotumika katika wimbo huu ni kwamba, mume anaonywa asimtese mke wake. Pengine katika jamii hii waume hutokea kuwatesa na kuwatumisha wake zao kufanya kazi za sulubu. Labda kwa sababu hii, wanakumbushwa kupitia wimbo huu MMH.3. Mume anatakiwa awe muadilifu kwa mkewe. Mume asiwe ni mwenye kumtumisha na kumfanyisha kazi za sulubu mkewe. Katika maisha ya ndoa mume anawajibika kumlinda, kumheshimu na kumtimizia mkewe mahitaji yote ya lazima kama kula, mavazi na malazi.

Kinachosisitizwa katika wimbo huu ni kuwa, mke si mfanyakazi au mtumishi wa nyumbani. Mke ni mwenzi wa kushauriana naye na kujenga familia bora.

*Kigongo* ni taashira ilioibuliwa katika wimbo MSG.5. KUNA ILA MOJA huu ufutao hapa chini.

<i>MSG.5</i>	<i>KUNA ILA MOJA</i>
<i>Kungwi:</i>	<i>Kuna ila moja ila ila baba ila,</i> <i><u>Kigongo</u> mkononi ila.</i>
<i>Watani:</i>	<i>Kuna ila moja ila ila baba ila,</i> <i><u>Kigongo</u> mkononi ila.</i>
<i>Kungwi:</i>	<i>Kuna ila moja ila ila baba ila,</i> <i>Kusimbilia mke ila.</i>
<i>Watani:</i>	<i>Kuna ila moja ila ila baba ila,</i> <i>Kusimbilia mke ila.</i>

Wimbo huu huimbwa katika muktadha wa kumsinga mwari wa kiume. Wanapoimba waimbaji huwa wako nje ya chumba anachosingwa mwari. Aidha, hakuna ukataji kiuno kama inavyofanyika katika singo ya mwari wa kike. Mwari wa kiume husingwa na watani na mashangazi zake na huvalishwa bukta, tofauti na mwari wa kike ambaye huvalishwa kisutu. Singo ya mwari wa kiume, shughuli yake huwa ni ya utani zaidi kuliko kufunzwa. Isitoshe singo ya mwari wa kiume haialikiwi sana kama inavyofanyika singo ya mwari wa kike.

*Kigongo* ni taashira iliyotumika kwenye wimbo MSG.5 kumuhusu mwari wa kiume. *Kigongo* ni kipande cha mti mfano wa fimbo aghalabu hutumika kupigia. Maana ya kitaashira ya *kigongo* jinsi iliviyotumika katika wimbo huu husimamia *kupiga*. Wimbo unaeleza mambo ambayo hayafai kufanywa katika maisha ya ndoa. Mwari wa kiume anaonywa asiwe na tabia ya kumpiga mke. Kama ilivyoelezwa katika baadhi ya nyimbo huko nyuma kuwa "mke hupigwa kwa nguo na chakula", yaani, mke hulishwa na kuvishwa. Wimbo umetumia taashira *kigongo mkononi* inayohuishwa na ile tabia ya kila wakati mume kumpiga mkewe. Haya yameelezwa na Bi. Rehema Makame (25/10/2009). Tabia ya kumpiga mke katika jamii ya Waunguja wanaiona ni udhaifu au ila kwa upande wa mume. Kama usemavyo wimbo katika baadhi ya mishororo: *Kuna ila moja ila ila baba ila, kigongo mkononi ila.* Umuhimu wa matumizi ya taashira hii katika wimbo MSG.5 ni kutoa mafundisho ya msingi na nasaha kwa mume/waume wanaooa, wanaotaka kuoa na walioa. Yaani wimbo unawakanya wasiwe na tabia ya kumpiga piga mke. Jambo hili likizingatiwa litafanya ndoa iwe imara na yenye masikizano.

Wimbo MSG.1. BISUMILLAH ulibeba taashira ya kioo na ini kama zinvyoonekana hapa chini.

**MSG.1. BISUMILLAHI**

*Kungwi:*      *ee oo yaa ee bisumilahi ndio ya kwanza ya kuondokeaa,  
bisumillahi ndio ya kwanza.*

*Watani:*      *ee oo yaa ee bisumilahi ndio ya kwanza ya kuondokeaa,  
bisumillahi ndio ya kwanza.*

*Kungwi:*      *ee oo yaa eee amana Allahi amana rasulli, nenda mwanangu,  
amana allahu amana rasuli ee.*

*Watani:*      *ee oo yaa eee amana Allahi amana rasulli, nenda mwananguuu,  
amana allahu amana rasuli ee.*

*Kungwi:*      *ee oo yaa eee muenge enge kama kioo mume nduguyoo,  
munge enge kama kioo mume nduguyoo oo.*

*Watani:*      *ee oo yaa eee mume muenge enge kama kioo mume nduguyoo,  
munge enge kama kioo nduguyoo oo.*

*Kungwi:*      *ee oo yaa eee na mama yangu shoti awepo wote ni mama ee,  
na mama yangu shoti awepo wote ni mama*

*Watani:*      *ee oo yaa eee na mama yangu shoti awepo wote ni mama ee,  
na mama yangu shoti awepo wote ni mama*

*Kungwi:*      *ee oo yaa eee enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini,  
enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini ee.*

*Watani:*      *ee oo yaa eee enyi wazazi yote mwayafahamu mwana ni ini,  
enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini.*

*Kungwi:*      *ee oo yaa eee akikuaga mpe ruhusa mwana anakwao ee,  
akikuaga mpe ruhusa mwana anakwao ee.*

*Watani:*      *ee oo yaa eee akikuaga mpe ruhusa mwana anakwao oo,  
akikuaga mpe ruhusa mwana anakwao.*

Huu ni wimbo maarufu wa kuanzia singo. Singo ni tukio muhimu katika harusi za Waunguja . Mwari husuguliwa mwili. Wasingaji/watani huimba huku wakipiga makofi na kukata viuno. Kungwi humusiya mwari na kumuelezea majukumu yake kupitia taashira zilizomo katika nyimbo anazoimbiwa.

Wimbo MSG.1 BISUMILLAHI ulikuwa na taashira zilizotambuliwa *kioo* kama vitu vya nyumbani na *ini* kama sehemu ya mwilini. Maana ya kawaida ya *kioo* ni kitu kilichotengenezwa kwa madini ya jamii ya ulanga ambacho hutumiwa kujitazamia. Taashira ya *ini* japo imetambuliwa katika wimbi MSG.1 tulielezea katika sehemu za mwili.

Maana ya kitaashira ya *kioo* husimamia mume. Mume anapigiwa mfano wa taashira ya *kioo*, kitu cha thamani. Yaani mume ni mtu wa thamani na muhimu katika maisha ya mwanamke. Katika wimbo MSG.1 mke anausiwa kumtunza, kumwangalia na kumjali mume wake kama kinavyotunzwa *kioo*. Iwapo *kioo* hakitunzwi vizuri ni rahisi kuvunjika. Hoja ya utunzaji pia inafafanuliwa na Bi Kidude aliyehoziwa tarehe 20/10/2009, anaeleza, "... mke ni yule anayemdhiliti mume na kuilinda ndoa yake". Ama majukumu ya mume kumtunza mke yameelezwa na Topan (1995:103) alipofafanua wimbo wa '**vugo kubwa**' wakati bwana harusi anapoenda kuingia ndani. Kifungu cha ubeti chenye kubeba wazo hili la mume kumtuna mke kina jitokeza hapa chini.

*Mwanganie sana*  
*Mwanagu naye ni mwana*  
*Mpaka filjana*

Topan (1995:013) anaeleza kuwa, wimbo huu hapa juu unamkumbusha mume atambue wajibu wake juu ya mkewe. Mke ni amana aliyopewa mume. Mume anatakiwa aitunze amana hiyo kwa vizuri hadi siku ya kuingia peponi. Lakini ujumbe unaotolewa katika wimbo MSG.1 unaeleza jukumu la mke kumtunza mume.

Kwa mujibu wa matumizi ya taashira ya *ini* iliyotumika katika MSG.1, maana ya kitaashira ya *ini* inasimamia *mapenzi*. Haya ni mapenzi yaliyopobaina ya mama na mwanawe. Mapenzi ya mamake mwari yanaonekana kupitia wimbo MSG.1 kwenye mishororo hii hapa chini anapoosema:

*ee oo yaa eee enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini,*  
*enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini ee.*

Kwenye mishororo hii hapa juu, mamake mwari anasisitiza na kuonyesha mapenzi yake ya dhati kwa mwanawe. Anasisitiza hoja yake kwa kuwahusisha wazazi kama mashahidi kutokana na maneno aliyoyasema, "*enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini ee*". Anawataja wazazi kwani wao ndio wanaojua mapenzi na uchungu wa mwana zaidi kuliko mtu mwengine yejote. Sawa na ile methali isemayo "uchungu wa mwana aujuae ni *mzazi*".

Taashira ya *kioo* iliyotumika katika wimbo MSG.1, inasimamia upendo. Umuhimu wa taashira hii ni kutoa mafundisho ya upendo kwa jamii. Aidha, hueleza majukumu kwa wanandoa kuwa ya upendo na utunzaji wa kila mwenza. Yaani waume kuwajali na kuwatunza wake zao hali kadhalika wake kuwajali na kuwatunza waume zao katika maisha ya ndoa.. Hali hii huwafanya wanandoa kuishi kwa uzuri na kuifanya ndoa yao iwe ni yenye kudumu.

### **3.Sehemu za Mwili**

Sehemu za mwili zilizotajwa katika nyimbo kama taashira zilihusisha sehemu zipatikanazo kwa binadamu na wanyama.Taashira hizi ni pamoja na: *pembe, mvi ,ini, jicho* na *kidonda*. Sehemu hizi zimepigiwa mistari kama taashira katika nyimbo zifuatazo.

Kama tulivyonangulia kutaja kuwa katika wimbo MSG.1.BISUMILLAH vilevile ulibeba taashira inayorejelea sehemu za mwili nayo ni *ini*. Katika ubeti wa wimbo ufuatao *ini* limetajwa na kutumika kama taashira hapa chini.

#### **MSG.1.BISUMILLAH**

*Kungwi:*      *ee oo yaa eee enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini,*  
*enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini ee.*

*Watani:*      *ee oo yaa eee enyi wazazi yote mwayafahamu mwana ni ini,*  
*enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini.*

Kadhalika wimbo huu huimbwa wakati wa kumsinga mwari. *Ini* ni sehemu muhimu ya ndani katika mwili, hufanya kazi ya kurekebisha sukari. Ini ni kiungo muhimu na chenye thamani kwa mwanadamu. Ini huhitajika kutunzwa kwa uangalifu mkubwa. Ni rahisi kuharibika iwapo halitunzwi na si rahisi kurekebishiwa linapoharibika.

Kwa mujibu wa matumizi ya taashira ya *ini* iliyotumika katika MSG.1, maana ya kitaashira ya *ini* inasimamia *mapenzi*. Haya ni mapenzi yaliyopobaina ya mama na mwanawewe. Mapenzi ya mamake mwari yanaonekana kupitia wimbo MSG.1 kwenye mishororo hii hapa chini anapoosema:

*ee oo yaa eee enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini,*  
*enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini ee.*

Kwenye mishororo hii hapa juu, mamake mwari anasisitiza na kuonyesha mapenzi yake ya dhati kwa mwanawe. Anasisitiza hoja yake kwa kuwahusisha wazazi kama mashahidi kutokana na maneno aliyoyasema, "*enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini ee*". Anawataja wazazi kwani wao ndio wanaojua mapenzi na uchungu wa mwana zaidi kuliko mtu mwengine yejote. Sawa na ile methali isemayo "uchungu wa mwana aujuae ni mzazi".

Umuhimu wa taashira ya *ini* katika wimbo MSG.1, unatoa nasha kwa waume kuwapenda na kuwahurumia wake zao. Ukumbusho huu wa nasaha unatolewa na mamake mwari katika MSG.1 kuwa, mwanawe ni mtu wa thamani kwake na anahitaji kupendwa na kutunzwa. Kadhalika hali hii huwafanya wanandoa kuishi kwa uzuri na kuifanya ndoa yao iwe ni yenye kudumu.

Taashira nyengine ni ya pembe imetumika katika nyimbo mbili nazo ni MSG.17. HUYO YUWAJA na MKN.1. KINYEMI CHA MWANA. Katika wimbo MSG.17 kama unavyoonekana hapa chini.

*MSG.17. HUYO YUWAJA*  
*Huyo yuwaja yuwaja mpeni ndia,*  
*Huyo yutukuzie pembe na pembe mwana mema X 2*  
*Atukuze akatuwe mzigo kitwani.*

Maana ya kawaida ya *pembe* ni kitu kama mfupa chenye uwazi ndani na chenye ncha upande mmoja kinachomea kwenye vichwa vyta wanyama kama vile ndovu, mbuzi na ng'ombe. Katika lugha ya kawaida wimbo MSG.17. unaeleza kuhusu mwari anayetaka kupishwa njia apite kwa sababu amebeba pembe kama mzigo. Wimbo MSG.17 uliimbwa wakati mwari alipotolewa uzioni na kupelekwa chumbani. Kama ada ya Waunguja, mwari anapopelekwa chumbani huelekwa na kungwi mgongoni. Hadhira huzidisha shangirio wanapomuuona mwari anapopitishwa mbele za watu akiwa anapelekwa chumbani. Hadhira huimba, kukata viuno, hupiga makofi na vigegele. Kila mtu huwa na hamu ya kumuona mwari ili kumpongeza.

Wimbo mwengine uliyotumia taashira ya *pembe* ni MKN.1. KINYEMI CHA MWANA huu hapa chini.

*MKN.1. KINYEMI CHA MWANA*  
*Nimepewa pembe*

*Nalilia pembe ee x2*  
*Nalilia pembe langu x2*  
*Napewa ni mama*  
*Nalilia pembe langu x2*  
*Sikupewa ni baba*

Wimbo unaeleza kuhusu bib harusi mwenye majonzi anayelilia *pembe* lake ambalo alipewa na mama. Wimbo MKN.1 uliimbwa na kikundi cha kina mama (wapishi) kilichokodiwa wakati wa shughuli ya mapishi harusini. Katika kikundi cha kina mama hawa baadhi yao huwa wanapika na wengine wanaimba na kucheza.

Maana ya kawaida ya *pembe* ni kitu kama mfupa chenye uwazi ndani na chenye ncha upande mmoja kinachomea kwenye vichwa vya wanyama kama vile ndovu, mbuzi na ng'ombe. Kutokana na muktadha na maana ya kitaashira ya *pembe* iliyoibuliwa katika wimbo MSG.17 *pembe* inasimamia majukumu. Tafsiri hii imetolewa kulingana na jinsi taashira hii ilivyotumika katika wimbo ulivyosema "*Huyo yutukuze pembe na pembe mwana mema, Atukuze akatuwe mzigo kitwani*". Maana ya tafsiri hii pia ilielezwa na Topan (1995: 104) alipochambua wimbo huu. Topan anaeleza kuwa, taashira ya *pembe* kusimamia majukumu inatokana na maeleo yaliyopo katika mshororo wa mwisho wa wimbo MSG 17 usemao "*Atukuze akatuwe mzigo kitwani*". Neno mzigo ndio hiyo pembe lakini kimaana si mzigo wa kawaida bali ni majukumu atakayobeba pindi atakapokuwa mke wa mtu. Kawida katika ndoa huwa kuna majukumu ambayo mke atakiwa kuwa nayo kama vile kulea watoto, kulinda mali ya mume, usafi wa nyumba na kadhalika.

Ama maana ya kitaashira ya *pembe* iliyotumika katika wimbo MKN.1 ilisimamia uume uliosimika. Tafsiri hii ilitokana na sababu mbili. Kwanza jinsi umbo la pembe lilivyo (yaani urefu uliokaza wenyе umbo la duara na kupinda kidogo na lenye ncha upande mmoja). Pili jinsi taashira hii ilivyotumika katika wimbo uliposema "*nalilia pembe langu*". Katika wimbo huu mke anaonekana ana majonzi pengine hajakutuna na mumewe kwa muda au wametengana naye. Hivyo anakumbuka mazoea ambayo yanamfanya kulililia hilo *pembe*. Yaani mke yuko kwenye huzuni na simanzi ya kumtamani mumewe kwa ajili ya tendo la ndoa

Taashira ilizotumiwa kwenye wimbo MSG.17. HUYO YUWAJA ilikuwa na umuhimu wa kumuandaa mwari kisaikolojia kufahamu majukumu katika maisha ya ndoa. Mwari anaambiwa kuwa si mtoto tena. Ataoleta na atakiwa afahamu kuwa katika ndoa kuna matatizo. Hivyo awe tayari kupambana nayo yatakapotokea. Awe tayari kubebe dhamana na majukumu katika maisha ya ndoa.

#### 4. Viumbe

Viumbe vilivytambuliwa kama taashira ni *mamba*, katika *koko*, dudu, njija, dakitari na pap. Taashira za viumbe zimepigiwa mistari katika nyimbo zifuatazo.

Koko kama taashira ilibainika katika wimbo huu hapa chini.

##### *MMH.4 TULIVUNILE JANGA*

*Nyumba ya mwari aingia koko: paramia.*

*Utango nautambae: uwe mwana wa Baraka.*

*Mpishe bwana apite: ende kwao ende kwa wazee wake wamzalie*

Muktadha wa matumizi ya taashira hii unakwenda sambamba na jinsi ilivyotumika katika wimbo MMH.4. Wimbo unahusishwa na lile tendo la watu kutoka upande wa mume kuja kwa kina mke kutoa mahari. Jamaa zake mume wanapokwenda kutoa mahari, huenda kwa vishindo na majigambo kwa kina mke. Wanapofika wenyeji wao huwapokea kwa wimbo MMH.4 huku wakipiga makofi na vigelegele. Mahari yakishapakelwa huandaliwa mipango ya ndoa. Dhima kuu ya ndoa ni kuwa watapatikana watoto kwa njia ya halali.

Koko ni taashira iliyotambuliwa katika wimbo MMH.4. Koko neno linalotumika katika lahaja ya Kitumbatu kumaanisha jogoo au jimbi. Jogoo ni kuku wa kiume. Jogoo ana sifa ya kutembea kwa majigambo na matao anapowaendea na kuwapandia kuku wa kike. Baada ya kumaliza shauku yake na kuku wa kike jagoo huwika. Uwikaji huu unaashiria kujigamba kuwa yeye ndiye 'mume'.

Kwa mujibu wa muktadha wa matumizi ya taashira hii maana ya kitaashira ya *koko* inasimamia *mume*. Mume ni *koko* anayekuja ingia nyumbani kwa kina mke kutaka kuoa kama inavyoolezwu katika wimbo "*nyumba ya mwari aingia koko...*".

Umuhimu wa taashira iliyotumika katika wimbo MMH.4. TULIVUNILE JANGA ulioambatana na utendaji wa mume kwenda kwa kina mke/mwari unaonyesha thamani ya mwanamke. Tendo hili la mume na watu wake kwenda kwa kina mwari na kutoa mahari linaonyesha hadhi ya mwanamke aliyonayo katika jamii. Yaani ukitaka kuoa ni uende kwa wazizi wa mke kupata idhini yao na kutoa ada hiyo (mahari) ambayo ni haki ya mke. Isifahamike vibaya kuwa kutoa mahari ni kumnunua mke.

## 5. Mimea

Taashira nyengine zilizotambuliwa kama mimea inayopatikana katika jamii ya Waunguja ni : *utango, mbegu, kisiki, uvumba na udi, mtango na mche*. Matumizi ya mimea hii ilibainika kubeba maana za kitaashira kama ilivyoolezwa katika nyimbo zifuatazo hapa chini.

### MSG.3 KISIKI

<i>Kungwi:</i>	<i>Hasa kwani nitumwa na kwenda alika,</i>
<i>Watani:</i>	<i>Kenda alike,</i>
<i>Kungwi:</i>	<i>Tangu Mogadishu hata Merika,</i>
<i>Watani:</i>	<i>Hata Merika,</i>
<i>Kungwi;</i>	<i>Ni <u>mbegu</u> njema ee sio shaka,</i> <i>Na mwenye kupanda hutumaini.</i>

Wimbo huu unabeba taashira ya *mbegu* inayoonyesha umuhumu wa mwanamke. Maana ya kawaida ya *mbegu* ni kitu kama vile kiini, punje, konde au kokwa kinachopandwa ili kutoa mmea. Wimbo huu huimbwa katika muktadha wa kusingwa mwari. Mwari husingwa kwa kusuguliwa mwili na watani na kungwi. Aidha, usingaji huambatana na uimbaji wa nyimbo mbalimbali zenye mafunzo. Maana ya kitaashira ya *mbegu* iliyotumika katika wimbo MSG.3 inasimamia kizazi. Tafsiri hii ilitolewa na Bi. Hafuswa aliyehojo wa tarehe 9/8/2008. Alifafanua kuwa kizazi kilichokusudiwa ni kizazi cha mke. Ufafanuzi huu aliurejelea mshororo katika wimbo usemao – " *mbegu njema isiyo shaka na mwenye kuipanda hutumaini*". Mshororo huu unamaanisha kuwa, mume atakayemuoa binti huyo anayealikiwa hatojutia. Mume huyo atakuwa amepata mke atakayeendeleza kizazi. Mke anapigiwa mfano wa *mbegu* inapopandwa na kutoa mimea. Dhana ya *mbegu* kupandwa na kutoa mmea inafananishwa na mke kuzaa watoto. Kupitia taashira hii iliyotumika, wimbo unaelezea umuhimu wa kuendeleza kizazi kama dhima kuu katika ndoa. Hivyo basi, jamii inakumbushwa kupitia wimbo huu kuwa, wanaotaka kuoa watafute wake wanaozaa (yaani wanawake wenye kizazi). Wanawake wa aina hii hujulikana kutokana na familia au ukoo wanaotoka.

Hizi ni baadhi ya taashira za vitu zilizoibuliwa katika nyimbo. Njia hii ilitumiwa kuchanganua na kufasiri taashira za vitu zilizoibuliwa katika nyimbo. Taashira nyingine za vitu zimetumiwa kusaidia kufafanua maana za kitaashira katika kuchanganua na kufasiri taashira za tendo. Kutokana na uchanganuzi na ufasiri uliofanywa hapa juu, imedhihirika kwamba, Waunguja hutumia vitu vilivyowazunguka kama taashira (lugha fiche) katika nyimbo zao za harusi kupitisha ujumbe waliokusudia. Vilevile lugha hii ya kitaashira hutumika hususan kueleza mambo ambayo yasingewezekana kueleza waziwazi hadharani.

Wimbo mwengine uliobebea taashira ya mmea ni huu hapa chini.

#### MKH.1 NITUMWA NA MAMA

*Nitumwa na mama kwenda alika,  
Tangu Mugudisho hata Marika,  
Ndio mbegu njema isiyo shaka,  
Na mwenye kupanda hutumaini.*

Taashira iliyotumika katika wimbo MKH.1 ni *mbegu njema*. Kitaashira *mbegu njema* inamaanisha kizazi. Hivyo, bibi harusi mtarajiwa anafananishwa na mbegu njema. Yaani mke mwenye kizazi. Mke ambaye ataendeleza kizazi katika familia ya mume wake. Katika jamii nydingi za Kiafrika wakiwemo Waunguja sifa mojawapo muhimu ya mke ni yule mwenye kuzaa watoto (kizazi). Mke hata akiwa mrembo kama lulu au almasi lakini akiwa hana kizazi yaani hazai hathaminiwi. Hata kama mume wake ameridhika na hali hiyo ya kutokuwa na kizazi lakini jamaa wa mume humsimanga na humletea matatizo. Ukweli wa mambo ni kwamba, mke kuwa na kizazi au kutozaa ni uwezo kutoka kwa Allah (Mungu). Allah kwenye Qur'ani sura ya Shura aya 49-50 anasema:

Ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu; Anaumba Apendavyo, Anampa Amtakaye watoto wa kike na Anampa Amtakaye watoto wa kiume. Au Huwachanganya (watoto) wa kiume na wa kike (kwa mtu mmoja), na Humfanya tasa Amtakaye hakika Yeye ni Mjuzi, Muweza. (Al-Farsy:1993).

Utaona kuwa katika aya hizo mbili juu kuwa mtu kuwa na kizazi, au utasa au ugumba ni fani (maumbile) kutoka kwa Mungu. Hakuna haja ya kumlaumu mtu ambaye hazai. Hata hivyo, mbali na jamii ya Waunguja amba ni Waisilamu kufahamu jambo hili, bado wimbo MKH.1. NITUMWA NA MAMA unajaribu kumtangazia au kutoa taarifa kuhusu binti yao kuwa ni mke mwenye kizazi. Mke kuwa na kizazi hutambuliwa kutokana na wazazi au familia ya msichana.

Wanajamii wanafahamu familia fulani Mungu ameibariki kuwa na kizazi. Nyimbo nyingine wanazoimba ni pamoja na zile wanazoimba siku ya kupeleka mahari.

Taashira ya mmea tunakutana nayo tena katika wimbo ufuatao ambao hutumika sana kuimbwa baada ya nikaha kufungwa:

***MBN.6. FURAHA***

*Na iwe leo ee naiwe leo furaha  
Baba amepata mama,  
Na iwe leo furaha.  
Mama amepata baba,  
Na iwe leo furaha.  
Mtango na utambae,  
Na iwe leo furaha.  
Wende ndani ukaza,*

...

Wimbo MBN.6 japo unaashiria furaha lakini pia umebeba ujumbe maalumu kupitia taashira iliyotumika ya *mtango*. Maana ya kitaashira ya *mtango* husimamia kizazi. Tafsiri ya *mtango* kuwa kizazi, imetokana na hulka ya mti wa mtango unaotambaa na kutoa matango mengi. Wimbo unaonyesha dhima kuu ya ndoa katika jamii ya kuwepo na kizazi. Yaani baada ya kuoana kupatikane watoto. Ufasiri huu umeelezwa na Bi. Hafuswa aliyeojiwa tarehe 10/12/2009.

**4.2.Uchanganuzi na Maana zaTaashira za Tendo katika Nyimbo na Umuhimu wake**

Taashira za tendo ni matendo yaliyotajwa katika nyimbo. Matendo hayo yaliaminika kubeba maana za kitaashira. Maana za kitaashira hizi zilipatikana kutokana na mambo yafuatayo. Kwanza maelezo ya wasailiwa wliota kuhusiana na taashira husika ilioibuliwa katika nyinbo. Pili fasiri ya maana nyengine zilitolewa kulingana na matendo yaliyotajwa katika kila wimbo kwa kuzingatia muktadha wa uwasilishwaji wake. Pili, mtafiti alitumia baadhi ya maana za taashira za vitu ili kuweza kusaidia kupata maana za taashira za tendo.

Utafiti umegundua kuwa, maana za taashira za tendo zimehusishwa na matendo yaliyomuhusu mwari/bibi harusi, bwana harusi na mamake mwari/bibi harusi yaliyotajwa katika nyimbo. Mwongozo uliotumika kuchanganua taashira za vitu ndio pia uliotumika kuchanganua taashira

za tendo/matendo.Ufuatao ni uchanganuzi na ufasiri wa maana za kitaashira za tendo kutoka nyimbo mbali mbali:-

### **1.Taashira za Tendo zilizomuhusu Mwari**

Taashira za tendo/matendo yaliyomuhusu mwari au bib harusi yalikuwa kama vile: *bibi aingile chooni kwa maulidi na angile koga* kutoka wimbo MSG 13. MWARI AINGILE CHOONI . *ukafiche kuche na unamie chini* kutoka wimbo MSG.4. KERO SI JEMA, *ukipata maji chamba* kutoka wimbo MSG.14. CHAMBA, *mama njoo unifiche dudu laja hilo* kutoka wimbo MKN.7. MAMA NJOO, *kitamchoma kisiki cha mpera na patie dawa sana pasije pakabana pakamkera bwana* kutoka wimbo MKN.8 KITAMCHOMA, *kula muhogo utauona utamu wake* kutoka wimbo MKN.9. KULA MUHOGO, *asiache ufunguo* kutoka wimbo MKN.10. UFUNGUO, *mwanangu udumbe ee taimbo wa kizungu kazi yake punde* kutoka wimbo MBN.15. SHINDWE *utampara samaki, samaki ana magamba* kutoka wimbo MBN.20. UTAMPARA SAMAKI na MSG.21. *Bibi anakunwa chai* kutoka wimbo, CHAI SHARUBATI LOZI. Taashira za tendo zilizomuhusu mwari zilitambuliwa kwa kuzipigia mistari katika nyimbo. Taashira zilizotambuliwa zilikuwa na maana za kitaashira kama tulivyoonyesha katika uchanganuzi wa nyimbo zifuatazo:

Wimbo MSG 13 hapa chini unaonyesha taashira za tendo zilivyoonyesha kumuhusu mwari.

#### **MSG 13 KISIKI**

*Kungwi:      Ukafiche kuche ee, ukafiche kuche ee, ukafiche kuche ee,  
                  Unakwenda mijini mwa watu, ukafiche kuche.*

*Watani:      Ukafiche kuche ee, ukafiche kuche ee, ukafiche kuche ee,  
                  Unakwenda mijini mwa watu, ukafiche kuche.*

*Kungwi:      Unamie chini ee unamie chini, unamie chini ee unamie chini  
                  Unakwenda mijini mwa watu, unamie chini.*

*Watani:      Unamie chini ee unamie chini, unamie chini ee unamie chini.  
                  Unakwenda mijini mwa watu, unamie chini.*

Huu ni mionganoni mwa nyimbo ndefu zilizokusanya wakati wa kukusanya data. Ni wimbo uliokuwa ukiimbwa kwa mapokezano baina ya lahani na waitikiaji (yaani kungwi na watani). Wimbo huu uliimbwa katika muktadha wa kumsinga mwari. Wasingaji/watani wa mwari wakiwa chumbani, huimba huku wakipiga makofii.Wimbo ulikuwa unaimbwa kwa mwendo wa

polepole kama ule wa kuongolewa mtoto. Kungwi humuusia mwari na kumuelezea majukumu yake kupitia taashira zilizomo katika nyimbo anazoimbiwa. Waalikwa ambao si warombo huwa wako ukumbini, hucheza kwa kufuata wimbo unaoimbwa chumbani anamosingwa mwari.

Taashira zilizoibuliwa ni katika wimbo MSG.4 ni *ukafiche kuche* na *unamie chini*. Maana ya kawaida *ukafiche kuche* ni tendo la kuficha kucha zisionekane. Kucha ni sehemu imeayo katika ncha za vidole iliyongumu na hutumiwa kukwaruza. Ama *unamie chini* ni tendo la kuinama chini au kujificha.

Kulingana na muktadha wa matumizi ya taashira katika wimbo MSG.4, maana ya kitaashira ya *ukafiche kuche* inasimamia kutokuwa mkali au kutokuwa na vurugu (kuficha tabia mbaya). Mke akifika kwa wakweze anastahili awe mtulivu asionyeshe tabia mbaya kama wimbo ulivyokuwa ukimnasihi mwari ukimwambia *unakwenda mijini mwa watu ukafiche kuche*. Maana hii imetokana na dhana ya kucha kuwa na tabia ya kukwaruza. Kwa mfano binadamu au wanyama kabilia ya chui hutumia kucha zao kukwaruza wanapopigana au kuvamia. Ama maana ya kitaashira *unamie chini* linasimamia kuwa na haya, adabu na utii. Makame Somo aliyehojo wa tarehe, 6/11/2009 anaeleza kuwa, "kulingana na mila na desturi za Waswahili kijana awe (mvulana au msichana) aliyelelewa akaleleka na kufunzwa akafunzika ni yule anaposemeshwa na wakubwa zake huinamisha uso wake chini". Mzee Makame anasisitiza "tendo la kuinamisha kichwa chini linaonyesha haya, utii na adabu aliyonayo kijana huyo". Bi Salma (ameshatajwa) naye anaeleza kuwa, mdogo anaposemeshwa na wakubwa zake anapaswa kuinamisha kichwa chini. Hii ni dalili ya mtu kuwa na haya, adabu na utii. Si vyema kwa mdogo (mwari) kumtizama usoni mtu mzima anapozungumza naye. Bi Salma ameiona tabia hii ni ujeuri. Ameongeza kwa kusema "mwari anatakiwa awe na haya za uso na kuonyesha uoga sio kumtizama usoni mtu". Taashira zilizotumika katika wimbo huu zinatoa mafundisho kwa wari kuwa, watifu na wapole watakapoolewa. Wimbo unawakataza hasa wanawake kuwa na tabia ya ukali na vurugu. Tabia ya ukali au vurugu husababisha maisha katika ndoa yakawa ya kuchukiza. Mke bora ni yule mwenye haya na heshima mbele za watu.

Wimbo mwengine uliobeba taashira zinazomuhusu mwari ni huu hapa chini:

MSG.13. MWARI AINGILE CHOONI

*Bibi aingile chooni kwa maulidi*

*Angile koga marashi uvumba na udi*

*eeee oyaaa X 2*

*Uvumba na udi X 2*

Taashira za tendo zilizotumiwa katika wimbo MSG.13 ni mbili *bibi aingile chooni kwa maulidi* na *angile koga*. Maana ya kawaida ya *bibi aingile chooni kwa maulidi* inamaanisha kuwa, bibi ambaye ni (mwari) anapelekwa chooni sio bafuni. Anapelekwa sehemu ambayo iliyofungwa uzio. Neno *maulidi* limetumika katika wimbo huu, kuonyesha kitendo cha mwari kupelekwa chooni ni cha heshima. Neno hili *Maulidi* ni neno lenye asili ya Kiarabu kumaanisha mazazi/kuzaliwa). Kimatumizi Waswahili Waisilamu wengi hulitumia kumaanisha sherehe ya kuadhimisha kuzaliwa kwa Mtume Mohamad (S.A.W). Maana ya kawaida ya *angile koga* ina maana ya mwari ameingia uzioni/chooni kuogeshwa.

Taashira hizo mbili (*bibi aingile chooni na angile koga*) ziliambatana na matukio yanayofanyika wakati wa uimbaji. Ziliimbwa wakati ambao kungwi anamueleka mwari mgongoni na kumpeleka chooni/uzioni. Akifika nae mwari hufunzwa mambo kadhaa na kisha humwaiwa maji.

Kulingana na muktadha wa taashira iliyotumika katika wimbo MSG.13, tendo la kuogeshwa au kumwaiwa maji husimamia mwari kutoka hatua ya utoto na kuingia daraja la utu uzima. Tafsiri hii inafafanuliwa na Bi Sihaba (ameshatajwa) kuwa, "mwari anapopelekwa chooni huchukuliwa kuwa bado ni mtoto". Utoto uliokusudiwa hapa ni kuwa, mwari hajajua mambo ya siri ya mwanamke. Haya ni mambo kama ya unyumba, mitindo ya kufanya tendo la ndoa usafi wa mwili na kadhalika. Mwari akishayafahamu mambo haya wanaona kuwa anakuwa mtu mzima. Baadhi ya mambo haya ni kutokana na yale mwari anayofunzwa na kufanyiwa akiwa chooni/uzioni. Bi Sihaba anaendelea kufafanua, "tendo la kumwaiwa maji/kuogeshwa lina maana ya kumtoa mwari ukoko wa usichana na kumfanya kuwa mrombo". Mrombo ni mwanamke aliyepata mafunzo unyagoni. Hivyo hali hii inamfanya mwari sasa kuwa mwanamke kamili. Hatua ya mwari kuwa mrombo, inamfanya awe ni mwenye kupata kibali cha kushiriki katika singo.

Umuhimu wa taashira iliyotumika katika wimbo huu inaonyesha dhima kubwa ya kumtoa mwari kutoka hatua ya usichana na kupanda daraja la utu uzima. Aidha, wimbo unatoa mafunzo muhimu kuhusu kunga katika maisha ya ndoa hasa kwa wari wanaokaribia kuolewa.

MKN.7. MAMA NJOO ni wimbo mwengine wenye taashira inayomuhusu mwari. Katika wimbo huu beti zote tatu (3) kama zinavyonekana hapa chini zinaonyesha uoga wa mwari kukutana na hilo dudu. Lakini mamake mwari anamzia moyo asiogope kama inavyoelezwa katika beti zifuatazo.

*MKN.7. MAMA NJOO*

Mama njoo unifiche dudu laja hilo ooo, x2  
Mwanangu usilie ukamiliza na miye,  
Ndiko kuolewa huko oo.

Mama njoo unifiche dudu laja huloo oo, x2  
Mama angu nitalia, eee mama angu nitalia,  
Sijaya ozoweya hayo.

Mama njoo unifiche dudu laja hilo ooo x2  
Mwanangu usilie ukamiliza na miye  
Utalizoeya hiloo ooo.

Muktadha wa wimbo huu uliimbwa wakati bibi harusi yuko chumbani anamsubiri bwana harusi kuja baada kufunga ndoa. Waimbaji huimba huku mmoja mmoja akija mbele ya bibi harusi na kukata kiuno katika mitindo mbali mbali.

*Mama njoo unifiche dudu laja hilo* ni taashira iliyopatikana kutoka wimbo MKN.7. Neno la msingi lililotumiwa kama taashira ni *dudu*. *Dudu* kwa mujibu wa neno hili lilivyotumika katika wimbo huu linarejelea aina ya mdudu aliyemkubwa yaani kiumbe Aghalabu chenye mbawa na miguu sita na bila uti wa mgongo anayengata. Maana ya kawaida ya taashira hii inamzungumzia mwari ambaye anamtaka mama yake amfiche ili asingatwe na hilo *dudu* (mdudu).

*Dudu* kama taashira iliyotumika katika muktadha wa wimbo MKN.7 inasimamia uume. Tafsiri ya *dudu* kusimamia uume inafananishwa na ile sifa ya mdudu ya kung'ata na kutoa damu. Kama inavyoelezwa katika wimbo "*mama njoo unifiche dudu laja hilo*" Yaani bibi harusi anaogopa kung'atwa na dudu. Kung'atwa huku ni kukatwa kizinda cha bibi harusi na bwana harusi na

kumuondoshea ubikira wake. Ukataji huu unafananishwa na mdudu anayeng'ata na kutoa damu. Bibi hurusi anaonekana kuogopa kukatwa na kutokwa na damu. Hata hivyo, katika mshororo wa mwisho wa wimbo anajibowi na kuambiwa na mamake "*mwanangu usilie ukamiliza na miee utalizoea hiloo*".

Taashira hii ya tendo ilivyotumika katika wimbo MKN.7, inajaribu kuwapa matumaini na kuwaondoshea wari (mabibi harusi) uoga wa kukutana na waume zao kimwili. Wimbo unawaandaa kisaikolojia wale wanaokaribia kuolewa na wale walioolewa karibuni watafahamu kuwa, tendo la ndoa ni jambo la kawaida katika maisha kati ya mume na mke. Si jambo la kuogopwa. Vilevile wanatiwa moyo, na kuambiwa kuwa mwanzo ni mgumu lakini baadaye watazoea. Haya yamejiri katika wimbo wakati bibi harusi analalamika na kusema "*mama njoo unifiche dudu laja hilo, sijazoweya hayo*". Mamake harusi anamjibu mwanawe na kumtoa wasiwasi kwa kumwambia "*utalizoweya hiloo*".

Taashira za tendo nyengine zilizomuhusu mwari zimebainika katika wimbo huu hapa chini.

#### MKN.8. KITAMCHOMA

*Kitamchoma eee kitamchoma*

*Kisiki cha mpera*

*Wapi?*

*Hapa*

*Patie dawa sana pasije pakabana*

*Pakamkera bwana*

*Usiku na mchana.*

Wimbo MKN.8 watu hupenda kumuimbia bibi harusi akiwa chumbani anamsubiri bwana harusi kuja baada ya kufunga ndoa. Wimbo huu uliambatana na vitendo vilivyoonekana katika picha ya video iliyorekodiwa wakati wa tukio hili. Vitendo ambavyo waimbaji walivifanya walipokuwa wakiimba ile sehemu isemeyo "*kitamchoma kisiki cha mpera*". Waliimba kwa sauti ya juu huku wakivilekeza vidole katika sehemu ya mbele ya bibi harusi (sehemu za siri). Vilevile ilionekana waimbaji wengine walikuwa wakifanya kama mzaha, wanauliza "*kitamchoma wapi?*" Wengine hujibu "*hapa*". Wakionyesha ile sehemu ya mbele ya bibi harusi. Tendo la kuvilekeza vidole sehemu ya mbele ya bibi harusi iliifanya hadhira nayo kurudia kipande hicho cha wimbo

kisemacho *wapi*? na kujibu "hapa" kwa sauti ya juu. Hali hii ilimfanya bibi harusi kupata uoga na haya na kujiāmulia kutizama chini.

Wimbo MKN.8 ulikuwa na taashira mbili za tendo. Taashira ya kwanza, *kitamchoma kisiki cha mpera* na ya pili *patie dawa sana pasije pakabana*. Katika taashira ya kwanza - neno la msingi lililotumika ni *kisiki cha mpera*. – hiki ni kipande cha mti kilichobaki katika ardhi. Wimbo umetumia mfano wa kisiki cha mpera kwa sababu ya umbo la kisiki cha mpera chenye mapindi na jinsi kilivyochomoza wima juu ya ardhi. Katika taashira ya pili neno la msingi ni *dawa*. Maana ya kawaida ya dawa ni kitu kinachotumiwa kutibu maradhi.

Maana ya kitaashira ya *kisiki* iliyoibuliwa kwenye wimbo MKN.8 inasimamia uume uliosimika. Tafsiri hii imetolewa kutokana na sababu mbili. kwanza kuwa umbo la kisiki cha mpera huwa na mapindi kama uume. Pili jinsi kisiki cha mpera kilivyochomoza wima juu ya ardhi kama uume uliosimika. Hivyo, maana kamili ya kitaashira *kitamchoma kisiki cha mpera* ni kuwa, bibi harusi atakutana na mumewe kimwili (kwa mara ya kwanza). Ama maana ya kitaashira *patie dawa* inasimamia kufanya tendo la ndoa. Tafsiri imetokana na jinsi taashira hii ilivyotumika katika wimbo inamaanisha kwamba bibi harusi alikutwa bikira na bado ana maumivu. Yaani kwa mujibu wa wimbo inaonekana kuwa bibi harusi ana maumivu au jeraha alilolipata kwa kuondolewa ubikira wake baada ya kuchomwa na "*kisiki cha mpera*". Hivyo kuondosha maumivu au jeraha hilo ni kuendelea kufanya tendo la ndoa. Taashira zilizotumiwa katika wimbo huu zinatoa mafundisho kwa wari au mabibi harusi wapya.

Umuhimu wa wimbo huu unatoa mafundisho zaidi kwa wari au mabibi harusi wapya nini cha kufanya baada ya kukutana kimwili kwa mara ya kwanza na waume zao. Yaani kutambua kuwa, tendo la ndoa katika maisha ya ndoa ni jambo la kawaida. Pia kutambua kuwa kuna jeraha au maumivu watakayoyapata baada ya kuondolewa ubikira na waume zao. Lakini cha msingi kufahamu ni kuwa maumivu watakayopata baada ya tendo hilo ni ya muda mfupi. Vilevile wimbo unatoa ujumbe kwa mke kutambua majukumu yake katika ndoa. Moja ya jukumu la mke ni kumstarehesha mume. Haya yameelezwa kupitia mshororo ufuatao unaosema: "*patie dawa sana pasije pakabana, pakamkera bwana*".

Wimbo mwengine uliotumiwa kutoa nasaha na mafundisho kwa mwari kwa kutumia taashira iliyobuliwa kama inavyoonekana katika nyimbo ifuatayo.

*MKN.10. UFUNGUO*

*Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo,  
Ee kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

*Kama hakumwita bwana, watamwitia wenziwe,  
Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

*Kama hakupokea, watapokea wenziwe,  
Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

*Kama hakumsugua, watasugua wenziwe,  
Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

*Kama hakutandika, watatandika wenziwe,  
Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

*Kama hakumchezea, watachezea wenziwe,  
Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

*Tena umwambie sana, asiache ufunguo,  
Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

Wimbo huu huimbwa wakati mwari akiwa chumbani baada ya kutolewa uzioni. Chumbani ndiko mwari hufunzwa mambo ya kiutuzima. Neno la msingi lililotumika kama taashira ni *ufunguo*. *Ufunguo* ni kifaa kinachotumika kufungulia au kufungia kufuli au kitasa. Maana ya kawaida ya *asiache ufunguo* ni kuwa, mwari anaambiwa asiuache *ufunguo* popote endako.

Kwa mujibu wa Bi. MwanaKheri aliyehojo wa tarehe 2/2/2010 *ufunguo* kwa maana ya kitaashira husimamia amana ya kumtunza mume. Yaani mume ni amana kwa mke, na anastahili kutunzwa kama wimbo unavyosisitiza katika kibwagizo cha kila ubeti "*Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo*". Wimbo unaeleza mambo ambayo mke anatakiwa amfanyie mumewe ili aweze kumtunza. Kadhalika wimbo umeeleza tahadhari ya kupuza au kutokfanya mambo hayo kwa mume. Mambo hayo ni kama vile mke kumwita mumewe bwana jina la heshima na kama hakufanya hivyo wanawake wengine watamwita bwana. Mke kumpokea bwanake anapokuja nyumbani na kitu chochote alichobeba na kumkaribisha kwa bashasha. Mke anatakiwa kumsinga bwanake kama hakufanya atapata wanawake wengine kumsinga. Mke asiwe mvivu wa kutandika kitanda na kukinadhifhisha chumba kuwa maridadi kama hakufanya wanawake wengine

watafanya kazi hiyo. Mke anatakiwa kumstarehesha bwanake na kama atapuuza hili basi bwana atapata wanawake wengine kumstarehesha. Haya ni baadhi ya mambo ambayo mke anatakiwakuyafanya ili aweze kumtunza mume asiende kwa wanawake wengine. Mambo haya ndio yanarejelewa kama *ufunguo*. Taashira ya tendo ya *asiache ufunguo* iliyotumika katika wimbo MKN.10. UFUNGUO ina umuhimu kwa wanandoa kufahamu majukumu yao katika maisha ya ndoa. Majukumu ambayo yakitekelezwa yataimarisha na kuifanya ndoa iwe ni yenye kudumu.

Baada ya singo kukamilika, mwari huimbiwa na watani huku akinywa chai. Taashira ya tendo ya *bibi anakunwa chai na chai sharbati lozi* katika wimbo MSG.21.CHAI SHARBATI LOZI huambatana na unywaji chai wa mwari. Chai iliyoandaliwa kwa ajili ya mwari huwa ni ya kukata na shoka. Huwa na mapochopacho na vitafunio kama sambusa, kababu, katlesi, vitumbua, donasi, maini, supu ya pweza, samaki wa kupaka, mkate wa kumimina, tambi, mkate wa ufuta na chai ya maziwa iliyotiwa lozi. Hivi ni vyakula vyta tunu vyenye lishe bora.

Tendo la kunywa chai katika wimbo huu linabeba maana tatu. Maana hizo zimefanuliwa na Bi Khadija aliyehojo wa tarehe 10/3/2010 hapa chini.

Maana ya kwanza ni kwa ajili ya kumuonyesha na kumfunza mwari kuwa, atakapoolwa anatakiwa amuandalie mumewe. Kwani upishi ni sifa mojawapo ya mwanamke wa Uswahilini. Mwanamke ambaye si "mpishi bora", huwa ni aibu kwake na familia yake. Yaani huonekana hakupata mafuzo ya kutosha kutoka kwao. Mwanamke kama huyu huitwa *mziavu* (mvivu). Hivyo basi, mapishi katika jamii ya Waswahili humaanisha mke bora.

Maana ya pili ya wimbo huu ni kuwa, mapishi bora ya mwanamke humfanya mume atulie nyumbani kwake (kudumisha ndoa). Wanaume wa Uswahilini hupenda sana mapochopacho. Hivyo basi, mke anatakiwa awe analyzingatia hili. Iwapo atashindwa kumuandalia mumewe huenda mume akamtoroka kama atapata "mwanamke" (hawara) wa kimuandalia na kumtunza vizuri. Hivyo mapishi pia huashiria kudumu kwa mapenzi katika ndoa.

Maana ya tatu ya wimbo huu ni kuwa, mwari anaonyeshwa na kufunzwa ili afahamu vyakula gani awe anamuandalia mumewe. Ni lazima viwe vyakula venye virutubishi katika mwili. Vyakula ambavyo vitawapatia nguvu wote wawili ili watakapofanya tendo la ndoa kupatikane mtoto. Jamii ya Waswahili huwashauri waliooana kutumia supu ya pweza, maziwa na lozi. Wanaamini kuwa vyakula hivi huzidisha mbegu za uzazi (manii).

Tukiendelea na uchanganuzi wa utendaji wa kunywa chai ni kwamba, kabla mwari hajamaliza kula, waandalizi huja kuondosha chakula huku huimbwa wimbo ufuatao:

#### MSG.22. PASALIAPO BASI

Mmekula mmeshiba

Pasaliapo basi

*Vikombe vyako chukua*

Pasaliapo basi

*Mikate yako chukua*

Pasaliapo basi

*Chai yako chukua*

Pasaliapo basi

...

Katika wimbo MSG.22 hauna maana kwamba mwari ananyang'anywa chakula la. Bali, tendo la kubakisha na kuondosha chakula limesaidia kupata maana ya taashira ya mmekula mmeshiba na pasaliapo basi iliyojitokeza katika wimbo huu. Maana ya taashira inayopatikana katika wimbo huu ni kuwa, mtu atakapokaribishwa, asile chakula chote. Anatakiwa afanye ustaarabu wa kula na kubakisha (sio kubakisha makombo). Yaani ale huku akikumbuka watu wa nyumbani. Bi Khadija alieleza kwamba, desturi ya Waswahili wanapoandaa chakula hukileta chote kama ni mezani au kwenye mkeka. Hivyo, hutarajia kuwa atakae karibishwa atakula kiasi chake na kuwakumbuka wengine. Si ustaarabu wa kula chakula chote. Hivyo, wimbo huu unaonyesha ustaarabu wakati wa kula.

#### 2. Taashira za Tendo zilizomuhusu Bwana Harusi

Taashira za tendo zilizomuhusu bwana harusi zilipatikana katika nyimbo zilizoimbwa katika miktadha tofauti harusini. Taashira hii ni kama vile: *Ataka kitabu achore\_na kalamu ashachonga ; sikumpa jembe kwenda kulima, kigongo mkononi ila na kusimbulia mke, waja huo wembe,*

*usiche bwana, ukiona bahari utaogelea, leo ni leo tutauona mpambano; Dakitari huyoo yuwaja Ajakitia dawa kidonda\_na tumkoshe mau bwana kwa mai ya zamzam.* Upatikanaji wa maana za taashira hizi umechananuliwa katika baadhi ya nyimbo zifuatazo:

*MBN.16. KITABU*

*Eeee leo achore  
Eeee leo achore  
Bwana harusi asema  
Ataka kitabu achore  
Na kalamu ashachonga  
Ataka kitabu achore*

*Eeeh leo achore  
Eeee leo achore  
Bwana harusi asema  
Ataka kitabu achore  
Na kalamu ashachonga  
Ataka kitabu achore*

Wimbo huu huimbwa katika tukio la bwana harusi anapoingia ndani. (Hii ni siku ya kwanza kwa bwana harusi kukutana kimwili na bibi harusi. Bwana harusi anaweza kuingia ndani (yaani kukutana na mkewe) kwa kina bibi harusi au kumchukuwa mkewe nyumbani kwake au hoteli). Muktadha wa wimbo huu huambatana na uigizaji. Uigizaji ambao ulifanywa na wanawake wa upande wa bwana harusi. Wanawake walikuwa wakiigizia tendo la kuchora katika kitabu kwa kutumia kidole cha kati cha mkono wa kulia juu ya kiganja cha mkono wa kushoto. Aidha, wanawake wengine waliigizia kama mtu anayechonga kalamu ya penseli. Walikuwa wakipenyeza kidole cha kati kwenye kiganja cha mkono wa kushoto kilichofumbwa. Wengine walikuwa wakicheza na kupiga vigelegele. Wanawake hawa walipofika nje ya nyumba ya kina bibi harusi, waliimba kwa vishindo hasa walipofikia ile sehemu isemayo *ataka kitabu achore, na kalamu ashachonga*. Takriba wanawake wote waliokuwepo hapa walikuwa wamejipamba kwa rangi za midomo, wanja machini na hina viganjani na miguuni. Vilevile walikuwa wamevaa magauni na kujitanda mitandio. Wengine wamevaa mabaibui.

Kwa upande wa bwana harusi wakati huu alikuwa na vazi lake alilofungia ndoa. (Bwana harusi alivalia Kiomani. Wakati mwengine mabwana harusi hupenda kuvalia Kisaudia). Kiomani huvalia - kanzu nyeupe ya darizi, tumboni amejizungushia kitambi kama mkaja kilichofungia jambia. Juu yake amevaa juba jeusi na kichwani amejifunga kilemba. Amevaa na viatu vya

makubadhi). Iwapo bwana harusi amevalia Kisaudia huvalia – kanzu nyeupe na joho aghalabu jeusi au la rangi ya samli na kilemba. Kwa kweli huwa anapendeza.

*Ataka kitabu achore na kalamu ashachonga* ndio maneno ya kitaashira ya tendo yaliyotumika katika wimbo MBN.16 KITABU. Maneno ya msingi ambayo yatatumiwa katika uchanganuzi kwa ajili ya kupata maana ya kitaashira ni: *kitabu, achore na kalamu*. Maana ya kawaida ya *kitabu* ni maandishi yaliyoandikwa na kuhifadhiwa katika kurasa. *Achore/(kuchora)* ni tendo la kufanya picha ya kitu au mtu kwa kalamu. *Kalamu* ni kifaa kinachotumiwa kuandikia au kuchorea kwenye karatasi.

Kwa mujibu wa muktadha na taashira zilizotumika katika wimbo, maana ya kitaashira *kitabu* inasimamia uke. Taashira *achore* husimamia tendo la ndoa na maana ya kitaashira *kalamu* ilisimamia uume. Tafsiri hizi zimetolewa kutokana na utendaji ulioambatana na taashira hizi. Tendo la kuigiza kuchonga *kalamu* (uume) na *kuchora* (tendo la ndoa) juu ya kitabu (uke) lilikuwa na maana pana zaidi. Yaani pale taashira inapoeleza "... ataka kitabu achore ilimaanisha kuwa, bwana harusi anataka kukutana na mkewe kwa tendo la ndoa. Ama "...na kalamu ashachonga ilimaanisha kusisitiza kuwa, bwana harusi yuko tayari, kwani kalamu (uume) uko tayari kwa tendo hilo (la kukutana na mkewe kimwili). Yaani tunawezakusemakwamba wimbo huu unaonyesha ujasiri wa mabwana harusi kuwa wako tayari kukutana kimwili na wake zao. Kwamba wao ni wanaume hawaogopi.

Taashira nyengine ya tendo iliyohusishwa na bwana harusi iliibuliwa kutoka wimbo huo hapa chini:

#### MKND.1. DAKTARI YUWAJA

*Vumilia huyooo eee kumbe  
Chamtonesha kidonda*

Dakitari huyoo yuwaja  
Dikitari huyoo yuwaja  
Ajakitia dawa kidonda

Wimbo huu huimbwa katika muktadha wa bwana harusi kuingia ndani. Kuingia ndani ni siku ya kwanza ambayo bwana harusi anakwenda kukutana kimwili na mkewe. Kawaida watu wa

upande wa bwana harusi wanapokuja kwa kina bibi harusi huenda kwa vishindo.Taashira za tendo zilizoibainishwa katika wimbo MKND.1 ni Dakitari huyoo yuwaja na Ajakitia dawa kidonda. Maneno ya msingi yaliyotumika ni: *kidonda, dakitari na dawa.* *Kidonda* ni jeraha; *dakitari* ni mganga aliyehitimu katika elimu ya tiba ya dawa za kisasa; *dawa* ni kitu kinachotumiwa kutibu maradhi.

Taashira zilizotambuliwa katika wimbo MKND.1 zilikuwa na maana ya kitaashira zifuatazo:- Dakitari huyoo yuwaja inasimamia bwana harusi (mume) yuwaja na Ajakitia dawa kidonda inasimamia kufanya tendo la ndoa. *kidonda* ilisimamia *uke*. Tafsiri hii imetokana na maneno ya msingi yaliyotumika kama taashra (*daktari, dawa na kidonda*). *Dakitari* ilisimamia bwana harusi (mume). *Dawa* ilisimamia tendo la ndoa na *kidonda* ilisimamia *uke*. Fasiri hizi zimetokana na jinsi taashira zilivytumika kulingana na muktadha wa uwasilishwaji wa wimbo wenyewe. Maana ya jumla ya taasira hizi zilizomuhusu bwana harusi ni mume anataka kukutana na mkewe kwa ajili tendo la ndoa.

Kwa mujibu wa muktadha na taashira zilizotumika, wimbo huu ulionyesha kazi na jukumu katika kutekeleza haja za kimwili za mwanamke. Kwa upande mwengine wimbo unaeleza kuwa bibi harusi baada ya tendo la ndoa atakuwa na maumivu. Hivyo anaandalisha kimawazo kuwa tayari kukabiliana na tendo hilo. Ni jambo la kawaida kwa kila mwanamke anayeolewa.

Wimbo mwengine uliobebea taashira za tendo zilizomuhusu bwana harusi ni huu hapa chini.

#### MKND.4. USICHE BWANA

Usiche Bwana harusi usiche

Usiche Bwana harusi usiche

Usiche Bwana harusi usiche

Ukiona bahari utaogelea

Usiche Bwana harusi usiche

Ukiona bahari utaogelea uvuke

Usiche Bwana harusi usiche

Usiche Bwana harusi usiche

Wimbo huu huimbwa katika tukio la bwana harusi anapokwenda kutoa mkono. Jamaa wa upande wa bwana harusi hasa wanawake humshindikiza kijana wao kwa nyimbo mbalimbai ikiwemo hii MKND.4. Wanawake hawa humtia moyo na kumuondoshea uoga bwana harusi

kwa kumwimbia "*usiche bwana harusi usiche ukiona bahari utaogelea uvuke*". Huendelea kuimba mpaka wanapofika nje ya nyumba ya kina bibi harusi. Bwana harusi hukaribishwa na hushindikizwa mpaka chumbani alimokaa bibi harusi na kutoa mkono. Bibi harusi huwa amekalishwa juu ya kitanda akiwa amepambwa. Mikononi na miguuni huwa amechorwa kwa hina na piko. Aghalabu siku hii, huwa amevalishwa vazi ya rangi ya kijani na amefinikwa mtandio kutoka kichwani hadi usoni kama anavyoonekana katika picha hapa chini.



**PICHA 2. Bibi harusi Amefinikwa Anamsubiri Bwana Harusi Kuja Kutoa Mkono**

*PICHA 14 ni ya bibi harusi akiwa chumbani anamngojea bwana harusi kuja kutoa mkono. Ameva vazi ya rangi ya kijani na mtandio wa hariri umemfunika uso. Kwa mujibu wa Bi Sihaba aliyeojiwa tarehe 6/8/2010 anasema, bibi harusi siku hii kuvalishwa vazi la rangi ya kijani inabashiria kupata kizazi "fertility". Picha hii ilipigwa tarehe 10/6/2010, Kisauni - Unguja.*

Bwana harusi anapoingia, humuekea mkono kichwani bibi harusi kumuombea duwa kisha humpa mkono. Upeanaji mikono ni kama unavyoonekana katika ifuatayo.



### **PICHA 3. Maharusi Wakipeana Mikono**

*PICHA 15 mtu aliyesimama upande wa kulia ni bwana harusi anampatia mkono bibi harusi kabla ya kumfungua uso. Bi Sihaba anaeleza tena kuwa, tendo la bwana kumpa mkono bibi harusi linaashiria muungano. Picha hii ilipigwa tarehe 10/6/2010, Kisauni - Unguja.*

Katika wimbo MKND.4 USICHE BWANA maneno ya msingi yaliyotumika kwa ajili ya kupata maana ya kitaashira ni *bahari* na *utaogelea*. Maana ya kawaida ya *bahari* ni eneo kubwa la maji ya chumvi linalozingira mabara na visiwa. Ama *utaogelea* ni tendo la kuwa juu ya maji na kuenda bila ya kuzama. Maana za kitaashira za maneno yaliyotumika katika MKND.4, neno '*bahari*' kitaashira linasimamia uke wa mwanamke (bibi harusi), ambao bwana harusi anaambiwa katika wimbo, '*ukiona bahari utaogelea*'. Kitendo cha '*utaogelea*' kitaashira kinasimamia kufanya tendo la ndoa kama alivyoeleza Timamy (2002) katika kazi yake Tafsiri hii imehusishwa na dhana ya muogegeleji anavyoogelea anapokuwa majini. Vilevile, tendo la kuogelea baharini linahusishwa na uoga. Sio kila mtu anaweza kuogelea baharini. Kuogelea kunahitaji ujuzi na uzoefu. Hata hivyo, kuogelea huku kitaashira kuna maana ya jinsi bwana harusi atakavyofanya tendo la ndoa akiwa na mkewe kwa mara ya kwanza. Hii ni siku muhimu na ngumu kwa bwana harusi. Ni siku ambayo jamaa wa bwana harusi huwa wanasubiri kwa hamu na ghamu kutaka kujuu kama kijana wao atafanikiwa kuonyesha urijali wake. Haya yamefanuliwa na Haji Hamisi alipohojiwa tarehe 15/1/2010. Kwa mantiki hii, bwana harusi anachukuliwa anaogopa kufanya tendo la ndoa kwa sababu hana ujuzi (yaani hajawahi kufanya

tendo hili). Vilevile bwana harusi siku hii anatakiwa kuonyesha uanaume wake. Ndio katika wimbo anatiwa moyo kwa kuambiwa asiogope.

Wimbo huu unawahamasisha na kuwatoa uoga mabwana harusi kukutana kimwili na wake zao. Kawaida siku kama hii mabwana harusi huwa wanauoga fulani, kwa sababu nao ni wanagenzi kuhusu kufanya tendo la ndoa.

MKND.6. TUMKOSHE MAU BWANA ni wimbo mwengine unaoimbwa katika muktadha wa bwana harusi anapoingia nyumbani kwa kina bibi harusi kutoa mkono. Wimbo huu ulibeba taashira za tendo au matendo yaliyomhusu bwana pia. Taashira ya za tendo hilo ni tumkoshe mau bwana na mai ya zamzam. Kama ilivyoelezwa katika wimbo ufuatao:

*MKND.6. TUMKOSHE MAU BWANA*

*Tumkoshe mau bwana*

*Kwa mai ya zamzam.*

Katika wimbo huu hapa juu, maneno ya msingi yaliyotumiwa kuibua taashira ni *mau na mai ya zamzam*. *mau na mai* ni maneno yanayotumika katika lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu. *mau* ina maana ya miguu na *mai* ina maana ya maji. *Zamzam* ni maji yenye baraka yanayopatikana kwenye chemchemu maalum kwenye mji wa Makkah iliyoko Saudi Arabia. Maji ya zamzam mbali na kutumiwa katika matumizi mengine ya kawaida, hutumiwa kama dawa. Hivyo basi, maana ya kawaida ya taashira hii ni kumsafisha bwana harusi miguu kwa maji ya zamzam. Wimbo huu huimbwa huku ukiambatana na utendaji wa kuoshwa miguu bwana harusi.

Bwana harusi akifika nyumbani kwa kina bibi harusi hukaribishwa ukumbini. Hapa tena hukalishwa juu ya kiti na kuoshwa miguu kabla ya kuingia chumbani alimo bibi harusi. Bwana harusi huweza kuoshwa kwa maji ya zamzam au maji ya nazi. Iwapo bwana harusi atakoshwa kwa maji ya nazi, nazi hiyo hutobolewa kwa msumari kwenye mdomo wake na maji yake huoshewa miguu. Kungwi ndiye anayemuosha miguu bwana harusi huku wanawake wa upande wa bibi harusi wakiimba, kupiga makofi na vigelegele. Maji ya nazi yakishamalizika, nazi huvunjwa kwenye kizingiti cha mlango ili ivujike vipande vipande.

Kulingana na muktadha wa wimbo MKND.6 maana ya kitaashira ya tendo la kuoshwa miguu bwana harusi husimamia maana mbili - heshima na kutolewa nuhusi. Maana ya kwanza,

kuoshwa miguu kwa bwana harusi kunaonyesha heshima anayopewa kwa kukaribishwa nyumbani na jamaa zake mke. Maana ya pili ya tendo hili, ni tambiko analofanyiwa bwana harusi. Lengo hasa ni kumkinga na kumuondoshea nuksi. Huenda ikawa mume / bwana harusi amewekewa kitu kibaya njiani ili akikanyage na kumdhuru.

Maana ya kitaashira ya tendo la kuvunjwa nazi kizingitini husimamia kuondoa shari au kitu kibaya kilichowekwa mlangoni. Nazi inapopigwa kizingitini inatakiwa ivunjike vipande vipande. Kuvunjika vipande vipande kwa nazi kunaashiria kuwa shari au kitu kibaya kilichowekwa mlangoni nacho kimevunjika kama mfano wa nazi ilivyovunjika. Na iwapo nazi haikuvunjika, humaanisha kuwa bado shari haijatoka. Haya yameelezwa na Mzee Haji Gora (ameshatajwa).

Umuhimu unaopatikana katika wimbo huu, unaonyesha ada muhimu ambazo hufanyiwa bwana harusi wakati wa harusi. Tendo la bwana harusi kuoshwa miguu wakati wa uwasilishwaji wa wimbo huu, vilevile linaonyesha kuwa ni jambo adhimu na bwana harusi ni mtu muhimu katika jamii. Heshima anayopewa na tambiko afanyiwalo hawezi kufanyiwa kama mtu hajaoa. Baadhi ya hadhira kuhusiana na tendo la kuoshwa miguu walisema, 'Jambo hili huwatia moyo au kuwahamasisha vijana kuoa'.

### **3. Taashira za Tendo zilizomuhusu Mamake Harusi**

Taashira za tendo nyengine zilizobainika katika nyimbo kumuhusu mamake bibi harusi ziliwu ni: *mwanangu kipande cha papa, nateremka bonde na kicheko, dada Mwajuma kashaukata ubeleko, uchungu wa mwana ajuwaye Fatuma mzazi na tumejizungua kwa yasin tatu halitupati jicho la mtu.*

Kwa mfano wimbo MKU.3 unawakilisha sauti ya mamake bibi harusi kuiambia hadhira wasiwe na kijicho na mwanawe. Haya yameelezwa katika wimbo ufuatao hapa chini:

**MKU.3. TUMEJIZUNGUA**  
Tumejizungua kwa ya Yasin tatu  
Halitupati jicho lolote la mtu

Wimbo huu huimbwa wakati bibi harusi anapoingizwa ukumbini ('holini') akiwa amevalia kizungu. Yaani amevaa veli la rangi nyeupe na mikononi amebeba maua. Wakati anapoingizwa

na kupitishwa katikati ya hadhira iliyopo, kila mtu hutaka kumtazama. Wakati huu hadhira hupiga makofii na vigelegele huku wakiufuatilia wimbo MKU.3 unaoimbwa. Wimbo huu huweza kuimbwa na kikundi cha taarabu kilicho kodiwa au kutia kanda katika tepu na kusikika kwenye masipka makubwa. Baada ya bibi harusi kukalishwa kwenye kochi, sasa kila anayetaka huenda mbele ya ukumbi na kucheza wakiwa katika duara. Aghalabu, siku hii, wanawake walioalikwa huwa wamejipamba na kujitona. Holini huhanikiza harufu za udi walizojifukiza wanawake.

Wimbo huo hapa juu umetokea kubeba taashira mbili za tendo. Taashira ya kwanza, *tumejizingua kwa yasin tatu* na ya pili *halitupati jicho lolote la mtu*. Katika taashira ya kwanza: - neno la msingi lilitumika ni *yasin*. *Yasin* kwa maana ya kawaida ni sura ya thelethini na sita (36) katika Qur'ani tukufu. Ama katika taashira ya pili neno la msingi lilitumika ni *jicho*. *Jicho* ni kiungo cha mwili cha kuonea.

Kulingana na wimbo MKU.3 ulioambatana na muktadha wa kuingia holini maana ya kitaashira *tumejizingua kwa yasin tatu*. husimamia kinga au kujihifadhi. Maana hii imetolewa na Shk. Khamis Suleman aliyehojiwa tarehe 1/9/2010. Alieleza kuwa" sura ya *yasin* ni moyo wa Qur'ani tukufu. Hivyo basi, Waswahili Waisilamu huitumia sana kuisoma sura hii kwa ajili ya kujikinga na ubaya. Anaendelea kufafanua kuwa, jamii ya Waswahili Waisilamu wanaitikadi kuwa, mtu anapoisoma au kusomewa sura ya *yasin* jambo baya halimfiki.

Ama taashira ya pili ya neno *jicho*, inasimamia husuda inayoweza kumpata mtu. Hivyo maana kamili ya taashira hii jinsi ilivyotumika katika wimbo" *halitupati jicho lolote la mtu*" ina maana kwamba, hakuna husuda yoyote itakayompata (bibi harusi) kwa sababu wamejikinga kwa *yasin*. Kuhusudiana ni moja ya tabia walioyonayo Waswahili. Baadhi ya watu katika jamii hii huwa na tabia ya kuwaonea kijicho wana wa wenzao wanapopata mafanikio. (Husuda ni ile hali inayomfanya mtu kuhisi vibaya anapoona mwenziwe kaneemeshwa. Na wakati mwengine kumfanya hata kufikia hatua ya kumdhuru huyo mwenye kuneemeshwa). Kwa mfano, mtoto wa kike anapopata bahati ya kuolewa wengine huwa hawalipendelei jambo hili huanza kuwaonea kijicho au husuda.

Kwa kutilia msisitizo umuhimu wa kusoma au kusomewa *sura ya yassin* Mfaume Haji alipohojiwa tarehe 10/9/2010 alikuwa na maoni kama ya Shk Khamis Suleiman. Mfaume alielezea kuwa "sura ya Yasin ni dawa na ni kinga unapoisoma". Kwa mujibu wa muktadha na taashira zilizotumika, wimbo huu unajaribu kuwaonya au kuwakemea wale wote wenye tabia ya kuhusudu wana wa wenzao. Aidha, kupitia taashira hizi wimbo unaonyesha umuhimu wa baadhi ya sura katika Qur'ani tukufu kutumiwa kama kinga dhidi ya ubaya.

Mamake bibi harusi anasikika tena akimpa nasaha mwanawewe wakati wa kumuaga kupitia wimbo ufuatao:

*MKND.9. MAJUMBANI*

*Mama ukakae na mumeo*

*Vumilia mambo ya nyumbani*

*Mwanangu kipande cha papa*

*Vumilia mambo ya nyumbani kunga.*

Wimbo MKND 3 huimbiwa bibi harusi nyumbani kwao kabla hajapelekwa kwake. Wimbo huu hutumiwa kama nasaha kwa bibi harusi jinsi ya kwenda kuanza maisha yake na mumewe. Hadhira iliyopo wakati huu ni pamoja na kungwi na jamaa wachache (wanawake) wa bibi harusi. Kwa niaba ya mamake bibi harusi, kungwi ndiye anayeimba wimbo MKND 3 wenye nasaha na watu wengine wanaitikia kwa kupiga vigelegele na makofi.

Mshororo wa tatu (3) sauti ya mama inasikikika ikimwambia mwanawewe (bibi harusi)"*mwanangu kipande cha papa vumilia* ni taashira ya tendo iliyobuliwa katika wimbo MKND 3. Maneno ya msingi yaliyotumika kwa ajili ya kupata maana ya kawaida na ya kitaashira ni *kipande cha papa*. Maana ya kawaida *kipande cha papa* kama inavyofahamika na wengi ni sehemu ndogo ya nyama ya papa (aina ya samaki) aliyekaushwa, mfano wa ng'onda.

Maana ya kitaashira ya *kipande cha papa* husimamia maisha ya tabu (katika ndoa). Tafsiri hii imetolewa kulingana na mtazamo wa jamii ya Waswahili wanavyotumia papa. Papa huchukuliwa ni kitowea cha rahisi (duni). Watu wa jamii hii hulazimika kutumia papa/ng'onda pale inapotokea mtu hana kitu nyumbani. Kutokana na ukosefu wa mtu kumudu kitoweo kama samaki mbichi au nyama na kuambulia ng'onda huchukulia kuwa hiyo ni taabu.

Hivyo kulingana na matumizi ya taashira hii, bibi harusi anatakwa awe ni mwenye kustahamili kwani maisha ya ndoa sio kustarehe tu bali kuna matatizo. Pia anatakiwa asitoe siri za nyumba nje kama wimbo unavyoeleza '*mambo ya nyumbani kunga*'. Yaani asimueleze mtu ye yote mambo ya nyumbani kwake. Hivyo basi, wimbo unatoa nasaha na mafundisho kwa jamii kufahamu upande mwengine wa maisha katika ndoa. Yaani katika maisha ya ndoa kuna panda shuka. Vilevile, huelezea majukumu kwa wanandoa jinsi ya kuishi na kuifanya ndoa yao iwe ni yenye kudumu. Muhimu kwa wanandoa (wenza) wanatakiwa wawe ni wenye kuvumilia na kuhifadhi siri za ndani katika maisha ya ndoa.

### **4.3. Matokeo ya Utafiti**

#### **4.3.1 Matokeo ya Maana za Taashira za Vitu Tendo**

Utafiti uligundua kuwa, baadhi ya taashira za vitu katika nyimbo, zilitolewa maana ya kitaashra kwa kunasibishwa na umbo na utenda kazi wa kitu. Kwa mfano, taashira mbalimbali zilizotumiwa katika nyimbo kuhusu umbile la uume kama vile: *muhogo, kisiki na kijiti* umetokana na jinsi maumbo ya taashira hizo husimamia **umbile la uume uliosimika**. Ama *samaki mwenye jicho moja* amenasibishwa na **umbile la uume lenye "jicho" moja**. Taashira kama *pembe, kalamu na mtaimbo* zimetumiwa kusimamia umbile la **uume wenye ncha mbele**.

Taashira za viumbe kama *koko* ilisimamia **mume/bwana harusi** na *njiwa* ilisimamia **mke/bibi harusi**. Tafsiri ya mke kuwa njiwa imetokana na uzuri wa sura ya njiwa. Vilevile katika muktadha mwengine taashira za *mtango, mche na utango* na jinsi zilivotumika katika nyimbo zilisimamia **kizazi**. **Mke/bibi harusi** harusi anatarajiwa baada ya kuolewa aendeleze kizazi. Taashira za mimea hii *mbegu na utango* zilitumika pia kusimamia **mke/bibi harusi**.

Taashira nyingine kama vile: *kidonda, kitabu na kijungu* zilisimamia **uke**. Aidha, tendo la ndoa limeashiriwa na taashira za vitu kama: *dawa, bahari na kuchora*. Utendaji kazi wa taashira za vitu kama *jembe* ilisimamia **kazi ngumu**. Uume pia uliashiriwa na taashira kama vile: *mtaimbo, dudu, mashini na wembe*. Tafsiri hii, ilitolewa kwa kuhuishwa na ile dhana ya uume unavyofanya kazi ya kuvunja au kukata ubikira (kizinda cha mwari) sawa na unavyofanya kazi mtaimbo kuvunja mawe au wembe kukata kitu kwa makali na kutoa damu.

### **4.3.2 Matokeo ya Maana za Taashira za Tendo**

Matendo yaliyotajwa katika wimbo ndio yaliyotambuliwa kama taashira za tendo. Utafiti umegundua kuwa, maana ya taashira za tendo zimejikita zaidi kwa kuhusishwa na matendo yaliyomhusu mwari/bibi harusi, bwana harusi na machache kuhusu mamake harusi. Mathalani:

#### **Taashira za Tendo zilizomhusu mwari**

Taashira za tendo zilizomhusu mwari kama vile *muenge kama kioo, uwe mke siti mwenye mahaba na ukaone haya zilimaanisha*, mwari amhudumie mumewe kwa upendo, heshima na awe na haya. Taashira kama *mama njoo unifiche dudu laja hilo na kitamchoma kisiki cha mpera zilisimamia kufanya tendo la ndoa*. Taashira *kipande cha papa vumilia ilisimamia shida katika maisha ya ndoa*.

#### **Taashira za Tendo zilizomhusu bwana harusi**

Taashira za tendo zilizomuhusu bwana harusi kama vile: *sikumpa jembe kwenda kulima, raha ya mume ee kula na nguo, na maneno mema yenyе kituo; kigongo mkononi; kusimbilia mke*. Taashira hizi zilisimamia majukukumu ya mume kwa mkewe. Ama taashira kama: *ataka kitabu achore na kalamu ashachonga; waja huo wembe waja huo wembe, dakitari ajakitia dawa kidonda na usiche bwana ukiona bahari utaogelea*. Taashira hizi vilevile zilisimamia bwana harusi kukutana kimwili na mkewe (tendo la ndoa).

#### **Taashira za Tendo zilizomhusu mamake harusi**

Taashira za tendo zilizomuhusu mamake harusi kama vile: *.nateremka bonde nakicheko, dada Mwajuma kashaukata ubeleko na uchungu wa mwana ajuwaye Fatuma mzazi*. Ufasiri wa taashira hizi ni kwamba, mamake harusi anafuraha ya kumuozesha mwanawe baada ya taabu ya malezi aliyopata. Taashira ya *tumejizungua kwa yasin tatu halitupati jicho la mtu ilimaanisha kupata kinga kutoka kwa Mungu*.

### **4.4 Hitimisho**

Sura hii imeshughulikia data ya utafiti ambayo ni taashira za vitu na tendo. Data hiyo imewasilishwa na kuchanganuliwa kwa mujibu wa Nadharia ya Semiotiki. Katika sehemu ya kwanza ya sura hii utafiti ulishughulikia taashira za vitu vilivyoibuliwa katika nyimbo,

vilifasiriwa na kutolewa maana ya kitaashira. Taashira za vitu nyingi zilibainika kurejelela vitu vinavyopatikana katika mazingira yaliyowazunguka pamoja na vitu wanavyovitumia katika maisha yao ya kila siku. Ama sehemu ya pili ya sura hii, utafiti ilijikita zaidi katika taashira za tendo zilizotajwa nyimboni. Taashira za tendo nyingi zilizotumika zilimuhusu mwari au bib harusi. Taashira za tendo chache zilimuhusu bwana harusi. Hii ina maana kuwa nyimbo nyingi za harusi huwa zinawalenga wanawake hasa bib harusi na wari. Ndiyo utaona kuwa ujumbe unaotolewa katika nyimbo za harusi nyingi zinawarejelea mabibi harusi na wari.

Katika sura ya tano utafiti ulishughulikia uchanganuzi wa utendaji uliokuwa ukifanyika wakati wa uimbaji. Huu ulikuwa ni utendaji uliokuwa ukifanywa na waimbaji na wachezaji. Halikadhalika utendaji huu uliaminika kuwa na maana wa kitaashira.

## **SURA YA TANO**

### **UCHANGANUZI WA UTENDAJI WAKATI WA UIMBAJI**

#### **5.0 Utangulizi**

Sura hii imejihuisha na uwasilishaji pamoja na uchanganuzi wa data ya utafiti huu ambayo ni utendaji uliokuwa ukifanyika wakati wa uimbaji nyimbo za harusi pamoja na maana zilizotolewa na wasailiwa kuhusu utendaji uliofanywa wakati wa nyimbo.

Kwa vile madhumuni yetu ya tatu ya utafiti huu yalikuwa ni kubainisha na kutoa maana ya utendaji wakati wa uimbaji nyimbo za harusi kwa hiyo, data iliyokusanywa imewasilishwa ili kujibu maswali ya utafiti huu, ikachanganuliwa kimaaelezo kutokana na mwongozo wa Nadharia ya Utendaji. Hivyo basi, kutokana na maelezo haya, sura hii imegawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ilishughulikia utendaji uliombatana na taashira wakati wa kucheza na kuimba. Sehemu ya pili imejihuisha kuchunguza na kufasiri utendaji katika matukio yanayoashiria mambo ya kitaashira wakati wa uimbaji. Sehemu ya tatu imejikita zaidi kufasiri utendaji wa uigizaji wa vitu vya bibi harusi wakati wa kuimba nyimbo.

#### **5.1 Ufasiri wa Maana ya Utendaji wakati wa Uimbaji Nyimbo Harusini.**

Katika hatua hii mtafiti alijaribia nadharia tete ya tatu ya utafiti. Katika hatua hii, uchanganuzi ulizingatia utendaji uliyofanywa wakati wa uimbaji. Kama tulivyoeleza katika utangulizi kuwa kulikuwa na utendaji wa aina tatu. Kwanza utendaji ulioambatana na taashira wakati wa kucheza na kuimba. Pili utendaji katika matukio yanayoashiria mambo ya kitaashira wakati wa uimbaji. Tatuhu utendaji wa uigizaji wa vitu vya bibi harusi wakati wa kuimba nyimbo.

Kama tulivyoeleza katika usuli wa mada, kutokana na ufanuzi wa Askew (1997) na Ntarangwi (2001) kuwa maana katika uwasiliswaji wa nyimbo hutambuliwa kwa kukutanisha matini na utendaji ulijojumuisha matendo yajulikanayo kwa undani na wenyeji. Aidha, utendaji kama vile: ukataji kiuno, matendo ya wachezaji kama vile - miondoko na matumizi ya viungo wakati wa uimbaji yote haya huchangia kupata maana ya nyimbo.

Kutokana na mawazo ya Askew na Ntarangwi mtafiti aliamua kufanya uchanganuzi na ufasir wa kupata maana ya utendaji uliofanywa na washirika wakati wa uimbaji kulingana muktadha wa

tukio. Mtafiti alichunguza kwa undani uwasilishwaji wa kila wimbo kwa kutilia maanani vipengele vitano (5) vifuatavyo hapa chini:

- (i) Kudadisi utendaji unaofanywa na anayefanya wakati wa uimbaji.
- (ii) Ni nani anayefanyiwa?
- (iii) Matendo hufanyika wapi?
- (iv) Matendo hufanyika viper? (Yaani kuchunguza ishara za lugha na uambatano wa matendo ya wachezaji kama vile: miondoko na matumizi ya viungo).
- (v) Kuzingatia fasiri za wasailiya kuhusu maana ya utendaji.

Kila kipengele hapa juu kilikuwa na umuhimu wake. Vipengele hivi vilitumiwa na mtafiti kuchunguza kwa undani uwasilishwaji wa kila wimbo. Lengo ni kuangazia zaidi matukio na matendo yenye yanavyodhahirika. Uchanganuzi huu pia, ulimwezesha mtafiti kupata ufaafu wa nyimbo hizo kulingana na muktadha wa ndoa ya jamii ya Waunguja. Mtafiti alitumia mbinu ya kimaelezo kufasiri matendo ya washiriki kwa vile matendo husaidia pakubwa kupambanua maana za taashira katika nyimbo. Uchanganuzi wa utendaji ulitegemea zaidi data zilizorekodiwa kwa kamera ya video pamoja na kumbukumbu zilizoandikwa wakati wa ushiriki na uchunguzi nyanjani.

Utendaji uliotambuliwa na kuaminika kuwa na maana uliooredheshwa na kufasiriwa. Utendaji huo ulifasiriwa na kutolewa maana kulingana na muktadha wa kila wimbo. Mtafiti aliwaauliza wasailiya kuhusu matendo ya kitaashira yalikuwa na maana gani wakati wa uwasilishwaji wa nyimbo.

### **5.1.1 Utendaji Ulitoambatana na Taashira wakati wa Kucheza na Kumba**

Huko nyanjani ilidhihirika kwamba, baadhi ya nyimbo zilizokuwa zimetaja taashira ziliambata na utendaji tofauti uliofanywa katika miktadha tofauti harusini. Utendaji ulitoambatana na taashira wakati wa uimbaji ni huu ufuatao. Utendaji huu ulitolewa ufasiri wa maana zake kwa kila mmoja.

- (i) Wanawake kuviringisha vidole vya katikakati.
- (ii) Kukata/kuvitingisha viuno.

- (iii) Kupiga makofi.
- (iv) Kupiga vigelege.
- (v) Kuigiza Kupara samaki.
- (vi) Kuigiza kuchora na kuchongo kalamu
- (vii) Kupiga miguu chini.

## **1: Wanawake Kuviringisha Vidole vya Katikati**

Taashira ya (kitendo) *huyo ajaye mwana wa siwa* ni taashira katika wimbo wa kupeleka mahari MMH.2. Jahazi. Taashira hii iliambatana na utendaji wa wanawake kunyosha mikono na kuviringisha vidole vya katikati. *Siwa* ni baragumu kubwa aghalabu la pembe ya ndovu au lilichongwa kutokana na mti maalumu (TUKI: 2006:379). Topan (1993:96). anaelezea kuwa, "*siwa* ni baragumu linalopulizwa wakati wa harusi za Waswahili kwa baadhi ya familia wenye uwezo hapo zamani. Kwa kawaida *siwa* humilikiwa na watu wanaotoka tabaka la juu". Wanawake kutoka upande wa bwana harusi wanapoimba *huyo yuwaja mwana wa siwa* walikuwa wakijigamba kuwa kijana wao (bwana harusi) anatoka katika familia teule. Kwa sababu hii wanawake hawa walikuwa wakiimba kwa sauti, huku mikono yao ikiwa juu, wakiviringisha vidole vya katikati na wakijitingisha miili yao kama inavyooonekna hapa chini.



**PICHA 4 Kuviringisha Kidole cha Katikati.**

*Hawa ni wanawake wa upande bwana harusi wamekuja na vishindo na vurumai kwa kina bibi harusi. Wanaimba huku wakiviringisha vidole . Sokoni -Makunduchi.*  
10/10/2009.

Utendaji huu wa kuviringisha vidole vya katikati wa wanawake wa upande wa mume waliwafanyia wanawake wa upande wa mke. Utendaji huu ulisaidia kupambanua maana ya taashira ya huyo yuwaja mwana wa siwa katika wimbo MMH.2. Maana iliyoibuliwa ni kuwa, utendaji wa kuviringisha vidole vya katikati husimamia kujigamba. Haya yamefanuliwa na Bi Hafuswa aliyehojo wa tarehe 10/12.2009.

## **2: Kuigiza Kupara Samaki**

### **MBN.20. UTAMPARA SAMAKI**

*Umetaka mwenyewe kuolewa*

*Utampara samaki*

*Samaki anamagamba eee*

*Utampara samaki*

*Samaki anajicho moja eee*

*Utampara samaki*

Wimbo huu MBN.20 uliimbwa wakati bibi harusi anamsubiri bwana harusi kuja kutoa mkono na baadaye kumchukuwa mkewe. Wimbo huu uliambatana na uigizaji. Uigizaji ulifanywa na wanawake, wanaimba wakiigiza kwa mikono yao iliyokuwa mbele ya sehemu zao za siri jinsi samaki anavyoparwa. Walikuwa wakiviringish viuno. Uikizaji wa kupara samaki na kuviringisha viuno ulisimamia kufanya tendo la ndoa.

## **3: Kukata Kiuno**

Ukataji wa kiuno kwa wanawake ulikuwa ukifanyika katika matukio mbalimbali harusini wakati wa uimbaji. Ntarangwi (2001) anafafanua kuwa uchezaji na ukataji kiuno wakati wa uwasilishwaji wa nyimbo unachangia kupata maana ya nyimbo. Utafiti huu uligundua kwamba ukataji wa kiuno ulitofautiana kulingana na muktadha wa tukio harusini. Kulikuwa ukataji wa kiuno kwa ajili ya kujifurahisha tu. Kadhalika kulikuwa na ukataji wa kiuno kama mitindo au mizungu ya kufanya tendo la ndoa.

Ukataji wa kiuno kwa ajili ya kujifurahisha ulikwenda sambamba na uimbaji wa nyimbo kama vile: MKN.4. HODI, MKN.5.NOTI NAIRARWE na MKN 3.YUWAPI MAMIE HARUSI.

Kwa mfano katika wimbo MKN 3.YUWAPI MAMIE HARUSI uliimbwa na wanawake huku wakicheza kwa kukata viuno. Wimbo wenyewe ni huu hapa chini.

**MKN. 3.YUWAPI MAMIE HARUSI**

*Yuwapi eee,*

*Yuwapi eee,*

*Yuwapi mamie harusi,*

*Aje hapa tuangaike naye,*

*Aje hapa tuangaike naye*

Utafiti ulishuhudi kuwa wimbo huu MKN. 3 uliimbwa katika harusi tofauti huku ukiambatana na uchezaji wa kukata kiuno. Tazama ukataji wa kiuno kwa ajili ya kujifurahisha uliofanywa katika harusi ya mjini katika PICHA 5 na harusi ya shamba katika PICHA 6 hapa chini.



**PICHA 5 Ukataji Kiuno Kujifurahisha (Harusi ya Mjini)**



**PICHA 6 Ukataji Kiiuno Kujifurahisha (Harusi ya Shamba).**

PICHA 5 na PICHA 6 ni ukataji kiuno ulikuwa ni kwa ajili ya kujifurahisha na kucheza tu. Watani na waalikwa wakati wa uimbaji wa nyimbo hizi walikuwa wakiimba, wengine wakicheza kwa kusuasua mabega na wangine wakikata viuno. PICHA 5 ilipigwa katika harusi moja ya mijini iliyofanyika tarehe 12/12/2010, Vuga - Unguja. Ama PICH 6 ilipigwa katika harusi moja ya shamba iliyofanyika tarehe 5/9/2009, Gombani – Tumbatu.

Ama ukataji wa kiuno uliofanyika katika uimbaji wa nyimbo kama vile: MSG.14. CHAMBA, MKN.8. KITAMCHOMA, MKN.9 KULA MUHOGO na MBN.14. KUTANDIKA ulikuwa na maana ya kumfunza mwari au bibi harusi mizungu/mitindo ya kufanya tendo la ndoa. Picha hizi hapa chini zinaonyesha ukataji kiuno wa kumfunza bibi harusi mitindo ya kufanya tendo la ndoa.



**PICHA 7 Mizungu ya Ukataji Kiuno.**

*Katika PICHA 7 .Upande wa kulia ni mmoja wanawake akimwonyhesha bibi harusi mitindo ya ukataji kiuno. Upande wa kulia ni bibi harusi akiwa na mumewe wakiwa wamekalia kochi.. Picha ilipigwa tarehe 12/12/2010 Vuga- Unguja.*

Wimbo mwengine uliokuwa na utendaji kama huu wa kukata viuno mbele ya bibi katika mitindo mbalimbali ni huu ufuatao.

***MBN.20. UTAMPARA SAMAKI***

*Umetaka mwenyewe kuolewa*

*Utampara samaki*

*Samaki anamagamba eee*

*Utampara samaki*

*Samaki anajicho moja eee*

*Utampara samaki.*

Utendaji unaofanywa na maswali yanayozungumziwa katika uimbaji wa nyimbo MKN.8, MBN.15 na MBN.20 ndio yaliyopelekea bibi harusi au mwari kuinamisha kichwa chini. Wengine walio kuwa wakicheza mbele yake walikuwa watu anaowahishimu mfano shangazi lake. Jambo kama hili pia lilimfanya asiweze kuangalia yanayofanyika au kusemwa kwa sababu ya haya. Tendo hili la kuinamisha tumelidhihirisha katika picha ifuatayo hapa chini.



**PICHA 8 Bibi Harusi Anafundishwa Mizungu**

*Kushoto ni bibi harusi anatazama mitindo ya ukataji kiuno kwa haya nyingi. Anayecheza mbele yake ni shangazi yake amejifunga khanga kiunoni. Anacheza huku akimuonyesha mitindo mbalimbali ya ukataji kiuno. Wanawake wengine wanaimba, wanapiga makofi na vigelegele. Picha hii imepigwa katika moja ya harusi za mjini kabla nikaha kufungwa Kisauni - Unguja, 10/6/2010.*

Wimbo wa MBN 14. KUTANDIKA ni mmoja wa wimbo unaoimbwa huku wanawake wakikata viuno. Wimbo huwa umefungamana na ukataji wa kiuno wenye mitindo ya kufanya tendo la ndoa. Hii inatokana na maneno yaliyotumika katika wimbo wenywewe kama yanavyoelezwa kwenye wimbo hapa chini.

**MBN 14. KUTANDIKA**

*Naupiga papapa,  
Naupiga lolo.*

*Naupiga papapa,  
Naupiga lololo.  
Usione watu kutandika,  
Kutandika kuna maana yake.*

*Usione kutandika kitanda,  
Kutandika kuna maana yake.*

*Ukitaka mume asitoke,  
Akilala mguu mpachike.*

*Kumea mvi si utu uzima,  
Bora mashini kuwa nzima.*

*Kwenda na gongo si utu uzima,  
Bora kijiti kizima.*

*Ukitaka mume aishi,  
Kutandika ni kukaa uchi.*

*Naupiga papapa,  
Naupiga lololo.*

Kadhalika kulikuwa na ukataji wa kiuno kwa ajili ya kufanya tendo la ndoa katika muktadha wa kumsinga mwari. Hata hivyo wakati wa utafiti wasaidizi watafiti hawakuruhusiwa kupiga picha wakati mwari alipokuwa akisingwa. Lakini kilichotokea ni kuwa kungwi na wasingaji ndio waliokuwa wakikata viuno katika mitindo mbalimbali. Kama vile mtindo wa kupiga magoti (*mbwa kachoka*), kusimama, kulala na upande upande. Wakati huo, mwari anatazama na kujaribu kufanya. Mafundisho ya matendo haya, anatakiwa mwari/bibi harusi afanye atakapokuwa na mumewe wakifanya tendo la ndoa.

#### **4: Kupiga Makofi**

Takribani nyimbo zote zilizotambuliwa kuwa na utendaji ziliambatana na upigaji wa makofi wakati wa uimbaji. Kwa kawaida, kupiga makofi ina maana nydingi kulingana na muktadha wa tukio lenyewe. Mathalani katika mkutano, kupiga makofi humaanisha kukubali hoja ya msemajii. Wakati mwengine kupiga makofi hutumika kushangiria au pia kuita mtu. Lakini katika nyimbo za harusi, kupiga makofi hufanya kazi ya kulinda mapigo na pia kuchochea ari ya waimbaji. Utendaji huu unaonekana vyema katika hapa chini.



### **PICHA 9 Upigaji Makofi kwa ajili ya Kuchochea Ari.**

*Katika picha hiyo hapa juu katikati ni Bi Kidude (Mungu amrehemu) akipiga ngoma na wanawake waliomzunguka wanapiga makofi kulinda mapigo na pia kuchochea ari ya waimbaji na mpigaji ngoma. Tendo hili hufanya uimbaji wa wimbo kuwa na mizani na uburudishaji. Picha ilipigwa tarehe 12/12/2010 Vuga - Unguja.*

### **5: Kupiga Vigelegele**

Kigelegele ni sauti ya shangwe na inayotolewa, Aghalabu na wanawake kwa kuchezeshachezesha ulimi mdomoni. Vigelegele mara nyingi vinasikika vikipigwa katika shambrashambra, nderemo na hoihoi harusni au kwenye mikutano. Nyimbo nyingi zilizokuwa zikiimbwa katika harusi za Waswahili Waunguja zilishindikizwa na vigelegele. Vigelegele vilivyopigwa wakati wa uimbaji wa nyimbo harusini vilikuwa na maana tofauti kulingana na tukio mahasusi. Mathalani, kigelegele kilichopigwa na kungwi kabla ya kuimba wimbo MSG.11 kilikuwa ni maana ya kuwaarifu hadhira kuwa singo imekamilika. Wimbo MSG.11 ulikuwa na ujumbe uanaojulisha kuwa singo imekamilika. Ujumbe huo kama unavyonekana katika hapa chini wa wimbo MSG.11.

### MSG.11. KAWAIDA YA SINGO

Kungwi: *Iyo kawaida ya singo yoyoo !*

Waalikwa: *Iyoo yooo !*

Kungwi: *Salama Inshallah salmin !*

Waalikwa: *Inshallah salmin !*

Kungwi: *Salimin akbar shoo !*

Waalikwa: *Shoo !*

Kungwi: *Salimina akbar shoo malika ya umidina !*

Waalikwa: *Allaha Akbar !*

Kungwi: *Ya muswali !*

Waalikwa: *Ya Salaam !*

Kungwi: *Alaikum ghasia kwa mtoto wetu!*

Waalikwa: *(wanatoa vigelegele kwa sauti ya juu)!*

Kigelegele chengine ambacho hutumiwa kujulisha wanawake wengine katika harusi ni kile anachopiga kungwi katika wimbo MBN.1.CHEBA. Kigelegele hiki huwa na maana ya kuwalishya wanawake waliohuduria kwamba, ndoa imeshafungwa. Kwa kawaida katika harusi za Waswahili hasa wakati wa zamani, wanawake huwa wamekaa uani au ndani ya nyumba hivyo hawashuhudii nikaha inapofungwa. Kungwi huwa, amekaa upenuni huku akichungulia sehemu ambayo nikaha inafungwa. Kungwi anaposikia Kadhi au Sheikh aliyeozesha akisema "*al-fatiha*" ya kuhutimisha duwa ya kufunga nikaha, ndipo naye hupiga kigelegele na halafu hupiga cheba. Lakini siku hizi hali hii inapungua kwa sababu harusi nyingi nikaha hufungwa maholini au misikitini ambapo pia wanawake huwepo na kushudia nikaha ikifungwa.

Aidha, maana ya vigelegele vinavyopigwa na watani na waalikwa katika nyimbo MSG.1, MSG.17 na MSG.12 huwa ni kwa ajili ya kumshangilia mwari. Pia huwa na maana ya kujifurahisha na kufanya mandhari ya sherehe ya harusi kuwa hai. Mfano katika wimbo MSG.12, unaoimbwa wakati kungwi akitoka na mwari wake chooni akimpeleka cchumbani. Wimbo wenywewe ni huu ufuataao.

### MSG.12. NENDA NAYE

*Nenda naye mwanaao*

*Nenda naye nenda naye*

*Nenda naye mwanaao.*

## **6: Kuigiza Kuchora na Kuchonga Kalamu**

Wimbo ufuatao ni ulikuwa ni mmoja wa wimbo ambao utendaji wake uliambatana na taashira zilizotajwa wakati wa uimbaji.

### **MBN.16. KITABU**

*Eeee leo achore  
Eeee leo achore  
Bwana harusi asema  
Ataka kitabu achore  
Na kalamu ashachonga  
Ataka kitabu achore*

*Eeeh leo achore  
Eeee leo achore  
Bwana harusi asema  
Ataka kitabu achore  
Na kalamu ashachonga  
Ataka kitabu achore*

Taashira ya *bwana harusi asema, ataka kitabu achore, na kalamu ashachonga* katika wimbo MBN.16 iliambatana na uigizaji wa tendo la kuchora katika kitabu na kuchonga kalamu. Wanawake wa upande wa bwana harusi huimba kwa vishindo, huku baadhi yao wakiigizia kuchora kwa kutumia kidole cha kati cha mkono wa kulia juu ya kiganja cha mkono wa kushoto. Aidha, wanawake wengine waliigizia kama mtu anayechonga kalamu ya penseli. Walikuwa wakipenyeza kidole cha kati kwenye kiganja cha mkono wa kushoto kilichofumbwa. Matendo haya, yaliapambanua maana ya taashira ya *bwana harusi asema, ataka kitabu achore na kalamu ashachonga* ulimaanisha bwana harusi anataka kukutana na mkewe kwa tendo la ndoa.

## **8: Uchezaji wa Matao na Kupiga Miguu Chini**

Vile vile utafiti umebaini kuwa uimbaji na uchezaji wa wanawake harusini huwa katika duara. Ijapokuwa hatukupata picha ya uimbaji na uchezaji wa wanaume harusini lakini Makame Juma aliyehojo 2/12/2009 alieleza, uimbaji na uchezaji wa wanaume huwa katika misitari. Alipoulizwa kwa nini inakuwa uchezaji wa wanawake huwa katika duara na wanaume huwa katika misitari hakuwa na jawabu la kufafanua mitindo hiyo ya uchezaji. Alisema walikuta hivyo toka zamani.

Kama tulivyoeleza hapa awali kuwa nyimbo za harusi za shamba huimbwa nje ya nyumba na kikundi cha kina mama. Hiki ni kikundi maalum kilichokodiwa kwa ajili ya kupika na kuimba. Wakati wa upishi, kikundi hiki huimba nyimbo mbalimbali. Utafiti umeshuhudia kuwa uimbaji wa nyimbo zilizoimbwa ni kama vile:-MKN.2. TWASESERA , MKN.3. YUWAPI MAMAKE HARUSI, MKN.4. HODI, MKN.5. NOTI NAIRAWE na MKN.6. ZIPUKUTIKE PESA zilifungamana na utendaji wa kucheza. Kina mama hawa walikuwa wakiimba kwa kuzunguka duara. Wanapochoka kuimba na kucheza hupumzika kwa kuimba wimbo MKN.2. TWASESERA. Kawaida hawakatishi nyimbo na kuketi chini la, bali mapumziko yenewe yalikuwa ni kuimba nyimbo kwa mwendo wa polepole na uchezaji wa matao wa kupiga miguu chini. Ufuatao hapa chin ni mfano wa wimbo walioimba walipotaka kupumzika:

*MKN.2 TWASESERA*

*Kina mama twasesera*

*Haya*

*Kina mama twasesera*

*Haya.*

Wimbo MKN.2 huimbwa bila ngoma yoyote kupigwa. Wanawake hupiga miguu yao chini kila wanapoimba ***haya*** kama kibwagizo katika wimbo. Wanapiga miguu yao kwa pamoja na kutoa mshindo kama mdundo wa ngoma. Mdundo huu ultumiwa kutoa mizani ya wimbo waliokuwa wakiimba MKN.2. Tazama uchezaji na upigaji miguu katika picha hapa chini.



#### **PICHA 10 Upigaji wa Miguu Chini na Kutoa Mdundo**

*Wanawake hawa wanaimba na kuzunguka duara wakiwa bila ya viatu. Wanaimba bila ya kutumia ala zozote. wanapiga miguu yao chini na kutoa mdundo maalumu. Picha hii ilipigwa katika harusi ya shamba (kijijini) Gombani, Tumbatu, 5/9/2009.*

Wimbo mwengine unaoimbwa na kikundi cha kina mama wakati wakishughulika na kupika ni  
huu ufuatao:

##### **MKN.3 YUWAPI MAMAKE HARUSI**

*Yuwapi eee,  
Yuwapi eee,  
Yuwapi mamake harusi,  
Aje hapa tuangaike naye,  
Aje hapa tuangaike naye.*

Uchezaji ulikuwa tofauti baina ya wimbo MKN.2 na MKN.3. Uchezaji katika wimbo MKN.2 ulikuwa na utendaji wa kupiga miguu chini na kutoa mdundo bila ya kutumia ala za muziki. Ili

hali katika wimbo MKN.3 kina mama walicheza kwa kufuata ala za muziki zilizotumiwa wakati wa uimbaji. Hata hivyo kikundu cha kina mama hawa wanatoa ujumbe kuitia wimbo MKN.3 kuwaambia wenye shughuli hasa mamake bibi harusi au bwana harusi aje ili wacheze naye. Wimbo MKN.3 huimbwa huku wanawake wanacheza kwa kufuata mdundo unaopigwa kwa kutumia ndoo na kibati kama ala za muziki. Wimbo MKN.3 ulikuwa na vipengele vinne vikuu bora vyta kuelezea sifa za muziki wa Kiafrika kama alivyofafanua Ntarangwi (2001:5) akiwanukuu (Chernoff 1979; Dje Dje and Carter 1989; Merriam 1982). Misingi ya vipengele hivyo bora vinne ni: (a) lahani na waitikiaji, (b) ala za muziki, (c) uimbaji wa kughani wa silabi, (d) kurudiwa rudiwa mishororo mifupi. Tukitazama vipengele vinne hivi tulivyovitaja tumegundua vinastahili kufafanua wimbo MNK.3. Kwanza, sauti inayaotolewa wakati wa uimbaji wa wimbo huu inahusisha lahani na waitikiaji. Lahani akiwa kiongozi wa wimbo, huanza kuimba na waitikiaji hurudia wimbo baada yeye kumaliza. Pili, ala za muziki zilizotumika katika wimbo ni pamoja na ndoo, kibati na kifimbo. Ala hizi zilitumiwa kukamilisha mdundo wa wimbo na kuufanya uimbaji kuwa hai zaidi. Kwa sababu hii wachezaji kwa kufuata mdundo wa ngoma walipata motisha zaidi ya kucheza. Tatuhii, wakati wimbo ulipoimbwa, waimbaji walikuwa wakitamka silabi kwa kughani yaani kurefusha silabi za mwisho. Lahani alianza kuimba kwa kughani maneno mawili ya kwanza *yu wa pi eee* katika mshororo wa kwanza katika ubeti. Maneno haya yaliimbwa kwa kurefusha kama ifuatavyo *yuuuaapiiiyeeee*. Na nne mishororo ilirudiwa rudiwa huku ikifuata toni ya ala za muziki.

Tazama uchezaji wa kikundi cha kina mama wanaocheza kwa kufuata mdundo unaopigwa kwa kutumia ndoo na kibati kama ala za muziki katika pitcha ifuatayo hapa chani.



**PICHA 11 Uchezaji wa Matao kwa Kufuata Ala za Muziki**

*Upande wa kushoto kuna wapigaji ala za muziki. Ndoo, kibati na kifimbo vilitumika kama ala za muziki na kukamilsha utendaji huu. Kina mama wanaimba wakiwa katika duara na kucheza kwa matao kwa kufuata mdundo wa ala za muziki Uchezaji huu ni kwa ajili ya kujifurahisha na kuifanya sherehe ya harusi kuwa hai . Gombani, Tumbatu, 5/9/2008.*

### **5.1.2 Utendaji katika Matukio Yanayoashiria Mambo ya Kitaashira wakati wa Uimbaji**

Katika sehemu hii mtafiti alishughulikia kupata maana kutokana na utendaji unaofanyika katika matukio tofauti yenyе kuashiria mambo ya kitaashira wakati wa uimbaji harusini. Matendo yaliyofanyika katika matukio tofauti ni harusini ni haya yameorodhesewa hapa chini. Kuelekwa Mgongoni.

- (i) Mwari/Bibi Harusi Kuelekwa Mgongoni
- (ii) Kufukizwa.
- (iii) Kusingwa.
- (iv) Kupukuswa Mchele Kichwani Bwana harusi.
- (v) Kukamatana Mikono Bainya Babake Bibi Harusi na Bwana Harusi
- (vi) Bwana Harusi Kumsomea Kichwani Bibi Harusi.
- (vii) Kuregesha Sehemu ya Chakula katika Kombe la Bwana Harusi.
- (viii) Kulingwanishwa Dole Gumba la Mguu Bainya ya Bwana na Bibi Harusi..

- (ix) Babake Mke Kushikana Mikono na Bwana Harusi wakati wa Nikaha.
- (x) Bwana Harusi Kumsomea Kichwani Bibi Harusi na Kutompa Mgongo.
- (xi) Kifungua Mlango.
- (xii) Kuchinja Mnyama Mlaangoni.

## **1: Kusingwa**

Singo ni tukio muhimu katika harusi za Waunguja. Mwari husingwa faraghani chumbani huku akiimbiwa na kungwi nyimbo zenye mafundisho kuhusu kunga za maisha ya ndoa. Kungwi ndiye msimamizi mkuu wakati wa kumsinga mwari. Wasingaji humsinga mwari kwa kufuata maelekezo ya kungwi. Humuonyesha mwari na kuigiza mambo yote ya ndani ambayo hutakiwa mke na mume kuyafanya. Kama vile mizungu/mitindo ya kufanya tendo, jinsi ya kuviringisha kiuno na jinsi atakavyo msinga mumewe. Mwari huwekwa kwenye mkeka na shughuli nzima hufanywa akiwa hapa. Wasingaji huanza shughuli yao kwa kumsugua mwari kwa kutumia mchanganyiko wa rojo lililochanganywa kutokana na karafuu, mafuta yaliyopikwa kutokana na tui la nazi, liwa. Mwari husuguliwa mwili. Wasingaji/watani huimba huku wakipiga makofi na kukata viuno. Kungwi humusiya mwari na kumuelezea majukumu yake kupitia taashira zilizomo katika nyimbo anazoimbiwa.

Wakati wa kusinga mwari huvalishwa kisitu (aina ya lesso/khanga nyepesi maalumu) kuficha sehemu zake za siri tu. Mwari anavalishwa kisitu ili iwe rahisi kusingwa (kusuguliwa) mwili wake. Kungwi na watani/wasingaji wamevaa bukta na sidiria. Mavazi haya ni maalumu, huvaliwa wakati wa kumsinga mwari. Ni lazima kila anayeshiriki kuvaan bukta na sidiria. Ni miko mtu yejote kuingia chumbani anamosingwa mwari kama si mrombo. Waalikwa walioko ukumbini, baadhi yao hucheza kwa kufuata wimbo unaoimbwa chumbani anamosingwa mwari. Wengine hupiga vigelegele na kushangiria. Waalikwa wanaocheza huwa wamejifunga vibwebwe viunoni. Utendaji huu umedhihirika katika nyimbo kadhaa kama vile:

### **MSG.3. USILIE USILIE**

<i>Kungwi:</i>	<i>Usilie usilie eee mtoto</i>
<i>Watani:</i>	<i>Oyaa</i>
<i>Kungwi:</i>	<i>Ukaniliza na miyee ee mwanangu</i>
<i>Watani:</i>	<i>Oyaa mtoto nyamara kulia.</i>

*Kungwi:*      *Machozi yako ya weke ee mwanangu*

*Watani:*      *Oyaa*  
*Kungwi:*     *Nikifa unililie wee mwanangu*  
*Watani:*      *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*

#### *MSG.14. CHAMBA*

*Chamba ukipata maji chamba*  
*Eee chamba ukipata maji chamba*  
*Mbogo ya mgeni hailali*  
*Wee ukipata maji chamba*

Hata hivyo, matendo yaliyofungamana na taashira zilizomo katika nyimbo za singo yalikuwa na maana kama zifuatazo:- Kumtoa mwari katika hatua ya utoto na kumuingiza katika hatua ya utu uzima; Humtia ashki na kumfanya mwari kuwa tayari kukabiliana na tendo la ndoa; humfanya mwari kuwa na haya na hufanyiwa ili naye akamfanyie mumewe. Maelezo haya yalitolewa na Bi Sihaba aliyehojo wa tarehe 12/4/2010 pamoja na kikundi cha wa wasingaji wa kisasa (Bi. Riziki, Bi. Sauda na Bi.Mwanamvua) waliohojo wa tarehe 1/11/2009.

Hali hii inathibitisha kwamba, matendo yanayofanywa wakati wa singo yalisaidia kupata maana halisi ya singo. Bi Sihaba anaendelea kusema kuwa, Singo ni taasisi muhimu ya kuwafunza wari jinsi ya kuishi katika maisha ya ndoa kaitka utamaduni wa Waswahili. Kutokana na umuhimu wake katika utamaduni wa jamii ya watu hawa, mwari husingwa kabla ya kuolewa. Lengo hasa ni kuyapata mafunzo anayopewa wakati wa kusingwa ili kuweza kuyatumia baada ya kuolewa. Wakati wa kusingwa mwari ni warombo pekee ndio washiriki wanaoruhusiwa kuingia katika shughuli ya kusinga.

## **2: Mwari Kuelekwa Mgongoni**

Kungwi humueleka mgongoni mwari wake wakati wa kumpeleka chooni (uani) baada ya singo na kumtoa chooni. Nyimbo zinazoimbwa na kuambatana na tendo hili la kuelekwa mwari mgongoni ni pamoja na MSG.13. MWARI AINGILE CHOONI, MSG.15.TOKANE, MSG.16. RINGA NAYE na MSG.17. HUYO YUWAJA. Kwa mfano wimbo MSG.13 MWARI AINGILE CHOONI unaimbwa huku kungwi amemueleka mwari mgongoni. Wimbo MSG.13 una haya yakuleza:

### MSG.13. MWARI AINGILE CHOONI

*Bibi aingile chooni kwa maulidi  
Angile koga marashi uvumba na udi  
eeee oyaaa X 2  
Uvumba na udi X 2*

Wimbo MSG.13 ulipokuwa ukiimbwa ulikwenda sambamba na tendo la mwari kuelekwa mgongoni na kungwi kama inavyoonekana hapa chini.



### PICHA 12 Mwari Ameelekwa Mgongoni Anapopelekwa Uani Kuogeshwa

*Mwari amefunika kitambi/khanga bila ya kuonekana mwili akipelekwa uani kulikofungwa uzio.  
Amesimama nyuma na mikono yake ikiwa mabegani mwa kungwi. Mwari huyu alikuwa ni mzito*

*haikuwezekana kuelekwa. Lakini kama angelikuwa mwepesi, kungwi angelimweleka. Mtendeni – Unguja, 12/4/2008.*


Wakati wa kumtoa mwari uani huelekwa tena huku wakiimba nyimbo MSG.16.RINGA NAYE na MSG.17.HUYO YUWAJA. Maudhui yaliyomo katika wimbo MSG.17 ni haya yafutayo:

**MSG.17. HUYO YUWAJA**

*Huyo yuwaja mpeni ndia,  
Huyo yutukuzie pembe na pembe mwana mema,*

*Huyo yutukuze pembe na pembe mwana mema,  
Atukuze akatuwe mzigo kitwani.*

Watani na waalikwa huwa wanaimba na kupiga makofi huku wakimshangilia kungwi na mwari wake akiwa mgongoni kama inavyoonekana katika picha hapa chini.



**PICHA 13 Mwari Ameelekwa Mgongoni Anapelekwa Chumbani.**

*Mwari ameelekwa mgongoni na kungwi. Kungwi anampeleka mwari chumbani kufunzwa. Nyuma yao ni msaidizi wa kungwi. Picha hii imepigwa katika harusi nyengine kuonyesha namna mwari anvyoelekwa mgongoni na Kungwi. Mchangani – Unguja, 7/6/2008.*

Kwa mujibu ya maelezo ya Bi. Amina aliyehojoja tarahe 15/3/2010, alipouliwa kwa nini mwari hubebwa alikuwa na haya ya kusema. "Mwari hufanyiwa yote haya kwa vile amefaulu kwani ameweza kukamilisha kwa salama shughuli muhimu (singo) katika jamii. Baada ya hapa mwari huhesabiwa amekuwa mtu mzima tayari kubeba kunga katika maisha ya ndoa".

Tendo la kuelekwa mgongoni pia limedhihirika katika tukio la kumchukuwa bibi harusi. Tukio hili hufanyika baada ya kutoa mkono, kula na mambo mengine kama kupiga picha, ndugu zake bwana harusi humchukua mke wao. Bibi harusi huchukuliwa akiwa ameelekwa/amebebwa mgongoni kama inavyoonekana katika **PICHA** 14 huku wakiimbia wimbo huu ufuatao:

*MBN.18. TWATAKA MKE WETU*

*Twataka mke wetu*

*Twende zetu kwetu*



**PICHA 14 Bibi Harusi Ameelekwa Akitolewa Nyumbani.**

*Aliyeelekwa ni bibi harusi. Aliyemueleka ni mmoja wa jamaa wa bwana harusi. Hii ni siku ambayo bibi harusi anapelekwa kwa mumewe. Wimbo MBN.18 unaoimbwa umeambatana na utendaji wa bibi harusi anapotolewa nyumbani kwao. Kisauni - Unguja, 10/6/2010.*

Bibi anapotolewa kwao hutolewa kwa kuelekwa. Utendaji wa kuelekwa bibi harusi huwa na maana ya kumheshimu, kumpongeza na kumalizia utoto wake. Inamkinika baada ya hapa hataelekwa tena mgongoni. Wimbo unaimbwaa ni huo hapa juu MBN.18. TWATAKA MKE WETU.

Kadhalika Bi. Khadija aliyehojojiwa tarehe 10/3/2010 ambaye pia ni mnyakanga aliongezea kwa kusema, "... tendo la kuelekwa mgongoni mwari au bibi harusi, linamaanisha pongezi, heshima na furaha kwa vile mwari amefanikiwa kutimiza jambo muhimu katika maisha yake. Ndio maana kungwi anapomueleka mwari mgongoni anatangaza kwa watu na kusema", " leo ni siku muhimu ya mwari. Na mwari anastahiki kupongezwa".

### **3: Mwari Kupakatwa na Kumwagiwa Maji na Kungwi**

Kungwi ndiye anayempakata na kumwagia maji mwari wanapokuwa chooni. Tendo hili hufanyika wakati wa uimbaji wa nyimbo zifuatazo.

#### *MBN.3. NDEMBO AYOGA*

*Ndembo ayaga na mwanawe*

*Ndembo ayaga na mwanawe*

Wimbo mwengine unaoimbwa wakati mwari akiwa uani ni MSG.13. CHAMBA.

#### **MSG.14. CHAMBA**

*Chamba ukipata maji chamba*

*Eee chamba ukipata maji chamba*

*Mbogo ya mgeni hailali*

*Wee ukipata maji chamba*

Mwari anapokuwa chooni, hupakatwa na kungwi wake, huku wameelekezana uso. Wasingaji wakiwa mbele yao, huimba na kukata viuno. Huigiza mizungu (mitindo) tofauti kufanya tendo la ndoa. Baada ya hapa, kungwi husimama kumkogesha/kumwagia maji mwari huku akiambiwa kuwa sasa ameshakuwa mwanamke. Yaani tendo la kumwagiwa maji linamaanisha kuwa, sasa mwari ametoka hatua ya utoto na kuingia daraja la utu uzima

### **4: Mwari Kupishwa Njia Anapotoka Chooni kwenda Chumbani**

Tendo la mwari kupishwa njia limesaidia kupambanua maana ya taashira ya *Huyo yuwaja mpeni ndia* katika wimbo MSG.17.HUYO YUWAJA. Kungwi ndiye aliyekuwa akiimba alipokuwa akitoka na mwari wake chooni na kumpeleka chumbani kama ilivyooneka katika **PICHA 13**. Alipelekwa chumbani kwa ajili ya kufunzwa mambo ya kiutuzima. Jamaa wa mwari na waalikwa wakiwa wamesimama baina ya chooni na chumba, wanamshangilia na kumuimbia mwari anapopita kwenda chumbani. Mwari akiwa pamoja na kungwi wake wanapita katikati ya watu kwa matao na maringo baada ya kupishwa njia. Waalikwa wakiwashangiria huku wakiimba wimbo ufuatao.

#### **MSG.16. RINGA NAYE**

*Ringa naye ringa naye*

*Ringa naye mwanao*

*Ringa naye ringa naye  
Ringa naye mwanaao*

*Cheza naye cheza naye  
Cheza naye mwanaao  
Cheza naye cheza naye  
Cheza naye mwanaao.*

Kungwi kwa kufuata wimbo huu alikuwa akicheza na kuringa na mwari wake akiwa mgongoni. Kwa vile hii ilikuwa ni siku muhimu kwa mwari, kungwi anaitaka hadhira iliyoko wampe nafasi mwari apite bila ya kubughudhiwa. Kwa sababu mwari si mtoto tena na anastahiki kuheshimiwa. Hivyo basi, tendo la mwari kupishwa njia linamaanisha heshima aliyoipata mwari siku hii kuwa ni mtu muhimu sasa.

## **5: Kupukuswa Mchele Kichwani Bwana Harusi**

Tendo la kupukuswa au kumwagiwa mchele lilifanyika siku ambayo bwana harusi alipokwenda kutoa mkono nyumbani kwa kina bibi harusi. Tendo hii liliambatana na wimbo huu ufuatao hapa chini.

MHK.2. KOKO  
Koko wee koko  
Nyumba ya mwari aingia koko  
*Paramira.*

Wimbo MHK.2 uliimbwa huku bwana harusi anaingia nyumbani kwa kina bibi harusi. Tumekwisha toa maana ya taashira ya neno *koko* kuwa linasimamia mume/bwana harusi. Kama wimbo unavyoeleza kuwa "*nyumba ya mwari aingia koko*". Bwana harusi alipovuka kizingiti cha mlango kuingia ndani ya nyumba ya bibi harusi alipukusiwa mchele na jamaa wa karibu wa bibi harusi. Waliacha kumpukusa mchele wakati alipoingia chumbani alimo bibi harusi. Mchele uliopukusiwa bwana harusi, ulizolewa na kupewa njiwa au kuku kama sadaka. Tendo hili huashiria kutolewa nuhusi (yaani kisirani) kwa bwana harusi. Ufasiri huu umeelezwa na Mzee Alawi alipohojiwa tarehe 4/4/2010.

## **6: Kuregesha Sehemu ya Chakula kutoka katika Kombe La Bwana Harusi**

"Kombe la bwana harusi" ni chakula maalumu cha bwana harusi kinachoandaliwa siku ya Walima. Walima ni siku ya karamu ya chakula cha mchana. Aghalabu hufanywa upande wa bibi harusi. Wakati wa walima huwa kuna nyimbo mbalimbali hupigwa zikiwemo za taarabu. Baadhi ya nyimbo zilizorekodiwa ni hizi zifuatazo:

### **MHK.8 MUNGU KANIPA HIDAYA**

<i>Furaha nyangi moyoni</i>	<i>Rabi kanijaaliya</i>
<i>Vipi nikuelezeni</i>	<i>ili yapate weleya</i>
<i>Ndoto yangu ya zamani</i>	<i>leo imekamiliya</i>
<i>Siku zote peke yangu</i>	<i>nikiranda na duniya</i>
<i>'Napowaona wenzangu</i>	<i>husuda nawaoneya</i>
<i>Moyo kiona uchungu</i>	<i>fanaka kunifikiya</i>
<i>Umenitoka upweke</i>	<i>yangu yamekamiliya</i>
<i>Rabi amenipa mke</i>	<i>mzuri alotimiya</i>
<i>Karimu ni roho yake</i>	<i>imani yake tabiya</i>
<i>Mola kwa imani yake</i>	<i>yeye kanifikiriya</i>
<i>Tena kwa khiyari yake</i>	<i>mwenyewe kaniumbiya</i>
<i>Kisha kwa fadhila zake</i>	<i>miye kanitunukiya</i>

### **MBN.10. TANDIKA MGENI AKAE**

*Mama harusi tandika,  
Tandika mgeni akae,  
Mgeni shoga,  
Aaa tandika mgeni akae,  
Mgeni shoga,  
Aaa tandika mgeni akae,*

### **MKND.3. YUWAJA LEO**

*Yuaja leo yuaja honahona  
Yuaja na koti lake yuaja  
Horia horia*

Nyimbo tatu zote hizo hapo zimebeba maudhui ya kumkaribsha bwana harusi katika karamu. Katika nyimbo MBN.10 TANDIKA MGENI AKAE na MKND.3. YUWAJA LEO zinawaambia watu upande wa bibi harusi kutandika mikeke ili mgeni (bwana harusi) apate kuketi anadaliwe chakula kilicho kusudiwa kwa ajili yake yaani "kombe la bwana harusi".

Watu wanaoalikwa katika walima ni pamoja na bwana harusi, jamaa na marafiki zake. Kombe la bwana harusi huwa tofauti na chakula kilichoandaliwa karamuni kama vile *biriani* au *pilau*. Aghalabu kombe la bwana harusi huwa ni wali mweupe uliokolea nazi uliotiwa kwenye sinia na bakuli la mchuzi mzito wa kuku. Katikati ya sinia hiyo ya wali huwa kuna kisahani kidogo kimefunikwa na ule wali. Hivyo, bwana harusi anatakiwa akitoe hicho kisahani kikiwemo na wali kabla hajaanza kula. Kisha atafute kipande kizuri cha mnofu wa nyama ya kuku, na atie mchuzi juu ya kisahani hicho chenye wali na apelekewe bibi harusi. Kassim Dadi alipohojwa tarehe 6/4/2010 kuhusiana na kombe la bwana harusi alikuwa na haya ya kusema "Tendo hili la kuregesha sehemu ya chakula katika kombe la bwana harusi linamaanisha kuwa, bwana harusi anatakiwa kila wakati amfikirie mwenzake. Akipata chochote akumbuke kuwa nyumbani kuna mwenzake anamsubiri. Lengo la kufanya hivi ni kuonyesha kujali, kuthamini, kutunza na kuongeza mapenzi katika maisha ya ndoa".

#### **7. Kulinganishwa sawa Dole Gumba la Mguu baina ya Bwana na Bibi Harusi**

Tendo la kulinganishwa dole gumba baina ya bwana na bibi harusi hufanywa siku ya kutoa mkono. Bwana harusi akifika chumbani kwa bibi harusi husimamishwa pamoja na wakakoshwa miguu kwa marashi. Huku wimbo MKND.6. TUMKOSHE MAU BWANA unaimbwaa.

*Tumkoshe mau bwana  
Kwa mai ya zamzam.*

Baada ya wimbo kumalizika ndio huwadia wakati bwana harusi dole gumba la mguu wake linalinganishwa sawa na dole gumba la bibi harusi. Wakati huu bwana na bibi harusi huwa wanashindana vidole gumba visimpandane. Tendo hili humaanisha kuwa, bwana au bibi harusi ambaye dole gumba la mmoja wao litakuwa juu, atamta wala mwenzake. Hivyo, kila mmoja anajitahidi dole gumba liwe juu. Huu ni katika itikadi ya baadhi ya Waswahili wa Unguja wanavyoamini.

#### **8: Kushikana Mikono na Bwana Harusi wakati wa Nikaha**

Tendo la kushikana mikono baina ya babake bibi harusi na bwana harusi hufanyika wakati wa nikaha inaposomwa. Tendo hilo hufanyika kama linavyoonekana katika picha hii hapa chini.



#### **PICHA 15. Kushikana Mikono Kadhi na Bwana Harusi wakati wa Nikaha**

*Picha hiyo hapa juu, bwana harusi (kulia), anakamatana mkono na Sheikh (kushoto) wakati anapomuozesha. Sheikh anafanya kazi hiyo kwa idhini aliyopewa na babake bibi harusi. . Picha hizi zilipigwa tarehe 10/6/2010, Kisauini - Unguja.*

Kadhi au Sheikh ndio wanaosoma nikaha. Nikaha husomwa kwa kutumia baadhi za aya katika kuruani tukufu pamoja na hadithi za Mtume Mohammad (S.A.W) zinazohusu masuala ya ndoa. Kadhi anapomaliza kusoma aya hizo humpatia mkono bwana harusi kama inavyoonekana katika PICHA 15 hapa juu. Wakati wameshikana mikono hivyo, Kadhi au Sheikh husema maneno kumwambia bwana harusi maneno hayo ni kama yafuatayo " Nakuozesha binti ( fulani binti fulani) kama alivyoamrisha Mungu kwa mahari mliyokubaliana. Ukae naye kwa wema na ihsani na ikotokea kuachana muachane kwa wema na ihsani". Kisha Kadhi husema tena maneno kumwambia bwana harusi aseme. Maneno hayo ni " Nimekubali kumuoa fualani binti fulani kama alivyoamrisha Mungu kwa mahari tuliyokubaliana. Nitakaa naye kwa wema na ihsani " usemi huu hukaririwa mara tatu. Baada ya kumaliza maneno hayo, Kadhi hutia *al-fatihah* na kuwaombea maharusi, na wao huachana mikono. Tendo la kukamatana mikono lina maana ya kukabidhiana. Yaani babake bibi harusi anamkabidhi binti yake kwa bwana harusi. Mungu akiwa shahidi na watu wote waliohudhuria katika sherehe ile.

Kwa baadhi ya harusi kama nikaha itafyngwa nyumbani basi baada ya sheikh kufungisha nikaha huwa kuna kaswida huimbwa na watoto wa madrasa kwa ajili ya tukio hili. moja ya kaswida inayombwa ni hii hapa chini.

#### MKU.9. UTUPE KILA LA KHERI

*Leo ni siku tukufu,  
Hii ni siku adhima,  
Na sote waisilamu,  
Twakuomba ya Karima,*

*Harusi yetu adhima,  
Ni harusi ya (jina la bw na Bi. Harusi)  
Awe mtu mzuri,  
Twakuomba ya Karima,*

*Uijalie salama,  
Uwaondolee sahri,  
Na sisi utujaalie,  
Twakuomba ya Karima,*

*Uwape wato wema,  
Watoto wawe na kheri,  
Bibie mtunze bwana,  
Twakuomba ya Karima,*

*Yarabbi tupe salama,  
Utupe kila la kheri,  
Utuondolee shari,  
Twakuomba ya Karima,*

*waumini shangiria,  
Yarabbi katuletea,  
hima hima shangiria,  
utupe kila la kheri.*

*leo imetufikia,  
Yarabbi katuletea,  
Yarabbi kamuongoa,  
utupe kila la kheri.*

*ndoaa iwe ya adhima,  
leo na kesho kiama,  
ndoaa tuiifikilie,  
utupe kila la kheri.*

*wenye kheri na salama,  
duniani na kiama,  
ukae nae salama,  
utupe kila la kheri.*

*duniani na kiama,  
ujalie salama,  
za dunia na za kiama,  
utupe kila la kheri.*

MKU.9 ni kaswida iliyobeba dua yakuwaombea bwana na bibi harusi. Isitoshe imebeba ujumbe mzito juu ya majukumu anayotakiwa mume amfanyie mke wake. Naye mke anakumbushwa jinsi atakavyo mtunza mumewe katika maisha ya ndoa. Lengo ya yote haya ni ipatikane kheri na salama katika maisha ya ndoa hapa duniani na akhera. Katika mafundisho ya dini ya Kiisilamu inaeleza kwamba mume na mke walioowana kisheria na kuishi maisha mazuri ya kumcha Allah (S.W.) katika ndoa yao basi Allah (S.W.) atawajaalia hata akhera wawe pamoja. Katika pepo yake.

## **9: Bwana Harusi Kumsomea Kichwani Bibi Harusi na Kutompa Mgongo Mkewe**

Tendo la kusomewa kichwani bibi harusi hufanywa siku ambayo bwana harusi huenda kutoa mkono kwa kina bibi harusi. Bwana harusi hupelekwa ndani na watu wazima au masahibu zake. Huku ndani humkuta bibi harusi kafinikwa mtandio wa hariri usoni. Akifika huweka mkono wa kulia kichwani kwa bibi harusi na kusoma kimoyomoyo dua. Dua yenyewe ni " Ewe Mwenyezi Mungu ajaalie mke huyu awe mwema na wa kheri kwangu". Baada ya kumaliza kumsomea, humfunua bibi harusi mtandio usoni na kisha humpa mkono kama ilivyoonekana katika PICHA 3. Wakati huu bwana harusi humpa mkewe zawadi yoyote kama vile: pesa, kidani au saa. Baada ya hapa, bwana harusi hurejeshwa kinyume nyume asimpe mgongo mkewe mpaka mlangoni. Tendo la kumsomea kichwani bibi harusi humaanisha kuomba dua ili Mungu ajaalie awe mke wa kheri kwake. Ama, tendo la kutompa mgongo mkewe wakati wa kutoka lina maana yakuwa, mume asije akamdharaau au kumsahau au kumpuza mkewe.

Bwana harusi baada ya kumsomea kichwani bibi harusi kabla hajaanza kutoka watani huimba nyimbo tofauti wakati huu. Zifuatazo ni baadhi ya nyimbo zinazoimbwa katika tukio hili:

### **MBN.21. MWANANGWA**

*Huyo huyo mwanangwa  
Umpe chumvi mwanagwa  
Umpe kula mwanangwa  
Umpe nguo mwanangwa  
Usimpige mwanangwa*

Katika wimbo huu hapa juu, bwana harusi anakumbushwa majukumu yake kwa mkewe. Bwana harusi anatakiwa kumlisha na kumvisha pia anaonywa asiwe na tabia ya kumpiga mkewe kama inavyoelezwa katika mshororo wa tano wa wimbo MBN.21.

Wimbo mwengine unaoimbwa baada ya bwana harusi kumsomea kichwani bibi harusi ni MBN.31. LEO UMEPATA WAKO. Wimbo huu unatoa mafunzo kwa bibi harusi jinsi atakavyoweza kudumisha ndoa yake. Katika wimbo huu umetowa muungozo kwa bibi harusi jinsi atakavyojihadhari na watu wabaya. Nasaha hizi zinaelezwa katika wimbo huu hapa chini.

### **MBN.31. LEO UMEPATA WAKO**

*Leo umepata wako mahawara ni wakome  
Wakija mashoga zako sema nao dirishani*

*Wakija mawifi zako sema nao ukumbini  
Wakija shemegi zako sema nao mlangoni  
Upewacho kipokea haukupewa jimezee  
Utulizane ukae vumilia usikhini*

## **10: Kifungua Mlango**

Kifungua mlango ni ada inayotolewa wakati bwana harusi anakwenda kutoa mkono. Chumba ambacho yumo bibi harusi huwa kimefungwa. Nje ya mlango huwa kuna watu wamesimama. Watu hawa ni jamaa wa karibu ambaao kisheria wangeweza kumuoa bibi harusi. Kabla ya kuingia bwana harusi hutoa ada (kifungua mlango). Aghalabu hutoa pesa na hakuna kima maalumu. Kabla hajaingia, huulizwa asili ya mkewe, yaani mji waliotoka wazee wake, naye hutaja. Akimaliza kujibu hayo maswali, ndio hufunguliwa mlango na huruhusiwa kuingia ndani. Tendo hili lina maana zifuatazo. Kwanza kujuana. Wakati huu bwana harusi anapata fursa ya kuwatambua jamaa wa mkewe. Aidha, kuonyesha kuwa anamfahamu vyema mkewe anatoka wapi. Pili, bwana harusi anatanabahishwa kwamba, ajue kuna watu wengine wangeweza kumuoa mkewe. Si kwamba kumpata yeze amepata kitu ambacho hakitakiwi. Tatu, bwana harusi anawashukuru jamaa na walezi waliomlea bibi harusi.

## **11: Kuchinjwa Mnyama Mlangoni**

Tendo la kuchinjwa mnyama mlangoni hufanyika siku ambayo bibi harusi anaingia nyumba atakayoishi. Aghalabu, huchinja mbuzi au hata kuku kama mbuzi hamudu. Mnyama huchinjwa nje ya mlango, na wote wawili (bwana na bibi harusi) hukiuka damu hiyo. Tendo hili humaanisha kuwa, damu ya mnyama iliyomwagika mlangoni ni kafara ya maharusi hawa. Yaani linaashiria kinga dhidi ya ubaya katika nyumba hiyo kama upo. Uwe ubaya wa shetani au mtu.

## **12: Kuchoraji Hina**

Uchoraji hina ni moja kati ya miviga ya jamii ya Waswahili. Mviga huu hutumika katika sherehe au furaha inayofanywa katika matukio mbalimbali ya maisha ya Mswahili. Kwa kuwa harusi nayo ni tukio la furaha hushereheshwa kwa bibi harusi kutia hina. Bibi harusi katika jamii ya Waswahili Waunguja huchorwa hina siku mbili au tatu kabla ya kufungwa nikaha kama sehemu ya sherehe ya harusi. Moja ya dhima kuu ya upakaji hina kwa bibi harusi Wakiunguza ni kwa ajili ya kuonyesha hisia , furaha, upendo na zaidi kumvutia bwana harusi ili aweze kumtamani.

Hivyo uchoraji hina kwa wanawake ni njia moja ya kumtamanisha (kumtongoza) mume kumtamani kwa tendo la ndoa. Upakaji na uchoraji zaidi ya mapambo ya hina unamfanya mwanamke kupendeza na kuvutia zaidi.

Kiutamaduni, hina ina michoro yenye mitindo ya aina mbalimbali. Mitindo hiyo huwa inaashiria maana maalum. Mtindo wa kuchoro huteuliwa kwa kufuata ujumbe unaotakiwa kutolewa. Kwa mujibu wa Rachel Macneill ( 2013) katika masimulizi aliyokusanya anaeleza kuwa, uchoraji tofauti wa maua katika hina ni taashira inayosimamia maana mbalimbali zifuatazo :-

*Tausi husimamia urembo.*

*Ndege husimamia mjambe au malaika (baina ya mbinguni na duniani )*

*Kipepo husimamia mabadiliko ya uumbaji.*

*Njiwa husimamia mjambe wa mapenzi.*

*Samaki husimamia jicho la mwanamke.*

*Nge husimamia mapenzi na mahaba.*

*Maua husimamia furaha na sherehe.*

*Jua, mwezi na nyota husimamia mapenzi ya dhati na ya ndani walijonayo wapenzi wawili wapendanayo.*

*Msumeno husimamia mvua na kizazi.*

Hina inachukuliwa kama njia moja ya kupata "baraka". Jamii ya Waunguja wanaitikadi kuwa mpakaji hina mbali na kuwa ni furaha na urembo pia hupata baraka ya kuwa na bahati. Msingi wa dhana hii inatokana na mafunndisho ya Uiisilamu kuitia mtume Mohamad (S.A.W). Hata hivyo, imebainika kwamba upakaji na uchoraji hina unambadilisha mwanamke na kumfanya avutie. Haya yametokea kwa Mtume Mohamad (S.A.W) katika mafundisho yake ya kusitiza upakaji hina. Mtume Mohamad (S.A.W) aliwahi kumwambia mke wake Aisha (R.A) ikifika siku ya harusi yao apake hina kwenye mikono na miguu kama sehemu ya mapambo. Hali hiyo humfanya mume kuvutiwa zaidi na mkewe. Tukio hili lilipelekea kuathiri Waisilamu wote duniani kupaka hina kwa nia njema na hasa kwa wanawake kuwardhisha waume zao kwa lengo la kuwavutia zaidi. Isitoshe kufanya hivi ni kufuata "sunnah" yaani matendo aliyofanya au kuamrisha mtume Mohamad (S.A.W) kwa ajili ya kupta baraka na thawabu. Katika mafundisho

ya Uiisilamu Mtume Mohamad (S.A.W) anawahimiza Waisilamu wanawake kupaka hina kwenye kucha kwa ajili ya kujitofautisha na mikono na miguu ya wanaume.

Kulingana na mila za Waswahili wasichana ambao hawajaolewa hawaruhusiwi kujichora na kujiremba kwa mapambo ya hina kama wanawake walioolewa. Katika jamii hii, njia moja ya kujua kama mwanamke ameolewa au bado unaweza kumjua kupita hina. Kama amejichora hina yenye marembo basi atatambulikana kuwa ni mke wa mtu au ameolewa. Na iwapo atakuwa amejichora hina ya kawaida mfano kutia hina kwenye kucha basi atatambulikana hajaolewa. Rachel Macneill ( 2013) katika kukusanya masimulizi yake anaeleza kuwa, wanaume wengine ambao wanawivu wanawakataza wake zao kuchora hina kwa sababu ya kupekana na ushawishi wa kuwavutia wanaume wengine na hatimae kupelekea maovu. Wanawake wengine wanalazimishwa kuвая glovu mikononi wanapopaka hina ili kuficha urembo wao.

Hata hivyo falsafa iliyopo juu ya hina katika jamii hii ni kuwa, mwanamke hupaka hina kwa ajili ya mume wake. Mbali na kutumiwa na wanawake kupaka hina, dini ya Kiisilamu imewaruhusu waumini wanaume kutia hina katika nywele na ndevu zenye mvi kama kitendo cha sunnah. Mtume Mohamad (S.A.W) alikuwa akitia hina wakati nywele zake na ndevu zinapoota mvi. Hivyo jambo hili katika dini ya Kiisilamu ni sunnah na ni zuri kufanywa. Kwa muhtasari ni kwamba, upakaji hina katika jamii ya Waunguja ni kwa ajilli ya kuonyesha furaha, kufuata maamrisho ya dini na kutambulisha utamaduni wao. Ifutayo ni mifano hina iliyochorwa kwa bibi harusi.



#### **PICHA 16 Uchoraji hina katika Mikono na Vidole**

*Mikono hiyo hapa ni ya bibi harusi (Mariam) inaonyesha uchorahi wa maua mbalimbli ya hina aliyochorwa siku ya harusi yake. Picha hii imetolewa katika <http://www.elimuasilia.org/culture/174-henna-tree.html>.*



#### **PICHA 17 Uchoraji Hina katika Miguu na Mikono.**

*Katika picha hiyo hapa juu ni mikono na miguu ya (Fatma) inyoonyesha michoro ya majani kabla siku ya nikaha kufungwa. Picha hii imetolewa katika <http://www.elimuasilia.org/culture/174-henna-tree.html>.*

Rachel Macneill (ameshatajwa) anafafanua kwamba, mitindo ya uchoraji wa hinasi za zamani ulikuwa ni kama vile:- msumeno, mapeni, mkorosho, kochi na kadhalika. Siku hizi wasanii wa kuchora hina wamekuwa na mitindo mengi zaidi ya kuchora maua mazuri na yenye kupendeza.

#### **5.1.3 Utendaji wa Uigizaji wa Vitu vya Bibi Harusi wakati wa Kuimba Nyimbo**

##### **1. Kungwi anaigiza Matumizi ya Vitu vilivyomo katika Masanduku ya bibi harusi.**

Uigizaji wa matumizi ya vitu vilivyomo katika sanduku au masanduku ya bibi harusi hufanyika wakati wa uimbaji wa wimbo huu hapa chini.

###### **MKS.1. SASAMBU**

*Sasambu sasambu sasambu*

*Sasambre turore sasambre turore*

*Sasambre turore!*

Wanaoimba wimbo MKS.1 ni wanawake wa upande wa bibi harusi waliopokea masanduku kutoka kwa wanawake wa upande wa bwana harusi. Wanawake wa upande wa bibi harusi wanamtaka kungwi wa mwari ayafunguwe masanduku iliaanze kusasambua (kuonyesha) vitu vilivyoletwa. Wakati wanapoimba *Sasambure turore, sasambure turore*. Kungwi husasambura na kuonyesha kitu kimoja kimoja kilichomo katika masanduku ya bibi harusi yaliyoletewa. Masanduku ya bibi harusi hufungwa na khanga kama yalivyoonekana katika picha hapa chini.



**PICHA 18 Kusasambura Masanduku ya Bibi Harusi.**

Upande wa kulia ni wanawake kutoka kwa mume ndiyo waliioleta haya masanduku yaliyopo katikati. Upande wa kushoto ni wanawake wa upande wa mke ndio waliopokea. Wote hawa wanamsubiri kungwi aje kufungua masanduku kusasambura (Yaani kuonyesha kitu kimoja kimoja kilichomo katika masanduku). Kusasambura kunaambatana na wimbo MKS.1. Sokoni – Makunduchi, 10/10/2009.

Masanduku haya huwa na vitu kama shanga, sabuni, "*hanchifu*", kiwembe, chupi, sidiria, marashi, khanga, wanja na kadhalika. Wimbo MKS.1 huimbwa huku kila kitu kuonyeshwa kazi yake. Mfano "*shanga*" huonyeshwa kuwa zinavaliwa kiunoni, "*kiwembe*" kunyolea nywele zimeazo sehemu za siri, "*hanchifu*" kumpangusia bwana majasho ya sehemu zote baada ya tendo la ndoa na kadhalika. Uigizaji wa matumizi ya baadhi ya vitu hivi vilikuwa na maana ya ndani. Maana ya vitu hivi vilifasiriwa na Bi Mwanamkisi aliyeojiwa tarehe (10/10/2010) alipokuwa akisasambura vitu vilivyokuwemo katika masanduku ya bibi harusi. Mathalani:-

***Shanga***, kungwi aliigizia matumizi ya shanga. Alizivaa kiunoni huku akionyesha mitindo na mizungu ya kufanya tendo la ndoa. Uvaaji wa shanga ulimaanisha kumtia ashki bwana harusi anapofanya tendo la ndoa.

***Sabuni***, matumizi ya sabuni yalikuwa na maana ya kujisafisha na kunukia vizuri baada ya kuamka na kabla ya kulala.

"***Hanchifu***"(kitambara cha mkononi), matumizi yake yalikuwa na maana ya mke kumpangusa au kumfuta mumewe uume baada ya tendo la ndoa. *Hanchifu* nyingine ni kwa ajili ya kujifuta yeye mwenyewe.

***Kiwembe***, matumizi yake yalikuwa na maana ya mke kunyoa nywele za sehemu za siri ili awe msafi kabla ya kukutana na mumewe kimwili.

Bi Mwanamkisi alipozitoa ***khanga*** katika sanduku alianza kuonyesha matumizi ya ufungaji khanga na kueleza maana tofauti ya ufungaji khanga. Alieleza kuwa, mke anapojifunga khanga kichwani kama mfano wa kilemba humaanisha siku hiyo yuko kwenye siku zake (hedhi). Hivyo mumewe atafahamu na hatamuhitaji kukutana naye kimwili. Mke anapoitupia khanga juu ya mabega na kuteremkia kifuani, humaanisha kuwa ameshatoka kwenye siku zake. Hivyo, yuko tayari kukutana na mumewe kimwili. Anapojifunga khanga kiunoni kama mfano wa "*aproni*" humaanisha kuwa yuko na shughuli au kazi mbali mbali za nyumbani.

Hata hivyo, khanga katika jamii ya Waswahili ni vazi linalothaminiwa sana. Kwa mujibu wa Ali (2004) khanga ndio vazi la kwanza kufungwa mtoto anapozaliwa. Khanga ni zawadi muhimu anayopewa msichana kuanza kujitanda anapovunja ungo. Khanga kama vazi la heshima, hutumiwa na kinamama kujitanda wanapokwenda shambani, kubebeta mtoto (ubeleko), sokoni na matangani. Khanga pia, hutumiwa kumfunika maiti wa kike au wa kiume mwili mzima anapooshwa. Khanga hutumiwa kama alama inapofungwa juu ya jeneza. Huonyesha kuwa maiti aliyomo jenezani ni wa kike. Aidha, khanga huwa na majina, ambayo huwa yamebeba ujumbe mzito. Majina haya hutumiwa kufikisha salamu, dua, kijeli, kupigana vijembe, ari, na hata matusi wakati mwengine. Mfano wa majina haya ni kama vile: *Natosheka na kidogo chake, Mke mwanga wa nyumba, Wawili wakipendana adui hana nafasi, Kipendacho moyo dawa, Usione nimetulia mengi nimevumilia, Kitunze kidumu, Penye riziki hapakosi fitina, Mama nipe radhi kuishi na watu kazi, Chakukupa sina nakuombea duwa, Nani kama mama?*, na mengineyo.

## **2. Utendaji wa Mafundisho ya Kunga ya Maisha ya Ndoa kwa Kutumia Vitu vya Jikoni**

Mwari akishamalizwa kumwagiwa maji na kuchezeshwa huko uani hutolewa. Mwari hutolewa kwa wimbo, shangwe, nderembo na vigelegele huku akiwa ameelekwa mgongoni. Kungwi humueleka mwari na kumpeleka chumbani kwa ajili ya kufundishwa kunga za maisha. Tendo hili huambatana na wimbo ufuatao:

<i>MSG.15 TOKANAE</i>	<u>Kiswahili Sanifu</u>
<i>Tokanae myakanga,</i>	Tokanae kungwi
<i>Tokanae myakanga.</i>	Tokanae kungwi
<i>Ende nae akarore,</i>	Ende nae akajfunze
<i>Ende nae akarore</i>	Ende nae akajfunze

Baada ya kufukizwa, mwari hukalishwa kwenye mkeka kwa ajili ya kupewa mafunzo ya ndoa. Ukiingia chumbani wakati mwari anafunzwa, unaweza kusema watu wanataka kutwanga na kupika kwa sababu mwari husogezewa sufuria, mwiko, kinu, mchi, ungo pamoja na chungio. Baada ya hapa huelezwa maana ya kila kifaa na jinsi ya kikitunza. Katika wimbo MSG.15 mnyakanga (kungwi) anaambiwa atoke naye mwari na kumpeleka chumbani *akarore* yaani akajifunze mambo ya kunga katika maisha ya ndoa. Watafiti saidizi walishuhudia kuwa mwari anapofikishwa chumbani anamofunzwa hufukizwa. Baada ya kufukizwa, mwari hukalishwa kwenye mkeka kwa ajili ya kupewa mafunzo ya kunga ya katika maisha ya ndoa. Ukiingia chumbani wakati mwari anafunzwa, unaweza kusema watu wanataka kutwanga na kupika kwa

sababu mwari husogezewa sufuria, mwiko, kinu, mchi, ungo pamoja na chungio. Baada ya hapa huelezwa maana ya kila kifaa na jinsi ya kukitunza. Mafunzo ya mwari yalitolewa kwa maneno na vitendo kutokana na vitu vilivyoletwa hapo (*sufuria, kinu, mchi, unga, chungio na ungo*) vilikuwa na maana ya kitaashira kinyume na vile vinavyofahamika katika matumizi yake ya kawaida.

Bi Riziki Pembe (7/8/2008) mmoja wa manyakanga aliyekuwa huko chumbani, ndiye aliyetoa fasiri ya maana ya vitu hivi kimoja baada ya kimoja kwa mwari. Bi Riziki kwanza alichukua unga na kuutia kwenye chungio aliuchekcha ndani ya ungo. Kwenye chungio kulibakia chenga na kwenye ungo kulipatikana unga msafi. Mwari aliambiwa, **chenga** zilizobakia kwenye chungio ni *maneno mabaya* - k.v ufedhuli, ujuba na ujeuri hizi ni tabia mbaya. Hutakiwa azimwage chenga hizo. Yaani asiwe na tabia mbaya kwa mumewe wala ndugu za mumewe. Ule unga msafi ulioko kwenye **ungo** ni *maneno mazuri*. Haya ndio maneno anayotakiwa amwambie mumewe na ndugu zake mume.

Pili mwari alielezewa tena na Bi Riziki tafsiri ya matumizi ya vifaa alivyoonyeshwa huko chumbani. Vifaa hivi vilikuwa na umuhimu katika maisha ya ndoa na vilisimamia maana zifuatazo:-

*Mafya* (mafiga) maana yake ni huruma, heshima na mapenzi ambayo mke anatakiwa amfanyie mumewe. *Kuni* ni majirani. Mwari anatakiwa akae vizuri na majirani. *Moto* husimamia subira. Mwari anapewa nasaha ya kuwa na subira akiwa kwake. *Jivu* ni wazee awe na heshima nao. *Cheche* zinamaanisha wivu. Yaani asiwe na wivu kwa watu. *Sufuria* ina maana ya mke. Mwari anatakiwa ahakikishe kuwa watu katika familia wanapikiwa na kula. Hili ni jukumu lake la kupika chakula. Kama wasemavyo wahenga "*mke ni jiko*". *Chakula* kinasimamia aibu, *Mkungu* (mfuniko) umebeba maana ya kuwa na siri. Mwari anatakiwa asitoe siri za ndani ya nyumba nje. *Mvuke* husimamia mume. Anachoelezewa mwari ni kuwa, amchunge mumewe asije akamtoroka. *Moshi* ni mashoga (marafiki). Mwari anatakiwa atahadhari na marafiki wabaya wasije wakavunja nyumba yake. *Mwiko* ni ushirikiano katika maisha ya ndoa.

## **5.2 Matokeo ya Utafiti**

### **5.2.1.Utendaji wakati wa Uimbaji**

Utafiti huu umedhirisha kuwa kuna utendaji tofauti uliokuwa ukifanyika wakati wa uwasilishwaji nyimbo za harusi. Utendaji uliyojitokkeza ulikuwa ni wa aina tatu. Ambao ni utendaji uliombatana na taashira wakati wa kucheza na kuimba, utendaji katika matukio yanayoashiria mambo ya kitaashira wakati wa uimbaji na utendaji wa uigizaji wa vitu vya bibi harusi wakati wa kuimba nyimbo. Jumla ya utendaji uliojitokeza wakati wa uwasilishwaji nyimbo na uliochanganuliwa ulikuwa 22. Ufasiri huu wa kuapata maana za kitaashira wa utendaji uliwezekana kwa kutumia Nadharia ya Utendaji hasa wenye mihimili wa utendaji kama njia ya mawasiliano.

Kwa kujibu swal la utafiti la tatu utafiti huu, utafiti umedhihirisha kwamba, utendaji husaidia kupambanua maana za taashira katika nyimbo. Halikadhalika utendaji uliokuwa ukifanyika wakati wa uimbaji ulikuwa na maana ya kitaashira. Mtafiti aligundua kuwa, uwasilishwaji wa matendo, uchezaji, uigizaji, maleba na mazingira yalimuongoza mtafiti kupata maana za taashira kuhusiana na wimbo husika. Muhtasari wa matokeo ya maana ya utendaji huo ulikuwa ufuatao:-

Wanawake mikono juu wakiviringisha vidole vya katikati ilimaanisha kujigamba au kuionyesha. Tendo la kusingwa lilibeba maana tofauti kama vile:- kumtoa mwari katika hatua ya utoto na kumuingiza katika hatua ya utu uzima. Kumtia ashki mwari na kumfanya kuwa tayari kukabiliana na tendo la ndoa. Humfanya mwari kuwa na haya na mwisho mwari anafanyiwa singo ili naye akamfanyie mumewe. Aidha, ukataji wa kiuno ulibeba maana tofauti kulingana na muktadha wa uwasilishwaji wa nyimbo. Maana hizi zilikuwa kama vile, kuionyesha mizungu ya kufanya tendo la ndoa na kujifurahisha.

Upigaji kigelegele na makofi pia ulikuwa na maana tofauti kulingana na muktadha wa tukio. Kwa mfano: Vigelegele vilikuwa na maana kama vile: kuwaarifu hadhira, kushangilia au kumpongeza mchezaji anayechenza vizuri au muimbaji kwa kuimba vizuri. Pia humaanisha kuionyesha upeo wa juu wa furaha au kujifurahisha kwa lengo la kufanya mandhari ya sherehe ya harusi kuonekana hai. Aidha, upigaji makofi katika nyimbo za harusi, ulikuwa na maana ya kulinda mapigo ili uimbaji uwe na mizani, kuwapa nguvu waimbaji na kuwashirikisha hadhira

iliyoko katika uimbaji au uchezaji. Pia, husaidia kutambua kuwa, mwendo wa wimbo huo ni wa pole pole au haraka haraka.

### **5.3 Hitimisho**

Sura hii imeshughulikia data ya utafiti ambayo ni utendaji uliyofanyika wakati wa uimbaji. Data hiyo imewasilishwa na kuchanganuliwa kwa mujibu wa Nadharia ya Utendaji. Sura hii ilikuwa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ilikuwa utendaji uliombatana na taashira wakati wa kucheza na kuimba. Sehemu ya pili ni utendaji katika matukio yanayoashiria mambo ya kitaashira wakati wa uimbaji. Sehemu ya tau ni utendaji wa uigizaji wa vitu vyta bibi harusi wakati wa kuimba nyimbo.

Utafiti ulidhihirisha kuwa baadhi ya utendaji ulikuwa na kwa lengo la kumfunza mwari au bibi harusi kunga katika maisha. Mathalani utendaji uliokuwa ukifanywa katika tukio la singo zaidi ulikuwa ni kwa ajili ya kumfundisha mwari mambo ya usafi wa mwili, nguo, nyumba na mitindo ya kufanya tendo la ndoa.

Mtafiti aligundua kwamba ingawa utendaji ulikuwa tofauti uliodhirika wakati wa uimbaji, utendaji uliokuwa na mafundisho kwa ajili ya wari na mabibi harusi ndiyo uliokuwa mwingi. Kwa hiyo matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba utendaji wakati wa uimbaji ulisheheni utendaji wenye kutoa mafunzo kwa wari na mabibi harusi.

**SURA YA SITA**  
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**6.0 Utangulizi**

Sura hii imetoa muhtasari wa matokeo ya utafiti huu, hitimisho lake kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti na matlaba yake na mapendekezo kuhusu aina gani ya utafiti unaoweza kufanywa ili kuibua hazina iliyofichika zaidi katika nyimbo za harusi hasa kwa upande wa fasihi.

**6.1 Muhtasari**

Mada ya utafiti huu ni kwamba nyimbo nyingi za Waswahili wa Unguja zinazoimbwa katika harusi zilisheheni taashira na utendaji ambao kufikia sasa hakuwa umewekwa bayana kitaaluma hivyo, ilikuwa haujulikani. Kwa hiyo, utafiti huu ukafanywa kwa lengo la kubainisha na kufafanua taashira zilizomo katika nyimbo za Waswahili wa Unguja pamoja na kuangalia mchango wa utendaji katika kupatia kila taashira maana iliyokusudiwa kwa maharusi na hadhira.

Kutokana na tatizo hilo, madhumuni yaliyoangaziwa yalikuwa kubainisha kuainisha matumizi ya taashira katika nyimbo za harusi za Waswahili wa kisiwani Unguja, fanua maana za taashira mbalimbali katika nyimbo na umuhimu wake kulingana utamaduni wa jamii ya Waunguja na pambanua maana ya utendaji unaofanywa wakati wa uimbaji nyimbo za harusi. Utafiti huu umebainisha matumizi ya taashira kulingana na madhumuni hayo na maswali ya utafiti. Aidha umebainisha maana za taashira zilizoibuliwa katika nyimbo na umuhimu wake kulingana utamaduni wa jamii ya Waunguja. Halikadhalika utendaji unaofanywa wakati wa uimbaji nyimbo za harusi ultolewa maana kulingana na aina ya utendaji.

Ili kufanikisha kazi hii, Nadharia ya Semiotiki ilitumika sambamba na Nadharia ya Utendaji kama mwongozo. Data iliyokusanywa ilikuwa taashira pamoja na utendaji uliowasilishwa wakati wa uimbaji wa nyimbo za hurusi. Taasira zilipatikana kuititia nyimbo zilizorekodiwa kwa vinasa sauti na unukuzi wa maalumati na viziada vya lugha katika madaftari. Baadaye mtafiti aliwahoji wasailiwa wake kuhusu maana ya taashira hizo na umuhimu wake katika

jamii. Halikadhalika utendaji ulifanywa wakati wa uwasiliswhaji uliandikwa katika madafatari, kisha akachanganua data ili kufikia utatuzi wa tatizo la utafiti wake.

Utafiti ulionyesha kuwa kuna mchakato wa kutafsiri maana za taashira kwani baadhi ya taashira zilikuwa sio zile zinazofahamika kimataifa. Nyingi ya taashira zilitolewa maana kulingana na kueegemea utamaduni wa jamii hii ya Waunguja. Hali hii imeelezwa na Mutembei (2001) kuwa, waimbaji hutumia lugha kisanii ili kuunganisha maarifa, uzeofu wao, utamaduni, mila, desturi na hisia za mahali wanapozalishia kazi za sanaa. Kwa mnasaba wa kauli hii, nyimbo za harusi za Waunguja nazo zilitumia lugha ya kawaida na lugha ya kitaashira kuwasilisha ujumbe waliokusudia kutegemeana na maudhui, muktadha na wakati maalumu.

Uchunguzi umeonyesha kwamba nyimbo ni chombo cha kubeba taashira za aina tofauti. Taashira zilizoibuliwa katika nyimbo zilihusihwa na vitu vinyopatikana katika mazingira pamoja na utamaduni, tajriba na mwenendo wa jamii hii. Hali pia ameielezea Khamis (2004:61) katika kazi yake amehitimisha kwamba nyimbo za taarabu zimetumia taashira kumchora mwanamke wa Kiswahili kwa kunasibishwa na vitu au viumbe vinyopatikana katika utamaduni wao kama vile *kunguru, tasi* (aina ya samaki wa baharini) *lulu, nanasi, zambarau, mung'anye/mumunye* na kadhalika.

Uchanganuzi pia umeweza kubainisha maana za kitaashira zilizoibuliwa nyimboni pamoja na kuonyesha umuhimu wake kwa jamii. Dhamira kadhaa zimejitokeza katika nyimbo kulingana na taashira zilizotumika. Mathalani: mapenzi ya ndoa, umuhimu wa ndoa na umoja (mashirikiano) katika jamii, mwanamke kama chombo cha kazi, taasubi ya kiume na jukumu la mwanamke katika ndoa.

Hivyo nyimbo za harusi zimetumia lugha kitamathali ili kujenga dhamira zinazosawiri jamii kitaswira zaidi na kufanya utanzu huu kuwa ni utanzu wenye utajiri wa matumizi wa lugha ya kitamathali.

Lugha kama chombo muhimu cha kufikisha ujumbe, kukamilisha mawasiliano na hata kupunguza makali ya maneno. Hivyo, matumizi ya taashira katika nyimbo za Waunguza zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuficha maneno ambayo yanaonekana ni matusi kwa jamii. Au maneno ambayo yasingewezekana kuelezwu waziwazi hadharani hususan harusini. Hii ni kusema kwamba, mawasiliano ya kijamii kutokana na uwasilishwaji wa nyimbo na utendaji wake yameweza kuonyesha umuhimu wa nyimbo hizi katika kupidisha habari za siri kwa wanajamii. Aidha, utamaduni na historia ya Waunguza imeweza kubainishwa kupiditia mambo yafuatayo: - uimbaji, utendaji, maana zilizoibuliwa kutokana na nyimbo na matendo uliyodhihirika katika miktadha mbalimbali harusini. Mwisho tunasema kuwa, taashira na utendaji uliomo katika nyimbo za harusi zinaweza kutumika kama chombo cha kutafiti na kuchanganua utamaduni na historia ya jamii. Kwa sababu nyimbo ni dirisha muhimu la kutazamia utamaduni wa watu.

Hayo yote yamedhihirika kwa mwongozo wa Nadharia ya Semiotiki (N.S) ambayo imemwezesha mtafiti kuchunguza jinsi maana za taashira zilivyopatikana katika nyimbo za harusi. N.S imechangia sana utafiti huu kwa kudhihirisha taashira katika nyimbo ambazo zimejitokeza kama taashira za vitu vya baharini, vimbe, vitu vya nyumbani na mimea. Aidha imemwezesha kubainisha ujumbe uliotokana na taashira hizo. Kwa upande mwagine, Nadharia ya Utendaji (N.U) ilimwezesha mtafiti kupata ufasiri wa utendaji uliofanyika wakati wa uwasilishwaji nyimbo. Ufasiri huo ulimpelekea kutambua aina ya utendaji uliojitokeza wakati wa uimbaji na jinsi wachezaji na waimbaji walivyokuwa wakitenda matendo yao. Nadharia zote mbili zimedhihirisha uwezo mkubwa wa kuchambua semi katika nyimbo na utendaji uliokuwa ukifanywa katika matukio tofauti harusini.

Kabla ya kufikia matokeo na mahitimisho ya uchunguzi, ilibidi data ya utafiti huu ichanganuliwe. Data hiyo ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo kuhusu taashira zilizodhihirika katika nyimbo pamoja na utendaji uliodhihirika wakati wa uwasilishwaji nyimbo harusini. Zaidi ya hayo mfumo maalumu wa uchanganuzi ultumika. Mfumo huu ultumika kuonyesha aina za taashira na utendaji. Kila taashira na utendaji uliibainshwa ulifasiriwa kwa kutumia mwongozo wa mfumo huu wa uchanganuzi.

## **6.2 Hitimisho**

Utafiti huu ulikuwa na madhumuni matatu. Kwanza, Kubainisha na kuainisha matumizi ya taashira katika nyimbo za harusi za Waswahili wa kisiwani Unguja. Pili Kufafanua maana za taashira mbalimbali katika nyimbo na umuhimu wake kulingana utamaduni wa jamii ya Waunguja. Tatu Kupambanua maana ya utendaji unaofanywa wakati wa uimbaji nyimbo za harusi. Kutohana na madhumuni hayo, maswali ya utafiti yalikuwa: Je, Nyimbo za harusi za Waswahili wa kisiwani Unguja zina matumizi ya taashira. Je, taashira zilizotumika katika nyimbo za harusi zinabeba maana gani za kitaashira na huwa na umuhimu kwa jamii? Na Je, utendaji unaofanywa wakati wa uimbaji nyimbo za harusi una maana wowote?

Utafiti ulikuwa na maswali matatu. Maswali yote matatu yalijibowi na kuthibitishwa kama ifuatavyo:

Kwa kujibu swalii la kwanza, utafiti umedhihirisha kwamba, nyimbo za harusi za Waswahili Waunguja zina matumizi ya taashira. Taashira hizi zimebainika kuwa za aina mbili. Yaani taashira za **vitu na tendo**. Kwa mfano:

### **Matumizi ya Taashira za Vitu:**

Taashira za vitu zilizoibuliwa, katika nyimbo zilihusishwa na mazingira yaliyowazunguka pamoja na vitu vinavyopatikana katika maisha yao. Kwa mfano: **Vitu vya nyumbani:** *ubeleko, jembe, kioo, kigongo, marashi, ufunguo, gongo, kijiti, wembe, mfuniko na mtaimbo.* **Viumbe:** *mamba, dudu, njiwa, dakitari na papa.* **Mimea:** *uvumba, tumbaku, utango, mbegu, kisiki, , mashina, vilele, udi na mchele.* **Sehemu za mwili** kama vile: *pembe, jicho, ngolo, mkono, mvi na kidonda.* Vitu vingine ni kama vile *chuo, bonde, yasini, behewa na tundu.*

### **Matumizi ya Taashira za Tendo:**

Taashira hizi zilihusishwa na matendo yaliyotajwa katika nyimbo kulingana na muktadha wa kila wimbo. Kwa mfano, **Taashira za tendo zilizomuhusu mwari** ni kama: *unamie chini, ukaone haya, leo nimechoka, bibi aingile chooni kwa maulidi, ukipata maji chamba, mama njoo unifiche dudu laja hilo na kitamchoma kisiki cha mpera.* **Taashira za tendo zilizomuhusu bwana harusi** ni kama:-*sikumpa jembe kwenda kulima, , ataka kitabu achore na kalamu ashachonga, dakitari*

*huyo yuwaja ajakitia dawa kidonda na bwana harusi ukiona bahari. Ama **Taashira za tendo zilizomuhusu mamake harusi** ni kama:- uchungu wa mwana ajuwaye Fatuma mzazi, mama harusi twende ukalole, -tumejizungua kwa yasin tatu, halitupati jicho la mtu, nateremka bonde na kicheko na -mola nitone kipaji chema chenye sitara.*

Kwa mujibu wa swali ka kwanza inaonyesha kuwa, matumizi ya taashira za tendo katika nyimbo za harusi yalikuwa zaidi kuliko ya taashira za vitu. Matumizi ya taashira zote hizi yalifasiriwa na kutolewa maana ya kitaashira kuthibitisha swali la pili.

Swali la pili utafiti umethibitisha kuwa, nyimbo za harusi za Waswahili Waunguja zina maana ya kitaashira. Taashira za vitu, tendo na hali zilizoibuliwa katika nyimbo zilikuwa na maana zaidi ya kile kilichotajwa.

#### **Maana ya Kitaashira za Vitu:**

Taashira za vitu zilitolewa maana ya kitaashira kwa kunasibishwa na umbo la kitu, utendaji kazi wa kitu au vyote viwili na maelezo kutoka kwa wasailiwa. Kwa mfano, maana za kitaashira zilizotolewa kulingana na umbo la kitu (taashira) ni kama vile:

*Muhogo, kisiki na kijiti zilisimamia **uume uliosimika**.*

*Pembe, kalamu na mtaimbo umenasibishwa* **na uume wenye ncha mbele**. Aidha, utendaji kazi wa taashira za vitu kama vile: *mtaimbo, dudu, mashini na wembe* vilevile ulisimamia **uume**. Uhamishaji wa maana kutokana na kiashiria kingine pia umefafanulia na Wafula na Njogo (2007:80) wakimrejelea Freud katika kazi yao. Wanaeleza kwamba, Freud aliibuka na aina mbili za tamathali. Kuna tamathali zinazowakilisha jinsia ya kike, na zile zinawazowakilisha jinsia ya kiume. Tamathali zinazowasilisha jinsia ya kike zina sura ya mpanuko au 'mfunuko' kama ua na tamathali zinazoashiria jinsia ya kiume 'zimesimama' kama penseli au mkuki. Tamathali zote zinazosimama wima zinaashiria uume nazo zilizolala au za mviringo zinawakilisha uke.

Taashira za vitu vingine vilivyopatiwa maana za kitaashira kwa kuzingatia utendaji wa kazi wa vitu hivyo ni hizi zifuatazo:-

Taashira za vitu kama:, *mtango, mbegu, mche* na *koko* zilisimamia **mume/bwana**. harusi. (Mume/bwana harusi anatarajiwa baada ya kuoa aendeleze kizazi).

**Mke/bibi harus** ameashiriwa na vitu kama: *mbegu, utango na njiba*. (Mke anatarajiwa vilevile atakapoolewa alete kizazi).

Ufasiri wa taashira za vitu kama vile: *kidonda, kitabu na kijungo ulisimamia uke*.

**Tendo la ndoa** limeashiriwa na vitu kama: *dawa, bahari na kuchora*.

**Kizazi** kimesimamia taashira za vitu kama: *mtango, mche na utango*.

Taashira ya *jembe* imesimamia **kazi ngumu**.

Kwa mujibu wa maana za taashira za vitu, utafiti umebaini kwamba, Waunguja hutumia sana lugha fiche (taashira) katika nyimbo zao za harus. Haya yamedhihirishwa kutokana na kuwa nyingi ya taashira za vitu zilizopatikana katika nyimbo kama: MKN.9, MKN.1, MKN.8, MKND.20 na MBN.16. Taashira hizi, hutumika hususan kueleza mambo ambayo yasingewezekana kutajwa waziwazi hadharani kama vile:- **uume, uke na tendo la ndoa**. Hata hivyo, wakati wa ukusanyaji nyimbo, kulikuwa na nyimbo chache zilizokusanywa ambazo hazikutumia lugha fiche kama taashira.

### **Maana za Kitaashira za Tendo**

Maana za kitaashira zilitolewa kwa kuhusishwa na **matendo yaliyomuhusu mwari** kama vile:- *muenge kama kioo, uwe mke siti mwenye mahaba, kero si jema la vunja nyumba, mama njoo unifiche dudu laja hilo, kitamchoma kisiki cha mpera, kula muhogo utauona utamu wake, mbogo ya mgeni hailali, kumea mvi si utu uzima bora mashini kuwa nzima, , utampara samaki na kimenichoma kisiki cha mpera*. Baadhi ya taashira hizi zilimaanisha kuwa mwari anatakiwa amuhudumie mumewe kwa upendo, heshima, asiwe na kiburi na awe na haya. Nyingine zilimaanisha, mwari anaogopa wa kufanya tendo la ndoa.

Aidha, maana za **taashira za matendo yaliyomuhusu bwana harus**. kama vile: *sikumpa jembe kwenda kulima; raha ya mume ee kula na nguo, na maneno mema yenyе kituo; kigongo mkononi; kusimbulia mke; dakitari huyo yuwaja ajakitia dawa kidonda, usiche bwana ukiona bahari utaogelea*; Maana ya taashira hizi zilimaanisha kuwa, bwana harus anatakiwa amuhudumie mkewe kwa kumjali, kumpa mahitaji ya lazima. Amuenzi mkewe asiwe ni mwenye kumsimanga na kumpiga. Aidha, taashira nyingine zilimaanisha kuwa, bwana harus anakwenda kukutana kimwili na mkewe hivyo asiwe muoga.

Vilevile, **taashira za matendo yaliyomuhusu mamake harusi** kama vile, *nateremka bonde na kicheko, dada Mwajuma kashaukata ubeleko na uchungu wa mwana ajuwaye Fatuma mzazi.* Ufasiri wa maana ya kitaashira ni kwamba, mamake harusi anafuraha ya kumuozesha mwanawе baada ya tabu ya malezi aliyopata. Ama, taashira kama: *hongera mwanangu nami ni hongere.* Taashira hii ina maana zaidi ya kumpongeza bibi harusi anapokutwa bikira siku ya harusi. Maana nyininge *nami ni hongere*, inamaanisha heshima. Heshima hii anaipata mama mzazi au mlezi wa bibi harusi kwa malezi bora aliyomlea bintie. Tangu binti yake alivyovunja ungo hadi siku ya harusi jambo hili Iinadhihirisha kwamba, mamake bibi harusi alikuwa akimchunga mwanawе asiye akateleza na kuingia katika hadaa za ulimwengu.

Kuhusiana na swali la tatu, utafiti umethibitisha kuwa, utendaji wakati wa uimbaji ulikuwa na maana tofauti kulingana na jinsi utendaji wenyewe uliviyowasilishwa. Maana za utendaji hizi zilikuwa kama kiwasilishi cha utamaduni wa jamii ya Waunguja. Mawazo haya yanaelezwa pia na Ntarangwi (ameshatajwa) akimnukuu Erlmann (1960) "... muktadha wa utendaji husaidia kupata maana ya utamaduni wa jamii".

Ili kukidhi matlaba ya madhumuni ya tatu, mtafiti alifanya uchunguzi wa utendaji uliojitokeza wakati wa uimbaji. utendaji huwa ulikuwa kama ufuatao; Utendaji uliombatana na taashira wakati wa kucheza na kuimba, utendaji katika matukio yanayoashiria mambo ya kitaashira wakati wa uimbaji na utendaji wa uigizaji wa vitu vyta bibi harusi wakati wa kuimba nyimbo.

Utendaji huu husaidia pakubwa kupambanua maana za taashira katika nyimbo. Mtafiti aligundua kuwa, uwasilishwaji wa, uchezaji, uigizaji, maleba na mazingira yalimuongoza mtafiti kupata maana za taashira kuhusiana na wimbo husika. Mathalani, maana ya kitaashira ya utendaji kama vile:

**Wanawake kunyosha mikono juu na kuviringisha vidole vyta katikati** kulimaanisha kujigamba au kujionyesha mbele ya wanawake wenziwao. Matendo aliyofanyiwa mwari wakati wa **kusingwa** yalikuwa na ufasiri wa maana ya kumtoa mwari katika hatua ya utoto na kumwingiza katika hatua ya utu uzima; humtia ashki mwari na humfanya mwari kuwa tayari

kukabiliana na tendo la ndoa pia humfanya awe na haya. **Ukataji wa kiuno** ulikuwa na maana ya kuonyesha mizungu ya kufanya tendo la ndoa. **Tendo la kuoshwa miguu** linamaanisha kutolewa nuksi. Ama uchezaji na uigizaji kama vile **kupara samaki, kuigiza kuchora na kuchonga kalamu kwa kutumia kiganja na kidole** ulikuwa na maana ya kitaashira kushadidia mizungu (mitindo) ya kufanya tendo la ndoa. Upigaji **vigelegele** ulibeba maana tofauti kulingana na muktadha. Maana hizo ni kama vile: kuwaarifu hadhira, kushangilia au kumpongeza mchezaji au muimbaji kwa kuimba vizuri au kujifurahisha kwa lengo la kufanya mandhari ya sherehe ya harusi kuonekana hai. Ama upigaji **mamakofi** ulikuwa na maana ya kulinda mapigo ili uimbaji uwe na mdundo.

Kulingana na utendaji na maana zilizotolewa hapa juu, mtafiti alithibitisha kwamba, vitendo katika utanze wa nyimbo, husaidia kujenga ujumbe uliotolewa. Aidha, matendo yaliyoambatana na taashira katika nyimbo, yaliweza kusaidia kupata maana za kitaashira. Kwa mfano, maana za taashira zilizomo katika nyimbo kama vile, MKN.8 aliyoimbiwa bibi harusi zilifahamiika vyema. Kwa sababu, taashira katika wimbo huu humuhusu bibi harusi. Kwa upande mwengine kama wimbo huu angeimbiwa bwana harusi au kuimbwa nje ya muktadha wa harusi na utendaji wake, usingeweza kupata maana za taashira zilizotumika.

Mbali na maana iliyotolewa kuhusu kupiga mamakofi hapa juu, upigaji mamakofi ulichukua nafasi kubwa wakati wa uimbaji. Utafiti umebaini kuwa, upigaji mamakofi ulitumika sana katika nyimbo ambazo watu huimba huku wakiwa wamekaa au kusimama bila kucheza. Kadhalika upigaji mamakofi ulitumika kama vyombo ambavyo hupigwa na mikono kama vile pembe, vibuyu na kadhalika. Ama vigelegele vilitumika kama filimbi. Vyombo hivyo huw na umuhimu katika nyimbo na ndio mara nyingi husaidia kuita watu walio mbali waje kutazama wimbo au mchezo harusini.

Vilevile, utafiti umegundua kwamba, uimbaji wa nyimbo za harusi za Waunguja huwa na uhalisia. Kwani, hakuna sehemu ya mwili ambayo haishughuliki wakati wa uimbaji – kuanzia miguu, kiuno, tumbo, mabega, midomo na kichwa. Lakini nyimbo hizi zinapoandikwa zinapoteza karibu mambo yote ya madoido.

Mawasiliano ya kijamii kutokana na uwasilishwaji wa nyimbo na utendaji wake yameweza kuonyesha umuhimu wa nyimbo hizi katika kuitisha habari za siri kwa wanajamii. Aidha, utamaduni na historia ya Waswahili Waunguja umeweza kubainishwa kuitia mambo yafuatayo: - uimbaji, utendaji, maana zilizoibuliwa kutokana na nyimbo na matendo yaliyodhahirika katika miktadha mbalimbali harusini. Mwisho tunasema kuwa, taashira na utendaji uliomo katika nyimbo za harusi zinaweza kutumika kama chombo cha kutafiti na kuchanganua utamaduni na historia ya jamii kwa kutumia nyimbo kama dirisha maalumu la kutazamia utamaduni wa watu.

### **6.3 Mapendekezo**

Mtafiti ana mapendekezo yafuatayo:-

Huu ni utafiti uliojikita zaidi katika kutumia taashira na utendaji kupata maana za taashira katika nyimbo za harusi. Utafiti unapendekeza kwa watafiti wengine kuchunguza mitindo ya lugha ilivyotumika katika nyimbo za harusi. Vilevile, tunapendekeza kuwa utafiti zaidi ufanywe kuhusu nyimbo za harusi kwa kutumia nadharia tofauti na tuliyotumia katika tasnifu hii. Mathalani watafiti wengine wanaweza kuchanganua matumizi ya lugha katika nyimbo za harusi kwa kutumia nadharia ya kimitindo.

Ingawa mambo ya msingi na muhimu katika nyimbo za harusi ni kuonyesha jinsi miviga, imani na itikadi zinavyoteklezwa katika harusi lakini utafiti huu haukujishghulisha na hayo. Hivyo, utafiti unapendekeza kwa watafiti wengine kuchunguza masuala hayo katika nyimbo za harusi za Waswahili au jamii nyingine.

Nyimbo za harusi na zisizokuwa za harusi bado ni uwanja mpana sana ambao haujafanyiwa uchanganuzi wa kina. Utafiti huu umeona kuna umuhimu kwa watafiti wengine kuchunguza masuala ya mtindo kama vile toni, hisia na maghani katika nyimbo.

Kama dhima moja wapo ya fasihi ni kelimisha jamii. Utafiti unapendekeza kwa watafiti wengine kuchunguza katika nyimbo za harusi maudhui kuhusu uaminifu katika ndoa ili kujikinga na ugonjwa wa UKIMWI, uzazi wa mpango na athari za talaka katika jamii. Jambo ambalo utafiti huu haukulishughulikia.

Aidha, utafiti haukuchunguza taaluma ya utungaji muziki au nyimbo za harusi hizi bali ulijikita zaidi kuchunguza jinsi taashira zilivyoibuliwa na kutolewa maana za kitaashira. Hivyo basi, utafiti unapendekeza kwa watafiti wengine kuchunguza taaluma hizi.

Hata hiyo kama tanzu nyingine za fasihi simulizi, nyimbo za harusi za Waswahili hazijapata kuenezwa vyema kupitia katika vyombo vya mawasiliano na elimu kama Topan (1984) alivyosema. Hili ni tatizo ambalo linaweza kutinga maendeleo ya fani hii na fasihi simulizi kwa jumla. Wakati umefika ambapo fani hii na fasihi simulizi kwa jumla inapaswa, kuenezwa, kufunzwa na kutafitiwa kwa undani kwa manufaa ya maendeleo ya jamii zetu kwa jumla.

## MAREJELEO

- Abdulaziz, M.H.(1979) *Muyaka: 19<sup>th</sup> Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Abedi, K.A (1954) *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Al-Farsy, A.S (1994) *Qur'ani Takatifu*. Nairobi: The Islamic Foundation.
- Alhabib, E.A. (2012) " Matumizi ya Luga katika Nyimbo za Taarabu". Tasnifu ya uzamili Chuo Kiku Huria ha Tanzani, (haijachapishwa).
- Ali .O. H. (2004) "Khanga Writings" katika Swahili language and Culture, Free Encyclopedia.
- Allen, J. (1976a) "Swahili History Re-visited" makala ya semina iliyofanyika Institute of African Studies, Chuo Kikuu cha Nairobi. Novemba, 1976 (haijachapishwa).
- \_\_\_\_\_(1976b) "Swahilization: A Cultural Concept and its Signification in Kenya Today" Institute of African Studies, Chuo Kikuu cha Nairobi. Novemba, 1976.
- Askew, K.M. (1997) "Performing the Nation: Swahili Musical Performance and the Production of Tanzania National Culture". Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Harvard (haijachapishwa).
- Barthes, R. (1973) *Mythologies*. London: Made Simple Book.
- \_\_\_\_\_(1984) "Rhetoric of the Image" katika The Responsibility of Forms. (mfs) Heath. Oxford: Blackwell.
- Bauman, R. (1977) *Verbal Art as Performance*. Rowley, Mass: Newbury House.
- Beja, S.K. (2000) "Giriama Funeral Songs: A Functional - Aesthetic Study" Tasnifu ya uzamifu Chuo Kikuu cha Nairobi ( haijachapishwa).
- Berger, A.A. (1984) *Sign in Contemporary Culture*. New York: Longman.
- Blamires, H. (1991) *A History of Literary Criticism: Post Structure or Deconstruction*. London: Macmillan Press limited.
- Bukanya, A. Gachanja, M. na Nandwa, J. (1992) *Oral Literature a Senior Course*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Campbell, C.A. (1976) "An Introduction to the Music of Swahili Women" Institute of African Studies, Chuo Kikuu cha Nairobi. November, 1976.

- \_\_\_\_\_ (1983) " Nyimbo za Kiswahili: A Social-Ethnomusicological Study of a Swahili Poetic Form". Tasnifu ya uzamifu Chuo Kikuu cha Washington (haijachapishwa).
- Chai, F. (2003) "Gaining Access in Fieldwork" katika Kitetu, C.W. (mh) (2003) *Social Science Research Getting into the Field* makala zilizokusanywa katika warsha ya AICAD Idara ya Lugha na Isimu. Chuo Kikuu cha Egerton tarehe 15/11/2003.
- Chandler, D. (1998) "Semiotics for Beginners" imetolewa katika [WWWDocuments]  
<http://www.aber.uk/modia/Documents/S4B/semeo7.html> tarehe 1/10/2008.
- Coppens, F. (1980) "Wedding Customs in Lamu". Lamu:The Lamu Society.
- Culler, J. (1981) *The Pursuit of Sign: Semiotics, Literature and Deconstruction*. London: Routledge.
- Davidson, B. et al (1967) *The Growth of African Civilization. East Africa to the late 9<sup>th</sup> Century*. Nairobi. Longman.
- Eagleton, T (1976) *Criticism and Ideology*. New York: Verso Edition.
- Eco, U. (1977) *A Theory of Semiotics*. London: Macmillan Press limited.
- El-Maawy, A.A.A (2011) "Jawabu la Mwana Kupona: Mausyo ya Mke wa Kisasa na Waasiya wa Mwana Kupona". Dar es Salaam. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
- Farsy, A. (1967) *Ada za Harusi katika Unguja*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- \_\_\_\_\_ (1960) *Kurwa na Doto*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Fine, E.C. (1984) *The Folklore Text: From Performance to Print* Bloomington and Indianapolis:Indiana University Press.
- Finnegan, R. (1977) *Oral Literature in Africa*: London: OUP.
- \_\_\_\_\_ (1992) *Oral Traditions and the Verbal Arts. A Guide to Research Practices*. London:Routledge.
- Harries, L. (1962) *Swahili Poetry*. Nairobi: OUP.
- Hichens, W. (1962) *AL.Inkishafi*. Nairobi: Longman.
- Igobwe, E. S. (2007) "Taarabu and Chakacha in East Africa Transformation, Appreciation and Adaptation of Two Popular Music Genres of the Kenyan Coast" makala iliyowasilishwa katika Conference of Music in the World of Islam, Assilah, 8 – 13 Agosti, 2007.
- Indede, F. (2011) "Mwanamke Angali Tata katika Ushairi wa Kisasa?" katika *Swahili Forum* 18

(2011): 163-197.

Innis, R.E. (1985) *Semiotics*. London: Made Simple Books.

Jilala, H. (2008) "The Artistic Uses of Metaphore in Constructing Meanings and Messages in New Generation Songs in Tanzania". Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Dar –es-Salaam, (haijachapishwa).

Kezilahabi, E. (1978) *Ushairi wa Shaaban Robert*. Nairobi. Kenya Literature Bureau.

Khamis, A.H. (1981) " Sanaa za Utendaji kama Utanzu wa Fasihi Simulizi" katika *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Zanzibar: TAKILUKI.

\_\_\_\_\_ (2002) "Wondering about Change": The Taarab Lyrics and Global Openness. *Nordic Journal of African Studies* 11,2: 198-205.

\_\_\_\_\_ (1983) "Nafasi ya Fasihi Simulizi katika Jamii ya Kitanzania" katika *Mulika* Na. 15. Dar es Salaam: TUKI.

\_\_\_\_\_ (2004) "Images of Love in the Swahili Taarab Lyric: Local Aspects and Global Influence" katika *Nordic Journal of African Studies* 13(1): 30–64 (2004).

\_\_\_\_\_ (2005) "Clash of Influences and Conceptualisation of Taarab in EastAfrica. Sawahili Forum XII:133-159.

Khatib, M.S. (1992) "Taarabu Zanzibar" Dar es Salaam: Tanzania Publishig House.

\_\_\_\_\_ (1981) "Taarabu ni Fasihi – Simulizi?" katika *Makala za Semina yaFasihi Simulizi*. Dar es Salaam: TUKI.

\_\_\_\_\_ (1985) "Utenzi wa Mwana Kupona" katika *Mulika* 15. Dar es Salaam: TUKI.

King'ei, G.K. (1992) *Language, Culture and Communication The Role of Taarabu Songs in Kenya 1963-1999*.Tasnifu ya Uzamifu iliyochapishwa, Chuo Kikuu cha Howard.

Kirumbi, P. (1976) *Misingi ya Fasihi–Simulizi*. Nairobi: Shungwaya Publication.

Kitetu, C.W. (mh) (2003) "Social Science, Research Getting into the Field" makal zilizokusanywa katika warsha ya AICAD Idara ya Lugha na Isimu.Chuo Kikuu cha Egerton. Tarehe 15/11/2003.

Knappert, J. (1977) "Songs of Swahili Women" katika Africa *Und. Ubersee*.69:10 36.

\_\_\_\_\_ (1986) *Four Centuries of Swahili Verse*. Nairobi: Heineman.

Lawes, R. (ht) "LAWES: Demystifying Semiotics: Some Key Question Answerd". Imetolewa katika <http://www.lawes.consulting.com/-filedmystifying-semiotic> tarehe 23/1/2008.

Lugwiri, O.P. (2011) "Sitiari, Taashira na Tashibiha katika Uwasilishaji wa Dhamira katika Utensi wa Tambuka: Uhakiki wa Kimitindo". University of Nairobi. Tasnifu ya Uzamili. (Haijachapishwa).

Leech, G.N.(1969) *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group.

Mary, P na Elizabeth, T (1980) *Liguistics for Students of Literature*. New York: Harcourt.

Matteru, M.L. (1979) "Mbinu za Ukusanyaji wa Fasihi Simulizi za Hatima Yake" katika *Lugha Yetu* Na. 34. Dar es Salaam: BAKITA.

\_\_\_\_\_ (1981) "Uchunguzi katika Fasihi Simulizi. Vizingiti na Mikabala" katika *Makala za Semina ya Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbughuni P. (1981) "Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi Riwaya na Hadithi" katika *Makala za Semina ya Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: TUKI.

Milroy, J. (1987) *Observing and Analysing Natural Language*. Oxford: Basil Blackwell.

Milroy, L na Milroy, J. (1980) *Language and Social Networks*. Oxford: Basil Blackwell.

Miruka, O. (1994) *Encounter with Oral Literature*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Mlacha. S.A.K. (1995) "Fasihi Simulizi na Usuli wa Historia ya Pemba" katika *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mohamed, A.A. (1987) "A Guide to History of Zanzibar". Zanzibar: Good Wek Publication.

Momanyi, C.(2001) "Nafasi ya Mwanamke katika Ushairi wa Shaaban Robert" katika *Kiswahili*, Juzu 64. TUKI. 64: 57-64.

Mosha, E.S (2002) "The Usese of Metaphor in Chaga Folk Tales and Oral Petry". Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (haijachapishwa).

Moriaarty's. (ht) "Visemics: Aproposal/ for Marriage Between Semiotics and Visual Communication" imetolewa katika <http://spot.coorado.edu/~moriarts/visemimics.htm> tarehe 26/1/2008.

Mnenuka, A. (2012) Tofauti ya Dhana ya Mwanamke katika Taarab (*Mipasho*) na Nyimbo za Kibena" katka *Swahili Forum* 19 (2012): 23-44.

Mnyampala, M. (1965) *Diwani ya Mnyampala*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Msokile, M. (1981) "Nafasi ya Nyimbo za Fasihi Simulizi katika Jamii Inayoendelea" katika *Makala za Semina ya Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M.M na Kahigi, K. (1979) *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mulokozi, M.M. (1975) "Revolution and Reaction in Swahili Poetry" katika *Kiswahili Vol 45, No 2*. Dar es Salaam: TUKI.

\_\_\_\_\_ (1980) "Uchunguzi wa Fasihi Simulizi" katika *Makala za Semina ya Waandishi wa Kimataifa*. Dar es Salaam: IKR – UNESCO.

Mutembei, K.A. (2001) Poetry and aids in Tanzania: Changing Metaphore and Metonymies in Haya Oral Traditions Leiden: Research School CNWS, Leiden University, (CNWS Publication no 101).

Mwamzandi, I.Y. (2000) "Performance, Carnival and The Deconstruction of Social Meaning: the Case of Taarabu Among The Swahili" katika *Makala ya Kongamano la Kimataifa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mwamzandi, M.Y. (2002) "Kupungua kwa Michezo ya Kiswahili katika Sherehe za Drama za Kitaifa za Kenya: Nafasi ya Uandishi na Uwasilishaji. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Egerton. (haijachapishwa).

Nabahanny, S.A. (1985) *Umbuji wa Kiwandeo*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Nandwa, J. na Bukenya, A. (1983) *Oral Literature for Schools*. Nairobi: Longman.

Ngara, E. (1985) *Stylistics, Criticism and the African Novel*. London: Heneimann.

Ngugi, P.M.Y (2000) "Nafasi ya Muziki Uliyopendwa katika Fasihi ya Kiswahili", katika AAP 64 Swahili *Forum VII*. 145-152.

Ngure, A. (2003) *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Nkwera, F.V. (ht) *Tamrini za Fasihi Simulizi: Sekondari na Vyuo*. Dar: Business Printers Ltd.

Njozi, H.M (1990) "Utendi wa Mwanakupona and Reception Aesthetics". *Kiswahili Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam 57:55-67.

Ntarangwi, M. (2001) "A Socio - Historical and Contextual Perfomance Among the Swahili of Mombasa, Kenya." makala katika *Cultural Analysis* Vol.2:1-37. Chuo Kikuu cha California.

Okpewho, L. (1992) *African Oral Literature: Background Characters and Continuity*. Bloomington: Henemann.

- \_\_\_\_\_(1983) *Myth in Africa*. London: Cambridge.
- Omari, S. (2006) "Mitindo na Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipyta Tanzania" katika *Mulika*. Dar es Salaam: TUKI.
- Othman, S.Y na Yahya, A.S. (wh) (2004) *Howani Mwana Howani:Tenzi za Zaynab Hamid Mohammed*. Dar es Salaam: TUKI.
- Pierce, C. (1977) *Semiotics and Signifies*. Bloomington: Indiana University Press.
- Macneill. R. ( 2013) "Henna Tumbiri" imetolewa tarehe 23/9/2013 katika <http://www.elimuasilia.org/culture/174-henna-tree.html>.
- Reid, R.F. (1965) *Introduction to the Field of Speech*. Atlanta: Scot Forest and Company.
- Saussure, F de. (1966) *Course in General Linguistics*. Wade Baskin (mfs). New York: Mac Graw.
- Schechner, R. na Appel, W. (wh), (1995) *By Means of Performance: Intercultural Studies of Theatre and Ritual*. London Cambridge University Press.
- Sengo, T.S.Y. (1995) "Itikadi katika Jamii za Kiswahili" katika *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Shariff, I.N. (1988) *Tungo Zetu*. Trenton: Red Sea Press.
- Silverman, D. (2005) *Doing Qualitative Research*. London: SAGE Publication.
- Strobel, M. A. (1974) *Muslim Women in Mombasa 1890 – 1975*. New Haven: Yale University Press.
- Timammy. R (2002) *Mombasa Swahili Women Wedding Songs: A Stylistic Analysis*. Tasnifu ya uzamifu ChuoKikuu cha Nairobi.
- Tonya, L.M. (1978) *Misingi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Black Star Agencies.
- Topan, F. (1971) " Oral Literature in a Ritual Setting: The Role of Swahili Spirit Song in a Spirit Mediumship cult of Mombasa, Kenya. Tasnifu ya Uzamifu ya Chuo Kikuu cha London (haijachapishwa).
- \_\_\_\_\_(1984) "Fasihi Simulizi: Mwaka 2000 na Baadaye" makala iliyowasilishwa katika Kenya Kiswahili Association International Conference, Nairobi, Septemba, 1984.
- \_\_\_\_\_(1995) "Vugo: A Virginity Celebration Ceremony among the Swahili of Mombasa" katika Jarida la *African Languages and Cultures*. 8, 1:87-107.

- Tordova, T. (1983) *Symbolism and Interpretation*. London: Routledge and Kegan Paul.
- TUKI. (2006) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi:OUP.
- Turner, V. (1990) "Are there Universal of Performance in Myth, Ritual and Drama?" katika Schechner, R. Na Appel, W. (wh) *By Means of Performance: Intercultural Studies of Theatre and Ritual*. London Cambridge University Press. Cambridge: Cambridge University Press pp 8-18.
- Voloshinov, V. (1973) *A History and Philosophy in Language*. London: Seminar Press.
- Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi*: Nairobi, Phoenix Publishers Ltd.
- \_\_\_\_\_ (2003) *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*: Nairobi, Focus Books.
- \_\_\_\_\_ (2003) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*: Nairobi Focus Books.
- Whiteley, W.H. (mh) (1966) *Waimbaji wa Juzi*. Dar es Salaam: TUKI.

## **KIAMBATANISHO CHA I**

### **WASAILIWA WALIOHOJIWA**

Hawa ni baadhi ya wasailiwa waliohojiwa kuhusu taratibu za harusi za Waunguja na kutoa maelezo kuhusu maana za taashira na matendo wakati wa uimbaji.

Haji Gora: Mzee maarufu kutoka Tumbatu, anayefahamu utamaduni wa Waswahili Wazanzibar.

Pia ni shaha

wa kutunga nyimbo za taarabu na mashairi ya Kiswahili alihojiwa tarehe 12/10/2009 na 2/1/2010.

Bi. Kidude: Ni ajuza na mnyakanga maarufu katika kisiwa cha UNGUJA. Alihojiwa tarehe 20/10/2009. Aidha, watafiti wasaidizi walimshuhudia akiimba na kupiga ngoma mwenyewe wakati wa singo huku akimfunza mwari. (Sasa ni marehemu alifariki mwaka 2013).

Bi. Riziki, Bi Sauda na Bi. Mwanamvua wasingaji wa kisasa waliohojiwa tarehe 1/11/2009

Mzee Makame Somo: Shehe mtu mzima wa umri alihojiwa tarehe, 10/9/2010.

Bi Salma: Kungwi, alihojiwa tarehe, 12/11/2009 na 8/12/2009.

Makame Juma: Mshenga, alihojiwa tarehe 2/12/2009.

Bi Sihaba : Mnyakanga maarufu mjini UNGUJA anayefundisha wari mambo ya kunga katika maisha ya ndoa. Alihojiwa tarehe 3/12/2009 na 12/4/2010.

Bi. Hafuswa: Mwanamke mtu mzima anayefahamu mila, desturi na utamaduni wa Waswahili kwa undani. alihojiwa tarehe 9/8/2008 na 10/12/2009.

Bi. Rehema Makame : Kungwi alihojiwa tarehe 25/10/2009.

Bi. MwanaKheri : Mmoja wa waimbaji wa nyimbo za harusi, alihojiwa tarehe 2/2/2010.

Haji Hamisi: Mshenga, umri wa makamu alihojiwa tarehe 15/1/2010.

Bi Amina: Kungwi na mwimbaji wa nyimbo za unyago Makunduchi, alihojiiwa tarehe 15/3/2010.

Bi. Khadija: Mnyakanga anayefundisha wari mambo ya kunga wakati wa singo. Alihojiwa tarehe 10/3/2010.

Bi Riziki Pembe: Mnyakanga na mzoevu wa kuwafunda wari wa kike kunga za maisha. Alihojiwa tarehe 7/8/2008 katika shughuli ya singo iliyofanyika Mchangani – UNGUJA.

Mzee Alawi: Mwimbaji na mpigaji ngoma katika harusi. Mahojiano yalifanyika tarehe 4/4/2010 nyumbani kwake Mji Mkongwe.

Kassim Dadi: Mtu mzima anayefahamu mila, desturi na utamaduni wa Waswahili wa Unguja. Alihojiwa tarehe 6/4/2010.

Skh. Khamis Suleman: Imamu wa msikiti Maiti, aliyeojiwa tarehe 18/1/2010 na 1/9/2010.

Mfaume Haji : Mtu mzima anayefahamu mila, desturi na utamaduni wa Waswahili wa Unguja. Alihojiwa tarehe 15/3/2010.

## **KIAMBATANIISHO CHA II**

### **NYIMBO ZA HARUSI ZILIZOCHANANULIWA**

Jumla ya nyimbo ni tisini (90) zilizokusanywa nyanjani. Katika sehemu hii zimeorodheshwa nyimbo sitini (60). za harusi za Waswahili Waunguja . zilizotumiwa kwa uchanganuzi katika utafiti huu. Nyimbo hizi zimepangwa kulingana na muktadha wa tukio wa sherehe za harusi. Kila wimbo ulipewa jina na kifupisho (*song code*) cha jina chenyenambari. Vifupisho vya majina yenyenambari yalitumiwa ili iwe rahisi kurejelea nyimbo wakati wa uchanganuzi. Nyimbo zilizosalia zimeorodheshwa katika Kiambatisho cha II. Zifuatazo ni orodha ya nyimbo zenyenambari na vifupisho vyake zilizotumiwa katika tasnifu hii.

#### **(MMH) MUKTADHA WA KUPELEKA MAHARI**

##### **MMH 1. MNGANAMBA.**

*Mnganamba katumba kadogo,*

*Mwana huyu kamzaa nani? eeee!*

*Mwana huyu kamzaa nani?*

*Kidomo katiti kama kasiba  
Chenye mwanya kati mbwake haiba  
Ndiye mke siti mwenye mahaba  
Atwazaye watu mahadharani.*

*Nakwenda alika kwa guu langu  
Tangu majirani hata ndu zangu  
Asiyenijia kwa hili langu  
Akiwa na lake asitumai.*

##### **MMH.2. JAHAZI**

*Jahazi yetu twaipeleka kwa pepo njema.*

*Nenda mwanangu amana Llahu Amana Rasuli.*

*Huyo ajaye mwana wa siwa na matuwazi.*

##### **MMH.3. NATAKA TAMBUU**

*Nataka tambuu na popoo,*

*Na tumbako njema yenyenileo,*

*Ladha ya mume kula na nguo,*

*Na maneno mema yenyenileo.*

*Kijakazi change si cha kutuma,  
Sikumpa jembe kwenda kulima,  
Nilimpa chuo kwenda kusoma,  
Asome ilimu na Kuruani.*

#### **MMH.4 TULIVUNILE JANGA**

*Mama tulivinile janga eee,!*

*Eeee! Jangaa! Seuze langu mwenyewe.*

*Nyumba ya mwari aingia koko: paramia.*

*Utango nautambae: uwe mwana wa Baraka.*

*Mpishe bwana apite: ende kwao ende kwa wazee wake wamzalie*

#### **MKH MUKTADHA WA KUALIKA HARUSI**

##### **MKH.1. NITUMWA NA MAMA**

*Nitumwa na mama kwenda alike,  
Tangu Mugudisho hata Marika,  
Ndio mbegu njema isiyo shaka,  
Na mwenye kupanda hutumaini.*

*Wallahi Billahi sikuyawaza.  
Na moyoni mwangu sikuwelekeza,  
Haya ni ya Mungu yakwe majazi,  
Aliyonijazi Ulimwenguni.*

*Andika mwandishi khati utunze,  
Utie nukuta na irabuze,  
Isimu ya Mola utangulize,  
Na wenye kusoma siwalahini.  
Nimejipatia karume nduya,  
Wa kumliwaza wangu ukiwa,  
Japo nipa moja kwa nyaka piya,  
Lisiwele neno la kunaambia.*

#### **(MSG) MUKTADHA WA SINGO**

##### **MSG.1. BISUMILLAHI**

Kungwi:      *ee oo yaa ee bisumilahi ndio ya kwanza ya kuondokeaa,  
bisumillahi ndio ya kwanza.*

Watani:      *ee oo yaa ee bisumilahi ndio ya kwanza ya kuondokeaa,  
bisumillahi ndio ya kwanza.*

Kungwi:      *ee oo yaa eee amana Allahi amana rasulli, nenda mwanangu,  
amana allahu amana rasuli ee.*

Watani:      *ee oo yaa eee amana Allahi amana rasulli, nenda mwananguuu,  
amana allahu amana rasuli ee*

Kungwi:      *ee oo yaa eee muenge enge kama kioo mume nduguyoo,*

*munge enge kama kioo mume nduguyoo oo.*

Watani:        *ee oo yaa eee mume muenge enge kama kioo mume nduguyoo,*  
*munge enge kama kioo nduguyoo oo.*

Kungwi:        *ee oo yaa eee na mama yangu shoti awepo wote ni mama ee,*  
*na mama yangu shoti awepo wote ni mama*

Watani:        *ee oo yaa eee na mama yangu shoti awepo wote ni mama ee,*  
*na mama yangu shoti awepo wote ni mama*

Kungwi:        *ee oo yaa eee enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini,*  
*enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini ee.*

Watani:        *ee oo yaa eee enyi wazazi yote mwayafahamu mwana ni ini,*  
*enyi wazazi mwayafahamu mwana ni ini.*

Kungwi:        *ee oo yaa eee akikuaga mpe ruhusa mwana anakwao ee,*  
*akikuaga mpe ruhusa mwana anakwao ee.*

Watani:        *ee oo yaa eee akikuaga mpe ruhusa mwana anakwao oo,*  
*akikuaga mpe ruhusa mwana anakwao.*

#### MSG.2. USILIE

Kungwi:        *Usilie usilie eee mtoto*

Watani:        *Oyaa*

Kungwi:        *Ukaniliza na miyee ee mwanangu*

Watani:        *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*

Kungwi:        *Machozi yako ya weke ee mwanangu*

Watani:        *Oyaa*

Kungwi:        *Nikifa unililie wee mwanangu*

Watani:        *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*

Kungwi:        *Ujipige pige nachi wee mtoto*

Watani:        *Oyaa*

Kungwi:        *Watu wa kuzuie wee mwanangu*

Watani:        *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*

Kungwi:        *Nyamaa kulia waulize huyu nani wee mtoto,*

Watani:        *Oyaa,*

Kungwi:        *Huyu mtoto na mamaye ee mwanangu,*

Watani:        *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*

Kungwi:        *Nyamaa kulia usome Alamatarai we mtoto,*

Watani:        *Oyaa,*

- Kungwi: *Na birabilfalaqi wee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Wee utakuwa mtu bora we mtoto,*  
 Watani: *Oyaa,*  
 Kungwi: *Jamii na makhuluki we kijana,*
- Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Wee jilazimishe subira wee mwanangu,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Itakuepuka dhiki we mtoto,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Kijakazi mwanakombo wee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Bibi nyumbani akwita wee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Wende ukateke maji wee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Hadi ujaze birika we mwanangu,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Kisimani tele wee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Wala si ya kulimbika wee bibiyee,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Mama aliponizaa we mtoto,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Hakuniona mbaya ee mwanangu,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Akanipa kula kwema ee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Na nguo njema kuвая wee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Nyamaa kulia wee kila nini kila nini wee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Kilio chini ya mto ee mwanangu,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Nyamaa kulia na kichaa hakinipiti ee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Huish kunipa majuto ee mwanangu,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*

- Kungwi: *Ma juto ya kungungu manga wee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Na moyo ndiko ulipo wee mwanangu,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Mama aliponizaa ee mwenangu*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Kaniguna mara tatu wee mwanangu,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Nyamaa kulia akanitia ungoni ee kibibi,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Akawaonesha watu ee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Siliki sitafuniki ee bibiyee,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Jina langui nyanya mwitu ee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Nilipokuwa mgonjwa ee mwanangu,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Hukuja kunitazama ee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Kikombe chako cha uji ee mwanangu,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Uliona mali sana ee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*
- Kungwi: *Ulidhani nitakufa wee mtoto,*  
 Watani: *Oyaa,*
- Kungwi: *Upate kunila nyama ee mtoto*  
 Watani: *Oyaa mtoto nyamara kuilia.*

### MSG.3. KISIKI

*Kisiki wee sikia mumeooo,*  
*Kisiki wee sikia mumeo,*  
*Jambo la kwambia halatuli moyo,*  
*Kisiki wee sikia mumeoo.*

*Kibonongo ndio mumeooo,*  
*Kibonongwa ndio mumeooo,*  
*Jani la mkungu uzuri wa bure,*  
*Kibonongwa ndio mumeo.*

*Kanganga ndio mwenye uziwa,  
Kanganga ndio mwenye uziwa,  
Hili yungi yungi liletwa na mai,  
Kanganga ndio mwenye uziwa.*

Kungwi: *Hasa kwani nitumwa tamboo na popozee,*

Watani: *Na popozee,*

Kungwi: *Na tumbako njema ee zenyee kileo,*

Watani: *Zenyee kileo,*

Kungwi; *Raha ya mume ee kula na nguo,*

*Na manenomema yenze kituo.*

Watani: *ee oo yaa ee na manenomema yenze kituo,*

*Na tumbako njema ee zenyee kileo,*

*Raha ya mume ee kula na nguo,*

*Na manenomema yenze kituo.*

Kungwi: *Hasa kwani nitumwa na kwenda alika,*

Watani: *Kenda alike,*

Kungwi: *Tangu Mogadishu hata Merika,*

Watani: *Hata Merika,*

Kungwi; *Ni mbegu njema ee sio shaka,*

*Na mwenye kupanda hutumaini.*

Watani: *ee oo yaa ee na mwenye kupanda hutumaini.*

*Tangu Mogadishu hata Merika,*

*Ni mbegu njema ee sio shaka,*

*Na mwenye kupanda hutumaini. (vigelegele).*

Kungwi: *Hasa kwani kidomo katiti kama kaswiba,*

Watani: *Kama kaswiba,*

Kungwi: *Uwe mke siti wee mwenye mahaba,*

Watani: *Mwenye mahaba,*

Kungwi: *Mwenye mwanya kati ee wake haiba,*

*Atoae watu mahadharani.*

Watani: *ee oo yaa ee atoae watu mahadharani .*

*Uwe mke siti wee mwenye mahaba,,*

*Ni mbegu njema ee sio shaka,*

*Mwenye mwanya kati ee wake haiba,*

*Atoae watu mahadharani. (vigelegele).*

Kungwi: *Hasa kwani ni tumwa na nana, nenda ni kambe,*

Watani: *Nenda ni kambe,*

Kungwi: *Nikambe usubi ee hata ziumbe,*

Watani: *Hata ziumbe,*

Kungwi; *Watu wa kifumba mwanangu ee wewe usifumbe,*

*Sema wazi wazi wayafahamu.*

Watani: *ee oo yaa ee sema wazi wazi wayafahamu,  
Nikambe usubi ee hata ziumbe,  
Watu wa kifumba mwanangu ee wewe usifumbe,  
Sema wazi wazi wayafahamu. (vigelegele).*

Kungwi: *Hasa kwani kutwii mume kwanza asili,*  
Watani: *Kwanza asili,*  
Kungwi: *Wana wazuoni ee walifaswili,*  
Watani: *Walifaswili,*  
Kungwi; *Kwanza Mayasa wee biti Jabiri, yaya wa Fatuma biti Rasuli.*  
Watani: *ee oo yaa ee, yaya Fatuma biti Rasuli.  
Wana wazuoni ee walifaswili,  
Kwanza Mayasa wee biti Jabiri,  
Yaya wa Fatuma biti Rasuli. (vigelegele).*

#### MSG.4. KERO SI JEMA

Kungwi: *Kero kero kero kero, kero kero kero kero,  
Kero kero sijema, la vunja nyumba.*  
Watani: *Kero kero kero kero, kero kero kero kero,  
Kero kero sijema, la vunja nyumba.*  
Kungwi: *Kingia kero ee, kitoka kero , akikaa kero, akisimama kero,  
Kero kero si jema la vunja nyumba.*  
Watani: *Kingia kero ee, kitoka kero , akikaa kero, akisimama kero,  
Kero kero si jema la vunja nyumba.*  
  
Kungwi: *Ukanga mare ee ukanga mare, ukanga mare ee ukanga mare,  
Unakwenda mijini mwa watu, ukanga mare.*  
Watani: *Ukanga mare ee ukanga mare, ukanga mare ee ukanga mare,  
Unakwenda mijini mwa watu, ukanga mare.*  
  
Kungwi: *Ukafiche kuche ee, ukafiche kuche ee, ukafiche kuche ee,  
Unakwenda mijini mwa watu, ukafiche kuche.*  
Watani: *Ukafiche kuche ee, ukafiche kuche ee, ukafiche kuche ee,  
Unakwenda mijini mwa watu, ukafiche kuche.*  
  
Kungwi: *Unamie chini ee unamie chini, unamie chini ee unamie chini  
Unakwenda mijini mwa watu, unamie chini.*  
Watani: *Unamie chini ee unamie chini, unamie chini ee unamie chini.  
Unakwenda mijini mwa watu, unamie chini.*  
  
Kungwi: *Ukaone haya ee ukaone haya, ukaone haya ee ukaone haya ee .  
Unakwenda mijini mwa watu, ukaone haya.*  
Watani: *Ukaone haya ee ukaone haya, ukaone haya ee ukaone haya ee .  
Unakwenda mijini mwa watu, ukaone haya.*

## MSG. 5. KUNA ILA MOJA

Kungwi:*Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Uchafu uchafu uache ila.*

Watani:*Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Uchafu uchafu uache ila.*

Kungwi: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Kuwapuuza wakwe ila.*

Watani: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Kuwapuuza wakwe ila ila.*

Kungwi: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Kidogo nda kwetu ila.*

Watani: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Kidogo nda kwetu ila.*

Kungwi: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*

*Kila siku kwa mama ila.*

Watani: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Kila siku kwa mama ila.*

Kungwi: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Kusimbulia chakula ila.*

Watani: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Kusimbulia chakula ila.*

Kungwi: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Siwezi kupika ila.*

Watani: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Siwezi kupika ila.*

Kungwi: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Ujuba uuache ila.*

Watani: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Ujuba uuache ila.*

Kungwi: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Nyumbani kufagia ila.*

Watani: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Nyumbani kufagia ila.*

Kungwi: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Leo nimechoka ila.*

Watani: *Kuna ila moja ila ila mama ila,*  
*Leo nimechoka ila.*

Kungwi: *Kuna ila moja ila ila baba ila,*  
*Kigongo mkononi ila.*

Watani: *Kuna ila moja ila ila baba ila,  
Kigongo mkononi ila.*

Kungwi: *Kuna ila moja ila ila baba ila,  
Kusimbulia mke ila.*

Watani: *Kuna ila moja ila ila baba ila,  
Kusimbulia mke ila.*

#### MSG.7. KACHECHE

*Kachehe, Kachehe, Kachehe,  
Kuna mamba kanilia nguku wangu.*

#### MSG.11. KAWAIDA YA SINGO

Kungwi: *Iyo kawaida ya singo yoyoo !*

Waalikwa: *Iyoo yooo !*

Kungwi: *Salama Inshallah salmin !*

Waalikwa: *Inshallah salmin !*

Kungwi: *Salimin akbar shoo !*

Waalikwa: *Shoo !*

Kungwi: *Salimina akbar shoo malika ya umidina !*

Waalikwa: *Allaha Akbar !*

Kungwi: *Ya muswali !*

Waalikwa: *Ya Salaam !*

Kungwi: *Alaikum ghasia kwa mtoto wetu!*

Waalikwa: *(wanatoa vigelegele kwa sauti ya juu)!*

#### MSG.12. NENDA NAYE

*Nenda naye mwanaao*

*Nenda naye nenda naye*

*Nenda naye mwanaao.*

#### MSG.13. MWARI AINGILE CHOONI

*Bibi aingile chooni kwa maulidi*

*Angile koga marashi uvumba na udi*

*eeee oyaaa X 2*

*Uvumba na udi X 2*

#### MSG.14. CHAMBA

*Chamba ukipata maji chamba*

*Eee chamba ukipata maji chamba*

*Mbogo ya mgeni hailali*

*Wee ukipata maji chamba*

### MSG.15. TOKANAE

*Tokanae myakanga,  
Tokanae myakanga.*

*Ende nae akarore,  
Ende nae akarore,*

### MSG.16. RINGA NAYE

*Ringa naye ringa naye*

*Ringa naye mwanaao*

*Ringa naye ringa naye*

*Ringa naye mwanaao*

*Cheza naye cheza naye*

*Cheza naye mwanaao*

*Cheza naye cheza naye*

*Cheza naye mwanaao.*

### MSG.17. HUYO YUWAJA

*Huyo yuwaja mpeni ndia,*

*Huyo yutukuzie pembe na pembe mwana mema,*

*Huyo yutukuze pembe na pembe mwana mema,*

*Atukuze akatuwe mzigo kitwani.*

### MSG.21. CHAI SHARUBATI LOZI

*Bibi anakunwa chai*

*Chai sharabati lozi*

*Mkate wake laini*

*Chai sharabati lozi*

...

### MSG.22. PASALIAPO BASI

*Mmekula mmeshiba*

*Pasaliapo basi*

*Vikombe vyako chukua*

*Pasaliapo basi*

*Mikate yako chukua*

*Pasaliapo basi*

*Chai yako chukua*

*Pasaliapo basi*

...

## (MKN) MUKTADHA KABLA KUFUNGA NIKAHA

### MKN.1. KINYEMI CHA MWANA

*Nisingekuja ila kinyemi cha mwana  
Ooh kinyemi cha mwana  
Nipe kijungo nipete unga wangu usije mwaika  
Unga wa ndere usije mwaika*

*Uchungu ee wa mwana eee aujuwaye Fatuma mzazi x2  
Alipata tabu mashaka na kazi x2  
Ugonjwa ni suna Kufa ni faradhi x2*

*Nimepewa pembe  
Nalilia pembe ee x2  
Nalilia pembe langu x2  
Napewa ni mama  
Nalilia pembe langu x2  
sikupewa ni baba*

*Una ngolo gani eee  
Una ngolo gani kushinda karanga moto ya ngoto  
Una ngolo gani ngolo yako haizimi moto  
Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa kumi.*

### MKN.2. TWASERERA

*Kina mama twasesera  
Haya*

*Kina mama twasesera  
Haya.*

### MKN.7. MAMA NJOO

*Mama njoo unifiche dudu laja hilo ooo, x2  
Mwanangu usilie ukamiliza na miye,  
Ndiko kuolewa huko oo.  
Mama njoo unifiche dudu laja huloo oo, x2  
Mama angu nitalia, eee mama angu nitalia,  
Sijaya ozoweya hayo.*

*Mama njoo unifiche dudu laja hilo ooo x2  
Mwanangu usilie ukamiliza na miye  
Utalizoeya hiloo ooo*

### MKN.8. KITAMCHOMA

*Kitamchoma eee kitamchoma*

*Kisiki cha mpera  
Wapi?  
Hapa  
Patie dawa sana pasije pakabana  
Pakamkera bwana  
Usiku na mchana*

#### MKN.9. KULA MUHOGO

*Kula muhogo,  
Kula muhogo,  
Utauona utamu wake kula muhogo ,  
Utauona utamu wake kula muhogo .*

#### MKN.10. UFUNGUO

*Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo,  
Ee kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

*Kama hakumwita bwana, watamwitia wenziwe,  
Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

*Kama hakupokea, watapokea wenziwe,  
Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

*Kama hakumsugua, watasugua wenziwe,  
Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

*Kama hakutandika, watatandika wenziwe,  
Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

*Kama hakumchezea, watachezea wenziwe,  
Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

*Tena umwambie sana, asiache ufunguo,  
Kungwi mwambie mwario, asiache ufunguo.*

#### MKN.11. NJIWA

*Ajabu ya njiwa,  
Ajabu ya njiwa.  
Mtama kupewa,*

*Maji kaatilwa.  
Kalivunja tundu,  
Kaacha behewa.*

## (MBN) MUKTADHA BAADA YA NIKAHA

### MBN.1. CHEBA

Kungwi: *iyo kawaida ya harusi yoyo!*  
Waalikwa: *iyoyoo!*  
Kungwi: *saalamayee Allah salamaa.*  
Waalikwa: *inshaallah salama!*  
Kungwi: *salmina akbar shoo!*  
Waalikwa: *shoo!*  
Kungwi: *salimina akbari shoo maliki yaumi din !*  
Waalikwa: *allahu akbar*  
Kungwi: *ya muswali*  
Waalikwa: *ya salaam*  
Kungwi: *alaikum jawabu kwa harusi wetu!*  
Waalikwa: *vigelegele.*

### MBN.2. BIBI AINGILE CHOONI

*Bibi aingile chooni kwa maulidi*  
*Tukamkoshe kibibi, kwa maji ya zamzam,*  
*Wee oya, kwa maji ya zamzam,*  
*Aliyekoga marashi, uvumba na udi,*  
*Wee oya, uvumba na udi,*  
*Uvumba na udi.*

### MBN.5. CHEZA CHEZA LEO

*Harusi yooo,*  
*Harusi yooo,*  
*Harusi imeshatimia.*  
*Cheza cheza leo umepata bwana.*  
*Maneno hakuna*  
*Chezaa chezaa leo umepata bwana.*  
*Umbea hakuna*  
*Cheza cheza leo umepata bwana.*

### MBN.6. FURAHA

*Na iwe leo ee naiwe leo furaha baba amepata mama,*  
*Na iwe leo furaha.*

*Mama amepata baba,*  
*Na iwe leo furaha.*  
*Mtango na utambae,*  
*Na iwe leo furaha.*  
*Wende ndani ukaza,*  
*Na iwe leo furaha.*  
*Uwe mche wa Baraka,*  
*Na iwe leo furaha.*

*Uzae mke na mume,  
Na iwe leo furaha.  
Wameona wawili,  
Na iwe leo furaha.  
Wazae kumi na mbili,  
Na iwe leo furaha.*

#### MBN.7. NENDA MWANANGU

*Nalinilele likanondwa vumi la jaha  
Nenda mwanangu amana Llahu amana Rasulu  
Nenda mwanangu Bisimillahi ndio ya kwanza ya kuondokea  
Huyu ajae mwana wa siwa na matawazi  
Jahazi yetu twaipeleka kwa pepo nyngangu  
Nikivumbasi sachiharafi, kila nendapo*

#### MBN.8 UTANGO

*Mkono wee  
Mkono wangu  
Ugu mlimani*

*Ukauka ukenenda mkono wangu  
Utambale ubambale  
Utango na utambale*

*Uwe mche wa Baraka  
Utango na utambale*

#### MBN.9. TUNAO MTI

*Tunao mti tunao, twende nao pole pole  
Tukaupasue mbaao mashina hata vilele  
Mbao ee mbaao mashina hata vilele  
Msonobari kwa mbaao  
Mashina hata vilele*

*Mama alipo nizaa kanifinya mara tatu  
Akanitia ungoni akanioneshwa watu.  
Tunao mti tunao, twende nao pole pole  
Tukaupasue mbaao mashina hata vilele  
Mbao ee mbaao mashina hata vilele  
Msonobari kwa mbaao  
Mashina hata vilele.*

#### MBN.10. TANDIKA MGENI AKAЕ

*Mama harusi tandika,  
Tandika mgeni acae,  
Mgeni shoga,*

*Aaa tandika mgeni akae,  
Mgeni shoga,  
Aaa tandika mgeni akae,*

**MBN.11. TWENDE UKALOLE**

*Mama harusi twende ukalole,  
Twende ukalole mgeni kaingia,  
Mgeni wangu,  
Aaa ukalole mgeni kaingia  
Mgeni mwema,  
Aaa ukalole mgeni kaingia.*

**MBN.12. KICHEKO LEO**

*Niteremke bonde na kicheko,  
Kicheko leo, kicheko,  
Dada Mwajuma kasha ukata ubeleko.*

**MBN.13. MWARI WANGU WENDA KWAKO**

*Mwari wangu wenda kwako eee,  
Kuna mambongwa huko ooo,  
Kuna bibingwa huko ooo,  
Kuna dadangwa huko ooo.  
Kuna mamangwa huko ooo,  
Kuna babangwa huko ooo.*

**MBN.14. KUTANDIKA**

*Naupiga papapa,  
Naupiga lolo.*

*Naupiga papapa,  
Naupiga lololo.*

*Usione watu kutandika,  
Kutandika kuna maana yake.*

*Usione kutandika kitanda,  
Kutandika kuna maana yake.*

*Ukitaka mume asitoke,  
Akilala mguu mpachike.*

*Kumea mvi si utu uzima,  
Bora mashini kuwa nzima.*

*Kwenda na gongo si utu uzima,*

*Bora kijiti kizima.*

*Ukitaka mume aishi,  
Kutandika ni kukaa uchi.*

*Naupiga papapa,  
Naupiga lololo.*

#### MBN.15. SHINDWE.

*Mwanangu cheka eee,  
Taimbo wa kizungu haulali eee kacheka wee.  
Taimbo wa kizungu haulali eee kacheka wee.*

*Ee mwanangu udumbe eee,  
Taimbo wa kizungu kazi yake punde wee,  
Taimbo wa kizungu kazi yake punde wee.*

#### MBN.16. KITABU

*Eeee leo achore  
Eeee leo achore  
Bwana harusi asema  
Ataka kitabu achore  
Na kalamu ashachonga  
Ataka kitabu achore*

*Eeeh leo achore  
Eeee leo achore  
Bwana harusi asema  
Ataka kitabu achore  
Na kalamu ashachonga  
Ataka kitabu achore*

#### MBN.17. HODI YA MWANAMIRAMBO

*Hodi hodi we eee  
Hodi ya mwanamirambo  
Umeniita nimekuja  
Mgeni havunji kiambo.*

#### MBN.18. TWATAKA MKE WETU.

*Twataka mke wetu  
Twende zetu kwetu*

#### MBN.19. KUNGWI WA NANI

*Mwimbaji: Kungwi wa nini huyo  
Kungwi wa nini huyo*

*Mwanamwari anajua mamboye  
Kungwi wa nini*

- Witikiaji:      *Kungwi wa ndani huyo  
Kungwi wa ndani huyo  
Akamchote maji amuekee chooni  
Akampikie wali akamuekee chumbani*
- Kungwi wa ndani huyo  
Kungwi wa ndani huyo*

#### MBN.20. UTAMPARA SAMAKI

*Umetaka mwenyewe kuolewa  
Utampara samaki*

*Samaki anamagamba eee  
Utampara samaki*

*Samaki anajicho moja eee  
Utampara samaki*

#### (MKND) MUKTADHA WA KUINGIA NDANI

##### MKND.1. DAKTARI YUWAJA

*Vumilia huyooo eee kumbe  
Chamtonesha kidonda*

*Dakitari huyoo yuwaja  
Dakitari huyoo yuwaja  
Ajakitia dawa kidonda*

##### MKND.2. WEMBE

*Waja huo wembe waja huo wembe  
Mamaee mwari naajitenge  
Waja huo wembe waja huo wembe  
Mwambiee mwana naajitenge*

##### MKND.3. YUWAJA LEO

*Yuaja leo yuaja honahona  
Yuaja na koti lake yuaja  
Horia horia*

##### MKND.4. USICHE BWANA

*Usiche Bwana harusi usiche  
Usiche Bwana harusi usiche*

*Usiche Bwana harusi usiche  
Ukiona bahari utaogelea  
Usiche Bwana harusi usiche  
Ukiona bahari utaogelea uvuke  
Usiche Bwana harusi usiche  
Usiche Bwana harusi usiche*

*Usiche Bibi harusi usiche*

*Usiche Bibi harusi usiche  
Usiche Bibi harusiusiche  
Bwana akitaka tafadhali mpe  
Usiche Bwana harusi usiche  
Usiche Bwana harusi usiche  
Usiche Bwana harusi usiche  
Umetowa pesa kununua chako  
Usiche Bwana harusi usiche*

#### MKND.5. MPAMBANO

*Leo ni leo ooo  
Leo ni leo ooo  
Tutauona mpambano  
Kweli si uongo.*

*Mzuri wa umbo na wajihii mwema  
Mwingi wa urembo na hata kusema  
Mambo kanitenda bila ya huruma  
Leo ni leo ooo  
Leo ni leo ooo  
Tutauona mpambano  
Kweli si uongo.*

*Haifiki muda nahilo lijue  
Wote ni waongo mwenyewe ni wewe  
Baada ya shahada nakutaja wewe.*

#### MKND.6. TUMKOSHE MAU BWANA

*Tumkoshe mau bwana  
Kwa mai ya zamzam.*

#### MKND.9. MAJUMBANI

*Mama ukakae na mumeo  
Vumilia mambo ya nyumbani  
Mwanangu kipande cha papa  
Vumilia mambo ya nyumbani kunga.*

## (MHK) MUKTADHA BAADA HARUSI KUJIBU

### MHK.2. KOKO

*Koko wee koko  
Nyumba ya mwari aingia koko  
Paramira.*

### MHK.4. HONGERA MWANANGU

*Hongera mwanangu wee hongera  
Nami nihongere wee hongera  
Mwana jaha na jamali kajamili uso wake*

*Mwarichamba hayawi, mbona yaliwele  
Wake wacheni kunamba, mnong'ono na ukome  
Papa kwa papa walana, papa mkubwa kamla mwenzewe  
Mtama wangu mteto, rijali kaulimbuwa  
Mwanangu mkembe, hajajua jambo.*

### MHK.6. KIKAANGO

*Asaa kwa ninikikaango change  
Sicha kupika kina mfuniko  
Kama birika ukikifunua utachoka.*

### MHK.7. KIMENICHOMA

*Kimenichoma eee kimenichoma  
Kisiki cha mpera  
Wapi?  
Hapa  
Patie dawa sana pasije pakabana  
Pakamkera bwana  
Usiku na mchana*

### MHK.8. MUNGU KANIPA HIDAYA

<i>Furaha nyangi moyoni</i>	<i>Rabi kanijaaliya</i>
<i>Vipi nikuelezeni</i>	<i>ili yapate weleya</i>
<i>Ndoto yangu ya zamani</i>	<i>leo imekamiliya</i>
<i>Siku zote peke yangu</i>	<i>nikiranda na duniya</i>
<i>'Napowaona wenzangu</i>	<i>husuda nawaoneya</i>
<i>Moyo kiona uchungu</i>	<i>fanaka kunifikasiya</i>
<i>Umenitoka upweke</i>	<i>yangu yamekamiliya</i>
<i>Rabi amenipa mke</i>	<i>mzuri alotimiya</i>
<i>Karimu ni roho yake</i>	<i>imani yake tabiya</i>
<i>Mola kwa imani yake</i>	<i>yeye kanifikasiya</i>
<i>Tena kwa khiyari yake</i>	<i>mwenyewe kaniumbiya</i>
<i>Kisha kwa fadhila zake</i>	<i>miye kanitunukiya</i>

## **(MKU) MUKTADHA KUINGIA UKUMBINI**

### **MKU.1. MASOMASO**

*Masomaso mwanangu yasimuone  
Masomaso mwanangu yasimuone*

*Jicho la hasidi mwanangu lisimuone  
Jicho la hasidi mwanangu lisimuone*

### **MKU.3. TUMEJIZUNGUA**

*Tumejizungua kwa ya Yasin tatu  
Halitupati jicho lolote la mtu*

## **(MKS) MUKTADHA WA KUKABIDHI SANDUKU**

### **MKS.1. SASAMBU**

*Sasambu sasambu sasambu  
Sasambure turore sasambure turore  
Sasambure turore!*

## **KIAMBATANISHO CHA III**

### **NYIMBO ZA HARUSI ZILIZOSALIA**

Kama tulivyoeleza katika ukusanyaji wa data kuwa, nyimbo tisini (90) zimekusanywa na kuchanganuliwa nyimbo sitini (60). Utafiti umeonelea upo umuhimu wa kuzioredheshwa nyimbo zilizosalia kwa ajili ya kuzihifadhi na kutumiwa kama marejeo au kutumiwa na watafiti wengine pengine watazihitaji kwa uchanganuzi tofauti na huu. Nyimbo zilizosaliva na ambazo hazikuchanganuliwa ni hizi zifuatazo:-

#### **MUKTADHA WA SINGO (MSG)**

##### **MSG.6 SINYOMBE**

*Sinyombe sinyombe mwari wangu,  
Sinyombe mume apikiwa mwari ee sinyombe.*

*Sinyombe sinyombe mwari eee,  
Sinyombe ukitaka chumvi kwa jirani uombe.*

*Sinyombe sinyombe mwari wangu,  
Sinyombe ukiona mrimbangwa epenuni uombe.*

*Sinyombe sinyombe mwari eee,  
Sinyombe mume aitwa bwana, mwari ee sinyombe.*

*Sinyombe sinyombe mwari wangu,  
Sinyombe mume apokewa, mwari ee sinyombe.*

*Sinyombe sinyombe mwari eee,  
Sinyombe mume afuliwa, mwari ee sinyombe.*

##### **MSG.8. RUHANGA**

*Ukienda shamba msitupane,  
Muogope ruhanga na mwenziwe simba  
Muogope ruhanga na mwenziwe simba*

##### **MSG.9. UMBEA**

*Nasema na mume wangu eee,  
Kuna kikongwe chanichuma umbea.*

##### **MSG.10. MTENDEENI MWENZENU**

*Mtendeeni mwenzenu,  
Mtendeeni mwenzenu,*

*Mtendeeni mwenzenu,  
Kesho kutwa mambo yatakuwa kwenu.*

**MS.18. YUAKUNDUA NGUO**

*Yuakundua nguo ja manga  
Yuakundua nguo ja manga*

**MSG.19. MUME NI MOSHI**

*Huno ni wasia wako, mwanangu nakupa shika,  
Itunge heshima yako, upate kusitirika,  
Mume ni moshi wa koko, usipowaka wafuka.*

*Huno ni wasia wako, mwanangu nakupa shika,  
Mukae na mume wako, hatutaki mashaka,  
Mume ni moshi wa koko, usipowaka wafuka.*

**MSG.20. VITI VIWILI**

*Viti viwili mfano matendegu,  
Sawa sawa,  
Viti viwili mfano matendegu,  
Sawa sawa,  
Matendegu sawa sawa eee,  
Matendegu sawa sawa.*

**MSG.23. FIMBO**

*Wacha kukoroma aah bwana wacha kukoroma  
Fimbo ya kwanza aah hewallla bwana  
Fimbo ya pili aah hewallla bwana  
Fimbo ya tatu aah hewallla bwana  
Fimbo ya nne aah hewallla bwana  
Fimbo ya tano aah hewallla bwana  
Fimbo ya sita aah hewallla bwana  
Fimbo ya saba aah hewallla bwana  
Fimbo ya nane aah hewallla bwana  
Fimbo ya tisa kumanina unaniumza mtwana*

**MSG.24. ACHA KUKOROMA**

*Kila nikikuita wanayamaza kimya eee  
Chukua mapumbu uyaweke nyuma  
Wacha kukoroma nwana vitombe kuma  
Na mkuma wangu nimeusugua  
Na mavuzi yangu nimeyanyonyoa  
Wacha kukoroma vitombe kuma*

*Ashin ashin nalidhani mboo kumbe msuwaki  
Ati we mkuma wangu nimeusugua vyema  
Wacha kukoroma vitombe kuma  
Mume wangu wangu simwambii nacha  
Kila vijiti na utamu wake*

#### MSG.25. YUNO MWANA KAMZAA NANI

*Yuno mwana hana mamake kaa nae  
Tumbo lizalie mwana hilo  
Nilisema anakikuma kidogo  
Yuno mwana kamzaa nani?*

*Baba Juma nigiae rungu mimi  
Sina rungu, rungu lote liliwa na pumbu  
Ilobaki kuliwa ya mkundu*

*Humo mkobani mna nini?  
Kombe na kidagara  
Humo mkobani mna nini?  
Pumbu linagara gara  
Hamlala mna maradhi gani?  
Mkilala walalia pajani  
Hamlala mna maradhi gani?*

#### MSG.26. KUTWANGA BUMBWI

*Hulonja bumbwi langu  
Hulonja nishatia sukari  
Hulonja bumbwi langu*

*Natakata upeleleze mtaimbo  
Wateleza mtaimbo  
Kisha utambuwa mchungu  
Kisha utambuwa uchungu.*

#### MSG.27. TUKAMYOE MYAKANGA

*Tukamyoemnyakanga tukamyoemnyakanga  
Mwari wakuru wakamkague.*

*Tukamyoemnyakanga tukamyoemnyakanga  
Mwari wakuru wakamkague.*

#### MSG.28. HOWANI MWANA HOANI

*Howani mwana hoani, howa mwanganu howa  
Kitunguu na ubani, howa mtoto nyamaza kulia  
Kilenge lenge cha boga, howa nyamaza kulia  
Kutia nazi kunoga, howa nyamaza kulia*

*Mkono wataka kula, howa nyamaza kulia  
Roho ina ona woga, howa nyamaza kulia.*

#### MSG.29. JENDA NAE JENDA NAE

*Jenda nae jenda nae, jenda nae mwanawene  
Jenda nae jenda nae, jenda nae mwanawene  
Jenda nae jenda nae, jenda nae mwanawene  
Kula nae kula nae, kula nae mwanawene*

*Kula nae kula nae, kula nae mwanawene  
Kula nae kula nae, kula nae mwanawene  
Nawe ajawirere kwenda nae mgongoni.*

#### MSG.30. BISMILLAH AWALI

*Bismilahi wali ndoyo takayoanziaya  
Nahimidi ni ya pili na swala kufuatiya  
Nimeinyosha miwili ya kheri kukuombeya*

*Kwa marashi nimetuwa nipokeya wa jamali  
Sandal na lema liwa usinge wako muili  
Rwabi idumishe ndowa mahaba yaliyo ali*

### MUKTADHA KABLA KUFUNGA NIKAHA (MKN)

#### MKN.3. YUWAPI MAMAKE HARUSI

Yuwapi eee,  
Yuwapi eee,  
Yuwapi mamake harusi,  
Aje hapa tuangaike naye,  
Aje hapa tuangaike naye

#### MKN.4. HODI

*Hodi wee                    hodi hodi  
Mama shikamoo            marahaba saidi*

#### MKN.5. NOTI NAIRAWE

*Noti nairawe,  
Noti nairawe  
Mamake harusi kijana noti nairawe.*

#### MKN.6. ZIPUKUTIKE PESA

*Zipukutike pesa zipukutike,  
Zipukutike pesa zipukutike,  
Mamake harusi hana kitu kibambara kijembe*

#### MKN.12. RANGI YA MDOMO

*Mau ee maua  
Rangi ya mdomo ya ua  
Mau ee maua  
Rangi ya mdomo ya ua*

#### MKN.13. MAMA NJOO UNIFICHE

*Mama njoo unifiche babu laja hilo wee  
Mwanangu usiliye sikiliza nikwambia  
Ndiko kuolewa ukoo aaa nenda hamtege njiwa  
Njiwa wee njiwa njiwa aaa nenda hamtega njiwa.*

#### MKN.14. BABURAU

*Baburau ana marere ana mkia  
Wapataje?  
Wapata hivi na unyanda tele we na mkono tele ukabakia  
Vile likipwa lapataje?  
Lapata hivi na mkonowe na unyanda we na mkono tele ukabakia.*

#### MKN.15. MTAIMBO

*Hauna eeeh  
Hauna laika  
Eeeh laika eeeh  
Ooo hauna huo  
Haun laika  
Naupeleleza mtaimbo  
Unateleza mtaimbo  
Mtaimbo wa zamani  
Unateleza mtaimbo  
Mtaimbo oooh mtaimbo*  
  
*Hautaki kulala  
Hauna laika  
Ni kipara huo  
Hauna laika  
Mtaimbo oooh mtaimbo  
Nalia yomi kikumbuka mtaimbo wangu nalia  
Nalia yomi kikumbuka mtaimbo wangu nalia  
Mtaimbo wa ajabu  
Unateleza mtaimbo*

#### MUKTADHA BAADA YA KUFUNGA NIKAHA (MBN)

#### MBN.3. NDEMBO AYOGA

*Ndembo ayaga na mwanawewe*

*Ndembo ayaga na mwanawe*

**MBN.4. NDEMBO AWAYA NA MWANAWE**

*Ndembo awaya na mwanawe  
Ndembo awaya na mwanawe*

**MBN.21. MWANANGWA**

*Huyo huyo mwanangwa  
Umpe chumvi mwanagwa  
Umpe kula mwanangwa  
Umpe nguo mwanangwa  
Usimpige mwanangwa*

**MBN.22. HULONJO**

*Hulonjo hili hulonjo bumbwi langu*

*Nishatia sukari hulonjo wee.  
Hulonjo hili hulonjo bumbwi langu  
Nishatia sukari hulonjo wee.*

**MBN.23. HODI**

:      *Hodi wee*                  *hodi hodi*  
      *Mama shikamoo*              *marahaba saidi*

**MBN.24. MUME NDUGUYO**

<i>Myengetyenge kama kioo</i>	<i>mume nduguyyo</i>
<i>Akikuaga mperuhusa</i>	<i>mwana na kwao</i>
<i>Hiyo ni ila ya mwanamke</i>	<i>mara kwa mama</i>

**MBN.25. PEMBE**

*Pembe pembe  
Nalilia pembe langu  
Moja, mbili, tatu, nne, tano,  
Sita, saba, nane, tisa, kumi  
Nalilia pembe langu.*

**MBN.26. MAKIWA UTAMPARA**

*Makiwa Makiwa aaa mwenzenu kasha olewa  
Leyo anachukuliwa Makiwa utampara  
Huo utampara huyo ultaka kusudi kuolewa  
Utampara samaki aa utampara samaki.*

**MBN.27. HAURIRIMI**

*Hauririmi hauririmi msondo kama hojaja  
Bisamu gongo hauririmi msondo bila Juma*

*Kula mkule niachiye mwenyewe nibanje  
Ooo nibanje huwo mfupa wangu  
Wangu mbee arerererere.*

#### MBN.28. MKURUNGWA MKURUNGWA

*Mkurungwa mkurungwa,  
Pamrango penu parira ngoma.*

*Mkurungwa mkurungwa,  
Pamrango penu parira ngoma.*

#### MBN.29. UKENDA NDIYA

*Ukenda ndiya na nyuma ukirora  
Ukenda ndiya na nyuma ukirora*

#### MBN.30. HUKO PWANI

*Huko pwani kuna uwa lina rangi ya manjano  
Ukitaka kulichuma ulidunge sindano  
Kuolewa si besera haja ni masikilizano*

#### MBN.31. LEO UMEPATA WAKO

*Leo umepata wako mahawara ni wakome  
Wakija mashoga zako sema nao dirishani  
Wakija mawifi zako sema nao ukumbini  
Wakija shemegi zako sema nao mlangoni  
Upewacho kipokea haukupewa jimezee  
Utilizane ukae vumilia usikhini.*

#### MBN.32. KOMBO WEE KOMBO

*Kombo wee kombo, kanipa mapesa yangu  
Kilicho nitoa nyumba vivu wa mke mwenzangu*

*Uko Mwera mtarimbo uko Mwera eee  
Una nini bwana una nini bwana?  
Wapitish sukurubu mtarimbo haujaja ee.*

#### MBN.33. KAA NAYE SANA MUMEO

*Kaa naye sana mumeo  
Mpoke kwa lakwe na nguo  
Mkhadae kwa khadaa na esha  
Na nguoze zina masimbuo  
Kheri shuka kama shali isio maua*

#### MBN.34. HAOLEWI

*Mulisema haolewi  
Mbona kaolewa*

*Mulisema hampendi*

*Mbona kampenda*

*Mulisema hamuowi*

*Mbona kamuowa*

*Mulisema hamtaki*

*Mbona kamtaka*

*Mbona kaolewa leo eeeh*

*Mbona kaolewa leo eeeh*

*Mbona kaolewa leo eeeh*

*Mulisema hapendezii*

*Mbona kapendeza*

*Leo mbona kapendeza*

*Leo mbona kapendeza*

**MBN.35. SHEMEGI**

*Mama uisinipige bure kwa sababu ya shemegi*

*Mama uisinipige bure kwa sababu ya shemegi*

*Nilikuwa nimelala kaja usiku eee kanambiya twende*

*Nilikuwa nimelala kaja usiku eee kanambiya twende*

#### **MBN.36. MTAIMBO**

*Hauna eeeh*

*Hauna laika*

*Eeeh laika eeeh*

*Ooo hauna huo*

*Haun laika*

*Naupeleleza mtaimbo*

*Unateleza mtaimbo*

*Mtaimbo wa zamani*

*Unateleza mtaimbo*

*Mtaimbo oooh mtaimbo*

*Hautaki kulala*

*Hauna laika*

*Ni kipara huo*

*Hauna laika*

*Mtaimbo oooh mtaimbo*

*Nalia yomi kikumbuka mtaimbo wangu nalia*

*Nalia yomi kikumbuka mtaimbo wangu nalia*

*Mtaimbo wa ajabu*

*Unateleza mtaimbo*

## MUKTADHA WA KUTOA MKONO/ KUINGIA NDANI (MKND)

### MKND.7. MWENYE KARUME

*Mwenye karume na karume chake  
Mkande nyayo akurupuke.*

### MKND.8. SEJIOKOTEA MACHAKACHA

*Sejiokote machakacha  
Sejiokote machakacha*

*Mwanangu kapata ndume wa haja  
Sejiokotea machakacha*

### MKND.10. MAMBO NI LEO

*Mamae harusi asema mambo ni leo  
Mamae harusi asema mambo ni leo  
Mambo ni leo  
Ni leo  
Mambo ni leo  
Nduguze harusi wasema eee mambo ni leo  
Nduguze harusi wasema eee mambo ni leo  
Mambo ni leo  
Ni leo  
Mambo ni leo  
Shangazile harusi wasema eee mambo ni leo  
  
Shangazile harusi wasema eee mambo ni leo  
Mambo ni leo  
Ni leo  
Mambo ni leo*

## MUKTADHA BAADA HARUSI KUJIBU (MBHK)

### MBHK.1. MAME MWARI

*Mame mwari mgasema naye, mgachecha naye  
Mwaiona ngondo mwairekerere.*

*Mama usungu, mama usungu, nyamara mwanangu  
Sungura udere linauma mno eeh oyee*

*Joka kuru ramrari ra mpinga  
Chigumu cha waremerawatwanz.*

### MBHK.3. HONGERA - NYAMARA MWANANGU

*Hongera mwanangu hongera,  
Nami nihongere wee hongera*

*Mama uchungu mama uchungu  
Nyamara mwanangu ooee*

*Nyamara mwanangu tumbo la urere  
linauma mno oya linauma mno oya*

*Eee lina uma mno eee,  
Nipani pole wenzangu*

*Oyee lina uma mno eee oya.*

#### **MKND.12. SORORO**

*Bwana anakula sororo kwa manyama nyama  
Bwana anakula sororo kwa manyama nyama*

#### **MBHK.5. MUME MWOGA**

*Mume mwoga mkimbia ng;ombe  
Sitamwoza mwanangu.*

#### **MBHK.8. KESHA UONA**

*Alipouona Harusi wenu alikwenda mbio  
Ah! Ah! Eee sijabu tena  
Mtaimbo kasha uona*

### **MUKTADHA KABLA BIBI HARUSI KUPAMBWA (MKBK)**

#### **MKBK.1. MAMA FARADHI**

*Mama faradh mama faradhi,  
Za kwenda makka na za kurudi  
Huzur ziara ya Muhammaadi  
Na malaikae na masahaba  
Hiyo ni ila ya mwanamke, mara kwa mama  
Akikuaga mpe ruhusa mwana na kwao  
Mke nduguyo mwengeenge kama kiyoo  
Tumbuizeni msichokeni, mwana mbwa wema*

#### **MKBK.2. JIMBI LA WIKA**

*Kanitieni Sienu aye, jimbi la wika  
Mwana ni ini nanyimwayafahamu  
Mumenduguyi mweengeenge kama kiyoo*

#### **MKBK.3. NYUMBA YA NANA**

*Nyumba ya nana tuitandike kwa matandiko  
Tandika sawa.*

*Nyumba ya nana tuipambe kwa chandarua  
Tuipambe sawa*

#### MKBK.4. MKONO WANGU

*Mkono wee mkono wangu  
Ugu mlimani ukauka ukanenda mkonio wangu  
Utambale utambale utango na utambale  
Uwe mche wa baraka utango na utambale.*

#### MUKTADHA KUINGIA UKUMBINI (MKU)

##### MKU.2. MTOTO WA NANI

<i>Jamani wee yanani</i>	<i>yako wee wambiwa</i>
<i>Yuno mtoto wa nani</i>	<i>wako wee wambiwa</i>
<i>Sijapo sejawapo</i>	<i>wako wee wambiwa</i>
<i>Nilikwenda masomoni</i>	<i>wako wee wambiwa</i>

##### MKU.4. SUNA YA MTUME

*Mabibi mabwana na watoto pia  
Mlokuja hapa kushereheka  
Harusi ya bwana na bibie pia  
Weshata tekeleza suna ya Mtume.*

##### MKU.5. KHERI TWAKUTAKIA

*Ewe mwangu mtulivu  
Kheri twakutakia*

*Nenda kwako kwa salama  
Uje kwenu kwa salama  
Haya tuna kutakiya*

##### MKU 6. FUNUA MACHO

*Funua macho uone  
Usidhani mwandum*

##### MKU.7. WANAINGIA

Muimbajii:	<i>Bwana na Bi. Harusi</i>
Waitikiaji:	<i>Wanaingia</i>
Muimbajii:	<i>Aah wanaingia</i>
Waitikiaji:	<i>Wanaingia</i>
Muimbajii:	<i>Tushereheke wanaingia</i>
Waitikiaji:	<i>Wanaingia</i>
Muimbajii:	<i>Wanapendeza wanaingia</i>
Waitikiaji:	<i>Wanaingia</i>
Muimbajii:	<i>Vigelegele kidogo</i>
Waitikiaji:	<i>Wanaingia</i>

#### MKU.8. OWA

<i>Owa ndugu yetu owa,</i>	<i>kama ilivyo sheria X 2</i>
<i>Mtume kafunga ndoa,</i>	<i>na mahari akatowa X 2</i>
<i>Tuna muomba Karima,</i>	<i>kwa ndoa hii adhima.</i>
<i>Aijalie Rahimu,</i>	<i>kuijaza nyingi nuru,</i>
<i>Rabi utukubalie,</i>	<i>dua zetu waumini,</i>
<i>Baraka umjazie,</i>	<i>za nje na za ndani.</i>
<i>Malaika wenyе kheri,</i>	<i>Yarabi tuzidishie,</i>
<i>Watuombee mazuri,</i>	<i>ndoа itunyokee,</i>
<i>Kwa Baraka za Manani,</i>	<i>Am-biana Rasuli.</i>
<i>Pasiewe kwenda na kinyume,</i>	<i>kuhusu na jambo ili,</i>
<i>Yarabi kwa sifa zake,</i>	<i>twaombatukusalie,</i>
<i>Jaha ya Mtume wetu,</i>	<i>ije itushuhudie.</i>
<i>Mwisho tuna malizia,</i>	<i>Mtume wetu hashima,</i>
<i>Dua tunaiombea,</i>	<i>kwa ndoa hii adhiima.</i>

#### MKU.9. UTUPE KILA LA KHERI

<i>Leo ni siku tukufu,</i>	<i>waumini shangiria,</i>
<i>Hii ni siku adhima,</i>	<i>Yarabbi katuletea,</i>
<i>Na sote waisilamu,</i>	<i>hima hima shangiria,</i>
<i>Twakuomba ya Karima,</i>	<i>utupe kila la kheri.</i>
<i>Harusi yetu adhima,</i>	<i>leo imetufikia,</i>
<i>Ni harusi ya (jina la bw na Bi. Harusi)</i>	<i>Yarabbi katuletea,</i>
<i>Awe mtu mzuri,</i>	<i>Yarabbi kamuongoa,</i>
<i>Twakuomba ya Karima,</i>	<i>utupe kila la kheri.</i>
<i>Uijalie salama,</i>	<i>ndoа iwe ya adhima,</i>
<i>Uwaondolee sahri,</i>	<i>leo na kesho kiama,</i>
<i>Na sisi utujaalie,</i>	<i>ndoа tuiifikilie,</i>
<i>Twakuomba ya Karima,</i>	<i>utupe kila la kheri.</i>
<i>Uwape watoo wema,</i>	<i>wenyе kheri na salama,</i>
<i>Watoto wawe na khei,</i>	<i>duniani na kiama,</i>
<i>Bibie mtunze bwana,</i>	<i>ukae nae salama,</i>
<i>Twakuomba ya Karima,</i>	<i>utupe kila la kheri.</i>
<i>Yarabbi tupe salama,</i>	<i>duniani na kiama,</i>
<i>Utupe kila la kheri,</i>	<i>ujalie salama,</i>
<i>Utuondolee shari,</i>	<i>za dunia na za kiama,</i>
<i>Twakuomba ya Karima,</i>	<i>utupe kila la kheri.</i>

## **MUKTADHA WA KUKABIDHI SANDUKU (MKS)**

### **MKS.1. BABURAU**

*Baburau ana marere ana mkia*

*Wapataje?*

*Wapata hivi na unyanda tele we na mkono tele ukabakia*

*Vile likipwa lapataje?*

*Lapata hivi na mkonowe na unyanda we na mkono tele ukabakia*

## **KIAMBATANIISHO CHA IV**

### **MWONGOZO WA MASWALI KWA WASAILIWA**

#### **A.Mwongozo wa maswali kwa Waimbaji Wasaidizi**

1. Jina lako ni nani?
2. Nyimbo huimbwa katika sherehe zipi harusini?
3. (a) Je, nyimbo huimbwa katika miktadha gani?  
(b) Wakati gani nyimbo hizo huimbwa?  
(c) Nyimbo hizo huimbwa kwa hadhira gani?  
(d) Waimbaji wa nyimbo hizo ni kina nani?
4. Je kuna uchezaji wakati wa uimbaji?
5. Uchezaji huo ni wa aina gani?
6. Je, uchezaji huo una umuhimu gani?

#### **B.Mwongozo wa Maswali kwa Wasingaji/Makungwi**

1. Jina lako ni nani?
2. Ni kwa muda gani tangu uwe kungwi?
3. Ni bibi harusi wangapi umewahi kuwasinga?
4. Ni wakati gani bibi harusi huwa anasingwa?
5. Je, kuna nyimbo zinazoimbwa wakati wa kumsinga bibi harusi?
6. Ikiwa ndio, niimbie nyimbo unazozifahamu ni zisikie?
7. Je, kuna nyimbo mahasusi kwa ajili ya singo au ni nyimbo zozote huimbwa?
8. Je, nyimbo ziimbwazo wakati wa singo zinaweza kuimbwa katika muktadha usiokuwa wa singo?

9. Je kuna ala zozote za muziki zinazopigwa wakati wa kumsinga bibi harus?
10. Je, kuna tofauti yoyote ya uwasilishwaji nyimbo za singo na nyimbo nyingine katika sherehe za harus?
11. Je, kuna vitendo vyovyyote vinyavyoandamana na uwasilishwaji wa nyimbo wakati wa singo?
12. Wadhani nyimbo ziimbwazo wakati wa singo zikiimbwa bila ya kuwepo na vitendo zingefahamika?
13. Je, kuna taashira zozote katika nyimbo za singo?
14. Iwapo kuna taashira katika nyimbo hizi, je, maana ya taashira wadhani zinafahamika na kila mtu?
15. Nani hushirikishwa katika nyimbo za singo?
16. Washiriki hawa wanajukumu gani katika singo?
17. Singo la bibi harus lina umuhimu gani katika sherehe za harus?
18. Kama bibi harus hakufanyiwa singo, sherehe ya harus huwa haikamiliki?
19. Je, kuna tofauti baina ya singo la bibi harus na lile la bwana harus? Kama zipo, ni tofauti gani hizo?
20. Je, nyimbo ziimbwazo katika singo ya bibi harus hutafautianaje na zile ziimbwazo katika singo ya bwana harus?
21. Taashira nitakazo kutajia husimamia maana gani?

### **C. Mwongozo wa Maswali kwa Waimbaji**

1. Jina lako ni nani?
2. Unatoka wapi?
4. Hamu ya kupenda kuimba ilitokana na nini?
5. Nyimbo za harus ni nani anayezitunga?
6. Ni ala gani unazotumia wakati wa kuimba nyimbo?
7. Je, nyimbo za harus huimbwa katika miktadha gani harusini?

8. Taja sherehe hizo zinazoimbwa nyimbo.
9. Niimbie nyimbo unazozifahamu zinazoimbwa wakati wa sherehe?
10. Taja sherehe ambazo nyimbo haziimbwi?
11. Nyimbo hizo huimbwa kwa hadhira ya aina gani?
12. Waimbaji wa nyimbo hizo ni kina nani?
13. Je, utendaji katika uwasiliswaji wa nyimbo una umuhimu wowote katika sherehe ya harusi?
14. Kupiga makofi wakati wa uimbaji nyimbo husaidia nini? Au zina maana yoyote?
15. Je, vigelegele vinavyopigwa wakati wa harusi hutafautiana kimaanana?
16. Mitindo wa ukataji wa kiuno unaofanywa na wanawake wakati wa kuimba nyimbo una maana yoyote?
17. Je, unaweza kunionyesha mitindo wa kuataji kiuno wenye maana?

#### **D. Mwongozo wa Maswali kwa Mashehe**

1. Jina lako ni nani?
2. Sherehe za harusi huwa na matukio mangapi?
3. Harusi za Waswahili husherehekewa kwa siku ngapi?
4. Je, kuna tamaduni gani zinayofanywa wakati wa sherehe ya harusi?
5. Je, tamaduni hizi huambatana na uwasilishwaji wowote wa nyimbo?
6. Je, tamaduni hizi huambatana na vitendo gani?
- 7 .Je, tamaduni hizi zina umuhimu wowote katika sherehe ya harusi?